**10 FEBRUARI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

**Kikao cha Kumi – Tarehe 10 Februari, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. MARTHA N. GWAU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA *(PIC)*:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)* kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

Katibu.

**10 FEBRUARI, 2025**

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza kipindi chetu cha maswali na tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Swali la Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe, litaulizwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi.

Na. 158

**Kufanya Mabadiliko kwenye Kikokotoo cha Watumishi Nchini**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. NICODEMAS H. MAGANGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafanya mabadiliko kwenye Kikokotoo cha Watumishi nchini kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 Serikali ilifanya mabadiliko ya Kikokotoo kwa watumishi nchini na mwaka 2024/2025 imefanya maboresho zaidi kwenye kikokotoo hicho baada ya mjadala ndani ya Bunge lako kama ifuatavyo:-

(i) Kuboresha malipo ya mkupuo kutoka 33% hadi 40% kwa waliokuwa wanapata 50% na kutoka 33% hadi 35% kwa waliokuwa wanapata 25% kabla ya kuunganishwa kwa Mifuko mwaka 2018; na

(ii) Mwezi Januari 2025, Serikali imeongeza kima cha chini cha pensheni kutoka shilingi 100,000 hadi shilingi 150,000 kwa mwezi. Vilevile, Serikali imehuisha *(indexation)* pensheni ya kila mwezi kwa kiwango cha asilimia mbili kwa kuzingatia sheria na Kanuni zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, naomba kulijulisha Bunge kuwa, Serikali itaendelea kufanya tathmini ya kupima uhimilivu wa Mifuko kila baada ya miaka mitatu kama inavyoelekezwa kisheria ili kuangalia uwezo wa kuboresha mafao bila kuathiri uendelevu wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali kwa hizi hatua muhimu sana ambazo imekuwa ikizichukua kuhakikisha kwamba inaboresha maisha ya wafanyakazi na wastaafu, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; tunatambua nyongeza hii ya shilingi 50,000 kutoka 100,000 kwa wale wastaafu wa zamani, lakini ninaiomba Serikali kuendelea kufanya tathmini ya kina na kwa kuangalia uhimilivu wa Mifuko pia kwa kuangalia hali ya maisha ili kuona kwamba tunaweza tukawaongezea hawa wastaafu wa zamani ambapo 150,000 bado ni kiwango kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kumekuwa na utaratibu wa Serikali kufanya ufuatiliaji wa watumishi kwa kuangalia hali zao kama bado wako hai ama wamefariki. Kwa bahati mbaya sana wastaafu wengi ni wagonjwa na mara nyingi zoezi hili linafanyika katika ngazi ya mikoa ama nusu mkoa, kwa maana ya kwamba wanaweza wakawaambia wilaya tatu zikutane mahali fulani. Je, Serikali haioni kwamba Serikali inawadhulumu hawa watumishi ambao wametumikia Taifa kwa muda mrefu, ni vyema ikawafuata kule walipo ili kuweza kufanya hiyo tathmini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rashid Shangazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza katika swali lake la kwanza amegusia au kushauri Serikali kuendelea kufanya tathmini ya kina

ili kuweza kuangalia inadhibiti vipi malalamiko na hali za wananchi wake. Ninamwahidi Mheshimiwa Shangazi pia kuliahidi Bunge lako kwamba, Serikali inaendelea kufanya hivyo na kama tulivyoeleza kwamba kigezo kikubwa ni ustahamilivu wa Mifuko yetu kupitia ule utaratibu wetu wa kufanya *actuarial studies*, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, jambo hilo tunaendelea kulifanya na tutaendelea kulifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, juu ya wastaafu wengi ambao hali zao kiafya siyo nzuri na wanaishi pembezoni. Utaratibu wa sasa, ni utaratibu ambao ninaweza kusema kwa namna moja au nyingine unashirikisha mpaka chini. Kupitia Ofisi za Wakuu wetu wa Mikoa na Wilaya tumeweza kufanya utaratibu ambao taarifa za mstaafu mmoja mmoja katika kila eneo analoishi tunazipata na tunazifanyia kazi. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama wako wastaafu ambao kutokana na hali zao taarifa zao zinashindwa kufika huku, basi kupitia utaratibu huo Ofisi za Wakurugenzi wetu wa Wilaya, Ofisi za Wakuu wetu wa Wilaya na Ofisi za Wakuu wa Mikoa basi nimhakikishie kwamba tukishapata taarifa hizo tutalifanyia kazi na kuweza kutatua changamoto zilizopo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa, kuna baadhi ya watumishi walilipwa kwa ile asilimia iliyokuwa imepunguzwa na sasa hivi Serikali yetu imerekebisha na wengine bado hawajalipwa ile fidia. Je, nini kauli ya Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Serikali ni kwamba wale watu wote ambao wana madai yoyote yanayoendana na malipo ya kikokotoo kutokana na sintofahamu siyo tu hii aliyoizungumza Mheshimiwa Mbunge, lakini za aina yoyote ikiwemo hata taarifa kuwa hazijakaa vizuri, ningeomba ziwasilishwe katika ofisi yetu ili tuweze kuzifanyia kazi. Kwa sababu Serikali ya Awamu ya Sita kama nilivyoeleza, kitendo cha

kuongeza kutoka 100,000 mpaka 150,000 ni wazi inaonyesha kwamba mambo yetu ya kiuchumi yamekwenda vizuri na Mheshimiwa Rais yuko tayari kwa ajili ya kuwasaidia wote wenye mahitaji na ambao wana matatizo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako, kama wapo watu ambao wana malalamiko yoyote basi ofisi yangu iko tayari kupokea malalamiko hayo na kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri kutokana na jibu la msingi amesema ameweza kuongeza kutoka 100,000 mpaka 150,000. Mheshimiwa Waziri haoni kwamba maisha yamepanda yako juu sana, 150,000 kwa mstaafu haiwezi kumtosha. Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuongeza fedha hata angalau ifike 600,000 ili kumsaidia Mzee huyu aliyetumikia hili Taifa kwa muda mrefu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, karibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo analosema Mheshimiwa Mbunge ni wazo ambalo hata mimi binafsi yangu, kwa sababu nina wastaafu pale Chalinze na maeneo mengine ningependa wafike huko, lakini malipo haya ya kikokotoo yana vigezo vingi kimojawapo ikiwepo hali ya uchumi na uwepo wa ustahamilivu wa mifuko yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatamani sana kama ingekuwa tuna uwezo huo mkubwa ndani ya Mifuko yetu tuweze kulipa hata ikiwezekana 1,000,000, lakini kwa sasa tulipo hili ongezeko la 100,000 mpaka 150,000 ni sehemu ya haya makubwa ambayo yanafanyika ikiwemo na mambo mengine yanayoambatana na maongezeko hayo kama nilivyoeleza katika jibu la msingi, ikiwemo lile ongezeko la asilimia mbili za kiwango cha kila mwezi cha malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali na Mifuko itakapojenga uwezo huo nadhani tunaweza tukaangalia katika hayo, kwa sasa hivi, itoshe kumwambia Mbunge kwamba yapo mambo makubwa yanafanyika na Mheshimiwa Rais yupo tayari kwa ajili ya kuyasikiliza hayo.

**MWENYEKITI:** Swali la Mheshimiwa Toufiq Salim Turky, Mbunge wa Mpendae litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Asya Sharif Omar.

Na.159

**Upungufu wa Ajira kwa Vijana Nchini**

**MHE. ASYA SHARIF OMAR K.n.y. MHE. TOUFIQ SALIM TURKY** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuwandaa vyema Vijana kushindana katika soko la ajira ndani na nje ya Tanzania ili kukabiliana na upungufu wa ajira nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya Serikali katika kuwaandaa vijana ili waweze kushindana katika soko la ajira ndani na nje ya nchi ni kama ifuatayo kwa ufupi:-

(i) Kubuni na kutekeleza programu maalum zinazowawezesha vijana kujifunza kwa vitendo kupitia sekta zinazozalisha ajira kwa wingi kama vile Sekta ya Kilimo kupitia Jenga Kesho Iliyobora, ujasiriamali na programu za madini kama vile *Mining for a Better Tomorrow (MBT)*;

(ii) Kufanya maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la Mwaka 2023, ambayo yanasisitiza mafunzo kwa kuandaa wataalam;

(iii) Kupitia ujenzi wa miundombinu ya Kimkakati muhimu inayochochea uchumi, ambapo vijana wamepata nafasi ya kurithishwa ujuzi kutoka kwa wataalam wa nje kama vile katika Mradi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere na barabara za mwendokasi;

(iv) Kubuni na kutekeleza programu ya kukuza ujuzi ambayo inalenga kukuza ujuzi kwa nguvu kazi ili waweze kushindana katika soko la ajira, mfano mafunzo ya kuongeza ujuzi kwa wafanyakazi waliopo kazini na kwa wajasiriamali; na

(v) Kuweka msisitizo kwenye matumizi ya TEHAMA katika kuzalisha fursa nyingi za ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali itaendelea kusimamia na kuhakikisha vijana wanaandaliwa ili wapate ujuzi unaohitajika katika soko la ajira na hivyo kumudu ushindani wa ajira.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asya.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini nina swali moja la nyongeza. Ninataka kufahamu ni vijana wangapi ambao wamenufahika na ajira hizo na ni mikoa gani? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake lina maeneo mawili, moja ni vijana wangapi na pili ni Mikoa gani. Mheshimiwa Mbunge juu ya mikoa gani kama nitakuwa nimemsikia vizuri, sina takwimu halisi hapa za kuweza kumjibu Mbunge kwamba ni vijana katika mikoa gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya vijana mpaka sasa hivi ambao wamefanikiwa wanakaribia kufika 143,449. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu ya Serikali kwa swali la Mheshimiwa Mbunge. Tunaenda kwenye

Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mary Francis Masanja, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 160

**Kuanzisha Halmashauri Jiji la Mwanza**

**MHE. MARY F. MASANJA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuanzisha Halmashauri katika Jiji la Mwanza kwa kuwa linazidi kupanuka?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishaji wa maeneo ya utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura 287 na (Mamlaka za Miji), Sura 288 pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika mwaka 2022, Halmashauri ya Jiji la Mwanza ina jumla ya watu 594,834 na ina ukubwa wa eneo la kilomita za mraba 256, ambapo kilomita za mraba 184 ni ardhi kavu, na kilomita za mraba 71 zimefunikwa na maji ya Ziwa Victoria. Hivyo, Halmashauri ya Jiji la Mwanza kimsingi ina eneo dogo kijiografia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uhitaji wa kugawa baadhi ya maeneo mapya ya utawala, lakini kwa sasa Serikali imetoa kipaumbele katika kuboresha na kukamilisha miundombinu kwenye maeneo ya kiutawala yaliyopo ili yaweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na baadaye kuendelea na maeneo mengine kwa kufuata taratibu na vigezo vilivyoainishwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Francis Masanja.

**MHE. MARY F. MASANJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nianze kwa kuwapongeza Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa majibu mazuri ambayo wamenipatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza; kwa kuwa, Jiji la Mwanza sasa linakadiriwa kuwa na idadi ya watu 600,000 na Jiji hili lina tarafa moja tu mpaka sasa. Je, ni lini Serikali itaweza kuligawa Jiji hili ili kurahisisha maeneo ya kiutawala na kijamii na kurahisisha huduma za wananchi ili ziweze kuwafikia kwa urahisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Jiji la Mwanza na Manispaa ya Ilemela, wananchi wake wanapumulia katika Miji Midogo ya Kisesa na Usagara, Miji hii sasa imekuwa mikubwa. Je, Serikali haioni haja sasa ya kuanzisha halmashauri nyingine ili kuwarahisishia hawa wananchi ambao wanaenda kwenye Wilaya ya Magu na Misungwi kupata huduma za kijamii na kiutawala ili wawezeshe sasa kuanzishwa kwa Halmashauri mpya ili hawa wananchi waweze kuhudumiwa kikamilifu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge Mary Masanja, mara kwa mara amekuwa akifuatilia suala la ustawi wa wananchi wa Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwanza kumhakikishia Serikali inatambua kwamba idadi ya wananchi katika Jiji la Mwanza ni kubwa na ni kweli kwamba Jiji la Mwanza lina tarafa moja tu. Serikali tayari ilishapokea maombi kutoka Mkoa wa Mwanza kwa ajili ya kuanzisha tarafa nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imeshapokea maombi hayo na tutayafanyia kazi muda ukifika ili tuweze kupata tarafa nyingine kwa ajili ya kurahisisha huduma za wananchi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuhusiana na eneo la Kisesa na Usagara. Ni kweli wananchi wa Jiji la Mwanza na Ilemela wanapata huduma kwa wale walio jirani na maeneo hayo na wazo la Mheshimiwa Mbunge ni kuanzisha halmashauri nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba wakae pamoja na Mkuu wa Mkoa, Menejimenti nzima, halmashauri hizo na wananchi kwa pamoja, kwa kufuata sheria ya kuomba mamlaka mpya kwa maana ya halmashauri. Baada ya vikao hivi vya *DCC* na *RCC* wawasilishe Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ifanye tathmini na kuona uwezekano wa kuanzisha halmashauri nyingine pale itakapokuwa inawezekana. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhet Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Makao Makuu ya Mkoa wa Songwe yanahudumiwa na Mamlaka ya Mji wa Vwawa na Mlowo. Je, ni lini Serikali itaanzisha halmashauri ya mji au manispaa katika maeneo hayo kwa kuunganisha Mamlaka ya Mji wa Vwawa na Mamlaka ya Mji wa Mlowo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Makao Makuu ya Mkoa wa Songwe yapo katika eneo la Vwawa na eneo la Mlowo na tunatambua umuhimu wa kuwa na halmashauri ya mji au hata manispaa katika maeneo ambayo ni Makao Makuu ya Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge, kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Songwe wamekwishawasilisha hoja hiyo, Serikali inaendelea kuifanyia tathmini na kuona namna ya kwenda kwenye hatua hizo; kwa hiyo ni suala tu la muda. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeshalipokea. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jimbo la Bunda liko halmashauri moja na Jimbo la Mwibara, lakini halmashauri iko Mwibara. Kutoka Jimbo la Bunda kwenda Mwibara inabidi upite Halmashauri ya Bunda Mjini, ni kilometa 140 kwenda na kurudi. Je, ni lini sasa Serikali itawahurumia watu wa Jimbo la Bunda kwa kuwapa halmashauri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutumia nafasi hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kufanya vikao vya kisheria kwa mujibu wa taratibu pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Bunda pamoja na Mkoa mzima wa Mara ili kuleta ombi maalum kwa ajili ya kuanzisha mamlaka mpya. Serikali itafanya tathmini na kuona uwezekano wa kuanzisha mamlaka hiyo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa hapa kwamba ahadi za viongozi zinapewa kipaumbele na hazihojiwi. Sasa sisi tulivyokuwa tunafanya kampeni 2020, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano alitoa ahadi, kwamba kwa kuwa Halmashauri ya Moshi Vijijini ina majimbo mawili pamoja na manispaa, basi atatoa halmashauri kwa Jimbo la Vunjo ili kurahisisha shughuli za kiutawala. Tukaambiwa sasa kwamba tusubiri Serikali itakamilisha mchakato huo wa kumalizia miundombinu kwenye zile halmashauri ambazo zimeshaundwa, lakini mpaka leo hii, mnakaa hata miaka mitano, narudi jimboni naambiwa iko wapi ile halmashauri, nitajibu nini? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamhakikishia Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei kwamba ni kweli ahadi na maelekezo ya viongozi wa kitaifa hayahojiwi na yanatekelezwa. Ninamhakikishia tu kwamba ahadi hiyo ambayo ilitolewa, itatekelezwa. Jambo linalotokea, safari ni hatua, tumeona tuna mamlaka nyingi sana za halmashauri ambazo bado hazina miundombinu muhimu. Waheshimiwa Wabunge wote ni mashahidi kwamba tuna wilaya ambazo zilikuwa hazina Ofisi za Wakuu wa Wilaya na tuna wilaya zilikuwa hazina Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Serikali iliona ni vema ikaweka kipaumbele kuanza kukamilisha majengo ya halmashauri, Ofisi za Wakuu wa Wilaya, Ofisi za Wakurugenzi na baadaye tutakwenda kwenye mamlaka hizo mpya. Kwa hiyo ninamhakikishia Mheshimiwa Kimei kwamba, ahadi hiyo bado ni *valid* na itaendelea kufanyiwa kazi na baadaye tutaitekeleza kwa kadri ya ahadi ya Viongozi wa Kitaifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 161

**Kukamilisha Ujenzi Kituo cha Afya Magubike – Kilosa**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Kituo cha Afya Magubike – Kilosa utakamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022 hadi 2024/2025, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ilipokea shilingi bilioni 2.07 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya sita

kikiwemo Kituo cha Afya cha Magubike. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 866 ni fedha za mapato ya ndani. Vituo vya afya vitano kati ya sita vimeanza kutoa huduma, kikiwemo Kituo cha Afya cha Magubike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kituo cha Afya Magubike kilipokea shilingi milioni 309 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wazazi, jengo la upasuaji na maabara. Majengo haya yamekamilika na yanatoa huduma zikiwemo huduma za dharura za upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu iliyosalia likiwemo jengo la huduma za wagonjwa wa nje, jengo la mionzi, jengo la kufulia, jengo la kliniki ya mama na mtoto, jengo la kulaza wagonjwa na jengo la utawala katika Kituo cha Afya cha Magubike. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti. Ahsante sana. Ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri na ninaipongeza kwa kuendeleza ujenzi wa vituo vya afya hasa kwa kutenga fedha kwa Kituo cha Afya cha Magubike kwa sababu walikuwa wana tabu sana hasa kwenye wodi ya kuwalaza wagonjwa hasa wanaume. Swali langu la kwanza; je, ni lini uzio wa Kituo cha Afya Kidodi utajengwa kwa sababu kituo hiki kimepakana sana na wananchi na kiko kwenye Halmashauri ya Kilosa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Kituo cha Afya Mafisa kwenye Manispaa ya Morogoro kimepewa vifaa vyote vya upasuaji, lakini hakuna chumba wala jengo la upasuaji. Je, ni lini jengo hili litajengwa ili kuwanusuru wagonjwa hasa akinamama ambao wanashindwa kujifungua kwa njia salama waweze kupata huduma hii ya upasuaji? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, kwanza namhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ilishapeleka fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivi vya afya, lakini tunafahamu kwamba pamoja na uhitaji wa majengo ya vituo vya afya bado kuna uhitaji wa uzio kwa ajili ya usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga ni kuchagua, tuliona ni vema tukaanza kwanza na majengo ya huduma, yakamilike na baadaye tuje hatua ya kuweka uzio. Kwa hiyo naomba kutumia nafasi hii, kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, katika Kituo cha Afya cha Kidodi, waone uwezekano wa kuanza kutenga fedha za mapato ya ndani kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa *fence* wakati Serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya kituo hicho ambayo imesalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusiana na Kituo cha Afya cha Mafisa kilichopo hapo Manispaa ya Morogoro, ninaomba kutumia nafasi hii kumhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, vituo vyote vya afya ambavyo vina miundombinu pungufu, hususan majengo ya upasuaji na wodi za wanawake wajawazito, tayari zimeingizwa kwenye mpango wa Benki ya Dunia kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wodi hizo zinajengwa na huduma za upasuaji zinaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inaendelea kulifanyia kazi hilo na tutakwenda kujenga jengo la upasuaji katika kituo hicho cha afya. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Je, ni lini Kituo cha Afya cha Ndalambo kitaongezewa uwezo wake ikiwa ni pamoja na kujenga mochwari na majengo mengineyo ili kiwe na hadhi ya kuhudumia kata tano kazi ambayo kinafanya kwa sasa; Kata ya Nzoka, Kata ya Myunga, Kata ya Ikana, Ndalambo yenyewe pamoja na Nkangamo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Kituo cha Afya cha Ndalambo katika Jimbo la Momba kinahudumia kata zaidi ya tano na kina idadi kubwa ya wananchi. Namhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge, kwamba tumeshakiweka kwenye vituo vya mpango mkakati vya kipaumbele kwa ajili ya kujenga majengo yaliyopungua likiwemo jengo la mochwari na majengo mengine. Kwa hiyo namhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Momba kwamba Serikali imeshapokea ombi hilo na hoja hiyo na tunaendelea kuifanyia kazi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mathayo David Manyinyi.

**MHE. MATHAYO D. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika lile Jimbo langu la Musoma Mjini, licha ya vituo vya afya kuwa vichache katika kata mbalimbali, Kituo cha Afya cha Bweri kimechakaa na nimeendelea kukiombea fedha kwa zaidi ya miaka minne sasa na kila leo Mheshimiwa Waziri amekuwa akiahidi. Je, ni lini sasa tutapata fedha kwa ajili ya kukarabati kile kituo angalau kifanane na kituo cha afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Kituo cha Afya cha Bweri katika Jimbo la Musoma Mjini ni kikongwe na ni chakavu na ni kweli kwamba Mheshimiwa Mbunge mara kwa mara ameleta hoja hiyo Serikalini. Sisi tulimhakikishia tu kwamba tuko na awamu ya kwanza ya ukarabati wa hospitali za halmashauri kongwe na chakavu 91 na tayari hospitali 48 zimeshakarabatiwa. Tunakwenda awamu ya mwisho ya hospitali zilizobaki na baada ya hapo, tutakwenda kwenye ngazi ya vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba ahadi ya Serikali bado iko palepale, na tutahakikisha tunatoa kipaumbele kwa ajili ya ukarabati wa Kituo cha Afya cha Bweri. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tarafa ya Nampungu katika Kata ya Nampungu ilipokea shilingi 250,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa awali wa kituo cha afya. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka shilingi 250,000,000 ili kuweza kukamilisha kituo cha afya kile?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vyote vya afya kikiwemo Kituo cha Afya cha Nampungu ambacho kiko katika Wilaya ya Tunduru ni vituo ambavyo vimeingizwa kwenye bajeti ya Mwaka huu wa Fedha 2024/2025 kwa ajili ya ukamilishaji. Vile vituo vyote ambavyo vilipokea shilingi 250,000,000, vimetengewa tena fedha kwa ajili ya ukamilishaji. Kwa hiyo naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika mwaka huu wa fedha kwenye bajeti yetu tumeweka fedha kwa ajili ya ukarabati na ukamilishaji wa kituo hicho cha afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil David Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais mwaka jana, alipofika Jimbo la Ndanda tulisimama kwenye Kata ya Nanganga ambapo wananchi wa Nanganga walitoa hoja yao na Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba watahakikisha hivi karibuni wanajenga pale kituo cha afya na baadaye Katibu Mkuu wa Chama Mheshimiwa Dkt. Nchimbi naye alipita hapo na kutoa ahadi kama hiyo. Ninataka kufahamu, ahadi hizi za viongozi wakubwa zitatekelezwa lini? Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi za viongozi wa kitaifa ni kipaumbele nambari moja. Ninamhakikishia tu ahadi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kujenga kituo cha afya katika Kata ya Nanganga imeanza kufanyiwa kazi. Ni suala tu la muda Mheshimiwa Mbunge tutapata fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha afya. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Mayenga, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Songwa Wilayani Kishapu kinakabiliwa na tatizo kubwa sana la *walk way;* wagonjwa kutoka *theater* kwenda kwenye wodi wanapita katika mazingira magumu sana. Je, ni lini Serikali italifanyia kazi suala hili ambalo linawapa shida sana madaktari, wauguzi na manesi katika kituo hicho? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Songwa katika Wilaya ya Kishapu kina upungufu wa miundombinu katika kituo hicho na hususan *walk way*. Mheshimiwa Mbunge amefuatilia mara kadhaa na nilimwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri kwamba watenge fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kujenga *walk ways* hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba nitafuatilia baada ya kipindi hiki kuona utekelezaji ukoje, kwa sababu tulikubaliana ifikapo Disemba 30, wawe wamekamilisha ujenzi wa *walk way* katika kituo hicho cha afya kupitia mapato ya ndani.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali linalofuata, Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

**10 FEBRUARI, 2025**

Na. 162

**Ujenzi wa Makaravati na Madaraja Barabara ya Itimbo Kitelewasi**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, lini makaravati na madaraja madogo yatajengwa katika Barabara ya Itimbo – Kitelewasi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikijenga madaraja pamoja na makalvati katika Barabara ya Itimbo – Kitelewasi kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 hadi mwaka 2023/2024; ambapo katika mwaka wa fedha 2020/2021, ilijenga madaraja mawili na makalvati mawili kwa thamani ya shilingi 94,000,000. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilitumia shilingi milioni 469.9 kujenga makalvati 10, daraja moja, mitaro ya mawe mita 200, kuchonga barabara kilometa 21.5 na kuweka changarawe kilometa 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali ilitumia shilingi 15,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa makalvati manne. Serikali itaendelea kuihudumia barabara ya Itimbo – Kitelewasi kwa kujenga ma-*culvert* na madaraja madogo katika bajeti zijazo kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali kuna Barabara hii ya Boma la Ng'ombe inayopita Nyingula inakwenda Masisiwe, Idegenda mpaka Isanga, ni barabara ya kiuchumi, lakini wakati wa mvua haipitiki kabisa. Kuna maeneo tu korofi ambayo kama Serikali ingesaidia ikajenga yale maeneo korofi, basi hii barabara ingeweza kusaidia

kwa sababu kuna wagonjwa, wajawazito wanashindwa kwenda kwenye vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kuna hii barabara inatoka Kihesa Mgagao – Mwatasi – Masisiwe, hii barabara pia ina maeneo korofi, sasa hivi mabasi hayapiti. Sasa naomba Serikali iangalie kwa sababu uchumi umesimama kabisa ili iweze kupitika muda wote wa mwaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba barabara zetu na hususan barabara zote muhimu zinapitika wakati Serikali ikiendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge; kwanza kuhusiana na Barabara ya Boma la Ng'ombe, Masisiwe na Idegenda, eneo korofi la Masisiwe – Idegenda, natumia nafasi hii kumwelekeza Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Kilolo pamoja na Meneja wa *TARURA,* Mkoa wa Iringa, wapitie barabara hizi za Boma la N'gombe, Masisiwe, Idegenda pamoja na Kihesa, Mgagao, Mwatasi na Masisiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maeneo korofi ambayo yanasababisha barabara zisipitike kabisa, walete maombi ya dharura Serikalini ili Serikali iweze kupeleka fedha kwa ajili ya kuzikarabati barabara hizo ziweze kupitika vizuri. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selemani Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imefungua barabara nyingi kwenye maeneo ya Wilaya ya Tanganyika, ikiwemo Barabara ya kutoka Ikola kwenda Kata ya Isengule hadi Kasangatongwe. Je, ni lini Serikali itaenda kujenga madaraja ili njia hiyo iweze kukamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara unazingatia miundombinu yote muhimu ambayo itawezesha barabara kupitika. Kwa hiyo hatua ya kwanza ambayo Serikali imeifanya ni kujenga barabara hiyo na hatua ya pili inayofuata ni kujenga madaraja na ma-*culvert* katika maeneo hayo ili barabara iweze kupitika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mpango wa ujenzi wa barabara hiyo, makalvati na madaraja katika maeneo hayo korofi yamewekwa. Tutakwenda kuyajenga mapema iwezekanavyo ili barabara iweze kupitika vizuri. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa barabara zetu nyingi zinaharibika kwa kukosa mitaro na madaraja ya uhakika na tumesubiri fedha kwa muda mrefu sasa. Je, ni lini Serikali iko tayari kutupa fedha kwa haraka katika kipindi hiki ili mikataba ya wakandarasi inayoendelea iweze kufanya kazi na kuondoa changamoto hii tuliyonayo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekwishaweka mpango na utaratibu wa ujenzi wa barabara. Moja ya maelekezo ya Serikali ni kwamba kila barabara inayojengwa lazima iwe na mifereji au mitaro kwa ajili ya kutoa maji barabarani na kuwezesha barabara hizo kudumu kwa muda mrefu zaidi. Maeneo ambayo yanahitaji makalvati na madaraja, ni lazima makalvati hayo yajengwe ili kuwezesha barabara kupitika, lakini pia kudumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba kutumia nafasi hii, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kuwaelekeza mameneja wa *TARURA* wa mikoa na wilaya zote kote nchini, kuhakikisha kila kandarasi inayotolewa wanazingatia vigezo hivyo muhimu vya kujenga madaraja,

makalvati maeneo yanayohitajika, lakini na mifereji ili barabara zetu ziweze kudumu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mabula kwamba hiyo barabara ambayo ameitaja na yenyewe tutaipa kipaumbele katika utekelezaji wake. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pia napenda kuishukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa zilizofanyika katika miundombinu Jimbo la Kalenga. Swali, tunalo daraja ambalo linaunganisha Kata ya Nzihi na Kata ya Kiwele linaitwa Kigala, tulishaomba hapa tupewe fedha. Je, ni lini sasa Serikali itatuletea fedha ili tutengeneze hilo daraja na tuunganishe hizi kata mbili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya kazi kubwa sana kwenye sekta zote ikiwemo sekta ya barabara vijijini na mijini kupitia *TARURA,* ambapo bajeti ya Serikali imeongezeka kutoka shilingi 275,000,000,000 mpaka shilingi 710,000,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sote tuna kila sababu ya kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia tu Mheshimiwa Kiswaga kwamba Serikali itakwenda kuifanyia kazi barabara hiyo ya Nzihi ili iweze kupitika na daraja hilo litajengwa ili barabara iweze kupitika vizuri kama ilivyokuwa *designed* kwenye michoro yetu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Felister Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Ni lini Barabara inayotokea Mweka kupita *Kibosho Girls* mpaka *Kibosho Hospital* itajengwa kwa sababu barabara hii mvua ikinyesha haipitiki na hivyo kuhatarisha maisha ya wananchi wanaotoka *Kibosho Hospital* kuelekea *KCMC* Jimbo la Moshi Vijijini? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge ya Mweka, Kibosho *Girls* kwenda Kibosho *Hospital* ni barabara muhimu sana katika Jimbo hilo na Wilaya hiyo. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, Serikali sikivu ya Awamu ya Sita itakwenda kuiweka kwenye mpango na kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba barabara inatengenezwa na inapitika vizuri. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu, sasa aulize swali lake.

Na. 163

### Matengenezo ya Barabara zilizoharibiwa na Mvua ya *El-Nino* Kishapu

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za dharura Wilayani Kishapu ili kufanya matengenezo ya Barabara zilizoharibiwa na mvua za *El Nino* Mwaka 2023/2024?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania Wilaya ya Kishapu inao mtandao wa barabara wenye urefu wa kilometa 1,024.66 ambapo kilometa mbili ni barabara za lami, kilometa 405.64 ni barabara za changarawe na kilometa 617.02 ni barabara za udongo. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali ilifanya tathmini ya mtandao mzima wa barabara katika Wilaya ya Kishapu na kubaini ukubwa wa uharibifu ambapo jumla ya shilingi bilioni 2.55 zinahitajika ili kuzifanyia matengenezo barabara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali ilipeleka shilingi milioni 190 katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya dharura kwa baadhi ya maeneo na tayari yamefanyiwa kazi ikiwemo Barabara ya Mwamakanga hadi Mwanghiri kilometa 4.5 na makalavati saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inaendelea na usanifu wa ujenzi wa daraja katika Barabara ya Mwamala A kwenda Mwamala B ambalo awali liliathiriwa na mvua za *El Nino*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuzifanyia matengenezo barabara zilizoathiriwa na mvua kulingana na hali ya barabara hizo na itaendelea kufanya hivyo kwa awamu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusiana na tatizo kubwa la barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; Serikali imefanya tathmini na kuona kwamba kunahitajika zaidi ya shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya kurudishia hali ya miundombinu ya barabara katika Wilaya ya Kishapu, lakini hadi sasa imetoa shilingi milioni 200 tu. Kata ya Itilima pamoja na Kata ya Mwasubi ni kata ambazo sasa hazipitiki kabisa. Je, Serikali haioni haja ya kuhakikisha inaleta fedha za kutosha ili Kata ya Itilima na Mwasubi zianze kupitika

haraka kwa sababu huduma za msingi zimesimama kabisa katika kata hizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; tumekuwa tukipokea fedha za Mfuko wa Jimbo katika upande wa Barabara, lakini kimsingi fedha hizi zimekuwa zikija kwa kusuasua. Bado kuna changamoto kubwa ambayo imekuwepo hasa katika eneo la namna ya ugawaji wa fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila wilaya ina mtandao tofauti wa kilometa katika eneo la wilaya yake, lakini fedha hizi zimekuwa zikitolewa *equally* kwa maana ya kwamba kila jimbo, lakini ukweli kuna majimbo ambayo yana zaidi ya kilometa 1,000 na majimbo mengine yana kilomita chini ya 1,000. Sasa kwa nini Serikali isifike mahali ikaweka utaratibu wa kugawanya fedha hizi kulingana na ukubwa wa kilometa zilizopo katika kila jimbo au kila wilaya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunafahamu ili matengenezo ya barabara hizi alizoziainisha yaweze kukaa sawa, tunahitaji takriban shilingi bilioni 2.55 na Serikali imeshaanza kupeleka fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati njema siku chache zilizopita Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Waziri na Waziri wa Fedha walifanya kikao cha pamoja ambapo Wizara ya Fedha wamekubali kuanza kutoa fedha hizo kupeleka kwenye barabara hizo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali ilikuwa inaendelea na utaratibu wa ku-*mobilize* fedha na sasa tutaendelea kupeleka fedha hizo katika maeneo yenye barabara ambazo hazipitiki zikiwemo barabara ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusiana na mgao wa fedha za barabara kwa kila jimbo kuwa sawa. Katika vigezo vya fedha za bajeti za kila mwaka kwa kila halmashauri

kunatofautiana halmashauri moja kwenda halmashauri nyingine kwa vigezo vya hali ya hewa kwa maana ya mvua nyingi, milima, urefu wa mtandao wa barabara na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kigezo hicho kinatumika na tutaendelea kukitumia kuhakikisha kwamba tunapata fedha kulingana na ukubwa na maeneo ya kijiografia. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Tarime ni miongoni mwa wilaya ambazo zinapata mvua za mara kwa mara zinazopelekea uharibifu wa barabara kutokana na utengenezaji na uimara hafifu wa barabara hizi kulingana na mazingira halisia ya maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kutengeneza barabara hizi kwa uimara kulingana na mazingira ya maeneo husika yanayopata mvua za mara kwa mara ili kuweza kurahisisha usafiri wa usafirishaji kwa wananchi hawa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba hali za jiografia zinatofautiana kutoka sehemu moja na nyingine. Kuna maeneo yenye milima na miteremko mikali, kuna maeneo yenye mvua nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilishaweka utaratibu wa ujenzi wa barabara kulingana na hali za kijiografia. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge tunaendelea kufanya majaribio ya *design* ya barabara ambazo zitadumu kwa muda mrefu zaidi kwenye maeneo ya mvua nyingi na maeneo ya milima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kujenga barabara mara nyingine za mawe na tunaendelea kuboresha, hivyo kuhakikisha kwamba barabara hizo zinapitika vizuri. Kwa hiyo,

nimhakikishie Mheshimiwa Matiko kwamba, Serikali tunalifanyia kazi hilo na tayari tumeshaanza kulitekeleza kwa utaratibu huo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omari Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kilindi ni miongoni mwa maeneo machache sana ambayo yanaathirika na mvua za *El-Nino*. Miongoni mwa maeneo ambayo yamepata uharibifu mkubwa ni Kijiji cha Tamota, kwenye Kata ya Kilwa hali kadhalika kwenye Kata ya Pagwi na vijiji vyake vyote. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kutuletea fedha kama alivyoahidi mbele ya Bunge? Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii imeshafanya tathmini ya maeneo yote ya barabara zilizokatika kabisa na kuwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Kigua, Mbunge wa Jimbo la Kilindi kwamba, eneo hilo la barabara alilolitaja tayari kupitia *TARURA* Wilaya na Mkoa wa Tanga imewasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI na kama nilivyosema tuko kwenye utaratibu wa kupeleka fedha kwa ajili ya kufanya matengenezo katika maeneo hayo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Sonu kwenda Sawe imeharibiwa sana na mvua kiasi kwamba barabara ile haipitiki kabisa na kwa kweli imekuwa usumbufu mkubwa mno. Kwenye *groups* za *WhatsApp* huko sipumui kwa sababu ya hii barabara. Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa hii barabara iweze kupitika kipindi chote? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara hiyo ya Sonu - Sawe katika Jimbo la Hai, naomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumwelekeza Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Kilimanjaro na Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Hai kama hawajawasilisha maombi maalum na tathmini ya mahitaji ya fedha wafanye hivyo mara moja ili Serikali ipeleke fedha kwa ajili ya kurekebisha barabara hiyo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaelekea swali linalofuata, swali la Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Mbagala, litaulizwa na Mheshimiwa Festo Sanga.

Na. 164

**Ujenzi wa Barabara za Kata ya Kilungule**

**MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itazijenga Barabara za Chasimba, Cheketu, Kisiwani, Alfurkan, Kwa Kisauti, Maduka Manane, Kwa Mnyani, Fella Zahanati na Ofisi ya Mtaa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza ujenzi kwenye barabara za Kata ya Kilungule ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Barabara ya Chasimba yenye urefu wa kilometa 1.67 ilijengwa kwa zege urefu wa mita 160 kwa gharama ya shilingi milioni 75.98 na Mwaka wa Fedha 2024/2025 itajengwa kwa kiwango cha zege mita 180 kwa gharama ya shilingi milioni 100. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Barabara ya Kisiwani imepangwa kuchongwa urefu wa kilometa 0.9 na kujengwa kwa kiwango cha changarawe kwenye sehemu korofi kwa gharama ya shilingi milioni 30.38.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara za Cheketu, Alfurkani, Kwa Kisauti, Maduka Manane, Kwa Mnyani, Fella Zahanati na Ofisi ya Mtaa zimewekwa katika mpango wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi kwa kuchongwa na kuwekewa changarawe. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nitauliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Jimbo la Mbagala limekuwa na changamoto ya barabara nyingi ambazo ni mbovu ikiwemo Barabara ya Kipugani Mtaa wa Mbagala Kuu. Upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha inatenga fedha za kutosha za dharura kwa ajili ya kufanya marekebisho ya barabara hizi, ikitambulika kwamba Mbagala ni moja kati ya Jimbo ambalo lina watu wengi, lakini lina barabara nyingi ambazo ni mbovu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; wananchi wa Makete wanaulizia kuhusu wakandarasi wa Barabara ya Mang'oto - Ibaga, Luvulunge – Isapulano na Kinyika - Kikondo ambao wamesaini mikataba kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizi, lakini hawajafika *site*. Ni ipi kauli ya Serikali ili wananchi wa Makete tuondokane na adha ya barabara hizi, ikikumbukwa kwamba Makete ni wilaya ya kazi inayoongoza kwa uzalishaji wa mazao ambao nyie mnatumia huku mjini? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbagala ni kweli ni Jimbo lenye wananchi wengi na Serikali imeendelea kujenga barabara za mitaa katika Jimbo la Mbagala. Moja ya barabara ambayo imejengwa katika Jimbo la Mbagala ni pamoja na barabara ya mwendokasi pia kuna barabara kupitia Mradi wa *DMDP*. Pia, kuna barabara kupitia bajeti za kawaida za mapato ya ndani na kuna barabara ambazo zinajengwa kupitia *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kupeleka fedha kwa ajili ya kujenga barabara hizo na hususan barabara ambayo umeitaja ili wananchi wa Mbagala waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi mkubwa zaidi kwa kupita kwenye barabara ambazo ziko bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuhusiana na Jimbo la Makete. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwanza Serikali ikitoa zabuni ni wajibu wa mkandarasi kuanza kazi mapema iwezekanavyo. Kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI tulishatoa maelekezo kwamba hatuko tayari kuwavumilia wakandarasi waliopata zabuni lakini hawajaanza kazi mpaka sasa. Tutaendelea kuchukua hatua ikiwemo hatua ya kuwa-*black list* wakandarasi ambao wanatuangusha kwenye ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumwelekeza Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Njombe na wa Wilaya ya Makete wahakikishe wanakaa mara moja na wakandarasi hao na wawaelekeze kuanza kazi za ujenzi wa barabara kwa kadri ya mkataba na sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutafuatilia kwa karibu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel, aulize swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Jimbo la Arumeru Magharibi mazingira yake ni magumu sana kutokana na maporomoko makubwa ya milima na mabonde. Barabara za Malalua - Nduruma – Bwawani, Barabara ya Sanawari - Oldonyosambu, Barabara ya Ngulelo - Sokoni II na *Gomba Eastern* na TPRI - Likamba ni muda mrefu sasa haijapata matengenezo maalum. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa sababu hali ni mbaya na wananchi wanalalamika kweli kweli katika barabara hizo ambazo hazitengenezwi kwa muda mrefu mwaka mmoja na nusu sasa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara zote ambazo ni kipaumbele katika Jimbo la Arumeru Magharibi, Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi zikiwemo barabara ambazo amezitaja. Ni muhimu sana Meneja wa Wilaya ya Arumeru na Meneja wa *TARURA* waainishe na kuweka vipaumbele kwenye barabara ambazo ni chakavu zaidi, ni muhimu zaidi na ambazo hazijatengenezwa ili Serikali iweze kupeleka fedha kwa ajili ya matengenezo hayo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya *Breweries* - Ilemela – Mahakamani – Buzuruga - Miti Mirefu – Igogwe – Isanzu – Sangabuye, Mkandarasi alikabidhiwa *site* toka Septemba, 2024 na anatakiwa kukabidhi kazi Februari 2025, lakini mpaka leo hajaingia *site*. Ninataka kujua, ni lini mkandarasi ataanza kujenga barabara hizo kilometa mbili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kusisitiza utaratibu wa wakandarasi wa barabara hizi za *TARURA* kwamba, mara wakandarasi wanapokabidhiwa mkataba wa ujenzi wa barabara hizo ni wajibu wake kuanza ujenzi wa barabara hizo kwa wakati, wakati akiendelea ku-*raise certificate* kwa ajili ya malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwelekeza na kumsisitiza Meneja wa *TARURA,* Mkoa wa Mwanza na wa Wilaya ya Ilemela wahakikishe wanapitia mkataba huo, wakae na mkandarasi huyo na kumwelekeza

aanze kazi hiyo mapema iwezekanavyo ili barabara ijengwe kwa mujibu wa mkataba. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Hospitali yetu ya Wilaya ya Karatu imejengwa nje ya mji na barabara inayoelekea huko ni ya vumbi na kipindi cha mvua kunakuwa na tope jingi kiasi kwamba wagonjwa wanapata changamoto kubwa kufika hospitalini. Je, Serikali haioni umuhimu huo kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilishaelekeza maeneo yote ya huduma muhimu za kijamii lazima yapewe kipaumbele ya kuboresha miundombinu ya barabara. Naomba nitumie nafasi hii kuwasisitiza Mameneja wa *TARURA* kote nchini kuhakikisha kwamba maeneo ya hospitali ambako mara nyingine kuna magari ya wagonjwa na wagonjwa mahututi wanatakiwa kupelekwa kwenye hospitali nyingine za rufaa lazima yapitike na yawekewe kipaumbele kwenye ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Paresso kwamba barabara hiyo katika Hospitali ya Wilaya ya Karatu na maeneo mengine kote nchini, tutahakikisha tunaweka kipaumbele ili wananchi wasafiri vizuri na hususan wakati wa dharura za matibabu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutoa majibu kwa niaba ya Serikali.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, sasa aulize swali lake.

**10 FEBRUARI, 2025**

Na. 165

**Kiwanda na Mashamba ya *Tanganyika Packers* Mbalizi**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa matumizi endelevu ya kiwanda na mashamba ya iliyokuwa *Tanganyika Packers Limited* katika Mji wa Mbalizi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Naibu Waziri, Wizara ya Mipango na Uwekezaji.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha *Tanganyika Packers Ltd (TPL) - Mbeya Plant* kilikabidhiwa kwa *Export Processing Zone Authority*. Hata hivyo, mitambo ya kiwanda hiki licha ya kwamba haijawahi kutumika toka mwaka 1978 tayari imekwishapitwa na wakati *(Obsolete technology)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za mamlaka kupata mwekezaji katika awamu ya kwanza kiwanda hiki kilikuwa ni miongoni mwa viwanda vilivyotangazwa mwaka 2023 ili kupata wawekezaji. Hata hivyo hakuna mwekezaji aliyejitokeza na mpango uliopo kwa sasa ni kuwapa wawekezaji mbadala kwa njia ya kuwabaini bila ya kutangaza *(Investor Targeting)* na kufanya mazungumzo yenye lengo la kuvutia uwekezaji katika sekta hiyo ya uzalishaji wa nyama au sekta nyingine itakayovutia wawekezaji katika eneo kilipo kiwanda hicho kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa upande wa Shamba la *TPL-Nsalala*, Ofisi ya Msajili wa Hazina imekamilisha kuandaa Mpango Kabambe *(Master Plan)* kwa eneo hilo, ili kuongeza au kuwapa nafasi wawekezaji wengi. Kazi hiyo imefanywa na Chuo

cha Ardhi Morogoro na sasa Mpango huo upo kwenye hatua ya kusajiliwa na Mpimaji Mkuu wa Serikali (Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi). Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninashukuru kwa majibu ya Serikali. Kutokana na uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo pamoja na madini, kuna mahitaji makubwa ya kuongeza thamani ya hayo mazao ya kilimo pamoja na madini. Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kuwa eneo hili linakuwa mahususi na Sekta Binafsi inapewa nafasi ya kuwekeza kwenye viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo yakiwemo vilevile na madini ambayo kuna madini maalum sasa hivi ambayo yanazalishwa katika eneo hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa sababu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kiliomba eneo kwa ajili ya kujenga Ndaki ya Afya. Je, ni lini ujenzi wa Ndaki ya Afya utaanza katika eneo hilo la *Tanganyika Packers* - Msalala Mbalizi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Oran Njeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika swali la msingi kwamba, tayari sasa eneo hili limechukuliwa na *EPZA* kwa maana ya kuliendeleza hili eneo. Sasa hivi kuna mkakati kabambe ambao tumeshaandaa *master plan* ya kukaribisha wawekezaji mbalimbali ambao watakuja kuwekeza katika maeneo hayo anayoyazungumza Mheshimiwa Mbunge (maeneo ya mazao pamoja na *value addition)* kwenye madini yanayozalishwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, suala la Chuo Kikuu kuomba eneo hili, nadhani na lenyewe liko katika utaratibu ule ule

ambao nimeuzungumza awali na mkakati utakapokamilika, basi ujenzi huu utaendelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mkakati gani wa kutafuta wawekezaji mahiri na wenye tija wa kuendeleza mashamba ya maua na mbogamboga katika Mkoa wa Arusha ambayo inabeba ajira nyingi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Zaytun Swai, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Arusha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuna mikakati mingi ya kuhakikisha kwamba maeneo yote yenye uzalishaji wenye tija kwa kuzingatia kila mkoa una mazao ya kibiashara, tunaweka mkakati maalum wa kuhakikisha kwamba tunaongeza thamani kwenye mazao hayo, lakini vilevile tunaongeza tija katika masuala yote ya uzalishaji ili kuongeza nafasi za ajira, watu waweze kujishirikisha katika shughuli za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uzalishaji, basi kwenye upande wa *value addition* na penyewe tufungue wigo mkubwa ili tuweze kutengeneza ajira, lakini vilevile tuweze kuongeza thamani ya mazao yetu na tuweze kuuza ndani na nje ya nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kata ya Nkwenda ina eneo ambalo ni maarufu kama Nyaruziba ambalo kwa miaka mingi lilikuwa limetengwa kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo. Hilo eneo limeachwa kwa muda mrefu na halifanyi kazi, wakati Mji wenyewe umekuwa na hilo eneo limebaki katikati likiwa limezungukwa na makazi ya watu. Nini kauli ya Serikali kulitoa hilo eneo likatumika kwa kazi mbadala

au makazi ya watu kwa kuwa lilitelekezwa muda mrefu na sasa Mji umekuwa unahitaji maeneo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Anatropia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuna maeneo mengi sana ya mashamba ya wawekezaji ambayo yalikuwa yanatumika zamani. Maeneo ambayo mengi yako chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina, maeneo haya tunayaandalia mkakati, mengine yalikwishatangazwa kuuzwa yakakosa wawekezaji au yakakosa wanunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaandaa mkakati kabambe kwa kushirikiana na Serikali za Mikoa kutafuta wawekezaji wa ndani na nje tupunguze masharti, tuwape waweze kuwekeza kwenye maeneo haya, ili mashamba haya yawe na tija na siyo katika Mkoa wa Kagera peke yake, ni mikoa yote Tanzania mkakati huo tunao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa. Kata ya Mabogini ni eneo maarufu sana kwa kulima mpunga hapa nchini. Wakulima wa eneo hili walikuwa wana Kiwanda cha Kukoboa Mpunga na sasa hivi hakifanyi kazi kipo chini ya Msajili wa Hazina. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima hawa kufufua kiwanda hiki? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Profesa Ndakidemi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Shamba la Mabogini ambalo liko katika Kata ya Mabogini lilikuwa ni shamba ambalo liko chini ya Kampuni ya *Kilimanjaro Paddy Hulling Company Limited* na shamba hili Msajili wa Hazina mwaka 2022 alilitangaza kuliuza kwa *tender* ya wazi kabisa, lakini bahati mbaya hakupatikana mnunuzi au mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia mkakati ule ule kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa tumeshirikiana na Serikali ya Mkoa wa Kilimanjaro mwaka 2024 mwezi Februari tulipata mwekezaji mwingine ambaye anataka kuwekeza katika kiwanda hicho na tumekwishamkaribisha sasa hivi tuko kwenye majadiliano, anatoa *offer* kiasi gani na masharti yakoje? *Business plan* yake ikoje? Tukisharidhika tutampa kiwanda hiki aweze kuendeleza na wananchi wa maeneo hayo waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge amekuwa anafuatilia suala hili na kwa kweli namshukuru, na kumpongeza, wananchi wa eneo hilo wataendelea kupata tija kutokana na kiwanda hicho pale tunapokuwa tumemaliza maandalizi na mwekezaji huyu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati, swali la Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum, litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Husna Sekiboko.

Na. 166

**Kufikisha Umeme wa *REA* Mashuleni**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO K.n.y. MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja kupitia upya Mkataba wa *REA* kuhakikisha umeme unafikishwa mashuleni ili shule ziunganishwe na huduma za TEHAMA?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* inatoa kipaumbele katika kufikisha umeme kwenye taasisi zinazotoa huduma kwa jamii zikiwemo Taasisi za Elimu. Lengo kuu ni kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma ya umeme wa uhakika katika maeneo hayo. Hadi kufikia mwezi Januari, 2025 taasisi za elimu zilizopatiwa umeme kupitia *REA* ni 18,597. Aidha, Serikali kupitia *REA* itaendelea kupeleka umeme kwenye vituo vya huduma nchini kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Husna Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelekezo na taratibu hizo za Serikali bado taasisi nyingi za kutolea huduma hazijapelekewa umeme. Swali la kwanza; je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba taasisi zote za Serikali za kutolea huduma zinaunganishwa umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ni lini Serikali itapeleka umeme katika Shule ya Sekondari Makose katika Jimbo la Mlalo. Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge. Kuhusiana na mkakati wa Serikali wa kupeleka umeme kwenye taasisi zinazotoa huduma Serikali tunayo miradi mbalimbali, hivi karibuni kupitia Mradi wa *COVID* tumepeleka umeme kwenye vituo vya afya takribani 111, lakini hivi tunavyoongea tunao mradi mwingine ambao unapeleka umeme kwenye pampu za maji na tayari tumeshapeleka umeme kwenye pampu za maji takribani 411.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna mradi ambao unapeleka umeme kwenye maeneo ya kilimo pamoja na maeneo ya migodi na mpaka sasa hivi tumeshafikia maeneo 605 na miradi hii inaendelea. Katika taasisi za elimu kupitia miradi yetu ya vitongoji, vipaumbele vimebaki pale pale kuanza na taasisi hususan taasisi hizi za elimu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika Miradi ya Vitongoji na miradi mingine ambayo tunaendelea nayo tutaweka kipaumbele kwenye kufikisha huduma ya umeme kwenye taasisi za elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na shule hii ya Makose ambayo haina umeme. Shule hii ipo katika Kitongoji ambacho bado hakijafikishiwa umeme, lakini katika huu Mradi wa Vitongoji kwa mwaka huu wa fedha tutaenda kupeleka umeme kwenye Kitongoji cha Mgwashi ambapo shule hii ilipo tutajenga *line* ya *HT* umbali wa kilomita mbili pamoja na kuweka transfoma na hivyo kusababisha hii Shule ya Makose kupata umeme.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa maombi au mahitaji ya wananchi ni makubwa sana kwa ajili ya kupata umeme, je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza idadi ya vitongoji vya kupelekea umeme kwa mwaka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaona umuhimu wa jambo hilo na ndiyo maana tunaanza mradi mwingine wa kupeleka umeme kwenye vitongoji 8,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa mwaka huu pia tutaongeza idadi ya vitongoji ambavyo tutavipelekea umeme. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Kamonga, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Kapinga kwa kufanya ziara Ludewa na kutatua changamoto ya umeme Madope na Juhuma. Pamoja na pongezi hizo, ninaomba kufahamu nini mkakati wa Serikali, kutenga bajeti ya kutosha ili kuweza kurekebisha miundombinu na wazalishaji wale binafsi ili iendane na *standards* ya *TANESCO* kuzuia kukatikakatika kwa umeme Jimboni Ludewa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumeshaanza kufanyia kazi mwanzoni tulituma timu ya wataalam tukafanya uhakiki kuona gharama ambayo itakuwepo pale kwa ajili ya kubadilisha miundombinu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunatafuta fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati katika miundombinu hii ili wananchi wa Ludewa na wenyewe waendelee kupata umeme wa uhakika. Kwa hiyo, tutafuatilia, tutatafuta fedha kwa ajili ya kurekebisha miundombinu hii. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Shule ya Sekondari Daraja Mbili iliyopo Kata ya Maposeni? Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mojawapo ya vipaumbele vyetu ni kuhakikisha Taasisi za Elimu zinapata umeme, tayari nilishamwelekeza Meneja wa Mkoa wa Ruvuma aende katika shule hii ya Daraja Mbili Maposeni na wameshafanya uhakiki. Sasa hivi tupo katika taratibu za kuona ni mradi gani utatusaidia kuweza kupeleka umeme katika shule hii. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge jambo hilo tayari tunalifanyia kazi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali linalofuata, swali la Mheshimiwa Kabula Enock Shitobela, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 167

**Ruzuku ya Nishati Safi ya Kupikia**

**MHE. KABULA E. SHITOBELA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatoa ruzuku katika Nishati Safi ya kupikia ili kuwasaidia akinamama wasifanyiwe ukatili na kuuawa kutokana na imani potofu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia 2024-2034. Kupitia mkakati huo, Serikali imeanza kutoa ruzuku ya 20% hadi 50% ya bei ya mitungi ya gesi ya *LPG* kwa watumiaji wa mwisho. Aidha, Serikali inaendelea na hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusambaza majiko banifu 200,000 pamoja na kusambaza umeme ili kuhamasisha matumizi ya majiko ya umeme. Hii itasababisha wananchi wengi zaidi kutumia majiko haya kupikia na mwisho kupunguza matumizi ya kuni. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabula.

**MHE. KABULA E. SHITOBELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; nafahamu pamoja na masuala mengine Serikali inatoa mitungi ya gesi ya *LPG* ya ruzuku. Je, inatolewa kwa utaratibu gani ili wananchi wa Mkoa wa Mwanza nao waweze kufahamu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, mitungi hii inapatikana kwa Mawakala wapi ili wananchi wa Mkoa wa

Mwanza hasa akinamama wafahamu na kunufaika na fursa hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa maswali mazuri ya Mheshimiwa Mbunge na naomba niyajibu kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitungi hii tumeiwekea utaratibu, na utaratibu wa sasa hivi kila mtungi mmoja unaenda kwa mtu mmoja na inachukuliwa vilevile kwa namba ya *NIDA*. Yote ni kuhakikisha tunaweza kufikisha mitungi kwa wananchi wengi zaidi, lakini kwenye kila mkoa na kila wilaya tunao Mawakala ambao wanamitungi hii ambayo ipo takribani 452,000 na mpaka kufikia jana mitungi 78,500 imeshatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wa Mwanza tumetenga mitungi takribani 19,500 na katika Mkoa wa Mwanza Wakala ni *Lake Gas*. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Wananchi wa Mkoa wa Mwanza ambao wanataka kupata mitungi hiyo waende kwa Mawakala wote wa *Lake Gas* na watapata mitungi hii kwa nusu bei. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwa kinara wa nishati ndani ya nchi yetu, Afrika pamoja na dunia. Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuongeza Mawakala kwa mjini na vijijini kwa kuwa Watanzania wamepokea kwa mikono miwili wito wa Dkt. Samia wa kutumia nishati safi na salama? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa pongezi hizi kwa Mheshimiwa Rais ambaye yeye ndiye kinara wa masuala ya nishati safi ya kupikia. Tayari

Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati alishakaa na wadau katika sekta na tumekuwa na mkakati maalum kupitia huu mkakati ambao tunautekeleza wa kuhakikisha ya kwamba Mawakala wanaongezeka hasa katika maeneo ya vijijini ikiwemo Hanang ili kuweza kuhamasisha zaidi matumizi haya ya gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mbunge kupitia utekelezaji wa mkakati huu maeneo ya vijijini na yenyewe yataendelea kupata umeme kupitia Mawakala ambao tunawahamasisha wadau waendelee kuweka katika maeneo ya vijijini. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, Mbunge wa Busokelo sasa aulize swali lake.

Na. 168

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi Kandete- Busokelo**

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi Kandete- Busokelo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Daniel Sillo, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Kata ya Kandete Jimbo la Busekelo wamejitolea kujenga Kituo cha Polisi Daraja “C”. Ujenzi wa kituo hicho upo kwenye hatua ya msingi na mpaka sasa umetumia kiasi cha fedha shilingi 14,000,000. Serikali kupitia Jeshi la Polisi imefanya tathimini kwa ajili ya kumalizia ujenzi ili kuunga mkono juhudi na nguvu za wananchi na kiasi cha fedha shilingi milioni 500 zinahitajika. Maombi ya kupata fedha

yamewasilishwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi kwa ajili ya umaliziaji wa ujenzi wa kituo hicho. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fredy Atupele.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Jimbo la Busokelo tumejenga Kituo cha Polisi Lwangwa Mjini kwa gharama za wananchi kwa maana ya kujitolea na sasa tunajenga Kituo cha Polisi kingine eneo la Kandete, Bonde la Mwakaleli na Serikali imesema imetenga milioni 500. Je, ni lini fedha hizi zitaungana na juhudi za wananchi zaidi ya milioni 14 ili Kituo hiki kiweze kukamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri Busokelo ni halmashauri mpya na tunatamani afike akajionee namna ambavyo wananchi tunashiriki pamoja kwa nguvu kwa ajili ya kujenga hiki Kituo cha Polisi. Ni lini atapata nafasi ya kuja kuonana na wananchi hawa na kuwa-*support* katika ujenzi wa kituo hiki cha Polisi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Busokelo kwa kazi kubwa aliyofanya ya kujenga kituo cha Polisi cha kwanza na sasa anajenga cha pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha hizi milioni 500 tunatenga kwa Mwaka wa Fedha huu unaokuja wa 2025/2026 ili kuunga mkono kazi kubwa iliyofanywa na wananchi wa Busokelo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, kwenda kuambatana na Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge lako Tukufu kuahirishwa, basi tutapanga naye ratiba, tayari kutembelea kituo hicho na kuwatia nguvu na moyo wananchi kwa kazi waliyofanya.  Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha Festo.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Tanganyika hatuna kabisa Kituo cha Wilaya cha Polisi na wananchi wameonesha jitihada kwa kujichangisha wakishirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya pamoja na Ofisi ya Mbunge wa Jimbo. Je, ni lini Serikali italeta fedha kwa ajili ya umaliziaji wa kituo hiki cha Polisi katika Wilaya ya Tanganyika? Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Martha na wananchi hawa kwamba tayari wameshaanza kuchanga fedha kwa ajili ya Ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Tanganyika. Basi kama Serikali pia tumechukua na tutaunga mkono juhudi hizo, tutatenga kwenye mpango na hatimaye kutengea bajeti. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. Kituo cha Polisi Kilando hali yake ni mbaya na Kata hiyo ni miongoni mwa Kata ambazo ziko mpakani. Mimi Mbunge wa Jimbo pamoja na Jeshi la Polisi tumeanza kujenga Kituo cha Polisi kimefikia hatua ya lenta. Je, ni lini Serikali ita-*support* kumalizia hatua iliyobaki? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na Askari Polisi waliyochangishana kuhakikisha wanajenga Kituo cha Polisi kwa ajili ya usalama wa raia na wananchi na nimhakikishie kwamba Serikali imekichukua pia kituo hicho. Tunatenga fedha kwa ajili ya kumalizia kituo hicho ambacho wameshakijenga kwa hatua ya lenta. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru takribani miaka miwili sasa, Serikali imeahidi kufanya ukarabati kwenye nyumba za Maaskari na Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Ukerewe, lakini bado kazi hii haijafanyika na Askari na hawa wanaishi kwenye mazingira magumu sana. Ni lini sasa Serikali itafanya ukarabati kwenye hiki Kituo cha Polisi cha Wilaya? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mbunge wa Ukerewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakifahamu Kituo cha Polisi cha Ukerewe ni kichakavu, lakini pia na nyumba za Watumishi. Tumeshatenga fedha milioni 115 za kumalizia kituo hiki cha Polisi ambacho kimechakaa katika eneo la Ukerewe. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Florent Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi. Wananchi wa Kata ya Kanuni ndani ya Wilaya ya Misenyi ambao wako mpakani mwa nchi yetu ya Tanzania na Uganda. Usafiri takribani kilomita 70 kwenda Makao Makuu ya Wilaya kupata huduma za Kipolisi, wananchi hao kwa pamoja wameanza kujenga Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni mara ya pili nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuuliza, je, ni lini Serikali sasa itatuunga mkono kutupatia bajeti ya kuhakikisha kwamba kituo hicho kinakamilika ili wananchi hawa wapate huduma ya ulinzi kwa kuwa katika eneo lao wako karibu na mpaka wa Nchi ya Uganda ambayo itakuwa imewasaidia kiulinzi? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, kwenye maeneo yote ambayo wananchi wameshaonesha

jitihada za kujenga vituo vya Polisi. Serikali itapitia vyote na kufanya tathmini ya kuhakikisha kwamba kila kituo ambacho kimeanza, basi Serikali itaunga mkono juhudi hizo ikiwepo Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Misenyi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea swali linalofuata mtapata nafasi maswali yanayofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 169

**Kukamilisha Ujenzi wa Vituo vya Polisi**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Vituo vya Polisi vilivyojengwa kwa nguvu za wananchi – Mbeya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuchangia fedha na kumalizia ujenzi wa vituo vya polisi vinavyojengwa kwa nguvu za wananchi ili kuungwa jitihada zao. Serikali kupitia Jeshi la Polisi imeshatuma kiasi cha fedha jumla ya shilingi 236,408,000 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa Vituo vya Polisi Kambikatoto, Makongolosi, Sangambi na Igulusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini kwa ajili ya kujua gharama ya kumalizia Vituo vya Polisi Kandete, Itumbi, Igoma na Madibira imefanyika na fedha shilingi 1,429,000,000 zinahitajika. Maombi ya kupata fedha kwa ajili ya umaliziaji wa vituo hivyo, yamewasilishwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi. Aidha, Kituo cha Polisi cha Kapunga kinaendelea na ujenzi kwa ufadhili wa Mwekezaji wa shamba la mpunga na Kituo cha Ifumbo ujenzi wake unafadhiliwa na Mwekezaji wa madini Chunya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, ninaipongeza sana Serikali kwa juhudi zake, ambapo imepeleka fedha kwenye vituo vya polisi ambavyo wananchi waliweka nguvu kazi yao pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yangu mawili haya ni pamoja na Kata ya Ifumbo, Wilayani Chunya wananchi walitafuta fedha kiasi cha shilingi milioni 37; Kata ya Madibila Wilayani Mbarali wananchi walitafuta fedha kiasi cha shilingi milioni 25 ili kuanza kujenga maboma hayo, lakini vivyo hivyo Kata ya Ubaruku Kijiji cha Mabarali…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, tafadhali uliza swali.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Ubaruku Kata ya Mbarali, wananchi walitafuta fedha kiasi cha shilingi milioni 60, wameanza kujenga maboma hayo, lakini sasa yamebaki maboma kwa sababu hakuna fedha za umaliziaji. Sasa, je, lini Serikali itapeleka fedha za umaliziaji wa maboma hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Wilaya ya Mbarali haina Kituo cha Polisi cha Wilaya, wanatumia jengo la zahanati. Vivyo hivyo, Wilaya ya Chunya haina kituo cha polisi, wanatumia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Sasa, je, ni lini Serikali itapeleka fedha za ujenzi wa kituo hicho? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia sana Vituo vya Polisi vya

Mkoa wa Mbeya. Pia, ninapokea pongezi alizozitoa kwa Serikali kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, amesema kuhusu Kituo cha Polisi cha Ifumbo pamoja na Madibila. Kwanza, ninawapongeza wananchi kwa kuchangia fedha shilingi milioni 37, milioni 25 na milioni 60 katika vituo hivi. Kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi; katika maeneo yote ambayo wananchi wameonesha jitihada za kujenga vituo vya polisi Serikali itawaunga mkono ikiwemo na vituo vya polisi ambavyo amevitaja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, Wilaya ya Chunya na Mbarali ni Wilaya ambazo hazina kabisa vituo vya polisi. Tunavichukua vituo hivi na kuingiza kwenye mpango wetu, kutengea bajeti na tayari kujenga vituo vya polisi katika wilaya hizo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge ninaomba niwakumbushe, maswali yawe mafupi kadri inavyowezekana na yawe ya moja kwa moja. Pia, Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri majibu yenu yawe mafupi na ya moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Robert Maboto.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itakarabati Kituo cha Polisi Bunda pamoja na nyumba za wafanyakazi wa Polisi Bunda? Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Robert Maboto, Mbunge wa Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba vituo vya Polisi pamoja na Makazi ya Askari yanakuwa bora. Kwa hiyo, vituo hivyo alivyovitaja pia tutaingiza kwenye mpango na kuitengea fedha kwa ajili ya ukarabati. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ifikapo Julai mwaka huu Wilaya ya Liwale itafikisha miaka 50 na Wilaya ile Muasisi ni Mzee Rashid Kawawa, lakini haijawahi kuwa na jengo la Kituo cha Polisi. Lini Serikali itatujengea Kituo cha Polisi Wilaya ya Liwale? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amesema Wilaya hii ina miaka 50 haina Kituo cha Polisi. Ninaomba tukichukue tukiingize kwenye mpango na kutengewa bajeti kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Conchesta.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kasharunga, Kijiji cha Kasharunga Wilaya ya Muleba wamejenga Kituo chao na kimekamilika na nimeuliza swali hii ni mara ya tatu. Ni kwa nini Serikali inakuwa na ugumu wa kufungua kituo hicho? Serikali itoe sababu kusudi wananchi waelewe. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo alichokitaja Mheshimiwa cha Kasharunga tutaenda kukifungua.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Swali la Mheshimiwa Dorothy George Kilave litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani mimi ndiye niliyepewa majibu.

**MWENYEKITI:** Sikupata taarifa Mezani. Mheshimiwa Esther Matiko.

Na. 170

**Kuendelea na Ujenzi wa Nyumba za Askari Polisi *Kilwa Road*- Temeke**

**MHE. ESTHER N. MATIKO K.n.y. MHE. DOROTHY G. KILAVE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaendelea kujenga nyumba za Askari Polisi eneo la *Kilwa Road* Jimbo la Temeke?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa nyumba za ghorofa kwa ajili ya makazi ya kuishi Askari Polisi kwenye Kambi ya Polisi iliyopo kwenye Barabara ya Kilwa Temeke, Dar es Salaam ulianza Mwaka 2006 na lengo la Serikali ni kujenga nyumba 96.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika awamu ya kwanza ya ujenzi zimejengwa nyumba 28 ambazo zinaishi jumla ya familia za askari 336. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuendeleza awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba za makazi ya Askari Polisi katika eneo hilo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER M. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; Wilaya ya Kipolisi ya Tarime - Rorya ambayo ina Wilaya ya Nyamwaga, Sirari, Tarime, Kinesi na Shirati hawana nyumba za Polisi kabisa. Ni lini Serikali itaenda kujenga nyumba hizi kama inavyofanya kwenye maeneo mengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Askari Magereza wa Tarime hawana nyumba kabisa zenye hadhi ya familia na kutoa faragha kwa familia zao. Serikali haioni kwamba kuna haja ya

kujenga nyumba kwa Askari Magereza hao ambao wanafanya kazi kwa uaminifu kabisa? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Esther ametaja nyumba za Polisi kwa maeneo ya Tarime, Rorya. Tunafanya tathmini katika eneo hilo na kuona mahitaji halisi ni kiasi gani na tutaliweka kwenye mpango ujenzi wa nyumba za Polisi kwenye eneo la Tarime Rorya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuhusu Askari Magereza, kwanza ninawapongeza Askari wetu wanafanya kazi kubwa, lakini ni kweli yapo maeneo ambayo kwa kweli mazingira ni magumu kwa maana ya kutokuwa na makazi ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutalichukua na hili pia tuliingize kwenye mpango tayari kwa kutengewa bajeti na kujenga nyumba hizi za Askari Magereza katika eneo alilolitaja Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani wa kufanyia matengenezo nyumba ilizojengwa katika swali la msingi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, Mbunge wa Mbagala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za Askari katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, pia nyumba za askari ambazo zimejengwa

kuanzia mwaka 2006 kama nilivyosema ni kweli zinatakiwa matengenezo na tutafanya hiyo tathmini na kutengea fedha kwa ajili ya kufanya matengenezo nyumba za askari za katika eneo la *Kilwa Road*. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Yustina Rahhi, halafu Mheshimiwa Amar.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu mkubwa sana wa nyumba za Askari Polisi katika Kituo cha Mbulu Mjini na chache zilizopo zimechakaa. Ni upi mpango wa Serikali kwenda kuwajengea watumishi hao nyumba za kuishi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wiki iliyopita nilijibu swali la Mheshimiwa Issaay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini kuhusu upungufu wa nyumba za Askari na uchakavu katika Wilaya ya Mbulu. Tulisema kwamba, tutafanya tathmini kuona uhalisia wa fedha kiasi gani zinahitajika kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za Polisi za Mbulu Mjini. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hussein Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kujenga nyumba za Askari Polisi Wilaya ya Nyang'hwale kwa sababu tuna Askari Polisi zaidi ya 50 na nyumba za Polisi zipo mbili tu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la Mheshimiwa Amar pia kwa sababu halipo kwenye mpango tutalichukua tuliingize kwenye mpango ili itengewe fedha kwenye bajeti inayokuja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Sikonge tumepangiwa shilingi milioni 140 kujenga Kituo kidogo

cha Polisi Pangale pamoja na nyumba za Polisi. Ni lini fedha hizo zitakuja kutoka Serikalini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakunda, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumetenga fedha shilingi milioni 140 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi alichokitaja Mheshimiwa Mbunge na katika huu Mwaka wa Fedha 2024/2025 fedha zimetengwa na zitatolewa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa muda wako, tunakushukuru.

Waheshimiwa Wabunge, tunahamia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 171

**Kuongeza Bajeti ya Mikopo kwa Makundi Maalum**

**MHE. MARIAM M. NYOKA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Bajeti ya Mikopo ya Makundi Maalum kwa kuwa uhitaji ni mkubwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaendelea kufanya majadiliano na Wizara ya Fedha kwa lengo la kupata ongezeko la ukomo wa bajeti itakayowezesha upatikanaji wa fedha za kutosha kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wafanyabiashara

ndogondogo nchini, kwa kuzingatia idadi ya wanaotambuliwa na kusajiliwa kwenye mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majadiliano haya yataendelea baina ya Wizara na Taasisi za Fedha, ili waweke masharti na riba nafuu kwenye mikopo wanayotoa ili kuwezesha wafanyabiashara ndogondogo kupata mikopo yenye masharti na riba nafuu itakayowainua kiuchumi. Vilevile, Wizara itaendelea kuwahamisisha na kuwaunganisha wafanyabiashara hawa na fursa mbalimbali za uwezeshaji wananchi kiuchumi zinazopatikana Serikalini na kwenye Sekta Binafsi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Nyoka.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza; je, Wizara itatumia muda gani wa kuendelea kufanya majadiliano na Wizara ya Fedha, ili kupata ufumbuzi wa ongezeko la bajeti ya kundi hili maalum? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; je, Serikali ipo tayari kuhakikisha kwamba ongezeko la kibajeti litaonekana kwenye bajeti ya mwaka 2025/2026, ili kuweza kuhudumua kundi hili? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mariam, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la mwanzo linauliza kwamba, ni lini Serikali itamaliza maongezi na Wizara ya Fedha? Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mwaka huu wa fedha tutamaliza mazungumzo hayo na kuhakikisha kwamba bajeti hiyo inafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuhusu swali lake la pili, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan ni sikivu na inawajali sana wafanyabiashara wadogowadogo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Mwaka wa Fedha wa 2025/2026 tutaongeza bajeti ya wafanyabiashara ndogondogo ili kuwawezesha kujiinua kiuchumi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ninakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Serikali.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 172

**Tatizo la Maji katika Kijiji cha Kabulanzwili – Kigoma**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza tatizo la upungufu wa maji katika Kijiji cha Kabulanzwili – Kigoma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, karibu.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuboresha huduma ya majisafi na salama kwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma ikiwemo Kijiji cha Kabulanzwili kilichopo Wilayani Kasulu mkoani humo. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali inatekeleza Mradi wa Maji utakaohudumia vijiji viwili vya Kabulanzwili na Chekenya ambao upo katika hatua za mwisho za kusainiwa kwa mkataba. Kazi ya uchimbaji wa viwili visima virefu ambavyo vitatumika kama vyanzo vya maji katika mradi huo imekamilika, ambapo vina uwezo wa kuzalisha maji jumla ya lita 46,200 kwa saa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zingine zitakazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa matanki mawili yenye jumla ya ujazo wa lita 375,000, ulazaji wa mtandao wa mabomba umbali wa kilometa 36.6 sanjari na ujenzi wa vituo 29 vya kuchotea maji. Ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kuanza mwezi Machi, 2025 na kutarajiwa kukamilika ndani ya miezi tisa ili kuhudumia wananchi wapatao 14,138 wa Vijiji vya Kabulanzwili na Chekenya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Mkoa wa Kigoma umejaliwa kuwa na vyanzo vingi vya maji; Ziwa Tanganyika, Mto Malagarasi na mito mingi midogomidogo. Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza matatizo ya maji katika vijiji ambavyo havina maji, kwa kutumia vyanzo hivyo ambavyo tulijaliwa na Mwenyezi Mungu kwa maana ya Ziwa Tanganyika na Mto Malagarasi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; katika Halmashauri ya Kasulu *DC* katika Kata ya Lusesa kuna tatizo kubwa la maji. *Tank* linalotumika ni la muda mrefu, miaka mingi…

**MWENYEKITI:** Swali Mheshimiwa Mbunge. Swali tafadhali.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya watu imeongezeka, tanki hilo halina uwezo wa kuhimili maji hayo ambayo yanaweza kutosheleza watu wote. Je, ni lini Serikali itajenga *tank* jipya na kupeleka mabomba ili kusambaza maji kwa wananchi waweze kunufaika na maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali kwa ufupi.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya, lakini kubwa ninachotaka kumhakikishia ni

kwamba Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameshafanya kazi kubwa na tunatambua kabisa chanzo cha Ziwa Tanganyika tumeanza kukitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga mradi mkubwa wa zaidi ya shilingi bilioni 44 kata zote za Kigoma Ujiji zinapata huduma ya maji safi na salama. Mkakati wetu ni kuhakikisha Ziwa la Tanganyika linatumika na maeneo mengine yaweze kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa ipo miradi 27 yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 15. Mkakati wetu ni kuhakikisha kwamba miradi hii inakamilika ili wananchi hawa waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunatambua kwamba Mto Malagarasi na Ziwa Tanganyika ni vyanzo chochevu ambavyo mkakati wetu ni kujenga miradi mikubwa ambayo itahakikisha maeneo mbalimbali yanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine juu ya *tank* tumelipokea na tutalitengea fedha katika kuhakikisha wananchi hawa wanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Innocent Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Maji Lunyinya, Chanya, Kikukuru, Kimuli, Rutungu, Isungiro pamoja na Mabila wakandarasi wameondoka *site* kwa madai ya shilingi bilioni sita. Je, ni lini watalipwa ili miradi hii iweze kukamilika na wananchi wapate maji safi na salama? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha. Tumeshaanza kupokea fedha na kuwalipa baadhi ya Wakandarasi. Hata hivi ninavyozungumza tumepokea shilingi bilioni 16 kupitia Mfuko wa

Maji. Ninataka niwahakikishie Wakandarasi wa maeneo yote kwamba, fedha tumepata na ninawasihi Wahandisi wa Maji Mikoani, fedha zinazofika katika maeneo yao zilipwe mara moja, ili watu waweze kutekeleza miradi ya maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jonas Zeeland.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 tulipata fedha ya kuchimba visima katika Wilaya ya Mvomero, Kijiji cha Makuyu, Milama, Lugono pamoja na Manza, lakini toka huo mwaka 2022 mpaka leo yamebaki mashimo tupu. Je, ni lini Wizara itatupatia fedha sasa tujenge miundombinu ili tuondokane na tatizo la maji katika hivi vijiji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwahidi Mheshimiwa Mbunge tumelipokea kwa ajili ya utekelezaji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maimuna Mtanda.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi. Mradi wa Maji wa Mnima – Miyuyu ambao upo katika Jimbo la Newala Vijijini ni mradi wa muda mrefu, lakini hadi leo haujakamilika na wananchi wanapata shida ya maji. Je, ni lini mradi ule utakamilika ili wananchi wa Jimbo la Newala Vijijni wapate maji ya uhakika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge. Ninaahidi kupokea taarifa za Mradi huu wa Mlima Miyuyu haraka kwa ajili ya utekelezaji wa haraka na kuchukua hatua ili tuweze kukamilisha huu mradi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Fatma Toufiq kwa kifupi.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Mradi wa Bwawa la Farkwa utaanza ili kukabiliana na upungufu wa maji katika Jiji la Dodoma na hasa maeneo ya Nkuhungu? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mama yangu Fatma Toufiq amekuwa *champion* juu ya upiganaji hasa wa Mradi huu wa Bwawa la Farkwa, lakini ninataka nimhakikishie sasa hivi tupo hatua za usanifu, Mhandisi Mshauri tumeshampata, lakini tupo hatua za mwisho za kumpata Mkandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimhakikishie, hivi karibuni tutampata mkandarasi, tutasaini hadharani na tutamwalika juu ya utekelezaji wa huu mradi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Vita Kawawa.

**MHE. VITA. R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inaweza kuwaeleza wananchi wa Kata za Mchomoro na Mgombasi ni lini itamaliza mradi wa maji katika maeneo hayo, wenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 4.7? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, nilishafika Namtumbo na nimefika katika hilo eneo, ninataka niwaahidi wananchi wa Namtumbo. Kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya Mheshimiwa Mbunge wao tutatoa fedha, kwa ajili ya kukamilisha mradi ule na wananchi waweze kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi mingi iliyopo Wilaya ya Kilolo, ambayo ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri, lakini nina swali dogo. Mradi wa Maji wa Mkalanga na wa Kata ya Mlafu imesimama kwa muda kidogo kutokana na kukosekana hela ambazo ni kidogo tu. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kupeleka fedha hizo, ili miradi ile iweze kukamilika na maji yaanze kutoka? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwahidi Mheshimiwa Mbunge, tupo tayari na tutatoa fedha, kwa ajili ya ukamilishaji wa hiyo miradi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, ninaomba tuendelee na swali linalofuata. Ah, Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana kwa majibu.

Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, aulize swali lake.

Na. 173

**Kufufua Kilimo cha Pareto, Kisimiri Juu**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kufufua kilimo cha pareto, Kisimiri Juu, ili wananchi wa eneo hilo wanufaike kama ilivyokuwa miaka ya 60 na 70?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko *(COPRA)*, imeendelea kutekeleza mikakati ya kuongeza uzalishaji wa zao la pareto kwa kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora kwa wakulima katika

maeneo yote yanayozalisha zao la pareto nchini, ikiwemo Kisimiri Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *COPRA* kwa kushirikiana na Kituo cha Utafiti cha *TARI,* Uyole, imegawa bure kilogramu 890 za mbegu bora katika maeneo yanayozalisha pareto, ambapo Kisimiri Juu imepata kilogramu 100 ambazo zitapanda ekari 400 na kila ekari moja ina uwezo wa kuzalisha kilogramu 450 za maua ya pareto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ili kuwawezesha wakulima kupata miche bora, mbegu hizo zimekabidhiwa kwa Kampuni ya *Pareto PCT,* kwa ajili ya kuzalisha miche ambayo itagawiwa kwa wakulima wa Kisimiri Juu. Vilevile wakulima wapatao 300 wa Kisimiri Juu wamepatiwa mafunzo ya kilimo bora cha pareto ili waweze kulima zao hilo kwa tija. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo. *(Makofi)*

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Swali la kwanza; sambamba na kufufua kilimo cha pareto Kisimiri Juu, pale Usa *River* kuna Shamba la Maua la Loliondo ambalo lilitelekezwa na mwekezaji, wafanyakazi wakakosa ajira na stahiki zao. Je, ni nini hatima ya wale wafanyakazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Serikali haioni kwamba, ni busara sasa kwenda kuanzisha programu ya *BBT* pale, ili vijana ambao hawana kazi wa Arumeru Mashariki pamoja na wale wafanyakazi waliokosa kazi waweze kujiajiri? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kikubwa ambacho nimthibitishie ni tunatambua kuwa, Shamba la Oljoro halijatumika

kwa muda mrefu na kuna wafanyakazi wamepoteza kazi pale kwa muda huu. Hatima yao ni kwamba, sisi kama Wizara tunaendelea kufanya tathmini ya kuhakikisha lile shamba linafufuliwa na tuweze kuajiri watu wapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuanzisha programu mpya katika eneo hilo, ndiyo sehemu katika ule mpango kazi ambao tunauunda sasa. Kwa hiyo, ukishakamilika, basi tutakutaarifu Mheshimiwa Mbunge. Tutaongozana pamoja na mimi mwenyewe, twende tukafanye hiyo kazi kwa pamoja katika eneo hilo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Tunaelekea Wizara ya Fedha. Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, aulize swali lake.

Na. 174

**Asilimia 20 ya Kodi ya Ardhi Kurejeshwa Mtwara, Mikindani**

**MHE. HASSAN S. MTENGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itarejesha makusanyo ya Kodi ya Ardhi ya 20% kwa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara, Mikindani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, karibu.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Sheria ya fedha ya mwaka 2023/2024 ilifanya marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290, kwa kuzitaka Wizara za Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuingia Mkataba wa Makubaliano ya Ushirikiano *(MoU)* katika usimamizi wa ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi na kuweka utaratibu wa

urejeshaji wa 20% ya mapato kwa halmashauri ili kuziwezesha katika ufuatiliaji na ukusanyaji wa mapato hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliweka utaratibu huo ikiwa na lengo la kuhakikisha kuwa, tija inapatikana katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na pango la ardhi na kuondoa kero zilizokuwa zikiwakabili walipakodi kwenye maeneo husika. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, pale mkataba huo utakapokamilika na kuwasilishwa Wizara ya Fedha, fedha hizo zitarejeshwa kwa utaratibu unavyotaka.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga. *(Makofi)*

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakushukuru na ninashukuru majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, fedha hizi za mwaka wa fedha 2023/2024 na kwa mujibu wa sheria, hizi fedha zinatakiwa zirudi kwa wakati pale ambapo tunapeleka makusanyo. Je, ni lini Mheshimiwa Waziri atatuletea hizi fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; *TRA* imeingia kwenye mfumo wa kuunganishwa na *TBS*, ambapo mfumo huu kwa sasa unaleta kero kubwa sana. Watu ambao wanaagiza magari kutoka nje, watu ambao wananunua magari ya ndani, ya Serikali, hawawezI kupata *release* mpaka *TBS* watoe *release*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali tafadhali.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, swali langu ni; ni lini Serikali itafanya uamuzi kwa wale watu wote ambao wanadaiwa *storage*, tofauti na mazingira ambayo yapo kwa msamaha ambao unatakiwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge makini kabisa kwa maswali yake ya msingi ambayo yanaongelea mambo yanayojitokeza.

Nikianza na kipengele cha kwanza; kuna maendeleo, kuna hatua nyingine zimeendelea ndani ya Serikali ambapo, Wizara hizi tatu, Fedha, TAMISEMI pamoja na Ardhi, tunaendelea kuliangalia upya jambo hili ambalo kwa kweli, limekuwa na masuala mengi na punde tutakapokamilisha, ama ndani ya Bunge ama kupitia Kamati zetu, tutatoa *update* hatua ambayo tumefikia. Baada ya kuchukua hiyo hatua, tutakamilisha yale ambayo yatakuwa yalishafanyika, kwa maana ya fedha ambazo zimekusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili la pili ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliuliza, hiyo tutaifanyia kazi *case by case,* yaani kwa jambo mahsusi ambalo limetokea. Tutaongea na Mheshimiwa Mbunge hatua tunazozichukua.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 175

**Kumaliza Migogoro ya Ardhi Kati ya Wakulima na Wafugaji, Lindi**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji maeneo ya Liwale, Kilwa, Nachingwea na Lindi Vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kushughulikia migogoro ya ardhi baina ya watumiaji wa ardhi katika maeneo

mbalimbali nchini, ikiwemo Mkoa wa Lindi. Katika Mkoa wa Lindi jumla ya mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji 159 kati ya vijiji 386 imeandaliwa katika Wilaya za Lindi, Vijiji 34; Kilwa Vijiji, 59; Nachingwea, Vijiji 28; na Liwale, Vijiji 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kuandaliwa kwa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya vijiji, jumla ya vitalu 98 vyenye ukubwa wa ekari 500 kila kimoja vimetengwa, kwa ajili ya kugawiwa kwa wafugaji katika Wilaya ya Liwale, ambapo kati ya vitalu hivyo, upimaji wa vitalu 33 umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua hizo, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kutumia ardhi kwa tija, hususan kwa kuzingatia ufugaji wa kisasa na kilimo bora, kama njia mojawapo ya kuondoa migogoro iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwa halmashauri zote nchini kuendelea kutenga bajeti, kwa ajili ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji vilivyopo katika maeneo yao, ili kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji. Aidha, watumiaji wote wa ardhi wanahimizwa kuzingatia mipango ya matumizi bora ya ardhi iliyoandaliwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Pathan.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Wafugaji wanaingiza mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima na kusababisha njaa kali, mapigano na vifo. Je, Serikali haioni haja ya kuchukua hatua hizo kwa haraka ili ku-*rescue* hali iliyopo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Naomba kumuuliza Naibu Waziri wa Ardhi, je, anaweza kuambatana nami au anaweza kwenda kuwaona wananchi walioathirika kwenye

maeneo yao ili awasikilize, aone umuhimu wa suala hili? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA, NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wa karibu juu ya masuala haya yanayohusisha migogoro ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, Serikali imeendelea kupambana ili kupata fedha, kwa ajili ya kuhakikisha vijiji vyote vinawekewa mpango wa matumizi bora ya ardhi zao. Juhudi hizi zinaendelea, hivi karibuni tumekutana na Wizara ya Fedha na wameweka *commitment* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, vijiji vinaongezeka katika lile zoezi la kuviwekea mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, juu ya kuandamana au kutembelea maeneo haya, hii ni sehemu ya wajibu wetu, kwa sababu, tunapowafikia wakulima na wafugaji, kimsingi tunakwenda kuwaweka pamoja ili wajitambue tu kwamba, wao ni wananchi wa Tanzania na ardhi ile ni yao wote. Kinachozingatiwa pale ni namna nzuri ya kuitumia. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Yahya Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliunda Tume ya Mawaziri tisa kuzunguka Tanzania na kuangalia changamoto za ardhi. Ndani ya Wilaya yangu, Waziri wa Ardhi kama ndiyo kiongozi, walikuja na kubaini changamoto zilizopo katika Kata ya Mkonona katika Vitongoji vya Wanika, Libhambangoma, Nambunda na Namaromba. Wananchi wale wanatakiwa waondoke ili kupisha shughuli za Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, ninaomba uliza swali.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni mwaka wa pili wananchi hawajalipwa fidia. Ninataka kujua kauli

ya Serikali, msimamo upo au haupo ili wananchi wale waweze kufanya shughuli za maendeleo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA, NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka tu kumpa mwelekeo wa Serikali. Serikali inapoamua jambo hairudi nyuma. Kwa hiyo, msimamo wa Serikali ni kwenda kuwaondoa wale wananchi na sasa iko kwenye mchakato wa kutafuta fedha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Tunaelekea Wizara ya Madini. Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 176

**Madini ya *Tanzanite* Kuuzwa kwenye Masoko ya Ndani**

**MHE. MRISHO M. GAMBO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaruhusu kuuzwa kwa Madini ya *Tanzanite* kwenye Masoko ya Madini ya Ndani, kama Arusha, Mwanza, Mbeya, Dar es Salaam na Zanzibar?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa biashara ya Madini ya *Tanzanite* katika maeneo mbalimbali nchini, mwaka 2024 Wizara ilifanya marekebisho ya Kanuni ya 22 ya Kanuni za Eneo Tengefu la Mirerani za Mwaka 2019, ambapo kwa sasa umewekwa utaratibu bora zaidi wa biashara kupitia Kituo cha Uuzwaji wa Pamoja wa Madini ya *Tanzanite (Tanzanite Exchange Centre – TEC)*. Utaratibu huo unatoa nafasi ya kufanya biashara ya *Tanzanite* nje ya Mirerani kwa mwongozo ufuatao:-

(a) Biashara ya *Tanzanite* ghafi *(Rough Tanzanite)* itaruhusiwa kufanyika nje ya Mererani endapo mmiliki wa madini husika atakuwa na Leseni Kubwa ya Ukataji wa Madini *(Large Lapidary License)*; na

(b) Biashara ya Tanzanite iliyokatwa na kung'arishwa *(cut and polished)* itaruhusiwa kufanyika nje ya Mererani endapo mhusika wa madini husika atakuwa na leseni yeyote ya biashara ya ukataji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na marekebisho hayo, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara imepanga kufanya minada na Maonesho ya Madini ya Vito, ikiwemo *Tanzanite* katika maeneo ya Arusha, Mirerani, Mahenge, Dar es salaam na Zanzibar, ambapo tarehe 14 Desemba 2024 Wizara ilifanya mnada wa Madini ya Vito Mirerani. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa, kanuni zetu zinaruhusu kabisa Madini ya *Tanzanite* yaliyo chini ya *gram* mbili, baada ya kulipiwa kodi na tozo za Serikali, kuweza kuuzwa nje ya Tanzania kama Kenya, Uarabuni, Marekani na maeneo mengine. Je, ni nini kinazuia madini hayo hayo baada ya kulipiwa kodi kuweza kuuzwa Arusha, Dar es Salaam, Mwanza na Zanzibar? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili la nyongeza; taarifa zinaonyesha kwamba, baada ya Serikali kubadilibadili kanuni zinazohusiana na masuala ya Madini ya *Tanzanite*, Mwaka 2019 na Mwaka 2024, imesababisha kuporomoka kwa bei ya madini hayo na kushuka kwa mapato ya Serikali. Je, Serikali ina mpango gani wa kurejesha Soko Huria, ili Watanzania waweze kunufaika na madini yao kwa sababu, madini haya ni madini ya Taifa na wala siyo madini ya sehemu fulani peke yake? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Gambo kwa

anavyowatetea wachimbaji na wafanyabiashara wa *Tanzanite* katika Jimbo lake la Arusha na Watanzania wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kibali cha kuuza madini yaliyo chini ya gramu mbili katika masoko na minada ya nje ya nchi na kwa nini yasiuzwe na ndani; dhamira ya Serikali ilikuwa ni kuhakikisha kwamba, Madini yote ya vito na mengine mbalimbali nchini yanaongezwa thamani kabla hayajauzwa sokoni. Hii inasababisha kuweza kutengeneza fursa za ajira, kuongeza ujuzi wa kuongezea madini thamani na pia kupandisha bei yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi baada ya marekebisho mbalimbali ya kanuni madini haya yote, yaliyoongezwa thamani katika *size* mbalimbali, huruhusiwa kuuzwa katika masoko na minada mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la pili, bei kuporomoka, anavyosema kwamba, imesababishwa na mabadiliko ya kanuni zetu; sina hakika kama Mheshimiwa Mbunge ana tafiti iliyofanyika, awe na sababu ya kusema kwamba, ni mabadiliko ya kanuni na sheria ndiyo imeporomosha bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Madini ya *Tanzanite* baada ya kujaribu kuwekewa vikwazo, ili yasiendelee kusambaa kiholela na kupoteza umaarufu wake kama madini yanayopatikana Tanzania tu, duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vigezo vilivyowekwa na kushuka kwa bei havihusiani kwa sababu, sasa hivi katika dunia tuliyopo kuna madini mengine yanayoshindana na *Tanzanite*. Mpaka hata almasi inayotengenezwa viwandani inaitwa *Synthetic Diamond*, ipo sokoni kwa bei ya chini kabisa na hivyo, ushindani wa biashara ya madini ya aina mbalimbali huenda ikawa ndiyo sababu ya msingi ambayo sisi tunasema inaweza ikawa imeshusha thamani ya madini yetu ya *Tanzanite*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujaribu kupandisha thamani, tumeendelea kuja na huu mfumo sasa wa minada ya madini hayo. Minada hii inakwenda kusaidia mauzo ya pamoja kwa bei bora zaidi, Mnada wa kwanza ulionesha kwamba, una tija kabisa na tunategemea kwamba, bei ya madini haya itaendelea kuongezeka duniani.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali linalofuata, Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, aulize swali lake.

Na. 177

**Ujenzi wa Kiwanda cha Chumvi Nangurukuru, Kilwa**

**MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika mchakato wa ujenzi wa kiwanda cha chumvi eneo la Nangurukuru, Kilwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa kutatua changamoto ya wazalishaji wa chumvi, hususan Mikoa ya Kusini, Serikali imeanzisha Mradi wa Kujenga Kiwanda cha Kusafisha Chumvi *(Salt Refinery Plant)* katika eneo la Lingaula, Wilaya ya Kilwa, Mkoa wa Lindi. Hadi sasa eneo la ujenzi limepatikana, tayari limepimwa, hati imeshapatikana na kukabidhiwa kwa Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *STAMICO* imenunua mtambo wa kusafisha chumvi, kwa ajili ya mradi huo, ambapo awamu ya kwanza ya mtambo imewasili nchini na taratibu za kuutoa bandarini na kuusafirisha kwenda eneo la mradi zinaendelea. Aidha, shughuli za ujenzi wa jengo litakalosimikwa mtambo huo zinaendelea. Ujenzi wa mtambo huo unatarajiwa kukamilika ifikapo Mwezi Agosti, Mwaka huu wa 2025.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuona changamoto kubwa iliyokuwa ikiwakabili wazalishaji wa chumvi ghafi wa Mikoa ya Kusini na hatimaye kuanzisha kiwanda hiki pale Kilwa eneo la Lingaula Nangurukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa mradi huu ni mradi ambao unategemewa kusaidia wananchi wazalishaji wa chumvi katika Majimbo ya Kilwa Kaskazini, Kilwa Kusini, Mchinga, Lindi Mjini, Mtama...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, tafadhali tumetoa maelekezo Waheshimiwa Wabunge tuzingatie maswali mafupi. Naomba uende moja kwa moja kwenye swali lako Mheshimiwa, bila kuweka kwa kuwa.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa mradi huu ni mradi ambao unategemewa kusaidia wananchi wazalishaji wa chumvi katika Majimbo ya Kilwa Kaskazini, Kilwa Kusini, Mchinga, Lindi Mjini, Mtama, pamoja na maeneo ya Mkoa wa Mtwara. Je, ni lini sasa kiwanda hiki kinatarajiwa kuanza kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kiwanda hiki kitakapokuwa kimeanza rasmi kitakuwa na uwezo wa kuchukua tani ngapi za chumvi na kuhifadhi kabla ya kwenda sokoni kwa walaji? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mbunge, kwa kutetea wachimbaji wa sekta hii ya chumvi, niseme tu kwamba kiwanda hiki kama nilivyojibu kwenye majibu ya msingi, kiwanda hiki kinatarajiwa kukamilika mwezi Agosti mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya swali lake la pili kwa sababu ni cha mfano na ni kielelezo cha jinsi ambavyo viwanda vidogo vya uchakataji chumvi vinaweza vikarudufiwa katika

maeneo mbalimbali nchini kwa wawekezaji wadogo na wakubwa, kwa hiki cha kuanzia cha mfano kinaweza kuchakata tani tatu kwa saa na kina uwezo wa kuzalisha mpaka tani 60 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa kuhifadhi, ghala za kuhifadhi chumvi pia zinaenda kujengwa kulingana na jinsi mradi huu ulivyokuwa umeratibiwa na *STAMICO*.

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi Mheshimiwa Dkt. Stephen Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali ya nyongeza. Katika Halmashauri ya Manyoni, Kata ya Majiri, Mheshimiwa Naibu Waziri alishafika na wameshafanya utafiti kuhusu mashapo ya chumvi. Je, nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba tunawajengea kiwanda wananchi wa Kata ya Majiri Manyoni? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Chaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipotambua uhitaji mkubwa wa viwanda vya kuchakata chumvi nchini tulianza na hatua ya kwanza ya kutengeneza kiwanda cha mfano ambacho ndicho hicho kinaendelea huko Lindi. Baada ya kumaliza Kiwanda cha Lindi, *STAMICO* sasa watatumia uzoefu walioupata katika kuendelea kujenga viwanda vya kuchakata chumvi katika maeneo ya wazalishaji wa chumvi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia pia fursa hii kuwaasa wawekezaji wa ndani na nje wenye uwezo wa kujenga mitambo ya kuchakata chumvi nchini waendelee kusikia umuhimu wa kwenda katika maeneo ya Manyoni huko Singida na maeneo mbalimbali nchini ambapo kuna mazao ya chumvi ambayo bado hayajapata viwanda stahiki vya kuchakata.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu, unaweza ukarejea.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la wageni ambao tunao leo asubuhi, kwanza ni wageni waliopo jukwaa la Spika. Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha ambao ni Ndugu Lisius Mwenda, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu; Ndugu Chotto Sendo; Mkurugenzi Usimamizi wa Mali za Serikali; Dkt. Johnson Nyella, Kamishna wa Uchambuzi wa Sera; Ndugu Deni Simba, Mkurugenzi Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma; na Ndugu Daniel Msolwa, Mkurugenzi Takwimu za Uchumi, Ofisi ya Taifa ya Takwimu. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tunao Wageni 50 wa Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Mipango na Uwekezaji, ambao ni wanafunzi wanaosoma Shahada ya Kwanza ya Sera na Mipango ya Usimamizi katika Elimu kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Namtumbo, Mkoa wa Ruvuma.

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu ambao ni dada zake kutoka Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, Mbunge ambao ni wadogo zake kutoka Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Tunao wageni 20 wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge ambao ni viongozi wa Jumuiya ya Wazazi kutoka Wilaya ya Mbozi, Mkoa wa Songwe na wafanyakazi wa Shule ya Msingi Iyula Malaika kutoka Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, ambao ni wanafunzi 75 wa Taasisi ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma *(UDOPSSO)* kutoka Chuo

Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. Wageni wetu wote kwa pamoja tunawakaribisheni Bungeni. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)* Kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024 na Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti Kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza kipindi chetu cha maswali na majibu sasa tupo kwenye hoja za Kamati na sasa ninamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)* ili kuwasilisha taarifa yake.

**MHE. VUMA A. HOLLE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ifuatayo ni Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)* kuhusu Shughuli za Kamati kwa Kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mungu kwa kutujaalia uhai na kuweza kufika siku ya leo, kutokana na ufinyu wa muda naomba taarifa hii yote kama inavyosomeka katika kitabu cha Kamati iingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)* kuhusu Shughuli za Kamati kwa Kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, imetekeleza majukumu yake ya

kufuatilia uwekezaji katika Mashirika na Taasisi za Umma na makampuni ambayo Serikali ina hisa chache, hivyo mjadala wa Bunge kwa mambo yanayobainishwa katika taarifa hii una umuhimu mkubwa katika kusimamia na kuishauri Serikali kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kusimamia matumizi ya mitaji ya umma ili tija ya uwekezaji iliyokusudiwa iweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inakusudia kueleza yatokanayo na shughuli za Kamati kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma na kuliwezesha Bunge kujadili hali na kufikia uamuzi kwa mfumo wa hoja Bungeni. Ili kufanikisha azma hiyo, taarifa hii inaelezea kwa undani shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Kamati kuanzia mwezi Februari, 2024 hadi mwezi Januari, 2025, kama inavyoelekezwa na Kanuni za Kudumu za Bunge. Aidha, shughuli zinazotolewa taarifa ni zile ambazo hazikuwepo kwenye taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni tarehe 29 Oktoba, 2023 wakati wa Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba Kamati ilitoa taarifa tarehe 29 Oktoba ya hali ya uwekezaji nchini kwa yale ambayo tuliyazungumza wakati ule hapa kwenye taarifa hii hayamo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa shughuli za Kamati. Msingi wa shughuli zote za Kamati hii ni utekelezaji wa Madaraka ya Bunge yaliyofafanuliwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Aidha, Ibara ya 63(2) ya Katiba imelipa Bunge jukumu la kusimamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya wananchi. Vilevile Kamati imezingatia Kanuni za Kudumu za Bunge Kifungu cha 11(1) na (2) cha Nyongeza ya Kanuni za Bunge na Sheria ya Msajili wa Hazina kwenye kipengele cha mamlaka na majukumu Sura ya 370.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia zilizotumika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge, naomba kubainisha njia na mbinu zilizotumika kufanikisha majukumu ya Kamati kama inavyoelekeza. Katika kutekeleza majukumu yake Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ilitumia njia mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Kupokea, kuchambua na kujadili taarifa ya utendaji ya taasisi na mashirika ya umma ya Msajili wa Hazina kuhusu ufanisi wa uwekezaji wa umma, kwa lengo la kutathmini hali ya uwekezaji, mgawanyo wa uwekezaji na marejesho ya uwekezaji. Uchambuzi wa taarifa hii uliwasilishwa kwenye taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni tarehe 29 Oktoba, 2024 wakati wa Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge.

(ii) Kupokea na kuchambua taarifa ya utendaji wa taasisi na mashirika ya umma ya Msajili wa Hazina kuhusu uwekezaji katika taasisi na mashirika ya umma, maana yake hapo tumekutana na taasisi mbalimbali tukapokea taarifa za utendaji wa taasisi hizo.

(iii) Kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya uwekezaji iliyotekelezwa na taasisi na mashirika ya umma katika kipindi cha mwezi Machi, 2024. Kamati ilifanya ziara katika taasisi na mashirika ya umma katika Mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, Mtwara na Morogoro. Miradi iliyotembelewa inaonekana kwenye kiambatanisho namba mbili cha taarifa hii.

(iv) Kushiriki mafunzo, semina na warsha mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na taasisi na mashirika ya umma na wadau mbalimbali. Kamati ilipata nafasi ya kushiriki mafunzo na semina hapa Dodoma na nje ya Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi wa utendaji wa mashirika na taasisi za umma zinazotumia mitaji ya umma. Katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari 2025, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa taarifa za utendaji wa taasisi na mashirika ya umma 56 kuhusu hali ya uwekezaji wa mitaji ya umma kwa taasisi hizo. Uchambuzi huu ulilenga kujiridhisha iwapo uwekezaji unaofanyika katika mashirika na taasisi hizo ni wenye ufanisi na iwapo tija ya uwekezaji inapatikana, matokeo ya uchambuzi huo yamefafanuliwa katika taarifa hii. Aidha, baadhi ya hoja zilizochambuliwa na Kamati zimekwisharipotiwa kwenye taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni mwezi Oktoba, 2024 iliyokuwa na jumla ya maazimio 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa jukumu la usimamizi wa mali za Serikali zilizorithiwa na Msajili wa Hazina kutoka Shirika Hodhi la Mashirika ya Umma *(CHC)*. Ofisi ya Msajili wa Hazina imerithi majukumu yaliyokuwa yakitekelezwa na Shirika Hodhi la Mashirika ya Umma - *CHC* kama ilivyoelekezwa kupitia tangazo la Serikali namba 203 iliyochapishwa tarehe 27 Juni, 2014. Kwa muktadha huu, Ofisi ya Msajili wa Hazina inatekeleza jukumu la urekebishaji na ubinafsishaji wa mashirika ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufuatiliaji na tathmini ya mashirika yaliyobinafsishwa, ukamilishaji na ufilisi wa mashirika ya umma, ukusanyaji wa madeni yatokanayo na ubinafsishaji pamoja na iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara na malipo ya madai mbalimbali kwa maana ya pensheni ya stahiki ya waliyokuwa wafanyakazi wa mashirika yaliyopitia urekebishaji au ubinafsishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifahamishwa hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa jukumu hili walilolirithi ikiwemo mashirika manne yaliyokuwa chini ya usimamizi yaani - *TPC, MSCCL, XL* na *NIC* kuweza kuvuka hatua na sasa yanaweza kujiendesha. Kurejesha viwanda 20 kutoka kwa wawekezaji waliyokiuka baadhi ya vipengele vya mikataba ya mauzo kati ya viwanda 20 viwanda tisa vimekabidhiwa kwa taasisi za Serikali kwa ajili ya kuviendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada mbalimbali zilizofanywa na Msajili wa Hazina, katika kutekeleza jukumu hili, Kamati imebaini kuwa ofisi bado haijakamilisha zoezi la kutathmini na kubaini mali zote zilizorithiwa aidha Kamati imebaini kuwa kuna mali ambazo tayari zimeshatambuliwa ila hazijawekewa utaratibu wa kuziendeleza, jambo ambalo limebaki kama mzigo kutokana na kuendelea kuharibika *(depreciation)* na kuiongezea ofisi gharama za ulinzi ambapo kwa miaka mitatu mfululizo iliyochambuliwa na Kamati, Ofisi ya Msajili wa Hazina imelipa kiasi cha takribani shilingi bilioni 1.218 kwa ajili ya ulinzi wa mali hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia uchambuzi uliofanyika na thamani ya mali zilizorithiwa kutoka *CHC*, Kamati ina maoni kuwa zifanyike jitihada za makusudi na kukamilisha uhakiki wa mali alizorithi kutoka *CHC* na iandaliwe mikakati ya

kuzitafutia utaratibu mahsusi wa kuziendeleza au kuzitumia ikiwemo kuzitafutia wawekezaji mahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tija ndogo katika uendeshaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam *(BRT)*. Wakala wa mabasi yaendayo haraka - *DART* ulianzishwa kwa madhumuni ya kuhakikisha Jiji la Dar es Salaam linakuwa na usafiri wa uhakika na wa haraka ili kuondokana msongamano wa magari pamoja na kutumia muda mrefu kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam kusafiri kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lengo la kutekeleza dhumuni hilo, ulibuniwa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam *(BRT)*, mradi huo ulikuwa chini ya wakala wa mabasi yaendayo haraka *DART* ili kusimamia mradi huo pamoja na miundombinu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kuchambua taarifa ya utekelezaji wa mradi huu na kubaini kuwa tija ya ufanisi wa mradi huu ni ndogo. Serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika awamu tatu, ambapo kwa awamu ya kwanza na ya pili zilitumika jumla ya shilingi bilioni 847.03 na awamu ya tatu zimetumika dola milioni 148.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati imebaini kuwa katika awamu hizo tatu, awamu ya kwanza Kimara kwenda Kivukoni imekamilika ila matumizi yake ni madogo. Awamu ya pili Mbagala Rangi Tatu kwenda katikati ya Jiji imekamilika kwa zaidi ya mwaka mmoja, lakini haijapata mwendeshaji. Awamu ya tatu ya barabara ya Azikiwe na Maktaba kwenda Gongo la Mboto imefikia 55% lakini mchakato wa kutafuta mwendeshaji haujaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati haioni jitihada za makusudi za kutumia au kuendesha Mradi huu wa *BRT* kwa ukamilifu wake licha ya Serikali kufanya uwekezaji huu mkubwa ambapo sehemu ya fedha inayotumika ikiwa ni fedha ya mkopo, jambo hili linafifisha juhudi kubwa inayofanywa na Serikali. Ni rai ya Kamati kuwa *DART* ihakikishe inapata watoa huduma kwa awamu zote tatu ili mradi huu uweze kuendeshwa kwa ukamilifu wake *(full*

*capacity)* ili tija ya uwekezaji wa mitaji ya umma iweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba tatu changamoto ya mizania ya Shirika la Ndege *(ATCL)*. Shirika la Ndege Tanzania lilianzishwa kwa lengo kuu la kutoa huduma ya usafiri wa anga ndani na nje ya nchi, malengo mengine ya kuanzishwa kwa *ATCL* ni kuwa na mwenendo chanya wa faida, kupanua wigo wa utoaji wa huduma, kuendeleza utoaji wa huduma kwa kuzingatia ubora na usalama na kuongeza mashirikiano na mashirika mengine ya ndege na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia njema ya Serikali katika kufanikisha malengo haya inaonekana, ambapo kwa miaka tisa tumeshuhudia Serikali ikifanya uwekezaji mkubwa kwa kuanza kununua ndege za shirika na hadi Disemba 2024 jumla ya ndege 15 zimenunuliwa tena kwa kutumia fedha taslimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kuchambua taarifa ya uwekezaji wa *ATCL* na kubaini kuwa hali ya kifedha ya shirika siyo ya kuridhisha ambayo imepelekea kuathiri mizania ya vitabu vya shirika. Kamati imebaini kuwa, gharama za uendeshaji za shirika ni kubwa na zimeendelea kukua kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo na hivyo kuathiri uwiano wa mapato na matumizi ya shirika, pia, kupelekea kuzalishwa kwa madeni na Shirika kupata hasara kwa miaka mitatu mfululizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukua kwa gharama uendeshaji wa Shirika imechangiwa na gharama za ukodishaji wa ndege kutoka *TGFA,* ambapo kutokana na utaratibu uliopo sasa wa *TGFA* ndiye mmiliki wa ndege za Serikali na *ATCL* inalazimika kuzikodi ndege hizo. Katika utekelezaji wa utaratibu huo wa ukodishaji wa ndege *ATCL* imesababishiwa kuzalisha madeni makubwa ambapo 95% ya madeni hayo ni madai ya *TGFA* kutokana na ukodishaji wa ndege hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ina taarifa kuwa Serikali inaendelea na mchakato wa kuhamisha ndege kutoka *TGFA* kuzileta *ATCL* ili kurahisisha utendaji wa *ATCL.* Hata hivyo

mchakato huu umechukua muda mrefu na hivyo *ATCL* inaendelea kuathirika kutokana na utaratibu uliopo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ina maoni kubwa Serikali iharakishe kukamilisha mchakato huu wa kuhamisha ndege kutoka *TGFA* kuja *ATCL* ili kulipunguzia Shirika gharama za uendeshaji. Jambo hili litawezesha Shirika pia kuweza kujitanua katika masoko au katika nchi ambazo kwa sasa hawawezi kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa utekelezaji wa miradi ya uwekezaji iliyotembelewa na Kamati. Mwezi Machi, 2024 Kamati ilianza ziara na kukagua miradi ya uwekezaji ili kujiridhisha kama kuna tija ya kuwekeza mitaji ya umma katika miradi hiyo. Ziara ilifanyika katika Mikoa saba ambayo ni Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, Mtwara na Morogoro ambapo jumla ya miradi 19 ilikaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi iliyotembelewa imegawanyika katika maeneo tisa ambayo ni Miradi ya Umeme, Miradi ya Maji, Miradi ya Bandari, Mradi wa Bomba ya Mafuta *(EACOP),* Miradi ya Ujenzi wa Vitega Uchumi na Miundombinu na Hali ya Uendeshaji wa *National Housing, PSSSF, TIA* na Stendi ya Msamvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Miradi ya Ujenzi wa Makazi na Ofisi ya *TBA* na *DAWASA,* Miradi ya Gesi Asilia, Mradi wa Reli ya Kisasa *SGR* na Miradi ya Uzalishaji Viwandani. Taarifa ya miradi hiyo inaonekana kwenye Taarifa kubwa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, miradi ya maendeleo iliyokaguliwa kwa kipindi cha mwezi Machi, 2024, Kamati ilitoa ushauri wa jumla ufuatao kwa Serikali:-

(i) Kuhakikisha madai ya wakandarasi yanalipwa kwa kuzingatia mikataba, jambo litakalowezesha Serikali kuepuka mlundikano wa madeni ya wakandarasi na ongezeko la gharama zitokanazo na riba. Wakandarasi wengi wanadai pesa Serikali hailipi kwa wakati na kwa hiyo, gharama za riba zinakuwa kubwa

na hivyo gharama za mradi zinaongezeka. Ni hela za walipa kodi Watanzania; mabilioni ya shilingi yanaenda kulipa riba kwa sababu ambazo siyo za msingi. *(Makofi)*

(ii) Kuhakikisha mipango ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati inazingatia mawanda ya malengo uazishwaji wa miradi ili iweze kutekelezwa kwa ufanisi kwa lengo la kupata tija stahiki.

(iii) Kuhakikisha Serikali inasimamia mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa kuhakikisha mifumo ya Mamlaka ya Mapato *(TRA)* na taarifa nyingine inasomana ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji na udhibiti wa mapato pamoja na kuweza kuwa na taarifa sahihi na halisi. Mifumo mingi ya Serikali haisomani ipo mingi haisomani, kwa hiyo, kupata taarifa halisi na sahihi ni changamoto.

(iv) Kuhakikisha usimamizi wa wakandarasi wanaotekeleza miradi unaimarishwa kwa lengo la kuitekeleza kwa ufanisi na kukamilisha kwa wakati ili iweze kutoa tija iliyokusudiwa na kwa wakati. Wakandarasi wengi sana wanaomba kuongezewa muda kwenye miradi. Jambo hili ni changamoto, miradi haikamiliki kwa wakati.

(v) Kuhakikisha mchakato wa kupata wakandarasi wa utekelezaji wa miradi ya uwekezaji unazingatia ushirikishaji wa wakandarasi wazawa, hususani kwenye miradi ya kimkakati ili waweze kupata ujuzi;

Hapa ipo miradi ya kimkakati ambayo tunaendelea nayo kama Taifa, unakuta ushiriki wa Watanzania kwenye miradi hiyo ni mdogo na ni hafifu. Ni changamoto kwa sababu tunashindwa kuwa na uhakika kwamba baada ya wakandarasi hao kukamilisha miradi hiyo nani ambaye atabaki anafanya *maintenance* ya miradi hiyo; ni changamoto kubwa. Hata kuna sehemu nyingine unakuta kazi ambazo Watanzania wanaweza kuzifanya wanapewa wageni. *(Makofi)*

(vi) Mwisho, kuhakikisha mpango wa uwajibikaji kwa jamii *(CSR)*uliopitishwa kwa mujibu wa taratibu unasimamiwa kwa ufasaha ili wakandarasi wautekeleze ipasavyo na hivyo jamii

kutambua manufaa ya miradi; jambo litakaloimarisha ulinzi na uendelevu wa miradi husika. Hasa kwenye bomba la mafuta pale *CSR* ilikuwa ni ovyo kabisa; tulipiga makelele sana pale, ilikuwa ni vichekesho. Ukiangalia *CSR* ambazo walikuwa wanatoa ilikuwa ni changamoto kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki katika semina na warsha mbalimbali, katika kipindi cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati, Wajumbe walipata fursa ya kushiriki katika semina na warsha mbalimbali ambazo zililenga kuwajengea uwezo. Kamati inawashukuru wadau wote ambao walijitokeza katika kutoa semina za mafunzo na kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati. Tulijifunza mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya Kamati; kutokana na uchambuzi na ufuatiliaji wa uwekezaji wa mitaji ya umma uliofanywa na Kamati, yapo mambo maalum yanayotolewa maoni na mapendekezo kwa madhumuni ya kulisaidia Bunge kujadili na kuamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla kutokana na uchambuzi uliofanyika kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati. Baada ya kueleza shughuli za Kamati na maoni ya jumla, ninaomba kutoa mapendekezo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kukosekana kwa Kiwanda cha Uzalishaji katika Kampuni ya Mbolea *(TFC);*

KWA KUWA, mtaji wa umma unaotumika katika kampuni ya mbolea Tanzania una lengo la kuwezesha uzalishaji wa mbolea kwa kiwango cha kutosheleza mahitaji nchini na kuuza nje ya nchi, lakini mtaji huo hautumiki hivyo kutokana na kukosekana kwa kiwanda cha uzalishaji wa mbolea;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania hatuna kiwanda cha mbolea ila tunavyo viwanda vya kufanya *blending* kuchanganya mbolea. Kama kawaida tulikutana na *TFC;* kimsingi mbolea *UREA* ambao ndio kama mbolea mama ya kutengenezea mbolea nyingine tunaagiza na Tanzania inatumia zaidi ya dola bilioni 500 kwa ajili ya kuagiza mbolea ya *UREA* peke yake kila mwaka; lakini

ukiangalia gharama za kujenga kiwanda cha mbolea cha *UREA study* zinaonesha kwamba; na wao wenyewe walikiri zina-*range* kuanzia dola milioni moja mpaka dola milioni 1.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake nini; kama tukiamua kujenga kiwanda cha mbolea na tunaweza kwa sababu tumejenga miradi mikubwa sana kama Taifa; tukiamua kujenga kiwanda cha mbolea tunaweza dola milioni moja ni kama trilioni 2.7 mpaka trilioni 3.0. Tunaweza kujenga kiwanda siyo tu tutaokoa fedha za kigeni, lakini pia tutaweza ku-*export* mbolea kwa majirani; maana hapa *East Africa* hakuna ambaye ana kiwanda cha mbolea. *(Makofi)*

NA KWA KUWA, kukosekana kwa kiwanda cha uzalishaji mbolea kunasababisha *TFC* iagize mbolea kutoka nje ya nchi jambo linaloongeza gharama kwa *TFC* na kukwamisha manufaa ya mtaji unaowekezwa;

HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia *TFC* kwa kushirikiana na Sekta binafsi ijenge kiwanda cha kuzalisha mbolea kwa lengo la kuipunguzia Serikali mzigo wa gharama inayoingia katika kuagiza mbolea, na kuiwezesha *TFC* kutekeleza malengo mahususi ya kuanzishwa kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutotekelezwa ipasavyo kwa majukumu yaliyorithiwa kutoka Shirika Hodhi la Mashirika ya Umma – *CHC*

KWA KUWA, Msajili wa Hazina alipewa majukumu ya iliyokuwa *CHC* ili kuendeleza usimamizi wa mitaji, urekebishaji, ufuatiliaji na tathmini ya mali za umma lakini

(i) Hajakamilisha tathmini ya mali alizokabidhiwa kutoka *CHC* jambo ambalo linalosababisha watu kutumia mali hizo kwa manufaa binafsi;

(ii) Hawajatafutwa wawekezaji wanaoweza kubinafsishiwa au kukodishiwa mali hizi zilizotathminiwa; na

(iii) Yapo mashamba yaliyofanyiwa tathmini na hayatumiki na taasisi nyingine za umma zinahitaji kwa shughuli nyingine kama vile kiuchumi, utafiti na kilimo. Kwa mfano, kama *ASA* wanahitaji mashamba kwa ajili ya kuzalisha mbegu. Wao wanazalisha *potion* ndogo sana ya *market* ya mbegu. Wanataka mashamba makubwa zaidi ili wazalishe mbegu zaidi na hivyo waweze ku-*compete* na wauza mbegu wengine. Kwa hiyo, hakuna tija tena ya Msajili wa Hazina au Serikali kuendelea kushikilia mashamba hayo wakati Taasisi za Serikali, Hazina mashamba ya kutosha. *(Makofi)*

NA KWA KUWA, mambo hayo yanasababisha

(i) Ofisi ya Msajili wa Hazina kuingia gharama za utunzaji wa mali zinazosimamiwa bila matumizi yoyote; Tumesema ulinzi zaidi ya shilingi bilioni moja;

(ii) Uchakavu wa mali kutokana na kuchelewa kwa mchakato wa kupata wawekezaji; Tulikwenda pale Morogoro kwenye kile Kiwanda cha *MOPROCO*. Kwenye kile kiwanda kwa kweli miundombinu inaharibika majengo yanaharibika, lakini hamna kazi yoyote uchakavu unaongezeka hakuna chochote ambacho kinafanyika. *(Makofi)*

(iii) Kukosekana kwa manufaa ya mali zilizofanyiwa tathmini na ambayo yanaweza kutumika kwa shughuli nyingine;

(iv) Kuingia gharama za ulinzi bila manufaa kwa umma kutokana na kuendelea kwa migogoro baina ya Serikali na wawekezaji binafsi.

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali kupitia Msajili wa Hazina ikamilishe tathmini ya kubaini mali zote zilizorithiwa kutoka *CHC* na ziwe chini ya uangalizi wake;

(ii) Kwa mali zinazoweza kutolewa kwa wawekezaji ufanyike mchakato wa haraka wa kutafuta wawekezaji ili ziweze kuendelezwa na kutumika, ili kuondoa mzigo wa gharama za ulinzi ambazo zinalipwa huku zikiwa hazizalishi;

(iii) Mashamba yaliyokuwa chini ya uangalizi wa Msajili wa Hazina yakabidhiwe kwa taasisi za Serikali zenye uhitaji hususan taasisi za Utafiti na Kilimo; *(Makofi)*

(iv) Kwa mali ambazo bado zina migogoro na wawekezaji wake wa awali, kwa mfano hiyo *MOPROCO* na *Tembo Chip Board,* Serikali ikamilishe mchakato wa majadiliano na wawekezaji ili mali hizo zianze kutumika na kuzalisha. Tulikuta kuna kesi zipo Mahakamani.

(v) Sasa tukisema twende na mlengo huu wa Mahakamani inaweza ikatuchukua muda kidogo na uchakavu kwenye uwekezaji huo unaendelea. Ni afadhali Serikali ichague namna ya kwenda ya majadiliano ili waweze kumaliza migogoro hiyo kwa haraka na hatimaye kuepusha uchakavu ambao unaweza kuendelea kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa kuhusu tija ndogo katika uendeshaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam *(BRT)*

KWA KUWA, Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi Dar es Salaam unakabiliwa na changamoto kama vile:-

(i) Upungufu wa mabasi kwa awamu ya kwanza (Kimara – Kivukoni) yenye mabasi 100 yanayofanya kazi badala ya 305;

(ii) Kuchelewa kukamilika kwa mchakato wa kumpata mwendeshaji katika awamu ya pili (Mbagala Rangitatu – katikati ya Jiji);

NA KWA KUWA,

(i) Changamoto hizo zisipotatuliwa, mtaji mkubwa wa umma uliotumika katika ujenzi wa miundombinu utakuwa umepotea;

(ii) Mkopo wa fedha uliotafutwa kwa ajili ya kuwekeza kwenye miundombinu hiyo utarejeshwa bila ya manufaa ya uwekezaji kupatikana;

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali isimamie kikamilifu uendeshaji wa mradi huu kwa kuhakikisha awamu zote zilizokamilika zinaendeshwa kwa ufanisi kwa lengo la kupata tija ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali katika mradi huu ikizingatiwa kuwa sehemu ya fedha za kutekeleza mradi huu ni fedha za mkopo na zitahitajika kurejeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa mawasiliano ya barabara katika stesheni za mizigo kwenye reli ya kisasa *(SGR)*:-

KWA KUWA, chumo *(returns)* kutokana na mtaji mkubwa uliowekezwa katika *SGR* linategemea takribani 90% kutokana na usafirishaji wa mizigo na kwamba usafirishaji huo unategemea muunganiko wa reli na barabara; Tunategemea kwamba kama mizigo ikianza ku-*operate* 90% ya mapato ya reli yote yanatokana na mizigo; ndiyo *study* inaonesha duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa reli hii ya kwetu ambayo inabeba abiria inabeba na mizigo mara nyingi 90% ya mapato yake huwa yanatokana na mizigo halafu 10 inayobaki ya abiria.

NA KWA KUWA, kukosekana kwa miundombinu ya reli na barabara kunapunguza uwezekano wa kupata ufanisi wa *SGR* katika kuwezesha chumo la uwekezaji; maana hapa hakuna barabara ambazo zina-*connect* kati ya hizi stesheni za mizigo na reli. Lazima tuwe na barabara hizi. *Feeder roads* za kutoka kwenye *stations* za mizigo kwenda kwenye barabara kubwa.

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia *TARURA* na *TANROADS* iweke miundombinu wezeshi kwa maeneo yote

yenye stesheni za mizigo kwa ajili ya kufanikisha mawasiliano ya stesheni hizo na barabara za kusafirisha mizigo pindi inapofika. Walisema wataanza kusafirisha mizigo nadhani mwaka huu mwanzoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kusuasua kwa Matumizi ya Mtaji wa Umma katika Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania – *TEMESA:*

KWA KUWA, mtaji wa umma uliowekezwa kwa Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania ulilenga kuwezesha huduma za kiufundi kwa magari na mitambo ya Serikali;

NA KWA KUWA, mtaji wa uendeshaji wa *TEMESA* ulikaribia kwisha kwa 90% ambapo uliporomoka kutoka shilingi bilioni 19.8 mwaka 2021/2022 hadi shilingi billioni 1.9 mwaka 2022/2023, jambo linalosababisha kusuasua kwa matumizi ya mtaji wa umma. Hawa mwaka huu wa shilingi bilioni 19.8, halafu *the next* mwaka wa fedha wako na bilioni 1.9, wameporomoka mtaji kwa 90%.

NA KWA KUWA, hiyo ni ishara ya kudorora kwa *TEMESA* jambo linalohitaji mageuzi makubwa na mabadiliko ya sheria.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:

(a) Serikali kupitia Msajili wa Hazina ifanye mapitio ya *TEMESA* na uandaliwe mpango wa mageuzi kwa lengo la kufufua taasisi na kuiwezesha kujiendesha kwa ufanisi zaidi; na

(b) Serikali ifanye mabadiliko ya sheria na *TEMESA* iingizwe katika taasisi zinazojiendesha kibiashara kwa kuzingatia kuwa aina ya huduma inazotoa ni huduma zinazohitajika sokoni kwa ujumla na si kwa Serikali tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto ya mizania ya Shirika la Ndege Tanzania *(ATCL)*:

KWA KUWA, imebainika kuwa *ATCL* inakabiliwa na changamoto kubwa ya mizania ya hesabu zake kuwa vibaya,

hali inayotokana na kuendelea kukodi ndege kutoka *TGFA* na kubebeshwa mzigo wa malipo ya matengenezo na ukodishaji;

NA KWA KUWA, jambo hili linasababisha hali ya fedha ya shirika kutoakisi uhalisia na kuvuruga uwezo wa shirika kukopa kwa ajili ya kuendelea kibiashara;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali ikamilishe mchakato wa kuhamisha ndege kutoka *TGFA* kuja *ATCL* hadi kufikia Juni, 2025 ili kulipunguzia shirika gharama za uendeshaji na kuweza kujitanua katika masoko/nchi ambazo kwa sasa haiwezi kufika; na

(ii) Serikali ifanye mchakato wa kufuta madeni ya *TGFA* kwa *ATCL* kwa lengo la kuweka sawa mizania ya vitabu vya shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Bima la Taifa – *NIC* kuajiri kwa njia ya mkataba badala ya kuwa na ajira za moja kwa moja *(Permanent and Pensionable)*

KWA KUWA, manufaa ya mtaji wa umma unaowekezwa katika uwekezaji yanategemea uwezo wa watumishi wanaoajiriwa katika taasisi hizo;

NA KWA KUWA, shirika la bima limebainika kukosa mkakati bora wa ajira ya watumishi kwa ajili ya uendeshaji wa shirika, jambo linalosababisha:-

(i) Kutumia utaratibu wa kuajiri kwa mikataba ya muda mfupi; na

(ii) Shirika kuwa na watumishi wasiokuwa na uhakika wa ajira yao jambo linaloathiri uwezo wao wa kiutendaji. Wale asilimia kubwa ya wafanyakazi wa *NIC* wanapewa ajira za mkataba. Kwa hiyo, hata *confidence* ya kuwapeleka masomoni wasome wajiendeleze shirika halina, lakini wao wenyewe hawana uhakika wa kesho yao. Kwa hiyo, inaathiri sana utendaji wa shirika.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Msajili wa Hazina isimamie na kuhakikisha *NIC* inapata vibali vya kuwa na watumishi wa ajira za kudumu kwa lengo la kuleta tija katika usimamizi wa mtaji wa umma uliowekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto katika kutumia mfumo wa manunuzi wa *NEST* kwa mashirika ya kibiashara;

KWA KUWA, taasisi zote za umma yakiwemo mashirika ya umma yanayotumia mtaji wa umma kujiendesha kibiashara yanalazimika kutumia mfumo wa ununuzi wa *NEST* ambao una mlolongo usioendana na kasi ya kushindana kibiashara;

Unataka kununua kitu unafuata mfumo wa *NEST* halafu mwenzako ambaye unashindana naye *private sector* haendi kuwa *NEST,* hatimaye wewe ule mlolongo unakuchelewesha kupata kile ambacho unakitaka; halafu unakuta unakuja kupata *approval* ya kuendelea mwenzako ameshaenda. *(Makofi)*

NA KWA KUWA, masharti hayo kwa taasisi zinazotumia mtaji wa umma kujiendesha kibiashara yanazinyima uwezo wa kutumia mitaji ya umma ipasavyo kushindana kibiashara na hivyo;

(i) Kukosa ufanisi katika uendeshaji wa mitaji ya umma; na

(ii) Kutomudu ushindani katika tasnia za biashara zake.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye maboresho ya Kanuni hizi ili ziweze kuleta uhalisia na wepesi na kukidhi mahitaji ya wakati kwa mashirika ya umma yanayofanya biashara ili kuweza kutumia mfumo wa manunuzi kwa wepesi na haraka na kuyawezesha kuchangamkia fursa za biashara pale zinapojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Spika binafsi kwa uongozi wake makini wa kuliongoza Bunge letu Tukufu ikiwa ni pamoja na kunipa fursa ya kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. Utekelezaji wa majukumu ya Kamati umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na maelekezo ya kiti chake ikiwa ni pamoja na ushauri, miongozo na

msaada aliotupatia kwa kipindi chote cha mwaka mzima. Pia, naomba nimshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kutusaidia katika kuendesha Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha kunakuwa na usimamizi bora katika Taasisi na Mashirika ya Umma na kuweka msukumo wa hali ya juu katika kuimarisha uwekezaji wa Mitaji ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hii ni moja ya sababu baada ya kuona Taasisi za Umma zinaenda vizuri, zina-*improve* kuanzia *TRC*, *TANESCO*, ndiyo maana hata wana-CCM wameamua kwa kauli moja kumpitisha Mheshimiwa Rais kuwa mgombea wa Chama cha Mapinduzi na Katibu Mkuu kuwa mgombea mwenza. Nichukue nafasi hii kumpongeza na kumtakia kila la heri kwenye uchaguzi wa mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha, nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati na kunipa heshima ya kuiwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwatambua Wajumbe kwa majina yao kama yanavyoonekana kwenye taarifa, lakini kutokana na changamoto ya muda naomba nisiyasome ila naomba yaingie kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge. Wamefanya kazi kubwa sana watu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba kuwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Msajili wa Hazina wakiongozwa na Ndugu Nehemia Mchechu, Msajili wa Hazina kwa ushirikiano wa dhati walioutoa kwa Kamati. Wamesaidia kushauri namna bora ya kuzifanya taasisi na Mashirika ya Umma kuwa na ufanisi katika utendaji na uwekezaji wake kwa lengo la kuleta tija ya uwekezaji wa Serikali katika vitega uchumi vyake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Ildephonce Leonard kwa ushirikiano walioutoa ukiwa ni pamoja na kutoa ushauri stahiki ili kuwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa shukrani, lakini siyo kwa udogo, nawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kasulu Vijijini kwa kuendelea kuniamini kuwa Mbunge wao na kunivumilia wakati ambapo natekeleza majukumu ya Kamati. Niwakumbushe tu kuwa mwaka huu ni mwaka 2025, tuna jambo letu. Mbunge wao nipo imara, na nipo tayari kuwatumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja. Taarifa hii imetokana na uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)* kuhusu utekelezaji na usimamizi wa uwekezaji wa mitaji ya umma unaofanywa na taasisi na mashirika ya umma. Maoni na mapendekezo yanayotokana na uchambuzi huu, yanalenga kuishauri Serikali katika eneo la uwekezaji wa mitaji ya umma ili uwekezaji uweze kufanyika kwa ufanisi na hatimaye kuleta tija kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa liipokee Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuhusu Uchambuzi wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Kipindi cha Mwaka 2024, kuijadili na hatimaye kuridhia maoni na mapendekezo yake ili Serikali iweze kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**10 FEBRUARI, 2025**

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC) KUHUSU SHUGHULI ZA KAMATI KWA MWAKA 2023 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

*(Inatolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023*)

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kuhusu Shughuli za Kamati kwa kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025. Kanuni hiyo inailazimisha Kamati kuwasilisha Bungeni Taarifa ya Mwaka ya Shughuli zake, kwa madhumuni ya kujadiliwa katika Mkutano wa mwisho wa Bunge kabla ya Mkutano wa Bajeti. Mkutano huu wa Bunge ulioanza tarehe 28 Januari, 2025 ndio Mkutano wa mwisho wa Bunge kabla ya Mkutano wa Bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma imetekeleza majukumu yake ya kufuatilia uwekezaji katika Mashirika na Taasisi za Umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa. Hivyo, mjadala wa Bunge kwa mambo yanayobainishwa katika Taarifa hii una umuhimu mkubwa katika kuisimamia na kuishauri Serikali kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kusimamia matumizi ya mitaji ya umma ili tija ya uwekezaji iliyokusudiwa iweze kupatikana.

**Mheshimiwa Spika**, Ili kufuatilia vizuri mtiririko wa Taarifa hii naomba kueleza kwa ujumla kuhusu madhumuni na mawanda yake kama ifuatavyo: -

**10 FEBRUARI, 2025**

### 1.1.1 Madhumuni

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii inakusudia kueleza yatokanayo na shughuli za Kamati kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma na kuliwezesha Bunge kujadili hali hiyo na kufikia uamuzi kwa mfumo wa hoja Bungeni. Ili kufanikisha azma hiyo, Taarifa hii inaelezea kwa undani shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Kamati kuanzia mwezi Februari, 2024 hadi mwezi Januari, 2025 kama inavyoelekezwa na Kanuni za Kudumu za Bunge. Aidha, shughuli zinazotolewa taarifa ni zile ambazo hazikuwemo kwenye Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni tarehe 29 Oktoba, 2024 wakati wa Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge.

### 1.1.2 Mawanda (Scope)

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu Shughuli za umma zinazosimamiwa na Serikali kwa kutumia mtaji wa umma, Taarifa hii inagusa masuala yafuatayo: -

(i) Hali ya Mitaji ya Umma na Uwekezaji katika Mashirika ya Umma, Wakala za Serikali au Taasisi nyingine ya Umma; na

(ii) Hali ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma katika vitega uchumi (*investments*) ambapo Serikali ina hisa chache.

## 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inawasilishwa kukidhi masharti ya Kanuni za Bunge, Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge imeweka muundo wa Taarifa hii ambapo inaelekeza kuwa Taarifa iwe na sehemu tatu. Taarifa hii inazingatia sharti hilo na imegawanyika katika sehemu tatu zifuatazo: -

(i) Sehemu ya kwanza ambayo inatoa maelezo ya jumla, madhumuni ya taarifa, msingi wa Shughuli za Kamati na njia zilizotumika;

(ii) Sehemu ya pili ambayo inaeleza Shughuli za Kamati na mambo yaliyobainika. Aidha, sehemu hii inafafanua matokeo ya uchambuzi wa taarifa za uwekezaji wa mitaji ya umma; na

(iii) Sehemu ya tatu inayobainisha maoni ya jumla na mapendekezo ya kutatua changamoto zilizobainika. Sehemu hii pia imehitimisha na kutoa hoja.

## 1.3 Msingi wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa shughuli zote za Kamati hii ni utekelezaji wa madaraka ya Bunge yaliyofafanuliwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977. Aidha, Ibara ya 63 (2) ya Katiba imelipa Bunge jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya wananchi. Vilevile, Kamati imezingatia Kanuni za Kudumu za Bunge na Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu), Sura ya 370.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 11(1) na (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kimebainisha majukumu ya Kamati ambayo ni: -

(i) Kuchambua na kubaini iwapo utekelezaji wa miradi ya uwekezaji wa umma una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu na sheria na miongozo mujarabu ya biashara; na

(ii) Kuchambua na kujadili taarifa zinazohusu uwekezaji katika mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa.

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa kazi za Kamati unatokana na taarifa zinazohusu uwekezaji katika mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa. Katika utekelezaji wa shughuli hizo, Kamati imezingatia: -

(i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;
(ii) Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011;
(iii) Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001;
(iv) Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370;
(v) Sheria ya Mashirika ya Umma ya Mwaka 1992; na
(vi) Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na miongozo hiyo, Kamati ilipokea taarifa za uwekezaji wa mitaji ya umma kwa kila shirika na taasisi kadiri zilivyopangwa kulingana na matokeo ya mapitio ya taarifa kuu za Msajili wa Hazina. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa, uchambuzi wa taarifa hizo umeiwezesha Kamati kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma kama inavyoripotiwa.

### 1.4 Njia zilizotumika (Methodology)

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge, naomba kubainisha njia na mbinu zilizotumika kufanikisha majukumu ya Kamati kama inavyoelekeza. Katika kutekeleza majukumu yake Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ilitumia njia mbalmbali kama ifuatavyo: -

(i) Kupokea, kuchambua na kujadili taarifa ya Utendaji ya taasisi na mashirika ya umma ya Msajili wa Hazina kuhusu Ufanisi wa Uwekezaji wa Umma, kwa lengo la kutathimini hali ya uwekezaji, mgawanyo wa uwekezaji na marejesho ya uwekezaji. Uchambuzi wa taarifa hii uliwasilishwa kwenye Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni tarehe 29 Oktoba, 2024 wakati wa Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge.

(ii) Kupokea, kuchambua na kujadili taarifa ya Utendaji wa taasisi na mashirika ya umma ya Msajili wa Hazina kuhusu uwekezaji katika taasisi na mashirika ya umma. Katika kutekeleza hili, kamati ilikutana na taasisi na mashirika ya umma yapatayo hamsini na sita (56). Orodha ya taasisi na mashirika hayo ni kama inavyoonekana katika Kiambatisho Na.01 **cha taarifa hii**

(iii) Kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya uwekezaji iliyotekelezwa na taasisi na mashirika ya umma. Katika kipindi cha mwezi Machi, 2024, kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa miradi ya uwekezaji inayotekelezwa na taasisi na mashirika ya umma katika mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, Mtwara na Morogoro. Mantiki ya ukaguzi huo ni kuiwezesha kamati kufanya tathmini ya utekelezaji wa mradi husika pamoja na kubaini tija ya uwekezaji unaotekelezwa na taasisi hizo. Miradi

iliyotembelewa inaonekana katika **Kiambatisho Na. 02** cha Taarifa hii; na

(iv) Kushiriki mafunzo, semina na warsha mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na taasisi na mashirika ya umma na wadau mbalimbali.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI

### 2.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa madhumuni ya utaratibu wa kuripoti shughuli za Kamati ni kuliwezesha Bunge kubaini mambo ya kupatiwa ufumbuzi, napenda kubainisha Shughuli zilizotekelezwa. Aidha, nabainisha mambo yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa shughuli hizo ili kuliwezesha Bunge kuyajadili.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia dhima na majukumu ya Kamati hii, Shughuli zinazoripotiwa pamoja na yaliyojitokeza zinahusu uwekezaji wa mitaji ya umma. Shughuli hizo ni kama ifuatavyo: -

(i) Uchambuzi wa taarifa ya Utendaji ya Msajili wa Hazina kuhusu Ufanisi wa Uwekezaji wa Umma na taarifa za uwekezaji wa mitaji ya umma kwa taasisi na mashirika ya umma kwa lengo la kubaini iwapo uwekezaji huo una ufanisi na kwamba, umezingatia taratibu, sheria na miongozo mingine mujarabu ya biashara kama inavyoelekezwa na kifungu cha 11(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge;

(ii) Ziara za ufuatiliaji na ukaguzi wa miradi ya uwekezaji wa umma kwa lengo la kubaini iwapo utekelezaji wake unazingatia miongozo ya uwekezaji wa umma; na

(iii) Kupata mafunzo mbalimbali yanayohusu uwekezaji wa mitaji ya umma yaliyotolewa na taasisi na mashirika mbalimbali ya umma. Mafunzo hayo yameiwezesha Kamati kutoa ushauri kwa

taasisi hizo kwa lengo la kuboresha utendaji wao na kupata tija inayokusudiwa.

## 2.2 Uchambuzi wa Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa taarifa za utendaji wa taasisi na mashirika ya umma hamsini na sita kuhusu hali ya uwekezaji wa mitaji ya umma kwa taasisi hizo. Kamati ilitekeleza jukumu hili kwa lengo la kuliwezesha Bunge kujiridhisha iwapo uwekezaji uliofanywa na Serikali katika taasisi na mashirika hayo una tija na kama umezingatia sheria, taratibu na miongozo mbalimbali ya biashara.

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya hoja na masuala yaliyochambuliwa kwa kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025 yamekwisharipotiwa kwenye taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni mwezi Oktoba, 2024, iliyokuwa na jumla ya maazimio kumi (10), Kamati inaendelea na ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio hayo.

## 2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Utendaji wa Mashirika na Taasisi za Umma Zinazotumia Mitaji ya Umma

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua utendaji wa taasisi na mashirika ya umma ili kujiridhisha iwapo uwekezaji unaofanyika katika mashirika na taasisi hizo ni wenye ufanisi na iwapo tija ya uwekezaji inapatikana. Matokeo ya uchambuzi huo yalionesha mambo yafuatayo: -

### 2.3.1 Changamoto ya upatikanaji wa Mbolea Nchini na gharama kubwa inayoingia Kampuni ya Mbolea TFC katika kuagiza Mbolea nje ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati kwa taarifa ya uwekezaji wa Kampuni ya Mbolea Tanzania – *TFC* pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania – *TFRA* ulibaini kuwa, kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo Nchi yetu imeingiza jumla ya tani 1,708,153 za mbolea (mwaka 2020/21 tani 504,122, mwaka 2021/22 tani 379,927 na mwaka 2022/23 tani 824,104). Aidha, Nchi

ilitumia jumla ya shilingi 1.007 trilioni kwa ajili ya kugharimia mbolea hiyo (mwaka 2020/21 Tsh 157,432,378,000, mwaka 2021/22 kiasi cha Tsh 233,475,984,000 na mwaka 2022/23 kiasi cha Tsh 616,250,605,000).

**Mheshimiwa Spika,** kwa takwimu hizi inadhihirisha kuwepo kwa umuhimu na uhitaji mkubwa wa mbolea nchini lakini pia inabainisha kuwa tunatumia pesa yetu kuchagiza uchumi wa nchi nyingine (uchumi wa nje) ikiwa ni pamoja na kuchochea uzalishaji na pato la taifa kwa mataifa (GDP) na kuwatengenezea ajira. Aidha, kwa sababu zilizokuwa nje ya uwezo wetu kwa baadhi ya nyakati, mbolea imekuwa haifiki kwa wakati hivyo kupishana na misimu ya kilimo jambo ambalo huathiri shughuli za kilimo na kusababisha wakulima wetu kupata tija ndogo.

**Mheshimiwa Spika,** TFC ilishawahi kufanya shughuli za uzalishaji wa mbolea nchini ambapo ilizalishwa kwa ufanisi na kuweza kutosheleza soko la ndani, vilevile kuuza nje tena kwa bei ambayo ni himilivu na iliyokuwa ikikidhi uwezo wa wakulima wetu. Ni maoni ya Kamati kuwa ufumbuzi wa kudumu wa suala hili ni kujenga kiwanda nchini cha kuchakata mbolea kwa lengo la kupunguza gharama itokanayo na uagizaji wa mbolea. Jambo hili litapunguza bei ya mbolea, kuleta unafuu kwa wakulima na kuongeza ufanisi na tija ya kilimo nchini.

### *2.3.2* Utekelezaji wa Jukumu la Usimamizi wa Mali za Serikali zililorithiwa na Msajili wa Hazina kutoka Shirika Hodhi la Mashirika ya Umma – *CHC*

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Msajili wa Hazina imerithi majukumu yaliyokuwa yakitekelezwa na Shirika Hodhi la Mashirika ya Umma (CHC) kama ilivyoelekezwa kupitia Tangazo la Serikali Na.203 lililochapishwa tarehe 27 Juni, 2014. Kwa muktadha huu Ofisi ya Msajili wa Hazina inatekeleza jukumu la Urekebishaji na Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma; Ufuatiliaji na Tathmini ya mashirika yaliyobinafsishwa; Ukamilishaji wa Ufilisi wa Mashirika ya Umma; Ukusanyaji wa madeni ya yaliyotokana na Ubinafsishaji pamoja na ya iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara; na Malipo ya madai mbalimbali (Pensheni na Stahiki) ya waliokuwa

wafanyakazi wa Mashirika yaliyopitia Urekebishaji au/na Ubinafsishaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifahamishwa hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa jukumu hili walilolirithi ikiwemo mashirika 4 yaliyokuwa chini ya usimamizi (de-specification) - TPC, MSCL, ATCL na NIC kuweza kuvuka hatua hiyo na sasa yanweza kujiendesha; kurejesha viwanda 20 kutoka kwa wawekezaji waliokiuka baadhi ya vipengele vya Mikataba ya Mauzo. Kati ya viwanda hivyo 20, viwanda Tisa (9) vimekabidhiwa kwa taasisi za Serikali kwa ajili ya kuviendeleza.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Msajili wa Hazina katika kutekeleza jukumu hili Kamati imebaini kuwa Ofisi hii bado haijakamilisha zoezi la kutathimini na kubaini mali zote zilizorithiwa. Aidha, Kamati imebaini kuwa kuna mali ambazo tayari zimeshatambuliwa ila hazijawekewa utaratibu wa kuziendeleza jambo ambalo zimebaki kama mzigo kutokana na kuendelea kuharibika (*depreciation*) na kuiongezea Ofisi gharama za ulinzi ambapo kwa miaka mitatu mfululizo iliyochambuliwa na Kamati Ofisi imelipa kiasi cha takribani shilingi bilioni 1.218 kwa ajili ya ulinzi wa mali hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia uchambuzi uliofanyika na thamani ya mali zilizorithiwa kutoka CHC, Kamati inamaoni kuwa zifanyike jitihada za makusudi za kukamilisha uhakiki wa mali alizorithi kutoka CHC na iandaliwe mikakati kuzitafutia utaratibu mahususi wa kuziendeleza/kuzitumia ikiwemo kuzitafutia wawekezaji mahiri.

### 2.3.3 Tija ndogo katika uendeshaji wa Mradi wa Mabasi yaendeyo Haraka Dar es Salaam (BRT)

**Mheshimiwa Spika**, Wakala wa mabasi yaendayo haraka – *DART* ulianzishwa kwa madhumuni ya kuhakikisha Jiji la Dar es Salaam linakuwa na usafiri wa uhakika na waharaka ili kuondokana na msongamano wa magari pamoja na kutumia muda mrefu kwa wakazi wa jiji la Dar es Salaam kusafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Kwa lengo la kutekeleza dhumuni hilo ulibuniwa mradi wa mabadi yaendayo haraka Dar es Salaam (BRT). Mradi

huo uliwekwa chini ya Wakala wa mabasi yaendayo haraka (*DART)* ili kusimamia mradi pamoja na miundombinu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kuchambua taarifa za utekelelezaji wa mradi huu na kubaini kuwa tija na ufanisi wa mradi huu ni ndogo. Serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika awamu tatu ambapo jumla ya shilingi bilioni 847,030,979,399 kwa awamu ya kwanza na ya pili zimetumika na US Dollar 148.2 kwa awamu ya tatu.

Aidha, Kamati imebaini kuwa katika Awamu hizo 3, Awamu ya kwanza Kimara -Kivukoni imekamilika ila matumizi yake ni madogo, Awamu ya Pili Mbagala Rangitatu – Katikati ya jiji imekamilika kwa zaidi ya mwaka mmoja lakini haijapata mwendeshaji na Awamu ya Tatu ya Azikiwe na Maktaba - Gongolamboto imefikia asilimia 55 lakini mchakato wa kutafuta mwendeshaji haujaanza.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haioni jitihada za makusudi za kutumia/kuendesha mradi huu wa BRT kwa ukamilifu wake, licha ya Serikali hufanya uwekezaji huu mkubwa ambapo sehemu ya fedha inayotumika ikiwa ni fedha ya mkopo. Jambo hili linafifisha juhudi kubwa inayofanywa na Serikali, ni rai ya Kamati kuwa DART iharakishe kupata watoa huduma kwa awamu zote tatu ili mradi huu uweze kuendeshwa kwa ukamilifu wake (*full capacity*) ili tija ya uwekezaji wa mtaji wa umma iweze kupatikana.

### 2.3.4 Kukosekana kwa mawasiliano ya barabara katika Stesheni za Mizigo kwenye Reli ya Kisasa – *SGR*

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa uwekezaji wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) umekusudia kuchochea uchumi wa nchi kwa kuharakisha huduma za usafirishaji hususani bidhaa. Reli hii inakusudia pia kuunganisha na kuongeza ufanisi na tija ya njia nyingine za usafirishaji, mathalani njia ya barabara na maji. Ujenzi wa Miundombinu ya reli ya kisasa umezingatia usanifu wa stesheni za mizigo katika maeneo mbalimbali ya mradi.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamatu ilibaini kuwa baadhi ya maeneo yaliyosanifiwa na kujengwa stesheni za mizigo

yanakabiliwa na ukosefu wa barabara zinazounganisha stesheni hizo na barabara kuu hali inayoweza kuathiri usafirishaji wa bidhaa kwa njia ya barabara na hivyo kushusha ufanisi na tija ya Reli hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa lengo la kupata ufanisi na tija ya mtaji wa umma uliowekezwa katika mradi huu, Kamati inamaoni kuwa Serikali ihakikishe ujenzi wa reli uende sambamba na ujenzi wa Barabara zinazotoka na kuingia katika vituo vya SGR (SGR stations) ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo ikizingatiwa kuwa mapato ya yatokanayo na usafirishaji wa mizigo ndio inatarajiwa kuendesha reli hii ya kisasa.

**2.3.5 Utendaji Usioridhisha wa Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania – TEMESA**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kuchambua taarifa za uwekezji za miaka mitatu mfululizo za taasisi ya TEMESA na kubaini kuwa utendaji wa Wakala kwa kipindi hicho chote haikuwa nzuri. Ilibainika kuwa wakala imekuwa ikijiendesha nje ya viashiria vya utendaji/vigezo vya utendaji vilivyowekwa na Msajili wa Hazina. Baadhi ya vigezo ambavyo wakala imekuwa nje ni pamoja na kigezo cha ukuaji wa mapato, uwiano wa mapato kwa matumizi, utegemezi wa Ruzuku na Uwiano wa mali za muda mfupi kwa madeni ya muda mfupi.

**Aidha,** Kamati ilibaini kuwa utendaji usioridhisha wa Wakala umeathiri mtaji wa uendeshaji wa wakala ambao umeshuka kutoka shilingi bilioni 19.8 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 1.9 2022/23. Kushuka kwa mtaji wa uendeshaji kumesababishwa na kuongezeka kwa kiasi kikubwa kwa madeni. Kama jitihada za makusudi hazitachukuliwa, ni dhahiri kuwa wakala inaenda kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi.

**Mheshimiwa Spika,** inafahamika kuwa huduma za ufundi na umeme zinazotolewa na Wakala ni huduma muhimu sana na zinaweza kuingia katika soko la ushindani na kufanya vizuri jambo ambalo litawaweza kuongeza ufanisi kwa kuzingatia fursa nyingi zilizopo sokoni na hatimaye kuweza kutengeneza faida itakayoiwezesha kupata mapato yatakayoondoa Wakala katika

utegemezi wa ruzuku ya serikali na hatimaye kupunguzia Serikali mzigo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia uchambuzi uliofanyika TEMESA haitoweza kufikia malengo ya kuanzishwa kwake pasipofanyika mabadiliko ya kimuundo na kisheria yatakayotoa fursa ya Wakala kushindana katika soko. Mabadiliko hayo yaende sambamba na kupatiwa mtaji wa awali wa uendeshaji. Ni matarajio ya Kamati kwamba masuala hayo yakitekelezwa kikamilifu tutakuwa na TEMESA ambayo itaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa nchi yetu kwa kutoa huduma bora na za kisasa pamoja na kutoa gawio kwa Serikali.

### 2.3.6 Changamoto ya Mizania ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL).

**Mheshimiwa Spika**, shirika la ndege Tanzania lilianzishwa kwa lengo kuu la kutoa huduma ya usafiri wa anga ndani na nje ya nchi. Malengo mengine ya kuanzishwa kwa ATCL ni kuwa na mwenendo chanya wa faida; kupanua wigo wa utoaji wa huduma; kuendeleza utoaji wa huduma kwa kuzingatia ubora na usalama; na kuongeza mashirikiano na mashirika mengine ya ndege n.k.

**Mheshimiwa Spika,** nia njema ya Serikali katika kufanikisha malengo haya inaonekana ambapo kwa miaka tisa tumeshuhudia Serikali ikifanya uwekezaji mkubwa kwa kuanza kununua ndege za shirika na hadi Disemba, 2024 jumla ya ndege kumi na tano (15) zimenunuliwa tena kwa kutumia fedha Taslim.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kuchambua taarifa za uwekezaji za ATCL na kubaini kuwa hali ya kifedha ya shirika sio ya kuridhisha ambayo imepelekea kuathiri mizania ya vitabu vya shirika. Kamati imebaini kuwa gharama za uendeshaji za shirika ni kubwa na zimeendelea kukua kwa kipindi cha miaka 3 mfululizo na hivyo kuathiri uwiano wa mapato na matumizi ya Shirika na pia kupekekea kuzalisha madeni na pia shirika kupata hasara kwa miaka 3 mfululizo.

**Mheshimiwa Spika,** kukua kwa gharama za uendeshaji za shirika imechangiwa na gharama za ukodishaji wa ndege kutoka TGFA ambapo kutokana na utaratibu uliopo sasa TGFA ndio mmiliki wa ndege za Serikali na ATCL inalazimika kuzikodi ndege hizo. Katika utekelezaji wa utaratibu huo wa ukodishaji wa ndege ATCL imesababishiwa kuzalisha madeni makubwa ambapo asilimia 95 ya madeni ya shirika ni madai ya TGFA kutokana na ukodishaji wa ndege.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inataarifa kuwa Serikali inaendelea na mchakato wa kuhamisha ndege kutoka TGFA kuzileta ATCL ili kurahisisha utendaji wa ATCL. Mchakato hii umechukua muda mrefu na ATCL inaendelea kuathirika kutokana na utaratibu uliopo sasa. Kamati ina maoni kuwa Serikali iharakishe kukamilisha mchakato wa kuhamishia ndege kutoka TGFA kuja ATCL ili kulipunguzia shirika gharama za uendeshaji. Jambo hili litaiwezesha Shirika pia kuweza kujitanua katika masoko/nchi ambazo kwa sasa haiwezi kufika.

### 2.3.7 Shirika la Bima la Taifa – *NIC* kuajiri kwa njia ya mkataba badala ya kuwa na ajira za moja kwa moja (Permanent and Pensionable)

**Mheshimiwa Spika**, Shirika la Bima la Taifa kutokana na utendaji wake kwa kipindi kirefu lilikuwa limeainishwa kubinafsishwa na Serikali (Specified) na hivyo kwa muda wote huo ajira za watumishi wake zilibadilishwa na kuwa za mikataba ili Serikali ikamilishe taratibu zake za kulibinafsisha, kwani isingeingia gharama kubwa pamoja na kuliruhusu kujiendesha kama zinavyoendeshwa kampuni binafsi za bima.

Aidha, mnamo mwaka 2019 baada ya Serikali kuona kuna uimarishwaji katika utendaji wa Shirika, NIC iliondolewa kwenye orodha ya Taasisi zinazopaswa kubinafsishwa na sasa kuwa Shirika la Serikali ambalo linaweza kuendeshwa kwa taratibu sahihi za Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya mabadiliko haya NIC inatambulika kama shirika la umma na kwa mujibu wa sheria ya uanzishaji wa mashirika ya umma, waajiriwa wake wanapaswa kuwa watumishi

wa ajira za kudumu (parmanent and pensionable). Kwa mujibu wa taarifa za NIC bado wanatumia utaratibu wa ajira za mkataba wa miaka mitatu jambo ambalo Kamati imeona ni changamoto kwani shirika linashindwa kuwaendeleza watumishi wake kimasomo kwakuwa baada kuwajengea uwezo ndani ya miaka mitatu shirika halina uhakika wa kuendelea kuwa nao.

**Mheshimiwa Spika**, watumishi wa NIC wanakosa kujiamini (confidence) katika utendaji wao kutokana na kutokuwa na uhakika wa ajira baada ya mkataba kuisha jambo ambalo linaathiri pia ufanisi wa kampuni.

**Mheshimiwa Spika**, ni kweli NIC ilipitia vipindi vya mabadiliko kutoka kutaka kubinafsishwa, kuja kurudishwa chini ya Serikali, ambapo kwa vipindi hivyo vya mpito ajira ya makataba ilikuwa sawa, lakini kwasasa NIC ni shirika linalomilikiwa na Serikali kwa asilimia 100, hivyo ni shirika la umma, kuna haja ya kufanyiwa maboredho yatakayoruhusu NIC kuwa na watumishi wa ajira za kudumu. Ni maoni ya Kamati kuwa NIC kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina washirikiane na kuhakikisha wanakamilisha kushughulikia mchakato wa kupata vibali vya kuajiri watumishi wa moja kwa moja.

### 2.3.8 Changamoto katika kutumia Mfumo wa Manunuzi – *NEST* kwa Mashirika Ya Kibiashara

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati kwa baadhi ya taasisi na mashirika ya umma hasa yanayojiendesha kibiashara bado yanakabiliana na changamoto mbalimbali katika uendeshaji wake ikiwemo changamoto katika kutumia mfumo wa manunuzi – *NEST* jambo linalowapelekea kushindwa kushindana kwenye soko na hivyo kuathiri mtaji wa umma uliowekezwa kwenye taasisi husika.

**Aidha,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kifungu cha Arobaini na Tisa (49) cha Sheria ya manunuzi kinatambua uwepo wa mashirika yanayofanya biashara na kililenga kuweka utaratibu rasmi wa kutumiwa na mashirika ya umma katika mfumo wa Manunuzi. Sheria hii inaeleza kuwa Mashirika yanayojiendesha Kibiashara yatawekewa utaratibu mahususi wa kufanya manunuzi

lakini kanuni zilizotungwa bado zinaonekana kuwa changamoto, kwani bado haziyarahisishii ipasavyo mashirika ya kibiashara katika kufanya manunuzi.

**Mheshimiwa Spika,** ugumu uliopo sasa katika utekelezaji wa Mfumo wa manunuzi (NEST) unapelekea mashirika ya umma yanayofanya biashara kushindwa kuchangamkia fursa za biashara zinapojitokeza. Baadhi ya Mashirika yanayokabiliwa na changamoto hii ni pamoja na TFC, CPB, NFRA, TTCL, STAMICO, NIC, ATCL n.k.

**Mheshimiwa Spika,** mashirika haya yanafanya shughuli zake katika soko hivyo kikwazo kama hiki kinawachelewesha na kuwanyima fursa jambo ambalo linakwamisha ufanisi wao na kuathiri tija ya mtaji wa umma uliowekezwa katika mashirika husika. Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ifanye maboresho ya Kanuni hizi ili ziweze kuleta uhalisia na wepesi kwa mashirika ya umma yanayofanya biashara kuweza kutumia mfumo wa manunuzi kwa urahisi na haraka.

**2.4 Uchambuzi wa utekelezaji wa miradi ya uwekezaji iliyotembelewa na kamati**

**Mheshimiwa Spika**, mwezi machi, 2024, Kamati ilifanya ziara za kukagua miradi ya uwekezaji ili kujiridhisha kama kuna tija ya kuwekeza mitaji ya umma katika miradi hiyo. Ziara ilifanyika katika mikoa saba (7) ambayo ni Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, Mtwara na Morogoro na jumla ya miradi kumi na tisa (19) ilikaguliwa. Miradi iliyotembelewa imegawanyika katika maeneo tisa (9) kama ifuatavyo:-

(i) Miradi ya Umeme;
(ii) Miradi ya maji;
(iii) Miradi ya bandari;
(iv) Mradi wa Bomba la Mafuta (EACOP);
(v) Miradi ya Ujenzi wa Vitegauchumi/miundombinu na hali ya uendeshaji (NHC, PSSSF, TAA, STENDI YA MSAMVU);
(vi) Miradi ya Ujenzi wa Makazi na Ofisi (TBA na DAWASA);
(vii) Miradi ya gesi asilia;
(viii) Mradi wa reli ya kisasa (SGR); na

(ix) Miradi wa uzalishaji viwandani.

## (a) Miradi ya Umeme

### (i) Mradi wa kituo cha kufua umeme (Hale)

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unafanyiwa matengenezo makubwa ili kuhuisha uwezo wa uzalishaji wa kituo hicho (Megawati 21) kwa mtambo mmoja unaoendeleza uzalishaji umeme.

Matengenezo katika mradi huu yalianza mwaka 2016 kwa hatua za awali na utekelezaji wa mkataba ulianza tarehe 30 Agosti, 2022 na unatarajiwa kukamilika Agosti, 2025 kwa ufadhili wa Serikali ya Sweden kupitia SIDA na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa gharama ya TZS 42,707,388,052.6 kwa mgawanyo wa TZS 6,117,772,902 (Lot 1) na TZS 36,589,615,150 (Lot 2).

Kwa ujumla mradi huu umefikia 61.45% kwa mgawanyo wa 96.9% (Ujengaji wa njia na uchimbaji wa access tunnel) na 26% ya ukarabati wa miundombinu ya uzalishaji umeme na malipo yamefanyika kwa 50.29% na 15%.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa katika mradi huu, bado umekuwa ukikabiliwa na changamoto kama vile kusimama kwa shughuli za mradi kutokana na uwepo wa mvua, vilevile, Kamati imebaini kuwepo kwa ucheleweshwaji wa malipo kwa wakandarasi.

**Mheshimiwa Spika,** kukamilika kwa mradi huu kutakuwa na manufaa kwakuwa kutasaidia kuongeza kiwango cha umeme kinachozalishwa na kuimarisha gridi ya taifa jambo litakalo ongeza ufanisi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha inachukua hatua stahiki kutatua changamoto hizo ili kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati kama ilivyopangwa na hivyo tija iliyokusudiwa kuweza kupatikana.

**(ii) Mradi Wa Usimikaji Wa Mtambo Wa Kufua Umeme - Mtwara (Megawati 20)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu uliasisiwa baada ya kubainika hali ya upungufu mkubwa wa umeme katika mikoa ya kusini (Mtwara na Lindi) ikiwa ni jitihada za muda mfupi za kutatua changamoto ya upungufu katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi huu ulianza Desemba 2023 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 31 Machi, 2024 kwa gharama ya shilingi bilioni 2.9 ambapo wakati Kamati ilipofanya ziara, mradi ulikuwa umefikia 99% na malipo kufanyika kwa shilingi bilioni 1.6 sawa na 55%. Mradi huu ulitekelezwa na TANESCO kwa kuhamisha mtambo wa TM16 kutoka Ubungo kwenda Mtwara ambao unauwezo wa kuzalisha Megawati 20.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatarajiwa kuimarisha upatikanaji wa umeme katika ukanda wa kusini mwa Tanzania (Lindi na Mtwara) hali itakayowezesha kuibua fursa mbalimbali na kuchochea uchumi na ustawi wa jamii katika ukanda huo. Ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali ihakikishe malipo ya mkandarasi yanafanyika kwa wakati kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba.

**(iii) Miradi ya Usambazaji Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko Wa Pili (Wakala Wa Nishati Vijijini - REA)**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia REA inaendelea kutekeleza shughuli mbalimbali nchini. Katika mikoa ya Manyara na Arusha, Kamati ilitembelea na kukagua miradi ya usambazaji umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa pili (*Turnkey Phase* III Round II) inayotekelezwa katika vijiji 44. Jumla ya vijiji 28 sawa na asilimia 63.6 vimewashwa umeme na vijiji 16 vya mradi ambavyo ni asimia 36.4 vinaendelea na utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa miradi hii umebainika kukabiliwa na changamoto kama vile baadhi ya wakandarasi kuchelewesha miradi na malalamiko kuhusu ukubwa wa gharama za uunganishaji wa umeme kwa vijiji vilivyopo katika maeneo yenye hadhi za Miji au Manispaa. Hata hivyo miradi hii

inatarajiwa kutoa manufaa kwa kufungua fursa za kiuchumi katika sekta mbalimbali hali itakayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi katika maeneo ya vijijini, kuimarisha hali ya vipato vya wananchi, kuboresha hali ya huduma na ustawi wa jamii na kuliongezea wigo wa mapato Shirika la umeme (TANESCO). Ni ushauri wa Kamati kwa Serikali kuhakikisha inawasimamia kwa uthabiti wakandarasi waliopewa kutekeleza shughuli mbalimbali katika miradi hiyo, vilevile kuhakikisha linatatua changamoto ya gharama katika maeneo ya vijiji ili kufanikisha lengo la mradi na kuwezesha upatikanaji wa tija ya uanzishwaji wa miradi hiyo.

**(b) Miradi ya Maji**

**(i) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiji la Arusha (AUWASA)**

**Mheshimiwa Spika**, AUWASA ilikuwa ikisimamia utekelezaji wa mradi wa Maji katika Jiji la Arusha na maeneo mengine yanayohudumiwa na Mamlaka. Utekelezaji wa mradi huo uligharimu kiasi cha TZS bilioni 520. Katika utekelezaji wa mradi, Mamlaka ilikumbana na changamoto mbalimbali hali iliyosababisha ucheleweshwaji katika kukamilisha mradi. Miongoni mwa changamoto hizo ni Kuchelewa kupata msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa wakandarasi kipindi cha kuanza utekelezaji wa mradi, ugumu wakati wa kuomba kuongezewa muda kwa msamaha wa kodi (Kuongeza muda wa Government Notice na VAT Exemption Certificates) zilizokwisha muda wake, Mlipuko wa homa ya mapafu (UVIKO-19), uwepo wa mvua nyingi hususani mwaka 2019 na 2020 zilizoathiri shughuli za mradi, kukosekana kwa maeneo kwaajili ya ujenzi wa miundombinu ya huduma za majisafi na majitaka yaliyotengwa na mipango miji na hivyo kuongeza gharama kwa kulipa fidia, uwepo wa miamba migumu katika maeneo ya mradi wa uchimbaji wa visima na kuchelewa kwa fedha za mchango wa Serikali kwenye mradi.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatarajiwa kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama na kuongeza mapato ya mamlaka.

### (ii) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi (MUWSA)

**Mheshimiwa Spika**, MUWSA inatekeleza majukumu yake ya kutoa huduma za Majisafi na usafi wa Mazingira katika maeneo ya Manispaa ya Moshi, Wilaya ya Hai na Moshi Vijijini kwa mujibu wa Sheria ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019, na pia kwa kuzingatia tangazo la Serikali GN No. 573 ya tarehe 5/10/2018 na GN No. 585 ya tarehe 9/08/2019 pamoja na GN. 113/2016. Katika kuboresha utoaji wa huduma kwa wateja, Mamlaka ilitekeleza mradi wa Majisafi Miwaleni-Njiapanda utakao kuwa na uwezo wa kuzalisha lita za ujazo 2,592,000 na Karanga-Darajani wenye uwezo wa kuzalisha lita za ujazo 3,888,000 ambayo ilianza kati ya tarehe 20/12/2021 na kukamilishwa tarehe 01/03/2023 ambayo iligharimu kiasi cha TZS 2,378,561,732.29 na TZS 789,838,198.00. Hata hivyo, baada ya kutembelea na kukagua miradi hiyo pamoja na kupokea taarifa ya utendaji Kamati ilibaini kukosekana kwa mikakati madhubuti katika ujenzi wa miundombinu ya majitaka na upungufu wa fedha za kutekeleza miradi ya maji.

**Mheshimiwa Spika,** miradi hii ukiacha kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Manispaa ya Moshi na maeneo mengine ya huduma, vilevile itasaidia kuongeza mapato kwa Mamlaka na hivyo kuimarisha uwezo wa kiutendaji na kiuendeshaji.

### (iii) Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji Tanga

**Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA) ilipanga kutekeleza mradi wa uboreshaji wa Huduma ya Maji Tanga kwa awamu mbili zaidi yaani Awamu ya II na III. Mradi huu ulianzishwa kwa lengo la kukabiliana na changamoto ya maji kutokidhi mahitaji ya huduma kwa wakazi wa Jiji la Tanga pamoja na Mji wa Muheza na maeneo mengine ya huduma.

Utekelezaji wa mradi kwa Awamu ya II ulianza Septemba 2021 na ulipangwa kutekelezwa kwa uwezo wa ndani chini ya mpango wa *Investment Financing Facility – Output Based Aid (IFF – OBA) for Tanzania Water Utilities.* Awamu hiyo ya mradi ilitarajiwa

kukamilika katika kipindi cha miezi 12. Hata hivyo, mradi huu ulichelewa kutokana na uwepo wa baadhi ya changamoto na hivyo kuongezewa muda wa ukamilishwaji katika kipindi cha miezi 20 ambapo ulikamilika kufikia Mei 2023. Utekelezaji wa mradi katika Awamu ya II ulikabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni Kuchelewa kupata hati ya Msamaha wa Kodi ya ongezeko la thamani (VAT exemption Certificate), uwepo wa miamba migumu katika maeneo ya mradi na kuchelewa kuwasili kwa baadhi ya vifaa (Filtyer noizle na Lamela plates) kutoka China kutokana na vita baina ya China na Taiwan June, 2022 na athari za UVIKO.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kukamilika kwa Awamu ya II, Awamu ya III ya mradi imepangwa kutekelezwa kupitia uwekezaji wa Hatifungani (Green bond) ili kukusanya kiasi cha TZS Bilioni 53.12 ambayo ilizinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango mnamo tarehe 22/02/2024. Mradi huu pamoja na kuimarisha upatikanaji wa maji katika jiji la Tanga, Muheza na maeneo mengine ya huduma, pia unatarajiwa kuiongezea Mamlaka uwezo wa kimapato na uwezo kiuendeshaji.

**(c) Miradi ya bandari**

**(i) Mradi wa Maboresho ya Bandari ya Tanga**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa uboreshaji wa Bandari ya Tanga ulitekelezwa chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Bandari (TPA). Utekelezaji wa mradi uligawanywa katika awamu mbili (2); awamu ya kwanza ilianza tarehe 01 Oktoba, 2019 hadi 15 Julai, 2022 na awamu ya pili ilianza tarehe 16 Disemba, 2020 na kukamilika 04 Aprili, 2023. Utekelezaji wa mradi huu kwa awamu zote mbili ulifanywa na Mkandarasi M/S China Harbour Engineering Company Ltd (CHEC) na kusimamiwa na Mkandarasi Mshauri M/S NIRAS AS kutoka Denmark kwa kushirikiana na M/S ANOVA ambaye ni mzawa. Utekelezaji wa mradi uligharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jumla ya TZS 429.1 bilioni, kwa mgawanyo wa TZS 172.3 bilioni katika awamu ya kwanza na TZS 256.8 bilioni katika awamu ya pili. Utekelezaji wa

mradi huo ulichelewa kutokana na kukwamishwa na changamoto ya mlipuko wa UVIKO-19.

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatarajiwa kuwa na manufaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa uwezo na ufanisi wa bandari kwa kuongeza ukubwa wa Meli na mizigo inayohudumiwa na kuharakisha uhudumiaji wa Meli zinazoingia na kutoka, kuongeza mapato na kupungua kwa gharama za bandari kutokana na maboresho hayo.

**(ii) Mradi wa Maboresho ya Bandari ya Dar Es Salaam (TPA_Dar Es Salaam)**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam unatekelezwa na serikali chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Bandari (TPA). Mradi huu unatekelezwa kwa awamu mbili: Awamu ya kwanza ililenga kufanikisha upanuzi wa gati kuanzia gati namba 7- hadi 11 ambayo ilianza kutekelezwa katika kipindi cha mwaka 2017 mpaka 2024, na awamu ya pili imekusudia kutekeleza ujenzi wa gati 12-15 ambayo mpaka Kamati ilipotembelea mradi ulikuwa katika hatua ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa ujenzi wa gati hizo.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi huu unakusudia kuongeza ufanisi wa Bandari ya Dar es Salam katika kuhudumia mizigo na kuimarisha utoaji wa huduma zinazokidhi viwango vya Dunia na kuiongezea mapato na uwezo wa kiundeshaji TPA_Dar es Salaam. Ni maoni ya Kamati, Serikali kuhakikisha mradi unatekelezwa katika viwango stahiki na kukamilisha kwa wakati ili kupata tija ya uwekezaji iliyokusudiwa.

**(iii) Mradi wa Maboresho ya Bandari ya Mtwara**

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa uboreshaji wa Bandari ya Mtwara ulitekelezwa na serikali chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Bandari (TPA). Mradi huu ulitekelezwa katika kipindi cha mwaka 2017 hadi mwaka 2024. Mradi uligawanyika katika maeneo matano (5) ambayo ni Ujenzi wa Gati Moja (Wakandarasi: M/S China Railaway Construction Engineering Group na China Railway Major Bridge Engineering Group Co.Ltd), Ujenzi wa mita ya kupima

mafuta (Mkandarasi: M/S Endress+Hauser kutoka Uswiss kwa ushirikiano na BQ Contractors Ltd kutoka Tanzania), Ununuzi wa Ship to Shore Gantry Crane (Mkandarasi: M/S Liebherr Container Cranes Ltd kutoka Ireland), Ununuzi wa Boti Moja na Ujenzi wa Barabara inayounganisha Gati Jipya. Utekelezaji wa mradi huu uligharimu kiasi cha TZS 253,584,362,289.78 katika Ujenzi wa Gati Moja, ununuzi wa Ship to Shore Gantry na Ujenzi wa barabara inayounganisha Gati jipya. Pia USD 1,696,068 zilitumika katika manunuzi ya Boti Moja (Pilot Boat) na TZS 43,537,198,818.21 kwaajili ya ujenzi wa mita za kupima mafuta (kwa bandari zote tatu).

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatarajiwa kuiongezea Mamlaka mapato, pia kuongeza ufanisi wa kiutendaji na kiuendeshaji katika bandari. Hata hivyo ilibainika kwamba kuna changamoto zinazoweza kushusha ufanisi na tija ya uwekezaji uliofanyika katika bandari ya Mtwara kama vile kukosekana kwa miundombinu ya reli inayotoka maeneo ya kiuchumi katika Kanda ya kusini na kuunganisha na bandari na kutokusomana kwa mipango baina ya taasisi hususani katika miradi ya kimkakati. Ni maoni ya Kamati, kwamba Serikali iweze kuzisimamia taasisi zinazogusa uwekezaji wa kimkakati ili kuimarisha ushirikiano, hivyo kuwa na shabaha ya pamoja kwa lengo la kupata tija stahiki ya miradi inayotekelezwa.

**(d) Miradi ya Ujenzi wa Vitegauchumi/miundombinu na hali ya uendeshaji (NHC, PSSSF, TAA);**

**(i) Jengo la Tatu la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa (JNIA)**

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Julius Nyerere ulitekelezwa katika kipindi cha June 2013 hadi Mei 2019. Jengo hili lilianza kutumika mnamo Agosti 2019 na mashirika ya ndege 19 yaliyokuwa yakitumia Jengo la Pili la Abiria kwa safari za kimataifa. Hata hivyo, mashirika mawili (2) ya ATCL na Precision Air yaliendelea kutumia Jengo la Pili la Abiria kutokana na kufanya safari zake za ndani na zile za kimataifa.

**Mheshimiwa Spik**a, Ukamilishwaji na kuanza kutumika kwa Jengo hilo kumeongeza ufanisi wa shughuli za Kiwanja cha Ndege cha

Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA). Hata hivyo uendeshaji wa Jengo la Tatu la Abiria umeendelea kukabiliwa na changamoto ya Upungufu wa watumishi 214 katika maeneo ya uendeshaji, Usalama na Ufundi. Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali itatue changamoto hiyo ili kuimarisha ufanisi katika utendaji na uendeshaji wa TAA.

**(ii) Mradi wa Uwekezaji Jengo La Biashara La PSSSF (Sam Nujoma-Dar Es Salaam)**

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa PSSSF umekuwa ukifanya uwekezaji kwenye maeneo mbalimbali ya vitega uchumi ikiwa ni miongoni mwa takwa la kisheria kwa lengo la kulinda thamani za fedha za wanachama dhidi ya mfumuko wa bei na kushuka kwa thamani ya fedha ili kuweza kulipa mafao ya wanachama pindi utumishi wao unapokoma kwa mujibu wa sheria. Hivyo katika kutekeleza jukumu la kuwekeza michango hiyo, mnamo Disemba 2015, uliokuwa Mfuko wa Pensheni (PPF) ulianza kutekeleza mradi, ambapo ulisainiwa mkataba wa kandarasi ya ujenzi kati ya kampuni ya Estim Construction Ltd na Mfuko wa PPF kwaajili ya ujenzi wa jengo la kibiashara kwa matumizi ya ofisi, maduka, kumbi za mikutano na maegesho ya magari wenye gharama ya jumla ya TZS 232,389,459,866.68 ikijumuisha VAT. Mpaka kufikia Machi, 2024 kiasi cha TZS 221,012,327,966.20 (asilimia 95) kilikuwa kimelipwa.

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi ulipangwa kutekelezwa katika kipindi cha miezi 36 kuanzia Disemba 17, 2015 hadi Disemba 16, 2018 kwa kutumia Mfumo wa Usanifu, ujenzi na matengenezo baada ya ujenzi kukamilika (Design, Build and Maintain). Hata hivyo, mradi ulichelewa kwa miezi 12 hali iliyopelekea kukamilika Disemba 2019 kutokana na changamoto ya Uvamizi uliofanywa na wakazi katika eneo la mradi na kusababisha mgogoro uliosimamisha shughuli za utekelezaji wa mradi hadi ulipotatuliwa na Mamlaka (Manispaa ya Ubungo), na kulazimu mkandarasi kuongezewa muda. Kwa mujibu wa masharti ya mkataba, mkandarasi anawajibika kusimamia matengenezo kwa uangalizi kwa kipindi cha miaka Mitano (5) baada ya kukabidhi hati ya ukamilishwaji wa mradi kuanzia Disemba 10, 2019 mpaka Disemba 10, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatarajiwa kutoa manufaa mbalimbali ikiwemo kuongeza mapato ya Mfuko, ajira na kukuza uwezo wa kulinda thamani ya fedha za wanachama dhidi ya mfumuko wa bei na kushuka kwa thamani ya fedha kwa kutumia fursa ya fedha za wanachama katika uwekezaji. Ni maoni ya Kamati kwamba, Mfuko uhakikishe unasimamia kwa uthabiti uendeshaji wa mradi huu ili uweze kuwa na ufanisi kwa lengo la kupata tija iliyokusudiwa.

**(iii) Uendeshaji Wa Stendi ya Msamvu**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulitekelezwa kwa ubia kati ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na uliokuwa Mfuko wa Pensheni wa LAPF kupitia kampuni ya pamoja "Joint Venture Company" iliyosajiliwa mwaka 2009 kwa mgawanyo wa hisa kwa asilimia 40 na 60.

Mradi wa ujenzi wa stendi ya Msamvu ulikuwa ni hatua ya kwanza ya mradi kutokana na mradi kuwa na hatua mbili ambazo ni ujenzi wa Stendi ya Msamvu na Hoteli ya kisasa. Ujenzi wa stendi ya Msamvu ulianza Januari, 2015 na kukamilika Novemba, 2016 chini ya ukandarasi wa Kampuni ya Group Six International Limited na mshauri mwelekezi ambayo ilikuwa ni Kampuni ya OGM Consultant na Sky Architect. Utekelezaji wa hatua ya kwanza ya mradi huu iligharimu TZS 14.76 bilioni.

**Mheshimiwa Spika**, kwasasa mradi huu unakabiliwa na changamoto ya kiuendeshaji kutokana na agizo lililotolewa na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Awamu ya Tano) Dkt. John Magufuli la kutaka mradi huu uachwe chini ya umiliki na usimamizi wa Manispaa ya Morogoro hali inayodhoofisha ufanisi na kuleta athari hasi kwa kushusha tija ya mradi.

Ni maoni ya Kamati kwamba, Serikali kwa kuwashirikisha wabia wa mradi itathmini hali ya uendeshaji wa Stendi hii ili kubaini changamoto zinazokabili na kubainisha namna bora ya uendeshaji.

**(iv) Miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa – NHC (Morocco Square, Kawe 711 Na Samia Housing Scheme)**

**Mheshimiwa Spika**, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) limekuwa likitekeleza miradi mbalimbali ili kutimiza takwa la kisheria la uanzishwaji wake. Katika kipindi cha Machi, 2024 Kamati ilitembelea na kukagua miradi ya Morocco Square, Kawe 711 na Samia Housing Scheme. Ukaguzi ulibaini kwamba utekelezaji wa mradi wa Morocco Square ulioanza mwaka 2014 umefikia asilimia 98, mradi wa Kawe 711 ulioanza mwaka 2014 umefikia asilimia 35 na mradi wa Samia Housing Scheme ulioanza mwaka 2022 umefikia asimia 54.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa miradi ya Morocco Square na Samia Housing Scheme unaendelea vizuri huku mradi wa Kawe 711 mwaka 2018 ulikumbwa na changamoto ya kukosa kibali cha kukopa kutoka Wizara ya Fedha hali iliyolifanya Shirika kusimamisha ujenzi wa mradi. Kwa sasa mradi unaendelea na utekelezaji tangu Januari, 2024 na unatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2026.

**Mheshimiwa Spika**, miradi hii inategemewa kutoa manufaa mbalimbali ikiwemo kupunguza kadhia za makazi kwa wakazi wa Dar es Salaam, kuongeza fursa na kuvutia uwekezaji kutokana na uboreshaji miundombinu ya biashara katika jiji la Dar es Salaam, kuongeza mapato na kuimarisha tija itokanayo na uwekezaji katika Shirika. Ni ushauri wa Kamati kuwa, NHC ihakikishe inatekeleza miradi hiyo katika viwango stahiki na kukamilisha kwa wakati ili kupata tija iliyokusudiwa.

**(e) Miradi ya Ujenzi wa Makazi na Ofisi**

**(i) Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)**

**Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Majengo Tanzania umekuwa ukitekeleza miradi katika maeneo mbalimbali ya nchi ili kuwezesha watumishi wa umma nchini kupata huduma bora za makazi ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Katika kipindi cha Machi 2024, Kamati iliweza kutembelea moja ya mradi wa majengo wa Magomeni kota wenye maeneo

manne (A, B, C, D) ya utekelezaji na kukagua maendeleo na hatua zilizofikiwa katika kutekeleza mradi huo ulioanza kutekelezwa mwaka 2021. Ukaguzi ulibaini kwamba jengo A na B ujenzi wake umekamilika na jengo C na D yapo katika hatua ya msingi.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatarajiwa kusaidia kupunguza adha ya makazi kwa watumishi wa umma katika Jiji la Dar es Salaam. Vilevile kuiongezea ukwasi na mapato Wakala wa Majengo (TBA) na hivyo kuimarisha uwezo wa kujiendesha. Ni rai ya Kamati kwamba, Wakala uhakikishe mradi huo unatekelezwa kwa ubora stahiki na kukamilika kwa wakati ili tija ya uwekezaji iweze kupatikana.

**(ii) Mradi wa Jengo la DAWASA**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa jengo la Ofisi za DAWASA ulianza kutekelezwa na Mamlaka kuanzia tarehe 13 Aprili, 2015 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 12 Aprili, 2017. Mradi huu ulitekelezwa na Mkandarasi M/S China Civil Engineering Construction Company (CCECC) wa China na Mhandisi Mshauri M/S Epitome Architects Ltd kwa gharama ya jumla ya TZS 49,977,205,783.97 kwa mchanganuo TZS 48,979,205,783.97 na TZS 998,000,000. Hata hivyo, kutokana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza, muda wa utekelezaji wa mradi ulikuwa ukiongezwa na unategemewa kukamilika tarehe 31 Mei, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, kukamilika kwa jengo hili kunatarajiwa kuboresha mazingira ya kazi na kuimarisha ufanisi katika usimamizi wa shughuli na utoaji wa huduma kwa Mamlaka. Mradi huu ulikabiliwa na changamoto za kuchelewa kwa malipo ya hati za madai kwa Mkandarasi, kwani mpaka mwezi Machi, 2024 Mkandarasi alikuwa akidai TZS 8,239,665,805.62 kwa hati namba 22 na 25 na kuchelewa kwa baadhi ya vifaa vilivyoagizwa nje ya nchi pamoja na mabadiliko ya viwango vya fedha za kigeni kutokana na uwepo wa mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO. Ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali ihakikishe inasimamia ili madai ya mkandarasi yalipwe na mradi ukamilike kwa wakati ili tija ianze kupatikana.

### (f) Mradi wa Bomba la Mafuta (EACOP)

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa bomba la kusafirisha Mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) mpaka Chongoleani (Tanzania). Mradi huu unahusisha wanahisa wanne (4) ambao ni TPDC (15%), Kampuni ya Taifa ya Mafuta Uganda (UNOC – 15%), Total Energies (62%) na CNOOC (8%) ambao wanaunda Kampuni ya mradi EACOP yenye jukumu la kutekeleza, kusimamia na kuendesha mradi. Utekelezaji wa mradi huu ulianza Januari 2024 ambao upo katika hatua za awali na unatarajiwa kukamilika mwaka 2026.

**Mheshimiwa Spika,** katika hatua za awali mradi huu umekuwa na manufaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na utoaji wa ajira kwa baadhi ya Watanzania, kuchangia kodi ya serikali, upatikanaji wa ujuzi na uzoefu kwa wazawa, na pia kuchangia kupitia miradi ya uwajibikaji kwa jamii (CSR). Hata hivyo, baadhi ya masuala yalibainika kuwa changamoto katika utekelezaji wa mradi, ambayo ni kama udanganyifu katika kutekeleza dhana ya Ushiriki wa wazawa kwa baadhi ya kampuni (local content), utekelezaji usioridhisha wa miradi ya uwajibikaji kwa jamii (CSR) na ukwepaji wa malipo ya Ushuru wa Halmashauri unaofanywa na Kampuni zilizopewa Zabuni ya kutekeleza mradi huo katika maeneo mbalimbali ya mradi. Ni maoni ya Kamati kwamba, Serikali kuhakikisha inatatua changamoto zilizojitokeza ili mradi uweze kutekelezwa kwa ufanisi na kutoa tija iliyokusudiwa.

### (g) Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR KIPANDE CHA DAR ES SALAAM – MOROGORO)

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC), inatekeleza mradi wa Ujenzi wa Reli mpya ya Kisasa ya Standard Gauge Railway (SGR). Mradi huu umegawanyika katika awamu mbili (Awamu ya Kwanza na awamu ya Pili). Ujenzi wa mradi katika kipande cha Dar es Salaam – Morogoro unaendelea kwa utaratibu wa Sanifu na Jenga (Design and Build) chini ya Wakandarasi kati ya Yapi Merkezi (Uturuki) na Mota Engil (Ureno) kwa mkataba uliosainiwa tarehe 03 Februari, 2017. Pia, Mhandisi Mshauri na msimamizi wa mradi huu ni KORAIL JV. Ujenzi wa kipande hiki mpaka kukamilika utagharimu kiasi cha Dola za

Marekani 1,215,282,000 (pamoja na kodi), na umefikia asilimia 98.9. Kazi zilizokamilika katika kipande hiki ni Ujenzi wa tuta, Ujenzi wa daraja la juu katika jiji la Dar es Salaam, Ujenzi wa Stesheni, Ujenzi wa Madaraja na makalvati, Mifumo ya ishara, mawasiliano na TEHAMA; na Ujenzi wa Miundombinu ya Umeme. Kwa upande wa kazi zinazoendelea ni Ujenzi wa vivuko vya juu (Overpass OP-6, 9 na 11) ambao umefikia asilimia 99; na Ujenzi wa njia ya Reli kuelekea Bandarini (Port Link) ambao umefikia asilimia 74.55.

**Mheshimiwa Spika**, Shirika linaendelea na maandalizi ya uendeshaji katika hatua mbalimbali kwa kipande cha Dar es Salaam – Dodoma ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa uzio maalum wa tembo kwa maeneo ya ngerengere, majaribio ya vitendea kazi ambavyo ni pamoja na vichwa na mabehewa, maandalizi ya nguvu kazi na ukamilishaji wa miongozo ya uendeshaji (Operational Manual). Mradi wa Reli ya kisasa unatarajiwa kuwa na matokeo chanya ikiwa ni pamoja na kuongeza ufanisi katika sekta ya uchukuzi na usafirishaji, kuchochea sekta mbalimbali za kiuchumi kama kilimo, biashara n.k na kuongeza uwezo wa kimapato na kiuendeshaji katika shirika. Ni maoni ya Kamati kwamba, Serikali ihakikishe inasimamia kwa ukaribu utekelezaji wa mradi huu ili uweze kutekelezwa kwa ufanisi na ubora na kukamilika kwa wakati ili kutoa tija inayotarajiwa.

**(h) Kiwanda cha Sukari – Mbigiri**

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa Kiwanda cha Sukari cha Mbigiri (Mbigiri Estate) ulianzishwa na Kampuni Hodhi ya Mkulazi kwa lengo la kuzalisha sukari ili kupunguza nakisi ya mahitaji ya sukari nchini. Kampuni hii inamilikiwa kwa ubia kati ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Magereza kwa mgawanyo wa 96% na 4%. Utekelezaji wa mradi huo unajumuisha shughuli ambazo zipo katika hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na ulimaji na upandaji wa miwa (93%), Ufungaji wa mifumo ya Umwagiliaji (75%), Ununuzi wa Vifaa na Mitambo (90%), Ujenzi wa barabara (85%) na Ujenzi wa Kiwanda ambao una awamu mbili zinazojumuisha usimikaji wa mitambo ya kuzalisha sukari ya majumbani ambayo imekamilika na usimikaji wa

mitambo ya kuzalisha sukari ya viwandani ambao unatarajiwa kukamilika Aprili, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, kukamilika kwa kiwanda hiki kutasaidia kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa sukari ya majumbani pamoja na sukari ya viwandani. Vilevile, itasaidia kuuongezea mapato Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Magereza. Hata hivyo, Mradi huo ulikabiliwa na changamoto kama vile Mkandarasi kuchelewa kukamilisha Ujenzi wa Kiwanda, Uwepo wa Mvua za Eli nino na Uwepo wa Mgao wa Umeme kutoka TANESCO. Ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali iwasaidie wawekezaji hao kutatua changamoto hususani changamoto ya kukatika umeme ili kuimarisha ufanisi wa Kiwanda na tija ya uwekezaji.

**(i) Mradi wa Kuchakata na Kuzalisha Gesi Asilia**

**Mheshimiwa Spika**, tangu mwaka 2009, mradi wa gesi asilia (Mnazi Bay) ulikuwa ukimilikiwa kwa ubia na Kampuni za M&P (48.06%), Wentworth (31.94%) na TPDC (20% sawa na TZS bilioni 42.7). Hata hivyo, Februari 2024, TPDC iliongeza hisa kwa 20% na kufikia 40%, huku kampuni ya M&P ikiongeza mpaka kufikia 60%. Hivyo kuanzia Februari 2024, umiliki wa mradi wa gesi asilia (Kitalu cha Mnazi Bay) upo kwa ubia wa M&P na TPDC. Kitalu hicho kina mashapo yenye uwezo wa kuzalisha gesi futi za ujazo wa 641 CTF. Pamoja na hilo, TPDC inaendelea kutekeleza mikakati ya kuongeza uzalishaji, uchakataji na usafirishaji katika vitalu vya Mnazi Bay, Songo Songo na NtoryaRuvuma ikiwemo kuchoronga visima viwili vya uzalishaji gesi, kutekeleza shughuli za utafutaji kwa kushirikiana na wawekezaji, kuongeza msukumo wa gesi kwenye visima na mabomba ya gesi, kukarabati kisima cha Songo Songo (SS7) na kusimika mitambo ya kuongeza mgandamizo wa gesi Kitalu cha Songo Songo. Utekelezaji wa mikakati hiyo umeanza mwaka 2024 na utakamilika Disemba 2026 na inatarajiwa kugharimu kiasi cha $166.25 Milioni.

**Mheshimiwa Spika**, miradi hii inatarajiwa kuongeza upatikanaji wa gesi asilia nchini, kuchochea uchumi kwa namna tofauti tofauti ikiwemo kuipunguzia Serikali gharama na matumizi ya fedha za kigeni (dollars) katika uagizaji wa nishati kama vile mafuta na

PNG. Vilevile itachochea uchumi kwa kuchangia nishati kwa matumizi ya uzalishaji viwandani, na pia kuliongezea mapato na uwezo wa kiundeshaji Shirika (TPDC). Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali ilisimamie Shirika la TPDC ili litekeleze miradi hiyo kwa ufanisi ili tija iliyokusudiwa iweze kupatikana.

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyokaguliwa kwa kipindi cha mwezi machi, 2024, Kamati ilitoa ushauri wa jumla ufuatao kwa Serikali:-

(i) Kuhakikisha madai ya wakandarasi yanalipwa kwa kuzingatia mikataba jambo litakaloiwezesha Serikali kuepuka mlundikana wa madeni ya wakandarasi na ongezeko la gharama zitokanazo na riba;

(ii) Kuhakikisha mipango ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati inazingatia mawanda ya malengo ya uanzishwaji wa miradi ili iweze kutekelezwa kwa ufanisi kwa lengo la kupata tija stahiki;

(iii) Kuhakikisha Serikali inaimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa kuhakikisha mifumo ya Mamlaka ya Mapato (TRA) na taasisi nyingine inasomana ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji na udhibiti wa mapato, pamoja na kuwezesha kuwa na taarifa sahihi na halisi;

(iv) Kuhakikisha usimamizi wa wakandarasi wanaotekeleza miradi unaimarishwa kwa lengo la kuitekeleza kwa ufanisi na kuikamilisha kwa wakati ili iweze kutoa tija iliyokusudiwa na kwa wakati;

(v) Kuhakikisha mchakato wa kupata wakandarasi wa utekelezaji wa miradi ya uwekezaji unazingatia ushirikishaji wa wakandarasi wazwa hususani kwenye miradi ya kimkakati ili waweze kupata ujuzi; na

(vi) Kuhakikisha mpango wa uwajibikaji kwa jamii (CSR)uliopitishwa kwa mujibu wa taratibu unasimamiwa kwa ufasaha ili wakandarasi wautekeleze ipasavyo na hivyo jamii

kutambua manufaa ya miradi jambo litakaloimarisha ulinzi na uendelevu wa miradi husika.

### 2.5 Ushiriki katika Semina na warsha Mbalimbali

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati, wajumbe walipata fursa ya kushiriki katika semina na warsha mbalimbali ambazo zililenga kuwajengea uwezo. Kamati inawashukuru wadau wote ambao walijitokeza katika kutoa semina za mafunzo na kuwajengea uwezo wajumbe wa kamati.

Semina na warsha hizo zimekuwa na manufaa makubwa katika kuongeza uelewa wa wajumbe kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu uwekezaji wa mitaji ya umma hivyo kuiwezesha Kamati kutoa ushauri wenye tija. Ni imani ya kamati kuwa ushirikiano huo utaendelea katika kuijengea kamati uwezo kwa maslahi mapana ya taifa letu.

## SEHEMU TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na uchambuzi na ufuatiliaji wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma uliofanywa na Kamati, yapo mambo maalumu yanayotolewa maoni na mapendekezo kwa madhumuni ya kulisaidia Bunge kujadili na kuamua.

### 3.2 Maoni ya Jumla

#### 3.2.1 Changamoto ya upatikanaji wa Mbolea Nchini na Kukosekana kwa Kiwanda cha Uzalishaji katika Kampuni ya Mbolea (TFC).

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miaka mitatu, mpaka kufikia mwaka 2022/23 jumla ya shilingi 1,007,158,967,000 zilitumika kuagiza mbolea kutoka nje ya nchi. Kiasi hiki kinaweza kubaki nchini kama Serikali kupitia TFC itaamua kujenga kiwanda cha

kuzalisha mbolea hapa nchini kama inavyoeleza kwenye malengo ya kuanzishwa kwa TFC.

### 3.2.2 Jukumu la Usimamizi wa Mali za Serikali zililorithiwa na Msajili wa Hazina kutoka Shirika Hodhi la Mashirika ya Umma – CHC

**Mheshimiwa Spika,** Msajili wa Hazina alirithi mali zilizokuwa CHC na alipaswa kutekeleza jukumu la kuendeleza mpango wa kuzibinafsisha, lakini kwa kipindi cha miaka 11 kuna baadhi ya mali bado zimebaki pasipo kutumika huku zikichakaa na kuingiza gharama za ulinzi. Ni maoni ya kamati kuwa Msajili wa Hazina asimamie kikamilifu jukumu hili, ili mali hizo ziweze kuendelezwa na Serikali ipate mapato badala ya kuingia gharama za kuzilinda pasipo kuendelezwa.

### 3.2.3 Tija ndogo katika uendeshaji wa Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (BRT)

**Mheshimiwa Spika,** nia njema ya Serikali kuamua kutekeleza mradi wa mabasi yaendayo haraka Jijini Dar es Salaam, inafifishwa na uendeshaji wa miradi hii ambapo miundombinu yake inatumika kwa kiwango kidogo jambo ambalo linashusha tija ya uwekezaji huu mkubwa. Ni vema taasisi husika zikaharakisha michakato ya kupata watoa huduma ili waweze kuendesha awamu zote za zilizokamilika kwa ufanisi na tija ya mtaji wa umma uliowekezwa iweze kupatikana.

### 3.2.4 Kukosekana kwa mawasiliano ya barabara katika Stesheni za Mizigo kwenye Reli ya Kisasa – SGR

**Mheshimiwa Spika,** changamoto ya kukosekana kwa mawasiliano ya Barabara katika vituo vya mizigo kwenye Reli ya Kisasa – SGR inafifisha tija ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali katika reli ya SGR.

Kwa maoni ya Kamati, hali hiyo inahitaji kupatiwa ufumbuzi ili mtaji wa umma unaotumika uweze kuwa na tija na ufanisi.

### 3.2.5 Utendaji Usioridhisha wa Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania – TEMESA

**Mheshimiwa Spika, TEMESA** imebainika kuwa utendaji wake hauridhishi jambo lililopelekea kuathirika kwa mtaji wake na kupungua kutoka bilioni 17.5 hadi kufika bilioni 1.9 licha ya kuwa huduma wanazozitoa kuwa na uhitaji kwenye soko. Ni maoni ya Kamati kuwa TEMESA ifanyiwe tathimini na kuandaliwa mpango wa kuibadilisha.

### 3.2.6 Changamoto ya Mizania ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL)

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) limebainika kupata hasara kwa miaka mitatu mfululizo. Hasara hii inatokana na kuwa na madeni makubwa yanayosababishwa na utaratibu wa ukodishaji wa ndege kutoka TGFA. Hasara inayopatikana inaathiri mizania ya shirika na kushusha sifa nzuri ya shirika (credibility). Kwa maoni ya Kamati, jambo hili linahitaji kupatiwa ufumbuzi ili mtaji wa umma unaotumika uwe na tija na ufanisi na mizania ya vitabu vya shirika ikae sawa.

### 3.2.7 Shirika la Bima la Taifa – NIC kuajiri kwa njia ya mkataba ya muda mfupi badala ya kuwa na ajira za moja kwa moja (Permanent and Pensionable)

**Mheshimiwa Spika,** ni utaratibu kuwa na ajira za kudumu kwa taasisi na mashirika ya umma. Kwa kuwa mchakato wa kulihuisha Shirika la Taifa la Bima ulishakamilika na sasa ni shirika la umma, Ni maoni ya kamati kuwa, Shirika liingie kwenye utaratibu wa ajira za moja kwa moja (za kudumu) kwa lengo la kuleta ustawi kwa watumishi wa shirika ili kuongeza ufanisi na kupata tija ya shirika.

### 3.2.8 Changamoto katika kutumia Mfumo wa Manunuzi – *NEST* kwa Mashirika Ya Kibiashara

**Mheshimiwa Spika,** kwa lengo la kuyawekea wepesi mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara, ni Vema Serikali ikakamilisha kanuni stahiki ili tija ya mtaji wa umma unaowekezwa katika mashirika husika iweze kupatikana.

### 3.3 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kueleza Shughuli za Kamati na maoni ya jumla, naomba kutoa Mapendekezo kama ifuatavyo: -

#### 3.3.1 Kukosekana kwa Kiwanda cha Uzalishaji katika Kampuni ya Mbolea (TFC)

**KWA KUWA,** mtaji wa umma unaotumika katika Kampuni ya Mbolea Tanzania una lengo la kuwezesha uzalishaji wa mbolea kwa kiwango cha kutosheleza mahitaji nchini na kuuza nje ya nchi, lakini mtaji huo hautumiki hivyo kutokana na kukosekana kwa kiwanda cha uzalishaji wa mbolea;

**NA KWA KUWA,** kukosekana kwa kiwanda cha uzalishaji mbolea kunasababisha TFC iagize mbolea kutoka nje ya nchi jambo linaloongeza gharama kwa TFC na kukwamisha manufaa ya mtaji unaowekezwa;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia TFC kwa kushirikiana na Sekta binafsi ijenge kiwanda cha kuzalisha mbolea kwa lengo la kuipunguzia Serikali mzigo wa gharama inayoingia katika kuagiza mbolea, na kuiwezesha TFC kutekeleza malengo mahususi ya kuanzishwa kwake.

#### 3.3.2 Kutotekelezwa Ipasavyo kwa Majukumu Yaliyorithiwa Kutoka Shirika Hodhi la Mashirika ya Umma – CHC

**KWA KUWA,** Msajili wa Hazina alipewa majukumu ya iliyokuwa CHC ili kuendeleza usimamizi wa mitaji, urekebishaji, ufuatiliaji na tathmini ya mali za umma lakini

(i) Hajakamilisha tathmini ya mali alizokabidhiwa kutoka CHC jambo linalosababisha watu kutumia mali hizo kwa manufaa binafsi;

(ii) Hawajatafutwa wawekezaji wanaoweza kubinafsishiwa au kukodishiwa mali hizo zilizotathminiwa; na

(iii) Yapo mashamba yaliyofanyiwa tathmini ambayo hayatumiki na taasisi nyingine za umma zinayahitaji kwa shughuli nyingine kama vile kiuchumi, utafiti na kilimo.

**NA KWA KUWA,** mambo hayo yanasababisha

(i) Ofisi ya Msajili wa Hazina kuingia gharama za utunzaji wa mali zinazosimamiwa bila matumizi yeyote;

(ii) Uchakavu wa mali kutokana na kuchelewa kwa mchakato wa kupata wawekezaji;

(iii) Kukosekana kwa manufaa ya mali zilizofanyiwa tathmini na ambayo yanaweza kutumika kwa shughuli nyingine;

(iv) Kuingia gharama za ulinzi bila manufaa kwa umma kutokana na kuendelea kwa migogoro baina ya Serikali na wawekezaji binafsi.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali kupitia Msajili wa Hazina ikamilishe tathimini ya kubaini mali zote zilizorithiwa kutoka CHC na ziwe chini ya uangalizi wake;

(ii) Kwa mali zinazoweza kutolewa kwa wawekezaji ufanyike mchakato wa haraka wa kutafuta wawekezaji ili ziweze kuendelezwa na kutumika, ili kuondoa mzigo wa gharama za ulinzi ambazo zinalipwa huku zikiwa hazizalishi;

(iii) Mashamba yaliyokuwa chini ya uangalizi wa Msajili wa Hazina yakabidhiwe kwa taasisi za Serikali zenye uhitaji hususani taaasisi za Utafiti na Kilimo;

(iv) Kwa mali ambazo bado zina migogoro na wawekezaji wake wa awali mfano MOPROCO na Tembo Chip Board, Serikali ikamilishe mchakato wa majadiliano na wawekezaji ili mali hizo zianze kutumika na kuzalisha.

### 3.3.3 Tija ndogo katika uendeshaji wa Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (BRT)

**KWA KUWA**, mradi wa mabasi yaendayo kasi Dar es Salaam unakabiliwa na changamoto kama vile:-

(i) Upungufu wa mabasi kwa awamu ya kwanza (Kimara – Kivukoni) yenye mabasi 100 yanayofanya kazi badala ya 305;

(ii) Kuchelewa kukamilika kwa mchakato wa kumpata mwendeshaji katika awamu ya pili (Mbagala rangitatu – Katikati ya Jiji);

**NA KWA KUWA,**

(i) Changamoto hizo zisipotatuliwa, mtaji mkubwa wa umma uliotumika katika ujenzi wa miundombinu utakuwa umepotea;

(ii) Mkopo wa fedha uliotafutwa kwa ajili ya kuwekeza kwenye miundombinu hiyo utarejeshwa bila ya manufaa ya uwekezaji kupatikana;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali isimamie kikamilifu uendeshaji wa mradi huu kwa kuhakikisha awamu zote zilizokamilika zinaendeshwa kwa ufanisi kwa lengo la kupata tija ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali katika mradi huu ikizingatiwa kuwa sehemu ya fedha za kutekeleza mradi huu ni fedha za mkopo na zitahitajika kurejeshwa.

### 3.3.4 Kukosekana kwa mawasiliano ya barabara katika Stesheni za Mizigo kwenye Reli ya Kisasa – SGR

**KWA KUWA,** Chumo (Returns) kutokana na mtaji mkubwa uliowekezwa katika SGR linategemea takribani asilimia 90 kutokana na usafirishaji wa mizigo na kwamba usafirishaji huo unategemea muunganiko wa reli na barabara;

**NA KWA KUWA,** kukosekana kwa miundombinu ya reli na barabara kunapunguza uwezekano wa mapato na ufanisi wa SGR katika kuwezesha chumo la uwekezaji;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia TARURA na TANROADS iweke miundombinu wezeshi kwa maeneo yote yenye stesheni za mizigo kwa ajili ya kufanikisha mawasiliano ya stesheni hizo na Barabara za kusafirisha mizigo pindi inapofika.

### 3.3.5 Kusuasua kwa Matumizi ya Mtaji wa Umma katika Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania – TEMESA

**KWA KUWA,** Mtaji wa umma uliowekezwa kwa Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania ulilenga kuwezesha huduma za kiufundi kwa magari na mitambo ya Serikali;

**NA KWA KUWA**, mtaji wa uendeshaji wa TEMESA ulikaribia kuisha kwa asilimia 90.4 ambapo uliporomoka kutoka shilingi bilioni 19.8 mwaka 2021/22 hadi shilingi billioni 1.9 mwaka 2022/23 jambo linalosababisha kusuasua kwa matumizi ya mtaji wa umma,

**NA KWA KUWA,** hali hiyo ni ishara ya kudorora kwa TEMESA jambo linalohitaji mageuzi makubwa na mabadiliko ya sheria.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba

a) Serikali kupitia Msajili wa Hazina ifanye mapitio ya TEMESA na uandaliwe mpango wa mageuzi kwa lengo la kufufua taasisi na kuiwezesha kujiendesha kwa ufanisi zaidi.

b) Serikali ifanye mabadiliko ya sheria na TEMESA iingizwe katika taasisi zinazojiendesha kibiashara kwa kuzingatia kuwa aina ya huduma inazotoa ni huduma zinazohitajika sokoni kwa ujumla na si kwa Serikali tu.

### 3.3.6 Changamoto ya Mizania ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL).

**KWA KUWA**, imebainika kuwa ATCL inakabiliwa na changamoto kubwa ya mizania ya hesabu zake kuwa vibaya, hali inayotokana

na kuendelea kukodi ndege kutoka TGFA na kubebeshwa mzigo wa malipo ya matengenezo na ukodishaji;

**NA KWA KUWA,** jambo hili linasababisha hali ya fedha ya shirika kutoakisi uhalisia na kuvuruga uwezo wa shirika kukopa kwa ajili ya kuendelea kibiashara;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali ikamilishe mchakato wa kuhamisha ndege kutoka TGFA kuja ATCL hadi kufikia Juni, 2025 ili kulipunguzia shirika gharama za uendeshaji na kuweza kujitanua katika masoko/nchi ambazo kwa sasa haiwezi kufika; na

(ii) Serikali ifanye mchakato wa kufuta madeni ya TGFA kwa ATCL kwa lengo la kuweka sawa mizania ya vitabu vya shirika.

**3.3.7 Shirika la Bima la Taifa – NIC kuajiri kwa njia ya mkataba badala ya kuwa na ajira za moja kwa moja (Permanent and Pensionable)**

**KWA KUWA,** manufaa ya mtaji wa umma unaowekezwa katika uwekezaji yanategemea uwezo wa watumishi wanaoajiliwa katika taasisi hizo;

**NA KWA KUWA**, shirika la bima limebainika kukosa mkakati bora wa ajira ya watumishi kwa ajili ya uendeshaji wa shirika jambo linalosababisha:-

i) Kutumia utaratibu wa kuajiri kwa mikataba ya muda mfupi; na

ii) Shirika kuwa na watumishi wasiokuwa na uhakika wa ajira yao jambo linaloathiri uwezo wao wa kiutendaji.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Msajili wa Hazina isimamie na kuhakikisha NIC inapata vibali vya kuwa

na watumishi wa ajira za kudumu kwa lengo la kuleta tija katika usimamizi wa mtaji wa umma uliowekezwa NIC.

### 3.3.8 Changamoto Katika Kutumia Mfumo wa Manunuzi – *NEST* kwa Mashirika ya Kibiashara

**KWA KUWA**, taasisi zote za umma yakiwemo mashirika ya umma yanayotumia mtaji wa umma kujiendesha kibiashara yanalazimika kutumia mfumo wa ununuzi wa NEST ambao una mlolongo usioendana na kasi ya kushindana kibiashara;

**NA KWA KUWA,** masharti hayo kwa taasisi zinazotumia mtaji wa umma kujiendesha kibiashara yanazinyima uwezo wa kutumia mitaji ya umma ipasavyo kushindana kibiashara na hivyo; (i) Kukosa ufanisi katika uendeshaji wa mitaji ya umma; (ii) Kutomudu ushindani katika tasnia za biashara zake.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye maboresho ya Kanuni hizi ili ziweze kuleta uhalisia na wepesi, na kukidhi mahitaji ya wakati kwa mashirika ya umma yanayofanya biashara ili kuweza kutumia mfumo wa manunuzi kwa wepesi na haraka na kuyawezesha kuchangamkia fursa za biashara pale zinapojitokeza.

## 3.4 Hitimisho

### 3.4.1 Shukurani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini katika kuliongoza Bunge letu tukufu ikiwa ni pamoja na kunipa fursa ya kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. Utekelezaji wa majukumu ya kamati umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na maelekezo ya kiti chako ikiwa ni pamoja na ushauri, miongozo na msaada uliotupatia kwa kipindi chote cha mwaka mzima. Pia, naomba nimshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kukusaidia katika kuendesha Bunge.

Kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu

Hassan kwa kuhakikisha kunakuwa na usimamizi bora katika Taasisi na Mashirika ya Umma na kuweka msukumo wa hali ya juu katika kuimarisha uwekezaji wa Umma.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kwa kutekeleza majukumu ya kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha, nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya kamati na kunipa heshima ya kuiwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako tukufu. Naomba kuwatambua wajumbe kwa majina yao kama yanavyoonekana hapo chini:-

1. Mhe. Augustine Vumma Hole, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Mary Fransis Msanja, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Abbas Gulam Tarimba, Mb
4. Mhe. Aeshi Alfan Hillary, Mb
5. Mhe. Aida Joseph Kenani, Mb
6. Mhe. Amina Daud Hassan, Mb
7. Mhe. Assa Nelson Makanika, Mb
8. Mhe. Bonah Ladislaus Kamoli, Mb
9. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb
10. Mhe. Charles Muguta Kajege, Mb
11. Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo, Mb
12. Mhe. Dkt. Pius Stephen Chaya, Mb
13. Mhe. Francis Kumba Ndulane, Mb
14. Mhe. Fratey Gregory Massay, Mb
15. Mhe. George Natany Malima, Mb
16. Mhe. Haji Amour Haji, Mb
17. Mhe. Maryam Azan Mwinyi, Mb
18. Mhe. Matha Nehemia Gwau, Mb
19. Mhe. Nora Waziri Mzeru, Mb
20. Mhe. Zuena Athumani Bushiri, Mb
21. Mhe. Santiel Erick Kirumba, Mb
22. Mhe. Nicholaus George Ngassa, Mb
23. Mhe. Angellah Jasmine Kairuki, Mb

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile, naomba kuwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Msajili wa Hazina wakiongozwa na Ndg. Nehemiah Mchechu (Msajili wa Hazina) kwa ushirikiano wa dhati

walioutoa kwa kamati. Wamesaidia kushauri namna bora ya kuzifanya taasisi na mashirika ya umma, kuwa na ufanisi katika utendaji na uwekezaji wake kwa lengo la kuleta tija ya uwekezaji wa serikali katika vitega uchumi vyake.

**Mheshimiwa Spika**, pia napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndg. Baraka Idelphonce Leonard, kwa ushirikiano walioutoa ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri stahiki na kuiwezesha kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati.

### 3.4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii imetokana na uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (*PIC*) kuhusu utekelezaji na usimamizi wa uwekezaji wa mitaji ya umma unaofanywa na taasisi na mashirika ya umma. Maoni na mapendekezo yanayotokana na uchambuzi huu, yanalenga kuishauri serikali katika eneo la uwekezaji wa mitaji ya umma ili uwekezaji uweze kufanyika kwa ufanisi na hatimaye kuleta tija kwa taifa.

Naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa liipokee taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuhusu uchambuzi wa uwekezaji wa mitaji ya umma kwa kipindi cha Mwaka 2024, kuijadili na hatimaye kuridhia maoni na mapendekezo yake ili Serikali iweze kuyafanyia kazi**.**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako sasa lipokee Taarifa ya Kamati na likubali Maoni na Mapendekezo yote ya Kamati kama yalivyo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Augustine Vumma Hole, Mb

**MWENYEKITI, KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA**

10 Februari, 2025

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. *(Makofi)*

Namwita sasa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ili aweze kuwasilisha taarifa yake.

**MHE. ORAN M. NJEZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa majukumu katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025, pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu Mwaka, Julai hadi Desemba, 2024 na mwelekeo hadi Juni, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yote ya Kamati iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa leo asubuhi. Mgawanyo wa taarifa pamoja na majukumu yaliyotekelezwa na Kamati ni kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya utekelezaji kwa mwaka wa bajeti 2023/2024 imeonesha ufanisi mkubwa sana wa utekelezaji wa Serikali, utekelezaji ulikuwa kwa zaidi ya 96%. Huu ni utekelezaji wa ufanisi wa hali ya juu, ni *outstanding performance* na tunampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utekelezaji huu ikiwa ni pamoja na changamoto zote za uchumi za kidunia, lakini Serikali yake kwa kweli imeweza kuonesha utekelezaji mzuri wa kiasi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ridhaa ya matumizi iliyotolewa katika kipindi hicho ilikuwa ni shilingi trilioni 42.95, ikiwa ni zaidi ya shilingi bilioni 24.6 ya fedha zilizokusanywa. Tofauti ya mapato na

ridhaa ya matumizi iliyotolewa iligharamiwa na mkopo wa muda mfupi kutoka Benki Kuu *(overdraft)* ambao unaruhusiwa chini ya Vifungu vya 34 na 35 vya Sheria ya Benki Kuu Sura ya 197. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo pia ulionesha kuwa bajeti iliyotengwa kwa ajili ya miradi kwa mwaka 2023/2024 ilikuwa shilingi trilioni 14.08 ambayo ilikuwa ni 31% ya bajeti yote ya Serikali; na kwa kipindi hicho fedha ambayo ilikuwa imetolewa ilikuwa ni shilingi trilioni 14.64 sawa na 104%. Hiyo ina maana kuwa fedha zilizotolewa zilikuwa ni zaidi kwa asilimia nne kuliko zile zilizokuwa zimepagwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipochambua utekelezaji wa mpango huu ilibaini changamoto ndogo ndogo zifuatazo: -

(a) Miradi kuchelewa kuanza kutekelezwa na kukamilika tofauti na muda uliopangwa;

(b) Majadiliano baina ya Serikali na wabia kuchukua muda mrefu na kuchelewesha miradi kuanza kutekelezwa;

(c) Uwepo wa malimbikizo ya madeni ya wazabuni na wakandarasi ambao umesababisha baadhi ya miradi kukwama utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hizo, Kamati ilishauri Serikali masuala yafuatayo: -

(a) Kutekeleza miradi michache ambayo itakamilika kwa wakati ili kuleta tija inayokusudiwa;

(b) Kuanzisha Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini *(M&E)* ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa ubora kulingana na thamani ya fedha pamoja na kuongeza uwajibikaji kwa Watumishi wa Umma;

(c) Ulipaji wa madeni ya wazabuni na wakandarasi upewe kipaumbele ili kupunguza gharama za riba zinazotokana na kutokulipa madeni kwa wakati; na

(d) Kuanzisha utaratibu maalum wa kusamehe ada za leseni kwa miradi ambayo inatekelezwa na Taasisi moja ya Serikali na kisha kulipa kwenye Taasisi nyingine ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa Mwaka 2025/2026 imeonesha kuwa Serikali inakusudia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi trilioni 55.06. Mgawanyo wa mapato na matumizi ni kama inavyoonekana katika jedwali Na. 2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha nusu mwaka 2024/2025 ilionesha viashiria vya uchumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pato la Taifa katika mwaka 2024 lilitarajiwa kukua kwa 5.4% na kwa ubora zaidi. Pia, utekelezaji wake ulikuwa zaidi ya 5.4%, ikiwa ni sawa na lengo la mwaka. Hivyo, ni dhahiri kuwa lililopangwa la 5.4% na zaidi, Kamati imebaini kuwa moja ya shughuli zilizochangia katika ukuaji huo ni pamoja na kuanza kwa uzalishaji wa umeme kupitia Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere ambapo mitambo nane kati ya tisa imeanza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutekeleza mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za kilimo kwa mwaka huu zimeongoza kwa kuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi kwa 24.4%, ikifuatiwa na ujenzi 13.2%. Pia, uchimbaji madini kwa 9.8%, na biashara 8.6% kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 1 kwenye Taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa ushauri ufuatao: -

(a) Kwa kuwa Sekta ya Kilimo ina mchango mkubwa katika pato la Taifa, Serikali ihakikishe kwamba mikopo inayoelekezwa katika sekta hiyo inajikita katika shughuli za uzalishaji wa kilimo badala ya uchuuzi au biashara za mazao;

(b) Serikali kuimarisha ushirikiano wa kibiashara na nchi nyingine ili kupata masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini kama vile chakula; na

(c) Kuweka mazingira wezeshi ya wachimbaji wadogo kupata mikopo nafuu kupitia mpango wa kuongeza uzalishaji wa dhahabu nchini *(Domestic Gold Purchase Program - DGPP)* kwa kutumia mifuko ya udhamini wa mikopo, Benki Kuu ikishirikiana na *STAMICO* na viwanda binafsi vya kuchenjua dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye sekta ya nje ilionesha kuwa katika kipindi cha Julai hadi Novemba, 2024 nakisi ya urari wa biashara ya huduma za uhamishaji mali nje ya nchi ilipungua kwa kufikia dola za Marekani milioni 364 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 807.8 kwa mwaka 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu utekelezaji au haya matokeo ni mazuri sana kwa vile imeonesha kuwa urari wetu umeweza kuwa bora kwa asilimia zaidi ya 100 ukilinganisha na mwaka 2023. Hii ilitokana na ongezeko la mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi hususan mapato yanayotokana na utalii na mauzo ya bidhaa asilia ikilinganishwa na kasi ndogo ya thamani ya uzalishaji wa bidhaa na huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Sekta ya Utalii imeendelea kuongoza katika kuliletea Taifa mapato ya kigeni, mafanikio haya yanatokana na maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipoamua kutangaza utalii kupitia filamu ya *Royal Tour* ya mwaka 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi wa takwimu zilizopo kwenye Jedwali Namba Tatu na ina ushauri ufuatao kwa Serikali: -

(a) Kuwekeza kwenye miundombinu ya utalii, kufanya mapitio ya gharama za kutembelea vivutio vyetu pamoja na kuvutia ujenzi wa hoteli za nyota tano ili sisi tuwe bora kuliko washindani wetu;

(b) Kuvutia uwekezaji kwenye ujenzi wa viwanda ili kuongeza thamani ya mazao yanayouzwa nje kwa sababu mazao ya kilimo ambayo hayajachakatwa kwa bei hubadilika kulingana na upatikanaji *(Elastic),* hivyo mazao yaliyoongezwa thamani yana uwezo wa kutunzwa kwa muda mrefu na kuyauza pale bei zinapopanda; na

(c) Kutafuta masoko ya mazao mengine ya biashara ambayo yanaweza kuchangia fedha za kigeni kama vile pareto, katani, chai, matunda na mbogamboga, kwa sababu kwa muda mwingi mazao tunayotegemea ni korosho, kahawa na tumbaku jambo ambalo ni hatarishi endapo bei za mazao haya itatetereka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu deni la Serikali. Deni letu la Serikali limeendelea kuwa himilivu. Pamoja na kuwa himilivu Kamati ina ushauri ufuatao:-

(a) Serikali ihakikishe inakopa zaidi mikopo yenye masharti nafuu *(concessional loans)* badala ya mikopo ya kibiashara yenye riba kubwa. Hatua hii itapunguza gharama za kuhudumia deni;

(b) Kuongeza makusanyo ya ndani ili yaweze kugharamia ulipaji wa deni; na

(c) Serikali kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kutumia njia mbadala za kufadhili miradi kama vile ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(PPP)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenendo wa Mapato na Matumizi. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba Serikali imeendelea kukusanya mapato kwa mwenendo mzuri. Hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha, inaweza kukusanya mapato kwa 100% au zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni la kupongeza, kwani mikakati iliyowekwa na Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

katika kutekeleza sera za kibajeti zimeonyesha ufanisi wa ukusanyaji wa mapato unaosimamiwa kuvuka malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio haya siyo tu yanadhihirisha usimamizi madhubuti wa fedha za umma, bali pia ni ishara ya juhudi ya dhati ya kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jedwali Namba Tano linaonyesha mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ambapo Serikali imeweza kukusanya mapato kwa zaidi ya 100% ikilinganishwa na lengo la nusu mwaka. Ufanisi huu umechangiwa na upatikanaji wa fedha kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo ambapo hazikuwepo katika maendeleo ya mapato yaliyoidhinishwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa ufanisi huo. Hata hivyo, Kamati inatoa ushauri ufuatao: -

(a) Serikali iendelee kuweka mikakati madhubuti ya kuongeza wigo wa walipa kodi, kwa kuwatambua na kuwapa motisha wafanyabiashara wadogowadogo wanaofanya biashara katika sekta isiyo rasmi;

(b) Serikali ichukue hatua thabiti za kupunguza matumizi ya fedha taslimu kwenye kufanya malipo; na

(c) Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* ihakikishe mifumo inasomana ili kurahisisha ulipaji wa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mwenendo wa ukusanyaji wa mapato hadi mwezi Desemba, nao umeonesha ufanisi mkubwa. Serikali imeweza kukusanya kama nilivyosema mwanzo katika nusu mwaka kwa asilimia zaidi ya 100 ya miezi sita. Hiyo ni pamoja na pesa za marejesho ya kodi ambazo ilikuwa ni shilingi trilioni 1.09 sawa na 105% ya lengo la mwaka la kufanya marejesho ya shilingi trilioni 1.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ufanisi huu wa ukusanyaji wa mapato na kufanya marejesho ya kodi kwa wafanyabiashara kusimamia vizuri na miongozo ya kukusanya kodi pamoja na kutimiza ulipaji wa kodi kwa hiari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba 72.05% ya mapato hayo ambayo ilikuwa ni shilingi trilioni 1.16 imetokana na mchango wa mafungu matatu tu kati ya 62 ya makusanyo yasiyo ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini mafungu 59 ya mchango mdogo katika makusanyo kwa sababu hayatumii mifumo kikamilifu katika ukusanyaji wa mapato. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa taasisi zote za Serikali zinatumia mifumo katika kukusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa katika shilingi trilioni 1.61 ya mapato yote yasiyo ya kodi Ofisi ya Msajili wa Hazina imekusanya shilingi milioni 479. Haya ni matunda ya mageuzi katika uendeshaji wa mashirika ya umma, kujiendesha kibiashara na yanayofanywa chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mwenendo wa matumizi umeonesha kuwa, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi trilioni 49.35. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 33 ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 15.96 ni fedha za matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Desemba, 2024 Serikali iliidhinisha matumizi ya jumla ya shilingi shilingi trilioni 55.78 ambayo ni sawa na 52% ya lengo la mwaka. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 16.27 ni matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 9.52 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilipitia na kuchambua matumizi hayo na kubaini yafuatayo: Wakati wa uchambuzi wa utekelezaji kwa kipindi cha nusu mwaka, Kamati ilibaini kuwa kulikuwa na

uhamisho wa fedha kiasi cha shilingi bilioni 898 ambapo zilikuwa ni fedha za matumizi mengineyo na shilingi bilioni 984 ni fedha za maendeleo ya ndani kwa Wizara, Idara zinazojitegemea na Taasisi za Serikali. Fedha hizo zilihamishwa na kupelekwa kwenye mafungu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti Sura 43, Kifungu cha 44(3)(c) kinaeleza kuwa jumla ya fedha zitakazofanyiwa uhamisho kutoka fungu husika kutozidi jumla ya matumizi yaliyoidhinishwa katika fungu hilo kwa mwaka huo wa fedha. Hata hivyo, uhamisho uliofanywa katika baadhi ya mafungu umeonesha uhamisho wa zaidi ya 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni bajeti iliyoidhinishwa kwenye Fungu namba Saba la Msajili wa Hazina, ambalo lilikuwa na shilingi bilioni 36.5; lakini uhamisho uliofanyika ni shilingi bilioni 115.5, sawa na 316%. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa uhamisho wa fedha katika mafungu unazingatia sheria na kanuni zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Kamati inaendelea kusisitiza Maafisa Masuuli kuzingatia vipaumbele vya msingi katika upangaji wa bajeti ili kutoathiri utekelezaji wa bajeti wa mafungu mengine unaotokana na uhamisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Kamati imebaini kuwa Serikali ilikuwa imepokea shilingi bilioni 945.7 ambazo hazikuwa sehemu ya makisio ya bajeti kufuatia mabadiliko hayo. Serikali inapendekeza kuongeza ukomo wa bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kutoka shilingi trilioni 490.35 hadi shilingi trilioni 50.19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mfumo wa bajeti wa mwaka 2024/2025 unaopendekezwa ni kama unavyoonekana katika kiambatanisho Na. 1(a).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza mipango ya Bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati inaishauri Serikali, kuwasilisha Bungeni marejeo ya bajeti *(supplementary budget)* kama Ibara ya 137(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 pamoja na Kifungu cha 43 cha Sheria ya Bajeti sura 439 zinavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tathmini ya utekelezaji wa maboresho ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2024. Katika mabadiliko ya sheria, mapato ya shilingi bilioni 439.56 yalitarajiwa kuongezeka kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2024, Serikali ilikusanya shilingi bilioni 283.01 ikiwa ni sawa na 64.38% ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa ufanisi huu ambao unaonyesha kwa nusu mwaka makusanyo yalikuwa ni zaidi ya 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya maboresho ya Sheria Na. 29 kama zinavyoonekana katika Taarifa ya Kamati. Serikali ilifanya marekebisho kwa kupunguza mrabaha kutoka asilimia sita hadi asilimia nne kwenye madini ya dhahabu yanayouzwa Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Desemba, 2024 *BoT* ilikuwa imenunua dhahabu zenye uzito wa kilo 2,323, sawa na 77% ya lengo la kilo 3,000 katika kipindi cha nusu mwaka. Aidha, dhahabu iliyonunuliwa ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 483, sawa na dola za Marekani milioni 198 na mrabaha uliokusanywa ni shilingi bilioni 19. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kwamba, Benki Kuu itavuka lengo la kununua dhahabu yenye thamani ya dola za Marekani milioni 350 kwa mwaka huu wa fedha wa 2024/2025 kwa sababu kumekuwa na mwitikio chanya kwa wachimbaji kuiuzia Benki Kuu. Hivyo, Benki Kuu imeiomba bodi yake kuongeza wigo wa fedha ili iweze kununua dhahabu kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali ilifanya mabadiliko ya sheria ili kuweka takwa la wamiliki wa leseni ya uchimbaji wa

madini na takwa la wamiliki wa leseni za wafanyabiashara wa madini kutenga kiasi cha madini kwa ajili ya kuchakatwa nchini na kuyeyushwa, ambayo ilikuwa ni 20% ya dhahabu yote. Hadi kufikia Desemba, kilo 3,238 zimechenjuliwa na kusafishwa nchini ikilinganishwa na kilo 411 tu za mwaka 2023/2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa mud awa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kidogo. Naomba uende sasa moja kwa moja kwenye maoni na mapendekezo mahsusi. *(Makofi)*

**MHE. ORAN M. NJEZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Pamoja na maelezo hayo, Kamati ina mapendekezo mahsusi yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukusanyaji wa Kodi ya Majengo:-

KWA KUWA, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea kusimamia utekelezaji wa jukumu la ukusanyaji wa kodi ya majengo kwa mujibu wa sheria ya fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 Kifungu cha 6(1)(f) na 7(1)(y);

NA KWA KUWA, moja ya mabadiliko yaliyofanywa na Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023 katika Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura 289 ni kuondoa jukumu la ukusanyaji wa kodi hiyo kutoka *TRA* kwenda katika Serikali za Mitaa.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia yafuatayo: -

(i) Kuhakikisha kiwango cha mapato cha 20% cha kodi ya majengo kinarejeshwa katika halmashauri kwa wakati, pamoja na kuangalia uwezekano wa kuongeza kiwango hicho;

(ii) Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali iongeze kiwango kinachorejeshwa kutoka 20% hadi 50% kwa kipindi cha zoezi la usajili wa majengo ili kuharakisha zoezi la uchambuzi wa uthamini ya majengo pamoja na kuandaa rejista na kisha kurudisha 20% baada ya zoezi hilo;

(iii) Kuboresho Mfumo wa Tausi ili kuwezesha ukusanyaji wa kodi ya majengo uwe ni sehemu ya usimikaji wa moduli za kodi ya majengo katika Mfumo wa Tausi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 137; na

(iv) Kuajiri wataalamu wa kutosha katika halmashauri kwa ajili ya kufanya zoezi la uthamini wa majengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu misamaha ya kodi:-

KWA KUWA, Serikali imekuwa inatoa misamaha ya kodi mbalimbali kwa wawekezaji pamoja na wafanyabiashara kwa lengo la kuvutia uwekezaji nchini;

NA KWA KUWA, kiwango cha utoaji wa misamaha ya kodi kinatakiwa kutozidi asilimia 1.3 ya pato la Serikali kwa mwaka 2024. Tafiti zinaonesha kwamba changamoto kubwa ya uwekezaji nchini ni mazingira mabovu ya ufanyaji biashara na uwekezaji na siyo viwango vya kodi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Serikali kufanya tathmini ya misamaha yote ya kodi ili kuhakikisha kwamba misamaha inayotolewa ina tija na inakuwa ndani ya kiwango kinachokubalika cha chini ya asilimia 1.3 ya pato la Taifa. Aidha, Serikali iendelee kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kupewa uwezo wa kufanya uchunguzi wa kodi *(tax Investigation),* Kamati inashauri *TRA* iwe inafanya uchunguzi wa masuala ya kodi ili kubaini ubadhirifu unaofanywa na kampuni au wafanyabiashara wasio waaminifu na kuwachukulia hatua

kwa mujibu wa sheria za kodi pale inapobainika mfanyabiashara au Kampuni ina makosa.

KWA KUWA, katika kufanya chunguzi hizo huwa wanatumia Askari Polisi ambao hawana utaalamu kuhusu masuala ya kodi na wakati huo ndiyo wanatakiwa kuchukua maelezo ya mtuhumiwa, hatua, hii imekuwa inafanya Mamlaka ya Mapato kupoteza kodi ambayo inatakiwa kukusanywa pindi shitaka linapofika mahakamani;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani pamoja na Wizara ya Fedha kufanya kikao cha pamoja kabla ya Vikao vya Kamati vya mwezi Machi, 2025 ili kubainisha utaratibu utakaotumika kuondokana na changamoto hii. Endapo itaonekana kuna ulazima wa kufanya mabadiliko ya sheria, mabadiliko hayo yafanyike katika Sheria ya Fedha ya Mwaka 2025. Aidha, Taarifa ya kikao hicho na maamuzi yake yawasilishwe kwenye Kamati ya Bajeti.

KWA KUWA, Serikali katika kipindi cha miaka mitatu imekuwa ikibainisha mikakati mbalimbali ya kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ikiwemo kupunguza ununuzi wa magari ya Serikali na badala yake kuanzisha utaratibu wa kuwakopesha magari watumishi wenye stahili hiyo.

NA KWA KUWA, mikakati hiyo imekuwa haitekelezwi ipasavyo ambapo katika mwaka wa fedha 2022/2023 kiasi cha shilingi bilioni 500 kilitengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Serikali ifanye marejeo ya kina ya matumizi ya Serikali na kupunguza matumizi yasio ya lazima kabla ya kuanza utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa miaka mitano unaotarajiwa kuanza mwaka 2025/2026 hadi 2030/2031. Tathmini hiyo itasaidia kupata fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, mifuko ya hifadhi ya jamii imekuwa inafanya uwekezaji usio na tija ambapo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, 2022/2023, Mfuko wa *PSSSF* umelipa mafao ya wastaafu yenye thamani ya shilingi trilioni 4.34

na kupata faida ya shilingi trilioni 1.8, takwimu hizi zinaonyesha kwa kiasi kinacholipwa ni kikubwa ukilinganisha na faida inayopatikana na uwekezaji wake; vilevile, kiwango cha uhimilivu cha Mfuko ni 36.4% ikilinganishwa na kiwango kinachokubalika cha 60% na lengo la chini la uhimilivu ni 40%. *(Makofi)*

KWA KUWA, usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hufanywa na Benki Kuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu kwa mujibu wa Sheria ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali ihakikishe kuwa mifuko hii inasimamiwa ipasavyo katika kuhakikisha kuwa, uwekezaji unaofanywa ni wa tija na unaendana na michango. Hatua hii itasaidia kupunguza vihatarishi na kuwezesha mifuko kulipa mafao ya wastaafu kwa wakati. *(Makofi)*

KWA KUWA, Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370 inaipa mamlaka Ofisi ya Msajili wa Hazina kusimamia uwekezaji wa mali nyingine za Serikali katika taasisi, mashirika ya umma pamoja na kampuni ambazo Serikali inamiliki hisa chache. Vilevile, Sheria inampa Msajili wa Hazina mamlaka ya kusimamia, kuweka malengo ya kifedha pamoja na kutathmini ufanisi wa utendaji kazi.

NA KWA KUWA, Mashirika mengi yamekuwa yakijiendesha chini ya ufanisi ambapo katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita kwa mashirika ambayo Serikali inamiliki hisa chache, Serikali imekuwa ikipata gawio kubwa ukilinganishwa na mashirika ambayo Serikali ina umiliki mkubwa. Vilevile, baadhi ya mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara na yalitakiwa kujitegemea bado yanapata ruzuku kutoka Serikali Kuu.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali kuondoa ruzuku kwa mashirika yanayojiendesha kibiashara, ili yaweze kujiendesha kibiashara, kukidhi bajeti zao na kutoa gawio kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekta ya Utalii:-

KWA KUWA, imeonekana kufanya vizuri kwa upande wa mapato yanayotokana na shughuli za utalii ambayo yamesababIsha kuimarika kwa urari wa biashara na huduma nje;

NA KWA KUWA, Taasisi za Uhifadhi wa Wanyamapori zinajiendesha kwa misingi ya kibiashara, utaratibu wa utolewaji wa fedha kama ilivyo kwa Wizara au Idara za Serikali umekuwa unaathiri utendaji kazi wake;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2025, ifanye mabadiliko ya kurejesha utaratibu wa taasisi hizi kukusanya na kutumia mapato yake kulingana na bajeti zilizoidhinishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifungu vitakavyotumiwa kufanyiwa marekebisho ni Kifungu cha Tisa cha Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura ya 282, Kifungu cha 12(2) cha Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro Sura ya 284 pamoja na Jedwali la Kwanza la Sheria ya Mamlaka ya Mapato Sura ya 399.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho haya yaende sambamba na kuondoa sheria hizo kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria ya Mamlaka ya Mapato Sura ya 399. Hatua hiyo itasaidia taasisi na mamlaka hizo kutumia mapato yake kuimarisha miundombinu ya msingi katika hifadhi ili kuvutia watalii zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ulipaji wa madeni ya wazabuni, wakandarasi na watoa huduma:-

KWA KUWA, changamoto ya ulipaji wa madeni ya wazabuni, wakandarasi na watoa huduma imekuwa ni jambo la muda mrefu na limekuwa likiathiri utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa miaka mitano mfululizo;

NA KWA KUWA, tangu mwaka 2022 ilipofanyika tathmini ya kina na kubaini Serikali inadaiwa shilingi bilioni 3,200 na tangu kipindi hicho haijafanyika tathmini ya kina kama hiyo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia masuala yafuatayo: -

(i) Serikali kufanya tathmini ya kina ya madeni yote ya wazabuni, wakandarasi na watoa huduma kuanzia mwezi Februari, hadi 30 Aprili, ili kubaini kiasi gani Serikali inadaiwa;

(ii) Serikali kuweka ukomo wa siku 90 wa uhakiki wa madeni kwa kufanya mabadiliko kwenye Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Sura ya 348, ili kuondoa kisingizio cha kuchelewesha kulipa kwa sababu ya kufanya uhakiki; na

(iii) Serikali kuwasilisha Taarifa ya tathmini kwenye Kamati ya Bajeti, sanjari na hatua za kulipa madeni hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizi zikifanyika zitaondoa madhira ambayo sekta binafsi nchini inapitia ikiwa ni pamoja na baadhi ya watu kufilisika kutokana na Serikali kutolipa kwa wakati. Pamoja na hayo maazimio, pia kulikuwa na mafanikio ambayo Kamati imeyaona.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kwenda kutoa hoja sasa tafadhali!

**MHE. ORAN M. NJEZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye hitimisho. Napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe. Bila kukushukuru, nisingekutendea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe pamoja na Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Rais wa *IPU* na Umoja wa Mabunge Duniani pamoja na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika kwa miongozo yenu ambayo imewezesha Kamati kuelekeza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; Mheshimiwa Hamad Chande, Naibu Waziri wa Fedha; Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Naibu Waziri Ofisi ya Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuwashukuru Dkt. Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha; Mlipaji Mkuu wa Serikali; Wataalamu kutoka Wizara ya Mipango na Uwekezaji wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Tausi Kida; pamoja na Wataalamu kutoka Tume ya Mipango ambao kwa ushirikiano wao, Kamati iliweza kufanya kazi yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge na Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kutekeleza Shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawapongeza kwa michango, maoni na ushauri wao ambao umesaidia Kamati kuisimamia Serikali ipasavyo. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama yalivyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru pia Ndugu Baraka Leonard Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake na kuratibu vyema Shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha kazi za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, naliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili taarifa na hatimaye kukubali maoni, ushauri, mapendekezo na maazimio Bunge ambayo yamewasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**10 FEBRUARI, 2025**

**TAARIFA YA MWAKA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI, 2024 HADI JANUARI, 2025 PAMOJA NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA NUSU MWAKA, JULAI HADI DESEMBA, 2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa majukumu katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025, pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu Mwaka Julai hadi Desemba, 2024 na mwelekeo hadi Juni, 2025.

### 1.1. Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu kumi kama ifuatavyo;

i. Sehemu ya kwanza ni Utangulizi;

ii. Sehemu ya Pili ni Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2023/24;

iii. Sehemu ya Tatu ni Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali Katika Kipindi cha Nusu Mwaka 2024/25;

iv. Sehemu ya Nne ni Tathmini ya Utekelezaji wa Maboresho ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2024;

v. Sehemu ya Tano ni Mwelekeo wa Viashiria vya Uchumi Jumla na Bajeti ya Serikali Hadi Juni, 2025;

vi. Sehemu ya Sita ni Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Kamati ya Mwaka 2024;

vii. Sehemu ya Saba ni Maoni na Mapendekezo ya Ujumla;

viii. Sehemu ya Nane ni Maoni na Mapendekezo Mahsusi;

ix. Sehemu ya Tisa ni Mafanikio na Changamoto katika Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati; na

x. Sehemu ya Kumi ni Hitimisho.

**1.2. Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa masharti ya Kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 pamoja na Nyongeza ya Nane, Fasili ya 9, ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilitumia nyaraka mbalimbali kama vile Hotuba za Bajeti za Serikali za mwaka Mwaka wa Fedha 2023/24 na 2024/25, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/222025/26), Mipango ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2023/24 na 2024/25, Taarifa mbalimbali za Taasisi za ndani na Kimataifa kama vile Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia (WB), Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na tafiti zilizofanywa na Taasisi binafsi za ndani na nje ya nchi.

**1.3. Majukumu yaliyotekelezwa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ilitekeleza majukumu yafuatayo: -

a) Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24;

b) Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha nusu mwaka 2024/25;

c) Kupitia na kujadili utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2023/24 na robo ya kwanza ya mwaka 2024/25;

d) Kuchambua na kujadili Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/25;

e) Kuchambua na kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha pamoja na mafungu tisa yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2023/24 pamoja na kuchambua na kujadili na kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha pamoja na Mafungu nane yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2024/25;

f) Kuchambua na kujadili utekelezaji wa Bajeti za Mifuko ya Mahakama, Bunge na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2023/24, pamoja na kujadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Mifuko hiyo kwa Mwaka wa fedha 2024/25;

g) Kuchambua na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26;

h) Kuchambua Taarifa za utekelezaji wa Bajeti na Utendaji kazi wa Wizara ya Fedha pamoja na Idara, Taasisi, Wakala na Mamlaka mbalimbali zilizo chini yake;

i) Kuchambua Taarifa ya utendaji kazi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2023/24 pamoja na kupokea na kujadili Taarifa kuhusu Usimamizi wa Mashirika ya Umma, ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi pamoja na Changamoto zilizopo;

j) Kushiriki mafunzo mbalimbali yenye lengo la kuwaongezea uwezo Wajumbe wa Kamati katika nyanja za kodi, fedha, uchumi, uwekezaji, ujenzi wa miundombinu pamoja na mifumo mbalimbali ya ukusanyaji na usimamizi wa mapato;

k) Kukutana na wadau mbalimbali kutoka sekta binafsi ili kupokea maoni, mapendekezo na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa sheria za kodi na zinazosimamia biashara na uwekezaji zinazoathiri Sekta binafsi;

l) Kufanya utafiti na uchambuzi wa vyanzo mbalimbali vya mapato na kutoa mapendekezo kuhusu vyanzo vipya vya mapato ili kupunguza utegemezi wa kibajeti;

m) Kutembelea na kukagua utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo; na

n) Kutembelea Taasisi mbalimbali ili kukagua utendaji kazi wake. Taasisi zilizotembelewa ni TRC, TAZARA, ATCL, TRA, DSFA na TPA.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2023/24

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2023/24 na katika utekelezaji wake ilibaini masuala yafuatayo:-

### 2.1. Viashiria vya uchumi jumla
### 2.1.1. Pato la Taifa

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2023 Pato la Taifa kwa bei ya kizio lilikua na kufikia **Shilingi trilioni 148.39** kutoka **Shilingi trilioni 141.25** mwaka 2022, sawa na ukuaji wa **asilimia 5.1** ikilinganishwa na **asimilia 4.7** mwaka 2022. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na shughuli za kilimo, ujenzi na uchimbaji madini ya thamani na vito. Ukuaji huu unaashiria kwamba Sera za kiuchumi za **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** zinaakisi malengo ya kupunguza umaskini.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kamati ilibaini kuwa sekta za huduma zilikua kwa kasi ikilinganishwa na sekta za uzalishaji kwa sababu ya uwekezaji mkubwa wa Serikali katika sekta hizo. Hivyo, Kamati

ilishauri kuendelea kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika ukuaji wa Pato la Taifa kwa kuweka mazingira bora ya biashara na uwekezaji kwa sababu sekta binafsi ndio injini ya ukuaji wa uchumi.

### 2.1.2. Mfumuko wa bei

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24 mfumuko wa bei ulikuwa **asilimia 3.2**, ikilinganishwa na **asilimia 4.7** ya mwaka 2022/23 kiwango ambacho kipo ndani ya lengo la nchi la kati ya **asilimia 3 hadi 5**, vigezo vya mtengamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (usiozidi **asilimia 8.0**) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (kati ya **asilimia 3 hadi 7**). Ufanisi huu ulichangiwa na kupungua kwa bei za nafaka hususan ngano, mchele, mahindi na mtama. Vyakula na vinywaji baridi vinabeba uzito wa **asilimia 28.2** ambayo ni kubwa kuliko bidhaa nyingine kwenye kapu la mlaji (*CPI*). Aidha, utekelezaji wa sera ya fedha ya kupunguza ukwasi na kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la Kimataifa katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24, kumechangia kupungua kwa mfumuko wa bei.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliishauri Serikali masuala yafuatayo: -

i. Ili kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei ni lazima Serikali iendelee kuongeza uwekezaji kwenye kilimo sambamba na kuimarisha hifadhi ya chakula; na

ii. Kuanzisha mkakati wa kuhifadhi akiba ya mafuta ya petroli pindi bei zinaposhuka na kuyatumia pindi bei zinapopanda ili kuepuka athari za mfumuko wa bei zinazoweza kusababishwa na kupanda kwa bei ya mafuta.

### 2.1.3. Mwenendo wa viwango vya ubadilishaji fedha

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2023, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa **Shilingi 2,516.9** ikilinganishwa na **Shilingi 2,320.5** mwaka 2022, sawa na kushuka kwa thamani ya Shilingi kwa **asilimia 8.5**. Kwa kiasi kikubwa kushuka kwa thamani ya Shilingi kulichangiwa na sera ya Marekani ya kuongeza viwango vya riba katika uwekezaji kwenye dhamana za Serikali

kutoka **asilimia 0.1 mwaka 2021** hadi **asilimia 5.3 mwaka 2024**. Hatua hiyo ilichangia kupungua kwa dola ya Marekani nchini na kushuka kwa thamani ya Shilingi.

**Mheshimiwa Spika**, madhara yaliyotokana na kushuka kwa thamani ya Shilingi ni kuongezeka kwa deni la Serikali, kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotegemea vifaa vinavyoagizwa kutoka nje na kuongezeka kwa gharama za bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi kama vile mbolea na mafuta ya petroli. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali ilichukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha thamani ya Shilingi dhidi ya dola ya Marekani inaimarika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliishauri Serikali njia pekee ya kuimarisha thamani ya Shilingi dhidi ya sarafu nyingine ni kuongeza mauzo ya bidhaa za asili nje, kuongeza thamani ya mazao, kuweka utaratibu mzuri wa kupokea fedha za uwekezaji unaofanywa na watanzania walio nje ya nchi na Benki Kuu ya Tanzania kuendeleza mpango wake wa kununua dhahabu.

### 2.1.4. Akiba ya Fedha za Kigeni

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/24, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa **dola za Marekani milioni 5,345,** kiwango kilichotosheleza malipo ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha **miezi 4.4**. Kiwango hicho kilichangiwa na ongezeko la **asilimia 14.7** la mauzo ya bidhaa na huduma nje, sanjari na kushuka kwa **asilimia 5.6** ya thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje katika kipindi hicho.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliishauri Serikali kuendelea kuchochea uzalishaji wa bidhaa za ndani ambazo zinaagizwa kutoka nje zinazoweza kuzalishwa ndani ya nchi mfano mafuta ya kula, mbolea, chuma, pamba na sukari sanjari. Pamoja na kuhamasisha matumizi ya gesi asilia ili kupunguza uagizwaji wa bidhaa kutoka nje, na kuendelea kuhifadhi dhahabu fedha kama sehemu ya akiba ya fedha za kigeni.

### 2.1.5. Deni la Serikali

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Juni, 2024 deni la Serikali lilikuwa **Shilingi bilioni 96,880** sawa na ongezeko la **asilimia 18.18** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 81,980** katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme na maji pamoja na kushuka kwa thamani ya Shilingi dhidi ya dola ya Marekani.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa takribani **asilimia 37.48** ya mapato ya ndani yaliyokusanywa katika mwaka 2023/24 yalitumika kulipa deni**.** Hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha mikopo inayopokelewa inaelekezwa katika miradi inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi pamoja na kuongeza wigo na ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuwa na uwezo wa kugharamia deni.

### 2.1.6. Mwenendo wa Mapato na Matumizi.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Serikali ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 44.39**. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2024 Serikali ilikusanya **Shilingi trilioni 42.92** kutoka vyanzo vya ndani na nje, sawa na **asilimia 96.7** ya lengo la mwaka. Kwa ufanisi huu wa utekelezaji wa bajeti, hakika **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** anastahili pongezi.

**Mheshimiwa Spika,** ridhaa ya matumizi iliyotolewa katika kipindi hicho ilikuwa ni **Shilingi trilioni 42.95**, ikiwa ni zaidi ya **Shilingi bilioni 24.6** ya fedha zilizokusanywa. Tofauti ya mapato na ridhaa ya matumizi iliyotolewa iligharamiwa na mkopo wa muda mfupi kutoka Benki Kuu (*overdraft*) ambao unaruhusiwa chini ya Vifungu vya 34 na 35 vya Sheria ya Benki Kuu Sura ya 197.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa bajeti Kamati ilibaini masuala yafuatayo:-

### 2.1.6.1. Madeni ya Wakandarasi

**Mheshimiwa Spika**, hadi mwaka 2022 Serikali ilikuwa ikidaiwa na Wazabuni, Wakandarasi na Watoa Huduma jumla ya **Shilingi bilioni 3,230**. Tangu kipindi hicho haijafanyika tathmini ya kina ya kubaini madeni yote Serikali inayodaiwa yaliyohakikiwa na ambayo hayajahakikiwa. Kamati ilifanya uchambuzi kuhusu sababu zinazosababisha ulimbikizaji wa madeni na ikabaini masuala yafuatayo: -

i. Ucheleweshaji wa malipo ya hati za madai zilizowasilishwa Wizara ya Fedha;

ii. Baadhi ya Maafisa Masuuli kufanya manunuzi bila ya kuwa na fedha za kulipia;

iii. Zoezi la uhakiki kuchukua muda mrefu zaidi ya siku tisini zinazokubalika kimataifa; na

iv. Matumizi ya dharura yanayoathiri Bajeti ya Mwaka husika na hivyo fedha za kulipia miradi inayotekelezwa kukosekana.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuondokana na changamoto ya malimbikizo ya madeni ambayo inaumiza wafanyabishara na sekta ya kibenki nchini, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya kina ya madeni inayodaiwa na baada ya kubaini kiasi halisi inachodaiwa ikope katika soko la ndani kupitia Hati fungani ya miaka 25 ili kuyalipa madeni yote kwa pamoja. Kutokufanya hivyo kunazidi kuiongezea Serikali gharama zinazotokana na riba na kupungua kwa ukwasi kwenye uchumi.

**Jedwali Na 1: Kiasi cha Madeni ambacho hakijalipwa hadi kufikia Tarehe 30 Juni, 2022**

| | MAELEZO | KIASI (Shillings) |
|---|---|---|
| 1. | Madeni yaliyohakikiwa lakini hayajalipwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 | 1,057,644,886,802.43 |
| 2. | Madeni ambayo Hayajahakikiwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 | 2,171,179,832,139.57 |
| | **JUMLA** | **3,228,824,718,942.00** |

**2.1.6.2. Uhamisho wa Fedha Ndani na Nje ya Fungu**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Uhamisho wa Fedha *(Re- allocation Warrant No.2 of 2022/23)* ilionyesha uhamisho wa jumla ya **Shilingi bilioni 1,610**. Aidha, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kiwango kikubwa cha uhamisho wa fedha kilisababishwa na baadhi ya Wizara, Idara na Taasisi kutozingatia vipaumbele vya msingi wakati wa upangaji wa bajeti. Hivyo, Kamati iliishauri Serikali kusimamia vyema kanuni za uhamisho wa fedha zilizotungwa chini ya Sheria ya Bajeti Sura ya 439.

**2.1.7. Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2023/24**

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2023/24 ulilenga kutekeleza miradi ya kielelezo na miradi ya kimkakati na bajeti iliyotengwa ya utekelezaji wa miradi na programu hizo ilikuwa ni **Shilingi trilioni 14.08** sawa na **asilimia 31.71** ya bajeti ya Serikali ya **Shilingi trilioni 44.39.** Hadi kufikia Juni 30, 2024 jumla ya **Shilingi trilioni 14.64** zilitolewa sawa na **asilimia 104.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua utekelezaji wa Mpango na kubaini baadhi ya changamoto zifuatazo: -

a) Miradi kuchelewa kuanza kutekelezwa na kukamilika tofauti na muda uliopangwa;

b) Majadiliano baina ya Serikali na wabia kuchukua muda mrefu na kuchelewesha miradi kuanza kutekelezwa;

c) Taasisi moja ya Serikali kudai ada au tozo za leseni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Taasisi nyingine ya Serikali. Mfano NDC kudaiwa na Wizara ya Madini ada ya leseni ya maeneo yenye madini yanayomilikiwa na NDC; na
d) Uwepo wa malimbikizo ya madeni ya wazabuni na wakandarasi ambao umesababisha baadhi ya miradi kukwama utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na changamoto hizo, Kamati iliishauri Serikali masuala yafuatayo: -

a) Kutekeleza miradi michache ambayo itakamilika kwa wakati ili kuleta tija inayokusudiwa;

b) Kuanzisha Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa ubora kulingana na thamani ya fedha pamoja na kuongeza uwajibikaji kwa Watumishi wa Umma;

c) Ulipaji wa madeni ya wazabuni na wakandarasi upewe kipaumbele ili kupunguza gharama za riba zinazotokana na kutokulipa madeni kwa wakati;

d) Kutoa kipaumbele kwenye utekelezaji wa miradi yenye sura ya kibiashara na yenye manufaa makubwa ya kiuchumi ili kupunguza gharama za utekelezaji endapo itachelewa kutekelezwa;

e) Majadiliano na wabia kufanyika kwa wakati ili kuepuka ucheleweshaji wa utekelezaji; na

f) Kuanzisha utaratibu maalumu wa kusamehe ada za leseni kwa miradi ambayo inatekelezwa na Taasisi moja ya

Serikali na inatakiwa kulipwa kwa Taasisi nyingine ya Serikali.

### 2.2. Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024 *(The Finance bill, 2024)*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliwasilisha Bungeni Taarifa ya maoni na ushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024 (The Finance Bill, 2024) kwa mujibu wa Kanuni ya 127 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Muswada huo ulilenga kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali, kulinda viwanda vya ndani pamoja na kuchochea ukuaji wa sekta mbalimbali za uchumi ambapo jumla ya Sheria 29 zilifanyiwa marekebisho.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua na kupokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali na baadaye ilifanya majadiliano ya kina na Serikali na kupendekeza marekebisho katika Muswada. Tathmini ya utekelezaji wa Sheria hii yamejadiliwa kwa kina katika sehemu ya Nne ya taarifa hii. Aidha, Kamati iliishauri Serikali kwa miaka ijayo kuwa inawasilisha Muswada wa Sheria ya Fedha sanjari na Hotuba ya Bajeti ya Serikali. Hatua hii itaisaidia Kamati pamoja na wadau kupata muda wa kutosha wa kupitia, kuchambua na kutoa maoni kuhusu muswada huo kikamilifu.

### 2.3. Hoja Mahsusi

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 117(3) na 124 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 Kamati ilishughulikia jumla ya hoja mahsusi **38**, kati ya hoja hizo **hoja 13** zilikuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (3),(4), (5) na (6) na **hoja 25** zilikuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 124 (1), (2) na (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023.

#### 2.3.1. Hoja zilizotokana na Kanuni ya 117

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea jumla ya **Hoja 13** zilizohusu utolewaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizokuwa zimepangwa katika mwaka wa fedha 2023/24. Baada ya majadiliano, Kamati ilikubaliana na majibu ya Serikali kwa hoja

zote 13. Hata hivyo, Kamati ilitoa maelekezo mahsusi kwa Serikali kuhusu hoja zifuatazo: -

i. Kutoa fedha kwa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) **Shilingi bilioni 394.51** kwa ajili ya kufanya shughuli za uzalishaji, ununuzi na utunzaji wa bidhaa za Afya, kulipa madeni ya washitiri na vituo vya kutolea huduma za Afya; na

ii. Kutoa **Shilingi bilioni 1** ya mkopo wenye masharti nafuu kwa vijana kwenye Mfuko wa Maendeleo wa Vijana kwa ajili ya kuanzisha au kuendeleza miradi ya uzalishaji mali.

**Mheshimiwa Spika,** hoja 11 zilizobaki Serikali iliahidi kutoa fedha kabla ya tarehe 30 Juni, 2024. Aidha, jumla ya **Shilingi bilioni 860.17** zilitakiwa kutolewa na Serikali ili kutekeleza shughuli zilizopangwa katika mwaka 2023/24.

**Mheshimiwa Spika,** jumla ya **hoja 25** zilihitaji nyongeza ya fedha ya **Shilingi bilioni 800.74**. Kati ya hoja hizo, Kamati ilikubaliana na majibu ya Serikali katika **hoja 19**, haikukubaliana katika **hoja 2** na hoja **4** zilitolewa maelekezo mahsusi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikukubaliana na majibu ya Serikali kwenye hoja mbili zifuatazo:-

i. Kuongeza kiasi cha **Shilingi bilioni 212.13** kwenye Fungu 46 (Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia) ili zitumike kwa ajili ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo pamoja na Mitaala mipya ya Elimu; na

ii. Serikali ilishindwa kutoa ufafanuzi wa takwimu sahihi za Bajeti kwa ajili ya Bodi ya Mikopo kwa mwaka wa fedha 2024/25 kati ya **Shilingi bilioni 787.42** iliyowekwa kwenye Fungu 46 au **Shilingi bilioni 832.42** iliyotengwa kwenye ukomo na Mfumo wa Bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** hoja zilizotolewa maelekezo mahsusi ni kama ifuatavyo: -

i. Kutenga fedha za ununuzi wa mtambo kwa ajili ya uchapishaji wa mitihani ya elimu ya Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ualimu pamoja na usahihishaji katika bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25;

ii. Kutopunguza fedha za mradi wa SGR kwa ajili ya kugharamia ujenzi na ukarabati wa barabara;

iii. Serikali kutoa Mapendekezo ya Mpango sambamba na Mwongozo wa Maandalizi ya bajeti ya mwaka 2025/26 mwezi Novemba, 2024; na

iv. Kuongeza fedha katika Mfuko wa Mandeleo ya Vijana.

**2.3.2. Hoja zilizotokana na Kanuni ya 124**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea jumla ya hoja 22 kwa mujibu wa Kanuni ya 124 (1), (2) na (3). Kati ya hoja hizo, Kamati ilikubaliana na Serikali hoja 18, haikukubaliana hoja mbili (2) na hoja 2 zilihitaji utekelezaji zaidi. Hoja ambazo Kamati haikukubaliana na Serikali ni kama ifuatavyo: -

i. Serikali kufanya mapitio ya shughuli za Mkopo wa Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati yaliyowasilishwa mwaka 2022/23; na

ii. Changamoto ya ujenzi wa barabara kwa Mfumo wa Uhandisi, Ununuzi, Ujenzi na Ufadhili *(Engineering, Procuring, Construction and Financing – EPC + F)*.

**Mheshimiwa Spika,** hoja zifuatazo zilihitaji utekelezaji zaidi kwa upande wa Serikali: -

i. Kufanya mabadiliko ya Sheria ili kuruhusu Taasisi za TANAPA, NCAA na TAWA kukusanya na kutumia mapato yao wenyewe. Hata hivyo, Sheria ya Fedha ya mwaka 2024 ilifanya mabadiliko katika Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura 282 na Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro Sura ya 284 kwa kuelekeza **asilimia 9** ya mapato ya Taasisi

hizo kuwekwa katika akaunti Maalumu iliyopo Benki Kuu na kati ya asilimia hizo, **asilimia 3** itatumika kwa ajili ya Mfuko wa Ulinzi kwa Wanyamapori na **asilimia 6** kwa ajili ya Tozo ya Maendeleo ya Utalii na **asilimia 91** iliyobaki itaelekezwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali; na

ii. Kufanya mabadiliko ya Sheria ili kuwezesha ukusanyaji wa tozo ya gati (wharfage) kukusanywa na Mamlaka ya Bandari (TPA) kwa kufanya marekebisho katika Kifungu cha 67 (3) cha Sheria ya Bandari Sura ya 166. Hata hivyo, Sheria ya Fedha ya Mwaka 2024 imefanya mabadiliko ya Sheria hiyo kwa kuelekeza mapato yote yanayotokana na tozo ya gati kuwekwa katika akaunti maalumu ya TPA iliyopo Benki Kuu, na utolewaji wa fedha hizo kwa ajili ya matumizi utakuwa ukiidhinishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati itaendelea kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa hoja zote zilizojadiliwa ili kuona endapo mapendekezo yaliyotokana na kikao cha Kamati ya Uongozi na Kamati ya Bajeti yametekelezwa.

### 2.4. Tathmini ya Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa Mwaka 2025/26 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26

**Mheshimiwa Spika**, mwezi Novemba, 2024 Serikali iliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2025/26 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2025/26. Kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1)(a) cha Sheria ya Bajeti Sura 439 na Kanuni ya 113 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 Kamati ya Bajeti ilifanya uchambuzi na kutoa maoni yake kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2025/26 Serikali imekusudia kukusanya na kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 55.06**. Mgawanyo wa mapato na matumizi ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Namba 2.**

**Jedwali Na. 2: Makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26 (TZS Bilioni)**

| | 2024/25 Bajeti iliyoidhinishwa | 2025/26 Makadirio ya Bajeti | Tofauti | Ukuaji/Ongezeko |
|---|---|---|---|---|
| **JUMLA YA MAPATO** | **49,345.69** | **55,061.61** | **5,715.92** | **11.58** |
| Mapato ya Ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri | 34,610.65 | 38,962.49 | 4,351.84 | 12.57 |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti | 1,489.77 | 1,741.02 | 251.25 | 16.87 |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi | 3,461.95 | 4,761.17 | 1,299.22 | 37.53 |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta | 178.89 | 189.74 | 10.85 | 6.07 |
| Mikopo ya Ndani kulipa mtaji Deni la Ndani *(Rollover)* | 4,022.37 | 3,325.56 | -696.81 | -17.32 |
| Mikopo ya ndani ya kibiashara (NDF) | 2,595.42 | 2,952.63 | 357.21 | 13.76 |
| Mikopo ya nje ya kibiashara | 2,986.64 | 3,129.01 | 142.37 | 4.77 |

***Chanzo:*** *Mwongozo wa Mpango na Bajeti 2025/26*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi na kuishauri Serikali masuala yafuatayo: -

### i. Madeni ya Wakandarasi, Wazabuni na Watoa huduma

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba Serikali haikutambua ulipaji wa madeni ya wazabuni, wakandarasi na watoa huduma kama kihatarishi kinachoweza kuathiri utekelezaji wa bajeti kutokana na ukweli kwamba baadhi ya miradi mipya inashindwa kutekelezwa katika mwaka husika kwa sababu fedha za miradi hiyo zinatumika kulipa madeni ya miaka uliyopita.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliishauri Serikali kuwa Mwongozo wa Uandaaji wa Bajeti uweke wazi kiasi ambacho kitatengwa kwa

ajili ya ulipaji wa madeni ya wakandarasi, wazabuni na watoa huduma wa ndani.

**ii. Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwepo na Idara ya Tathmini na Ufuatiliaji katika Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Kamati haikuona kama Idara hiyo inatosha kutekeleza majukumu hayo. Hivyo, Kamati iliishauri Serikali kuanzisha Mamlaka ya Ufuatiliaji na Tathmini ili kuhakikisha miradi inafuatiliwa kwa ukaribu.

**iii. Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliitaka Serikali kufanya mapitio ya Muundo wa Usimamizi wa Mfuko wa Mazingira pamoja na kutafuta chanzo mahsusi kwa ajili ya Mfuko huo kwa sababu athari za mazingira sio kihatarishi tena bali imekuwa janga. Aidha, kwa kufanya hivyo pia kutaiwezesha nchi kupata fedha kutoka kwenye mifuko ya kimataifa inayosaidia nchi zinazoendelea katika kuhimili na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi na uhifadhi wa mazingira. Vilevile, Kamati iliishauri Serikali kutenga walau **asilimia 1** ya mapato yanayotokana na biashara ya hewa ukaa (Carbon Credit) ili yaelekezwe kwenye Mfuko wa Mazingira.

**iv. Uchumi wa Kidigitali**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilishauri Serikali kwamba Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidigitali wa mwaka 2024 hadi 2034 utekelezwe na Afisa Masuuli wa Mamlaka ya Serikali Mtandao *(eGA)*, kwa kuwa ndiyo Mamlaka inayohusika na mifumo ya Serikali. Aidha, utaratibu huo utarahisisha mifumo itakayoundwa kusomana na kutotawanya rasilimali fedha katika mafungu mbalimbali ambazo kimsingi zinaenda kutekeleza shughuli ambayo ingeweza kutekelezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kuwa ndiyo yenye jukumu hilo. Vilevile, Kamati iliishauri Serikali kuweka mkakati wa kuendeleza matumizi ya akili bandia *(AI)* katika Sekta ya Umma ili kuchochea ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za Serikali na kuendana na kasi ya ukuaji wa teknolojia.

**v. Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa.**

**Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ushirikiano wa kimataifa na kikanda Kamati iliishauri Serikali kupitia upya Mikataba yote ya Utozaji wa Kodi Mara Mbili *Double Taxation Agreement* (DTA) ambayo hivi sasa iko 17 ili kubaini Mikataba ipi ina manufaa ili Taifa liendelee nayo na ipi haina manufaa ili isitishwe. Aidha, Kamati iliishauri Serikali kujenga majengo ya ubalozi kwenye nchi ambazo Tanzania ilipewa viwanja kwa ajili ya ujenzi. Vilevile, Kamati iliishauri Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje kuandaa mkakati wa kutumia sekta binafsi kujenga na kuendeleza maeneo ya balozi.

**vi. Ratiba ya Mpango na Bajeti**

**Mheshimiwa Spika,** muda kati ya kuandaa randama na kuziwasilisha Bungeni ni mdogo kwa Maafisa Masuuli kufanya marekebisho kulingana na ukomo wa Bajeti hasa pale wanapotakiwa kupunguza bajeti zao. Kamati iliishauri Serikali kuhakikisha ukomo wa Bajeti kwa Mafungu unaenda sambamba na uidhinishwaji wa mwongozo wa bajeti ili kuwapa Maafisa Masuuli muda wa kutosha kuandaa bajeti inayoendana na ukomo kabla ya kuwasilisha randama Bungeni kwa sababu hivi sasa randama zinazowasilishwa hazina uhalisia.

## 2.5 Ziara za Kamati za kukagua Miradi ya Maendeleo pamoja na mafunzo

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025, Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Singida, Morogoro, Zanzibar na Nchini Kenya. Ziara hizo zilikuwa na malengo yafuatayo:-

i. Kukagua miradi ya maendeleo ili kubaini endapo miradi iliyotekelezwa inaendana na thamani halisi ya fedha;

ii. Kupokea Taarifa za Utendaji kazi wa Taasisi zinazosimamiwa na Kamati na kubaini endapo kuna changamoto zozote za kifedha, kiutendaji, kiuendeshaji pamoja na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao;

iii. Kubadilishana uzoefu baina ya wabunge wa Kamati ya Bajeti ya Bunge la Kenya na Kamati ya Bajeti ya Bunge la Tanzania;

iv. Kubaini endapo matakwa ya Sheria ya Bajeti Sura 439 yamefuatwa kikamilifu katika utekelezaji wa Bajeti pamoja na miradi pamoja; na

v. Kuhudhuria Kongamano la Kodi la Kitaifa.

**2.5.1. Masuala muhimu yaliyojitokeza**
**2.5.1.1 Ziara Nchini Kenya**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara ya kikazi nchini Kenya kuanzia tarehe 2 hadi 8 Machi, 2024. Ziara hiyo ilikuwa na lengo la kutembelea na kujifunza masuala mbalimbali kama vile utekelezaji wa Miradi kwa njia ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi, Ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, uzoefu wa utendaji kazi wa Kamati ya Bajeti ya Kenya, ujenzi, ukarabati na usimamizi wa Reli ya Kisasa (SGR), mafanikio, changamoto pamoja na uendeshwaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ziara hiyo, Kamati ilipendekeza masuala yafuatayo yafanyiwe kazi na Serikali:-

i. Kuweka juhudi katika kutekeleza miradi mikubwa hasa ya miundombinu ya barabara kwa njia ya Ubia na Sekta Binafsi (PPP);

ii. Kufanya mabadiliko katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(Tanzania Investment Center* (TIC) ili kiweze kutoa vibali kwa wawekezaji katika muda mfupi;

iii. Kuweka mikakati endelevu ya kupanua wigo wa kukusanya kodi ya biashara mtandao inayofanyika ndani na nje ya nchi;

iv. Kuwekeza zaidi katika mifumo ya kidijitali ya ukusanyaji wa mapato ambayo itasomana na mifumo mingine;

v. Kukamilisha miradi kwa wakati ili kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi na kuleta tija iliyokusudiwa; na

vi. Kutambua na kurasimisha sekta isiyo rasmi pamoja na kuhamasisha miamala kufanyika kidigitali ili kukusanya mapato mengi zaidi.

**2.5.1.2 Utekelezaji wa Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR)**

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Reli Tanzania (TRC) linaendelea na uendeshaji wa reli ya kisasa ya SGR kati ya Dar es Salaam hadi Dodoma ambapo uendeshaji huu ulianza tarehe 14 Juni, 2024 kati ya Dar es salaam na Morogoro na tarehe 25 Julai, 2024 kati ya Dar es salaam na Dodoma. Hadi kufikia Desemba, 2024 jumla ya abiria **1,330,208** wamesafirishwa na jumla ya **Shilingi bilioni 37.6** zimekusanywa.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kupokea Taarifa ya Mradi pamoja na kukagua utekelezaji wake Kamati ilishauri masuala yafuatayo: -

i. TRC kushirikiana na viongozi wa ngazi ya chini katika maeneo ambayo reli ya SGR inapita ili kuwa na ulinzi shirikishi wa mali na vitendea kazi vya mradi na kuwafanya wananchi kuwa sehemu ya mradi huo;

ii. Serikali kumaliza ujenzi wa kipande cha reli kutoka Bandari ya Dar es salaam ili kuwezesha usafirishaji wa mizigo kutoka Bandari ya Dar es salaam;

iii. Kutekeleza mfumo wa watoa huduma binafsi kutumia miundombinu ya reli kwa makubaliano maalumu (*open access)* katika uendeshaji wa SGR ili kusaidia sekta binafsi kufanya biashara katika reli ya SGR; na

iv. Kuhakikisha usafirishaji wa mizigo kwa treni ya SGR kutoka Dar-es-Salaam hadi Dodoma unaanza.

### 2.5.1.3 Shirika la Ndege Tanzania (ATCL)

**Mheshimiwa Spika,** kwa sasa ATCL ina jumla ya ndege 16 za Boeing, Airbus Canada na DeHavilland Canada. Aidha, Mtandao wa safari za ndege umepanuka kutoka vituo 4 Mwaka 2016 hadi vituo 28 Oktoba, 2024. Vituo vilivyokuwa vinafanya kazi hadi mwezi Novemba 2024 ni 25 ambavyo kati ya hivyo, vituo 13 ni ndani ya nchi, 9 kikanda na 3 kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, Kamati ilitaarifiwa kwamba kutokana na kukosekana kwa hanga katika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Serikali imetoa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 20,000 kwa ajili ya kujenga Hanga kubwa ambalo litakuwa na uwezo wa kuingiza na kutengeneza ndege kubwa moja na ndege mbili ndogo kwa wakati mmoja. Makadirio ya gharama za ujenzi ni **Shilingi bilioni 66** na ujenzi huo utachukua miezi 36 hadi kukamilika na mpaka sasa hatua iliyofikiwa ni kupatikana kwa Mkandarasi na Mshauri Elekezi.

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara hiyo, Kamati iliishauri Serikali masuala yafuatayo: -

Kutokana na uwepo wa baadhi ya ndege kushindwa kufanyiwa matengenezo kwa sababu ya ukosefu wa vipuri, Kamati iliishauri Serikali kuweka masharti ya kuhakikisha kwamba vipuri pamoja na injini za ndege zinazonunuliwa zinapatikana katika soko;

i. Wizara ya Uchukuzi kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii ili kuhakikisha usafiri kwa njia ya anga unakuza shughuli za utalii; na

ii. Kwa kuwa Shirika la ATCL linadaiwa gharama za kukodi ndege na Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA), deni hilo limesababisha Shirika kuwa na mlundikano wa madeni ambao unaathiri mizania ya hesabu za Shirika, Kamati iliishauri Serikali kufuta madeni ya ATCL inayodaiwa na TGFA ili kusafisha vitabu.

**2.5.1.4 Mamlaka ya kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) Zanzibar**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea Ofisi ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) ambayo ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi na Maendeleo ya Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura 388. Lengo la ziara hiyo ni kuona namna shughuli za uvuvi wa bahari kuu unavyofanya kazi.

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara hiyo Wajumbe waliishauri Serikali yafuatayo:-

i. Kukamilisha mchakato wa kununua meli tatu (3) za uvuvi ili kuimarisha upatikanaji wa mazao ya uvuvi; na

ii. Serikali kuruhusu sekta binafsi ya ndani kulipa ada na tozo za uvuvi kwa kutumia Shilingi ya Tanzania ili kupunguza matumizi ya Dola ya Marekani na Kampuni za kigeni kulipa kwa Dola ya Marekani ili kuongeza fedha za kigeni.

**2.5.1.5 Mradi wa ujenzi wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara katika Mradi wa ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) uliopo Tarafa ya Chongoleani, Wilaya ya Tanga, Mkoa wa Tanga. Hadi kufikia Agosti 2024, utekelezaji wa mradi kwa ujumla ulikuwa umefikia **asilimia 39.2**. Katika ziara hiyo Kamati ilishauri masuala yafuatayo kwa Serikali:-

i. Kutumia miundombinu ya mradi huu kwa ajili ya kusafirisha mafuta ghafi ya petroli kwenda katika nchi jirani za Afrika Mashariki; na

ii. Kuhakikisha kwamba mradi unakamilika ndani ya muda uliopangwa ili kuleta tija na manufaa yaliyokusudiwa.

### 2.5.1.6 Kongamano la Kodi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata nafasi ya kuhudhuria Kongamano la Kodi la Kitaifa lililofanyika tarehe 27 na 28 Februari, 2024 Mkoani Dar es Salaam. Kongamano hilo lililenga kupokea maoni mbalimbali ya walipa kodi ili kufanya maboresho ya Sera katika uwekezaji, ukusanyaji wa mapato ya ndani na ukuaji wa uchumi jumuishi. Katika kongamano hilo, wadau walitoa maoni yafuatayo kwa Serikali: -

i. TRA kuendelea kutumia weledi na kutoa elimu katika ukusanyaji wa kodi;

ii. Serikali kuendelea kutanua wigo wa kodi, mfano **asilimia 80** ya kodi inayotokana na mapato ya kodi inatoka kwa kampuni 400 na **asilimia 20** kwa kampuni nyingine;

iii. Kurasimisha wajasiriamali wadogo ili wawe wanalipa kodi;

iv. Uwekezaji wa biashara uendelee na kuvutia uwekezaji mpya;

v. Kufungua maeneo ya kiuchumi ambayo bado hatujafikia;

vi. Kodi iakisi hali halisi ya sasa ya uchumi na gharama za makusanyo ya kodi zipungue;

vii. Kupitia upya usimamizi wa ushuru ikiwemo kuangalia tafsiri za sheria na uhalisia wa makisio ya kodi;

viii. Mchakato wa bajeti uwe wa uwazi na shirikishi na muda wa wadau kutoa maoni katika Sheria ya Fedha uongezwe;

ix. Kuangalia Sheria ya kodi ya wajasiriamali wadogo na itafsiriwe kwa kiswahili ili iwe rahisi kueleweka na itenganishwe na Sheria ya Mapato; na

x. Kuharakisha kutunga sera ya maendeleo ya sekta binafsi kwa ajili ya kuhakikisha wanaokwepa kodi hawatambuliki kwenye vyama vyao.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilipokea maoni hayo na kuahidi kuyafanyia kazi.

## 2.6 Mafunzo kwa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** ili kuwajengea uwezo na ujuzi Wajumbe wa Kamati katika kutekeleza majukumu yao, Kamati ilipata mafunzo mbalimbali kutoka katika Wizara, Idara, Mamlaka na Wakala za Serikali pamoja na Sekta Binafsi. Mafunzo hayo yalihusu: -

i. Mifumo ya Kukusanya Mapato ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ya TANCIS na IDRAS;

iii. Muundo na majukumu ya Mapato ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA);

iv. Uzoefu wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na utendaji kazi wa Bunge la Kenya;

v. Mfumo wa usimamizi wa Bajeti *Central Budget Management System* (CBMS) unavyofanya kazi;

vi. Kanuni za ugawaji wa mikopo ya Halmashauri ya **asilimia 10** kwa makundi maalumu ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu;

vii. Ufanisi wa Mfumo wa Malipo ya papo kwa papo *(Tanzania Instant Payment System –* TIPS);

viii. Ufanisi na changamoto za Akaunti Jumuifu ya Hazina *(Treasury Single Account);*

ix. Mwenendo wa ukopaji kutoka Benki Kuu ya Tanzania ili kuziba nakisi ya bajeti;

x. Namna Serikali kupitia Benki Kuu imejipanga katika ununuzi wa dhahabu fedha kama sehemu ya akiba ya fedha za kigeni;

xi. Usimamizi wa sekta ya fedha nchini;

xii. Uendeshaji wa Soko la Hisa la Dar es Salaam;

xiii. Kanuni za uendeshaji wa Sheria ya mfumo wa watoa huduma binafsi kutumia miundombinu ya reli kwa makubaliano maalumu *(Open Access);*

xiv. Vyanzo vya mapato vya Halmashauri;

xv. Uunganishwaji wa mifumo ya Serikali;

xvi. Namna ya kutafsiri Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; na

xvii. Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kushukuru Ofisi ya Bunge pamoja na Taasisi zote za Umma na Binafsi kwa kuipatia mafunzo ambayo yameboresha utendaji kazi wa Kamati ili kuishauri Serikali ipasavyo.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KATIKA KIPINDI CHA NUSU MWAKA 2024/25

**Mheshimiwa Spika,** dhima kuu ya Bajeti ya Mwaka 2024/25 ni ***"Mageuzi Endelevu ya Kiuchumi kupitia Uimarishaji wa Sera za Kibajeti na Uwekezaji katika Kuhimili na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi kwa Maendeleo ya Wananchi".*** Katika kutekeleza dhima hiyo, uchambuzi wa Kamati ulifanyika kwa kuzingatia shabaha zifuatazo: -

i. Mapato ya ndani kufikia **asilimia 15.8** ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 ikilinganishwa na **asilimia 15.4** mwaka 2023/24;

ii. Mapato ya kodi kufikia **asilimia 12.9** ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 ikilinganishwa na **asilimia 12.6** mwaka 2023/24; na

iii. Kuwa na nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) isiyozidi **asilimia 3.0** ya Pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25 kwa kuangalia viashiria vya uchumi jumla na mapato na matumizi ya Serikali kama ifuatavyo:-


### 3.1. Viashiria vya Uchumi Jumla
#### 3.1.1. Pato la Taifa

**Mheshimiwa Spika,** Pato la Taifa katika mwaka 2024 lilitarajiwa kukua kwa **asilimia 5.4**. Aidha, katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2024, Pato la Taifa lilikua kwa wastani wa **asilimia 5.4,** ikiwa ni sawa na lengo la mwaka. Hivyo, ni dhahiri kwamba mwenendo huu wa ukuaji wa uchumi utafikia lengo lililopangwa la **asilimia 5.4** na zaidi.

Kamati imebaini kuwa moja ya shughuli zilizochangia katika ukuaji huo ni pamoja na kuanza kwa uzalishaji wa umeme kupitia Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere ambapo mitambo nane kati ya tisa imeanza uzalishaji. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutekeleza mradi huu.

**Mheshimiwa Spika,** shughuli za kilimo ziliongoza kwa kuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa **asilimia 24.4**, ikifuatiwa na ujenzi **asilimia 13.2**, uchimbaji madini **asilimia 9.8**, na biashara **asilimia 8.6** kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 1.**

**Kielelezo Na. 1: Mchango wa Shughuli za Uchumi katika Pato la Taifa (Januari – Septemba, 2024)** *(Asilimia)*




***Chanzo:*** *Wizara ya Fedha*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuhakikisha kwamba uchumi wa Taifa unaendelea kukua licha ya migogoro ya Kimataifa inayoendelea duniani**.** Kamati inashauri masuala yafuatayo: -

a) Kwa kuwa sekta ya kilimo ina mchango mkubwa katika Pato la Taifa, Serikali ihakikishe kwamba mikopo inayoelekezwa katika sekta hiyo inajikita katika shughuli za kilimo na uzalishaji badala ya biashara ya mazao;

b) Kukamilisha mradi wa Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere sambamba na uboreshaji wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme ili kuwa na umeme wa uhakika na kuvutia wawekezaji katika shughuli za uzalishaji;

c) Serikali kuwekeza katika miundombinu ya teknolojia ya kisasa ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za kifedha na bima kwa wananchi, hasa katika maeneo ya vijijini;

d) Serikali kuendelea kutekeleza sera na sheria za udhibiti unaozingatia teknolojia ya fedha ili kuhakikisha kuwa

huduma za kifedha na bima zinazotolewa kupitia mifumo ya kidijitali ni salama, za kuaminika, na zinakidhi viwango vya kimataifa;

e) Kuimarisha ushirikiano wa kibiashara na nchi nyingine ili kupata masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini kama vile chakula; na

f) Kuweka mazingira wezeshi ya wachimbaji wadogo kupata mikopo nafuu kupitia Mpango wa kuongeza uzalishaji wa dhahabu nchini yaani *(Domestic Gold Purchase Program* - DGPP) kwa kutumia mifuko ya udhamini wa mikopo, Benki Kuu ikishirikiana na STAMICO na viwanda binafsi vya kuchengua dhahabu.

### 3.1.2. Mfumuko wa Bei

**Mheshimiwa Spika,** mfumuko wa bei ulitarajiwa kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa **asilimia 3.0** hadi **5.0** katika muda wa kati. Hadi kufikia Desemba 2024, wastani wa mfumuko wa bei ulipungua na kufikia **asilimia 3.1** ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 3.2** katika kipindi kama hicho mwaka 2023.

Mfumuko wa bei za vyakula na vinywaji baridi ulipungua na kufikia wastani wa **asilimia 2.8** ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 4.6** katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Kupungua kwa mfumuko wa bei kumechangiwa na utekelezaji wa sera madhubuti ya fedha pamoja na utoshelevu wa chakula nchini uliosababisha kupungua kwa bei za bidhaa za chakula.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na sababu zilizotajwa, kupungua kwa bei ya mafuta kwenye soko la dunia kumechangia kuimarika kwa mfumuko wa bei nchini. Kwa mujibu wa taarifa kutoka *U.S Energy Information Administration* bei ya mafuta katika soko la dunia inakadiriwa kuendelea kushuka hadi kufikia wastani wa **dola za Marekani 74** kwa pipa mwaka 2025 na **dola za Marekani 66** kwa pipa mwaka 2026. Hivyo, ni wazi kwamba jambo kubwa linaloweza kusababisha mfumuko wa bei ni bidhaa za chakula.

**Mheshimiwa Spika,** hali ya usalama wa chakula nchini imeongezeka na kufikia **asilimia 128**. Hata hivyo, utabiri wa Hali ya hewa uliotolewa na Kituo cha Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki *(The Intergovernmental Authority on Development* (IGAD) umeonyesha wasi wasi wa kuwa na ukame katika nchi za Afrika Mashariki.

Hivyo, hatari ya ukosefu wa chakula cha kutosha inaweza kujitokeza, Kamati inaishauri Serikali kuchukua tahadhari kwa kuhakikisha Wakala wa Taifa wa Uhifadhi wa Chakula - NFRA inaongeza akiba ya chakula kwenye msimu wa mwaka 2025/26.

**3.1.3. Sekta ya Nje**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2024, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nje ya nchi ilipungua na kufikia **Dola za Marekani milioni 364.2** ikilinganishwa na **Dola za Marekani milioni 807.8** katika kipindi kama hicho mwaka 2023.

Hii ilitokana na ongezeko la mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, hususan mapato yatokanayo na utalii na mauzo ya bidhaa asilia ikilinganishwa na kasi ndogo ya thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa sekta ya utalii imeongoza katika kuliletea Taifa mapato ya kigeni, haya ni mafanikio yanayotoka na maono ya **Mheshimiwa. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** alipoamua kutanga utalii kupitia filamu ya *Royal Tour* mwaka 2022.

**Jedwali Na. 3: Mwenendo wa Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamishaji Mali Nje ya Nchi**

*(Dola za Marekani Milioni)*

| AKAUNTI | 2023 | 2024 | % |
|---|---|---|---|
| **Urari wa Bidhaa (halisi)** | **-2,976.5** | **-2,109.2** | **-29.14** |
| Zilizouzwa nje | 4,325.9 | 5,686.6 | 31.45 |
| Zilizonunuliwa nje | -7,302.3 | -7,795.8 | 6.76 |
| **Urari wa Huduma (halisi)** | **2,335.2** | **2,236.2** | **-4.24** |
| Mapato | 3,516.9 | 3,657.2 | 3.99 |
| Malipo | -1,181.7 | -1,421.0 | 20.25 |
| **Urari wa Bidhaa na Huduma (halisi)** | **-641.3** | **127.0** | **-119.80** |
| Bidhaa na Huduma Zilizouzwa Nje | 7,842.8 | 9,343.8 | 19.14 |
| Bidhaa na Huduma Zilizonunuliwa Kutoka Nje | -8,484.1 | -9,216.8 | 8.64 |
| **Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi (halisi)** | **-821.2** | **-1,066.2** | **29.83** |
| Yaliyoingia | 95.7 | 126.2 | 31.87 |
| Yaliyotoka | -917 | -1,192.4 | 30.03 |
| **Urari wa Uhamisho Mali ya kawaida (halisi)** | **321.2** | **327.0** | **1.81** |
| Iliyoingia | 410.4 | 430.0 | 4.78 |
| Serikali | 52.3 | 90.1 | 72.28 |
| Iliyotoka | -89.2 | -103.0 | 15.47 |
| **Urari wa Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali** | **-1,141.3** | **-612.1** | **-46.37** |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa takwimu zilizopo kwenye jedwali namba 3 na ina ushauri ufuatao kwa Serikali: -

i. Kuwekeza kwenye miundombinu ya utalii, kufanya mapitio gharama za kutembelea vivutio vyetu pamoja na kuvutia ujenzi wa hoteli za nyota 5;

ii. Kuvutia uwekezaji kwenye ujenzi wa viwanda ili kuongeza thamani ya mazao yanayouzwa nje kwa sababu mazao ya kilimo ambayo hayajachakatwa kwa asili bei hubadilika kulingana na upatikanaji *(Elastic),* hivyo mazao yaliyoongezwa thamani yana uwezo wa kutunzwa kwa muda mrefu na kuyauza pale bei zinapopanda; na

iii. Kutafuta masoko ya mazao mengine ya biashara ambayo yanaweza kuchangia fedha za kigeni kama vile Pareto, Katani, Chai, Matunda na Mbogamboga kwa sababu kwa miaka mingi mazao tunayotegemea ni Korosho, Kahawa na Tumbaku jambo ambalo ni la hatari endapo mazao hayo yanateteleka katika Soko la Dunia.

### 3.1.4. Mwenendo wa thamani ya Shilingi

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2024 thamani ya Shilingi ya Tanzania ilishuka thamani dhidi ya Dola ya Marekani kwa kiwango cha wastani wa **asilimia 7.3** na kufikia wastani wa kubadilishwa kwa **Shilingi 2,647.5** kwa **Dola moja ya Marekani** kutoka **Shilingi 2,466.3** kwa mwaka 2023/24. Kushuka kwa thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani na sarafu nyingine kulitokana na changamoto katika uchumi wa dunia hususan ongezeko la bei za bidhaa katika soko la dunia. Hali hii ilisababisha mahitaji makubwa ya fedha za kigeni katika uchumi kufuatia utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kupunguza ukwasi katika nchi zilizoendelea ikiwemo Marekani.

**Mheshimiwa Spika,** thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani iliongezeka katika kipindi cha mwezi Novemba na Desemba, 2024 ambapo **Dola moja ya Marekani** ilibadilishwa kwa wastani wa **Shilingi 2,420.8** mwezi Desemba 2024 ikilinganishwa na **Shilingi 2,516.0** katika kipindi kama hicho mwaka 2023 sawa na ongezeko la thamani ya Shilingi kwa **asilimia 3.8**. Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada ilizochukua katika kuimarisha thamani ya Shilingi. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

i. Kuendelea na utekelezaji wa mkakati wa Taifa wa kuimarisha upatikanaji wa fedha za kigeni wenye lengo la kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi na kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi;

ii. Kuendelea na utekelezaji wa programu ya Benki Kuu ya ununuzi wa dhahabu fedha ili kuongeza akiba ya fedha za kigeni;

iii. Kuendelea kusimamia katazo la matumizi ya fedha za kigeni nchini kwenye mauzo ya bidhaa na huduma zinazotolewa ndani ya nchi; na

iv. Kuwekeza kwenye Sekta zinazoweza kuongeza mauzo ya nje ili kupata fedha za kigeni hususan sekta ya Kilimo, Utalii, Mifugo na Madini.

### 3.1.5. Deni la Serikali

**Mheshimiwa Spika,** hadi Desemba 2024, deni la Serikali lilikuwa **Shilingi bilioni 93,687** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 87,187** katika kipindi kama hicho mwaka 2023, sawa na ongezeko la **asilimia 7.45.** Kati ya kiasi hicho, deni la nje lilikuwa **Shilingi bilioni 61,038** sawa na **asilimia 65.1** ya deni lote na deni la ndani ni **Shilingi bilioni 32,649.** Ongezeko hilo limetokana na kupokelewa kwa mikopo mipya na ya zamani kwa ajili ya kugharamia miradi ya kimkakati na kielelezo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, nishati na huduma za jamii.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa juu ya mwenendo wa deni la Serikali kwa sasa inaonyesha kwamba deni letu ni himilivu. Hata hivyo, viashiria viwili vya ulipaji wa deni ambavyo ni Uwiano wa ulipaji wa deni kwa mapato ukomo ni **asilimia 18** na hivi sasa imefikia **asilimia 17.2** na kiashiria cha uwiano wa ulipaji wa deni kwa mauzo ya nje ukomo ni **asilimia 15** na hivi kiashiria hiki kimefika **asilima 13.9**.

**Jedwali Na. 1: Tathmini ya Uhimilivu wa Deni** (*Asilimia)*

| Viashiria Vya Uhimilivu | Ukomo | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Deni la Nje** | | | | | | | |
| Uwiano wa thamani ya sasa ya Deni kwa Pato la Taifa | **40** | 23.6 | 24.1 | 24.0 | 23.0 | 21.4 | 20.3 |
| Uwiano wa thamani ya sasa ya Deni kwa Mauzo ya Nje ya Nchi | **180** | 127.5 | 123.8 | 124.5 | 119.5 | 111.9 | 106.4 |
| Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mauzo ya Nchi | **15** | 11.7 | 13.9 | 12.8 | 12.3 | 12.8 | 12.6 |
| Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mapato | **18** | 14.5 | 17.2 | 15.5 | 14.8 | 15.2 | 14.8 |
| **Deni la Serikali (Ndani na Nje)** | | | | | | | |
| Uwiano wa Thamani ya sasa ya Deni kwa pato la Taifa | **55** | 41.1 | 40.3 | 39.5 | 38.1 | 36.8 | 36.5 |
| Uwiano wa Thamani ya sasa ya Deni kwa Mapato | **N/A** | 267.6 | 251.1 | 241.3 | 232.1 | 224.4 | 222.3 |
| Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mapato | **N/A** | 35.4 | 50.9 | 40.8 | 37.1 | 35.9 | 36.1 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Fedha*

Hivyo, Kamati inaishauri Serikali Masuala yafuatayo: -

i. Serikali ihakikishe inakopa zaidi mikopo yenye masharti nafuu *(concessional loans)* badala ya mikopo ya kibiashara yenye riba kubwa. Hatua hii itapunguza gharama ya kuhudumia za deni;

ii. Kuongeza makusanyo ya ndani ili yaweze kugharamia ulipaji wa deni; na

iii. Serikali kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kutumia njia mbadala za kufadhili miradi kama vile Ubia baina ya sekta ya Umma na sekta binafsi.

**3.1.6. Akiba ya Fedha za Kigeni**

**Mheshimiwa Spika,** shabaha ya Serikali katika akiba ya fedha za kigeni ni kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4). Hadi kufikia kufikia Desemba 2024 akiba ya fedha za kigeni ilifikia **Dola za Marekani bilioni 5.5** ambayo inakidhi uagizaji wa bidhaa na huduma usiopungua kipindi cha **miezi 4.5.** Ongezeko hilo lilitokana na utekelezaji wa programu ya Benki Kuu ya ununuzi wa dhahabu nchini pamoja na kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni yaliyotokana na kuongezeka kwa bei ya dhahabu, mauzo ya mazao ya biashara na kuongezeka kwa idadi ya watalii nchini.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini mchanganuo wa akiba ya fedha katika kipindi cha nusu mwaka, ni kama ifuatavyo: -

i. Mikopo ya kibajeti kutoka kwa taasisi za kimataifa **asilimia 51**;

ii. Mikopo ya kibiashara **asilimia 17**


iii. Ununuzi wa fedha za kigeni katika soko la jumla **asilimia 11**

iv. Misaada ya kibajeti inayotolewa moja kwa moja katika utekelezaji wa miradi **asilimia 6**; na

v. Vyanzo vinginevyo ikiwemo ununuzi wa dhahabu **asilimia 14.2.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kwamba nchi ina akiba ya fedha za kigeni ya kutosha, Kamati ilibaini kwamba sehemu kubwa ya akiba hiyo ni mikopo ambayo ni **asilimia 68.** Hivyo, Kamati iliishauri Serikali kuchochea mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, kuvutia mitaji ya uwekezaji kutoka nje na kuongeza ununuzi wa dhahabu fedha ili kuongeza akiba ya fedha za kigeni.

**Kielelezo Na. 2: Akiba ya Fedha za Kigeni**




***Chanzo:*** *Wizara ya Fedha*

### 3.2. Mwenendo wa Mapato na Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25 Serikali iliidhinishiwa bajeti ya **Shilingi trilioni 49.35**, kati ya fedha hizo **Shilingi trilioni 33.39** zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi trilioni 15.96** kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, Serikali katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2024 ilikusanya jumla ya **Shilingi trilioni 25.63** kutoka vyanzo vyote vya mapato, sawa na **asilimia 51.9** ya lengo la mwaka mapato yote yanayokadiliwa kukusanywa katika mwaka 2024/25.

**10 FEBRUARI, 2025**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba Serikali ikiendelea kukusanya mapato kwa mwenendo huu, basi hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha itaweza kukusanya mapato kwa **asilimia 100** au zaidi. Jambo hili ni la kupongeza kwani mikakati iliyowekwa na Serikali inayoongozwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** katika kutekeleza sera za kibajeti zimeonyesha ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ulioimarika na kuvuka malengo. Mafanikio haya siyo tu yanadhihirisha usimamizi madhubuti wa fedha za umma bali pia ni ishara ya juhudi za dhati za kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Jedwali Na. 5 linaonesha mwenendo wa ukusanyaji wa mapato, ambapo Serikali imeweza kukusanya mapato kwa **asimilia 51.9** ikilinganishwa na lengo la mwaka. Ufanisi huu umechangiwa na upatikanaji wa fedha za mikopo yenye masharti nafuu ambayo hadi kufikia Desemba 2024 ilikuwa imepokelewa kwa **asilimia 108.1** ikiwa imevuka lengo la mwaka la **Shilingi trilioni 1.49**. Ongezeko la upatikanaji wa fedha za mikopo limetokana na kupokea fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika **Shilingi bilioni 460** na **Shilingi bilioni 130** kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa ambazo hazikuwa sehemu ya makadirio ya mapato yaliyoidhinishwa na Bunge.

**Jedwali Na.5: Sura ya Bajeti na Utekelezaji wa nusu mwaka 2024/25**

(bilioni)

| Na. | Chanzo | Bajeti 2024/25 | Utekelezaji Nusu mwaka 2024/25 | Asilimia mwaka 2024/25 |
|---|---|---|---|---|
| | **MAPATO** | | | |
| 1. | **Mapato ya Ndani** | **33,254.3** | **16,717.6** | **50.3** |
| | Mapato ya Kodi | 29,415.3 | 15,111.7 | 51.4 |
| | Mapato yasiyo ya kodi | 3,839.0 | 1,605.9 | 42 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2. | **Mapato ya Halmashauri** | **1,356.3** | **697.8** | **51.4** |
| 3. | **Mikopo/Misaada kutoka nje** | **5,130.6** | **3,500.4** | **68.2** |
| | Mikopo ya Masharti Nafuu (GBS) | 1,489.8 | 1,611.1 | 108.1 |
| | Misaada na Mikopo ya miradi nje | 3,461.9 | 1,785.9 | 51.6 |
| | Misaada na Mikopo ya Kisekta | 178.9 | 103.5 | 58 |
| 4. | **Mikopo ya Ndani na Nje** | **9,604.4** | **4,720.5** | **49.1** |
| | Mikopo ya ndani | 2,595.4 | 1,312.5 | 50.6 |
| | Mikopo ya Ndani (roll over) | 4,022.4 | 1,852.7 | 46.1 |
| | Mikopo ya Masharti ya kibiashara | 2,986.6 | 1,555.3 | 52.1 |
| | **JUMLA YA MAPATO YOTE** | **49,345.70** | **25,636.40** | **51.9** |
| | **MATUMIZI** | | | |
| 5. | **Matumizi ya Kawaida** | **33,386.3** | **16,265.3** | **48.7** |
| | Mfuko Mkuu wa Serikali | 15,736.3 | 6,020.1 | 38.3 |
| | Mishahara | 11,767.9 | 5,526.9 | 46.96 |
| | Matumizi Mengineyo (OC) | 5,882.1 | 4,718.4 | 80.2 |
| 6 | **Matumizi ya Maendeleo** | **15,959.4** | **9,515.7** | **59.62** |
| | Fedha za Ndani | 12,318.5 | 6,320.0 | 51.3 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Fedha za Nje | 3,640.8 | 2,971.3 | 81.6 |
| | **JUMLA YA MATUMIZI YOTE** | **49,345.70** | **25,781** | **52.2** |
| | **NAKISI YA BAJETI (% OF GDP)** | **2.9%** | | |

***Chanzo:*** *Taarifa ya utekelezaji Nusu mwaka 2024/25*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa ufanisi huo. Hata hivyo Kamati inatoa ushauri ufuatao: -

i. Serikali iendelee kuweka mikakati madhubuti ya kuongeza wigo wa walipa kodi, kwa kuwatambua na kuwapa motisha wafanyabiashara wanaofanya biashara kwenye mfumo usio rasmi;

ii. Serikali kuchukua hatua dhabiti za kupunguza matumizi ya fedha taslimu kwenye kufanya malipo; na

iii. Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ihakikishe mifumo inasomana ili kurahisisha ulipaji wa kodi.

### 3.2.1. Mwenendo wa ukusanyaji wa Mapato hadi mwezi Desemba 2024

#### 3.2.1.1. Mapato yaliyokusanywa na TRA

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2024 mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yalikuwa **Shilingi trilioni 15.11** sawa na **asilimia 50.3** ya lengo la mwaka la kukusanya **Shilingi trilioni 33.25**. Makusanyo hayo ni baada ya kulipa marejesho ya kodi ya **Shilingi trilioni 1.09** sawa na **asilimia 105.8** ya lengo la mwaka la kufanya marejesho ya Shilingi **trilioni 1.03.** Kamati inaipongeza TRA chini ya uongozi wa Kamishna Mkuu Bw. Yusuph Juma Mwenda kwa ufanisi wa makusanyo hayo pamoja na kufanya marejesho kwa wafanyabiashara, kusimamia vizuri Sheria na miongozo ya kukusanya kodi pamoja na kuhimiza ulipaji wa kodi kwa hiari.

### 3.2.1.2. Mapato yasiyo ya kodi

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Desemba 2024, mapato yasiyo ya kodi na yanayokusanywa na Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali yalifikia Shilingi trilioni 1.61, sawa na asilimia 41.83 ya lengo la kukusanya Shilingi trilioni 3.84. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba **asilimia 72.05** ya mapato hayo (**Shilingi trilioni 1.16**) imetokana na mchango wa mafungu matatu tu kati ya 62, kulingana na fursa za mapato katika sekta husika. Hata hivyo, Kamati imebaini mafungu 59 yana mchango mdogo katika makusanyo kwa sababu hayatumii mifumo kikamilifu katika ukusanyaji wa mapato. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa Taasisi zote za Serikali zinatumia mifumo katika kukusanya mapato.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kati ya **Shilingi trilioni 1.61** ya mapato yote yasiyo ya kodi, Ofisi ya Msajili wa Hazina imekusanya **Shilingi bilioni 478.8.** Haya ni matunda ya mageuzi katika uendeshaji wa Mashirika ya Umma kujiendesha kibiashara yanayofanywa na Msajili wa Hazina Bw. Nehemia Mchechu chini ya uongozi wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**.

### 3.2.2. Uchambuzi wa Mwenendo wa Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25 Serikali kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 49.35.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi trilioni 33.39** ni fedha za matumizi ya kawaida na **Shilingi trilioni 15.96** ni fedha za matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia Desemba 2024, Serikali iliidhinisha matumizi yenye jumla ya **Shilingi trilioni 25.78** ambayo ni sawa na **asilimia 52.25** ya lengo la mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi trilioni 16.27** ni matumizi ya kawaida na **Shilingi trilioni 9.52** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kamati ilipitia na kuchambua matumizi hayo na kubaini masuala yafauatayo: -

### 3.2.2.1. Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika,** kati ya fedha zote zilizotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, **Shilingi trilioni 6.02** zilitumika kugharamia malipo ya deni la Serikali, sawa na **asilimia 45.85** ya lengo la

mwaka mzima la kulipa **Shilingi trilioni 13.13** na **asilimia 36** ya mapato yote ya ndani**.** Aidha, Kamati ilibaini kuwa kiasi cha **Shilingi trilioni 1.14** kilihamishwa kutoka Fungu hilo kwenda Mafungu mengine na hivyo kufanya bajeti ya kulipa deni la Serikali kuwa **Shilingi trilioni 11.99**.

**3.2.2.2. Matumizi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha **asilimia 59.65** ya lengo la mwaka. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba miradi ya mwaka 2024/25 haijatekelezwa kutokana na fedha hizo kutumika katika kugharamia miradi ya mwaka 2023/24. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kasi ya utekelezaji wa miradi inaenda sambamba na utolewaji wa fedha.

**3.2.3. Masuala yaliyobainika katika Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha Julai – Desemba Mwaka 2024/25.**

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka, Kamati ilibaini masuala yafuatayo:-

i. **Uhamisho wa fedha kwenye Mafungu**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha nusu mwaka Kamati ilibaini kwamba kulifanyika uhamisho wa fedha kiasi cha **Shilingi bilioni 898.5** ambazo zilikuwa ni fedha za matumizi mengineyo na **Shilingi bilioni 984.4** fedha za maendeleo za ndani kwa Wizara, idara zinazojitegemea na taasisi za Serikali. Fedha hizo zilihamishwa na kupelekwa kwenye mafungu mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 Sura ya 439, Kifungu cha 41(3)(c) kinaeleza kuwa, jumla ya fedha zitakazofanyiwa uhamisho kutoka Fungu husika kutozidi jumla ya matumizi yaliyoidhinishwa katika Fungu hilo kwa mwaka huo wa fedha. Hata hivyo, uhamisho uliofanyika, baadhi ya mafungu yamefanyiwa uhamisho wa zaidi ya **asilimia 100** ya bajeti iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika,** mfano, Bajeti iliyoidhinishwa katika Fungu namba 007 Ofisi ya Msajili wa Hazina ilikuwa ni **Shilingi bilioni 36.5** lakini uhamisho uliofanyika ni **Shilingi bilioni 115.5** sawa na **asilimia 316.** Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa uhamisho wa fedha katika mafungu unazingatia sheria na kanuni zilizopo. Vilevile, Kamati inaendelea kusisitiza Maafisa Masuuli kuzingatia vipaumbele vya msingi katika upangaji wa bajeti ili kutoathiri utekelezaji wa bajeti wa mafungu mengine unaotokana na uhamisho.

**ii. Nyongeza ya Bajeti**

**Mheshimiwa Spika,** hadi Desemba 2024, Serikali ilikuwa imepokea **Shilingi bilioni 460** kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na **Shilingi bilioni 130** kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF). Aidha, **Shilingi bilioni 256** zinategemewa kutoka Shirika la Kimataifa la Fedha-IMF ambazo hazikuwa sehemu ya makisio ya bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia mabadiliko hayo, Serikali inapendekeza kuongeza ukomo wa bajeti ya Serikali ya mwaka 2024/25 kutoka **Shilingi trilioni 49.346** hadi **Shilingi trilioni 50.191**. Aidha, mfumo wa bajeti wa mwaka 2024/25 unaopendekezwa ni kama unavyoonekena katika **kiambatisho 1A**. Kamati inampongeza **Mheshimiwa. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** kwa kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza mipango na bajeti ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa sehemu kubwa ya fedha hizo zimeelekezwa kwenye matumizi ya kawaida. Ambapo **Shilingi bilioni 492.424** sawa na **asilimia 58.22** zimepangwa kuelekezwa katika matumizi ya kawaida na **Shilingi bilioni 353.295** sawa na **asilimia 41.78** zimeelekezwa kwenye matumizi ya maendeleo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwasilisha Bungeni marejeo ya bajeti *(Suplimentary Budget)* kama ibara ya 137 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 pamoja na Kifungu cha 43 cha Sheria ya Bajeti Sura 439.

**10 FEBRUARI, 2025**

**SEHEMU YA NNE**

## 4.0. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MABORESHO YA SHERIA YA FEDHA YA MWAKA 2024

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Serikali ilirekebisha mfumo wa kodi, ushuru, ada, na tozo kupitia Sheria ya Fedha Na. 6 ya mwaka 2024, ikilenga kuvutia uwekezaji katika sekta za kimkakati kama viwanda, kilimo, madini, utalii, na miundombinu. Vilevile, maboresho yalilenga kukuza uchumi, kuongeza ajira, na kupunguza gharama za maisha kwa wananchi, sambamba na kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali ili kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali na kuchochea ukuaji wa uchumi jumuishi.

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya Sheria ya Fedha yalitarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **Shilingi bilioni 439.59** kwa mwaka wa fedha wa 2024/25. Katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2024, Serikali ilikusanya **Shilingi bilioni 283.01** ikiwa ni sawa na **asilimia 64.38** ya lengo la mwaka. Kamati inaipongeza Serikali kwa ufanisi unaoashiria kufanikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa kwenye Sera za kodi.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilifanyia maboresho Sheria 29 ambazo ni: -

i. Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura 342;
ii. Sheria ya Bajeti, Sura 439;
iii. Sheria ya Benki Kuu, Sura 197;
iv. Sheria ya Korosho, Sura 203;
v. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147;
vi. Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, Sura 196;
vii. Sheria ya Kudhibiti Uingizwaji wa Bidhaa Nchini, Sura 276;
viii. Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332;
ix. Sheria ya Ardhi, Sura 113;
x. Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura 289;
xi. Sheria ya Madini, Sura 123;
xii. Sheria ya Vyombo vya Moto (Kodi ya Usajili na Uhamishaji), Sura 124;

xiii. Sheria ya Taifa ya Utoaji wa Leseni na Usajili wa Viwanda, Sura 46;
xiv. Sheria ya Afya ya Mimea, Sura 133;
xv. Sheria ya Bandari, Sura 166;
xvi. Sheria ya Reli, Sura 170;
xvii. Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura 220;
xviii. Sheria ya Bima ya Afya kwa wote, Sura 161;
xix. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438;
xx. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148;
xxi. Sheria za Hifadhi za Taifa, Sura 282;
xxii. Sheria ya Wanyama Pori, Sura 283;
xxiii. Sheria ya Hifadhi ya eneo la Ngorongoro, Sura 284;
xxiv. Sheria ya kuendeleza Ufundi Stadi, Sura 82;
xxv. Sheria ya Huduma ndogo za fedha, Sura 407;
xxvi. Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290;
xxvii. Sheria ya Rufani za Kodi, Sura 408;
xxviii. Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41; na
xxix. Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura 251.

**4.1. Tathmini ya Utekelezaji wa Baadhi ya Sheria zilizokuwa kwenye Sheria ya Fedha kwa kipindi cha nusu mwaka**

**4.1.1. Sheria ya Reli, Sura 170**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Reli, Sura 170 kifungu cha 68 kwa kuongeza kiwango cha Tozo ya Maendeleo ya Reli *(Railway Development Levy)* kinachotozwa kwa bidhaa zote zinazoingia na kutumika nchini kutoka **asilimia 1.5** ya thamani ya mizigo ikifika bandarini (CIF) hadi **asilimia 2**. **Asilimia 50** ya mapato yanayotokana na tozo hii yalielekezwa katika Mfuko wa Dharura na **asilimia 50** ya mapato hayo yalielekezwa katika Mfuko wa Reli. Baada ya kufanya uchambuzi Kamati ilibaini masuala yafuatayo:-

i. Makusanyo yanayotokana na tozo ya maendeleo ya reli kwa kipindi cha nusu mwaka ni **Shilingi bilioni 353.11**, kiasi kilichopelekwa kwenye Mfuko wa Dharura ni **Shilingi bilioni 176.56** ikiwa ni nusu ya fedha zote zilizokusanywa kutoka chanzo hiki. Hata hivyo, Kamati ilibaini katika kipindi hicho Shirika la Reli Tanzania (TRC) lilipokea **Shilingi bilioni 14.57** sawa

na **asilimia 4.94** ya makusanyo yaliyotakiwa kupelekwa yenye jumla ya **Shilingi bilioni 145.05**. Kamati inaitaka Serikali kuwasilisha fedha zote zilizokusanywa kwenye mifuko husika kama zilivyokusanywa ili kutoathiri utekelezaji wa miradi; na

ii. Chanzo cha tozo ya Maendeleo ya Reli kina uwezo wa kukusanya **Shilingi bilioni 684.67** kwa mwaka ambacho kikigawanywa kati ya Mfuko wa Reli na Mfuko wa Dharura, kila mfuko unatakiwa kupata **Shilingi bilioni 342.3**. Hata hivyo, Kamati ilibaini Mfuko wa Reli katika mwaka 2024/25 ulipewa ukomo wa **Shilingi bilioni 294.80** ikiwa ni pungufu ya **Shilingi bilioni 47.54** ambazo mfuko ulistahili kutengewa. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa katika mwaka ujao wa fedha Mfuko wa Reli uidhinishiwe fedha kulingana na uwezo wa chanzo kukusanya.

**4.1.2. Sheria ya Kudhibiti Uingizwaji wa Bidhaa Nchini, Sura 276**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilifanya marekebisho kwenye Sheria hii kwa kuanzisha Tozo ya Maendeleo ya Viwanda (Industrial Development Levy) kwa baadhi ya bidhaa zinazoingizwa nchini kwa kiwango cha **asilimia 10** kwenye wire rods, bia pamoja na mvinyo (wine), **asilimia 5** kwenye bia zisizo na kilevi (non-alcoholic beer), **asilimia 5** kwenye vinywaji vya kuongeza nguvu *(energy drinks),* **asilimia 10** kwenye sabuni za unga *(detergents),* sabuni za maji, Sementi Klinka na Portland.

**Mheshimiwa Spika,** lengo la hatua hii ni kuvutia uwekezaji nchini, kuchochea mauzo nje ya nchi na kulinda uzalishaji wa ndani kwa kuwa bidhaa husika zinazalishwa kwa wingi nchini. Hadi kufikia Desemba 2024, Serikali ilikuwa imekusanya **asilimia 36.19** ya mapato yote yaliyokuwa yamekusudiwa ikiashiria kufanikiwa kwa sera ya Serikali ya kulinda viwanda vya ndani. Kamati inaishauri Serikali kuanzisha Mfuko maalumu ambapo fedha hizi zitatumika kwa ajili ya kuendeleza viwanda nchini ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Maeneo ya Usindikaji wa Mauzo ya Nje (EPZA) na Maeneo Maalum ya kiuchumi (SEZs)

### 4.1.3. Sheria ya Taifa ya Utoaji wa Leseni na Usajili wa Viwanda, Sura 46

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria hii kwa kuanzisha utaratibu wa Serikali kusaini Mikataba ya Utekelezaji *(Performance Agreement)* na viwanda vinavyolindwa na Serikali kwa kupewa unafuu wa kodi ikiwemo ushuru wa forodha kupitia utaratibu wa *Duty Remission*, Kodi ya Ongezeko la Thamani kupitia utoaji wa msamaha au utozaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri *(Exemption au Zero Rated)* pamoja na viwanda vitakavyolindwa na Serikali kutokana na sera za kuongeza kodi kwenye bidhaa zinazotoka nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Desemba, 2024, Serikali ilikuwa imeingia mikataba na **viwanda 104** ambavyo misamaha yake kupitia Sheria mbalimbali za kodi ina jumla ya kiasi cha **Shilingi bilioni 61.53**. Hatua hii kipekee imewezesha kuongeza udhibiti wa vivutio vinavyotolewa kwa viwanda vya ndani pamoja na kuweka urahisi wa ufuatiliaji wa viwanda hivyo.

Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya suala la kutumia misamaha ya kodi kama vivutio kwa wawekezaji. Uzoefu unaonyesha kodi sio kikwazo kwenye ufanyaji biashara na uwekezaji bali mazingira wezeshi ya uwekezaji na ufanyaji wa biashara. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuboresha mazingira ya ufanyaji wa biashara nchini ili kuondokana na utaratibu wa kutumia misamaha ya kodi kuvutia wawekezaji.

### 4.1.4. Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332

**Mheshimiwa Spika,** Sheria iliweka takwa kwa raia mkaazi (resident) na asiye mkaazi *(non- resident)* kukusanya kodi ya zuio kwa kiwango cha **asilimia 5** kwenye malipo yanayofanywa kwa mtengenezaji wa maudhui mkaazi *(resident digital content creator)*. Katika hatua hii, Serikali ilitarajia kukusanya **Shilingi bilioni 1.64** kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Desemba, 2024 hakuna kodi iliyokusanywa kutoka katika chanzo hiki kutokana na kutokuwa na mfumo wa ukusanyaji. Kamati imebaini kuwa Serikali

imekuwa ikianzisha kodi mpya bila kuwepo kwa mifumo madhubuti ya ukusanyaji. Mfano kodi ya majengo, kodi ya pango la Ardhi na ushuru wa maegesho ya magari.

Hali hii inasababisha Serikali kutokufikia malengo ya makusanyo yaliyokusudiwa. Ili kuondokana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali kabla kupendekeza vyanzo vipya vya mapato ni muhimu kuwa na utaratibu wa kukusanya ikiwa pamoja na mifumo. Hatua hii itahakikisha Serikali inafikia malengo ya makusanyo iliyojiwekea.

**4.1.5. Sheria ya Madini, Sura ya 123**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilifanya marekebisho kwa kupunguza mrabaha kutoka **asilimia 6** hadi **asilimia 4** kwenye madini ya dhahabu yatakayouzwa Benki kuu ya Tanzania (BOT). Hadi kufikia Desemba, 2024 BoT ilikuwa imenunua dhahabu yenye uzito wa **kilo 2,323.34** sawa na **asilimia 77** ya lengo la **kilo 3000** kwa kipindi cha nusu mwaka. Aidha, dhahabu iliyonunuliwa ilikuwa na thamani ya **Shilingi bilioni 483.33** sawa na **dola za Marekani milioni 197.72** na mrabaha uliokusanywa ni **Shilingi bilioni 19.42**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba, Benki kuu itavuka lengo la kununua dhahabu yenye thamani ya **dola za Marekani milioni 350** kwa mwaka 2024/25 kwa sababu kumekuwa na mwitikio chanya kwa wachimbaji kuiuzia dhahabu Benki Kuu. Hivyo Benki Kuu imeiomba bodi yake kuongeza wigo wa fedha ili iweze kununua dhahabu kwa wingi.

Vilevile, Serikali ilifanya mabadiliko ya Sheria ili kuweka takwa la wamiliki wa leseni za uchimbaji wa madini na wafanyabiashara wa madini kutenga kiasi cha madini kwa ajili ya kuchakatwa, kuyeyushwa, kusafishwa na kuuzwa nchini kisiwe chini ya **asilimia 20** ya dhahabu. Hadi Desemba 2024 **kilo 3,238.74** zimechenjuliwa na kusafishwa nchini ikilinganishwa na **kilo 411.46** za mwaka 2023/24.

Kamati inaipongeza Serikali ya **Mheshimiwa. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa hatua hii

na imedhihirisha kwamba Sera zikiwa nzuri madini yetu hayatatoroshwa na kunufaisha mataifa mengine.

#### 4.1.6. Sheria ya Bima ya Afya kwa wote Sura 161

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria hii kwa kuelekeza **asilimia 2** ya mapato ya Ushuru wa Bidhaa yanayokusanywa kutoka kwenye bidhaa za vinywaji vyenye kaboni, vileo na bidhaa za vipodozi kwenye Mfuko wa Bima ya Afya kwa wote. Lengo la hatua hii lilikuwa kupata fedha zitakazotumika kwa ajili ya kugharamia bima ya afya kwa wote. Katika hatua hii Serikali ilitarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi bilioni 18.8** na kupelekwa kwenye Mfuko wa Bima ya Afya.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Desemba, 2024, Serikali ilikusanya kiasi cha **Shilingi bilioni 61.45** sawa na **asilimia 326.86** ya lengo la mwaka**.** Kamati inampongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kulichukua suala hili kwa umuhimu wake na kulitafutia chanzo mahsusi na cha uhakika. Hata hivyo, Kamati inashauri kwa kuwa, Kanuni za kutekeleza Bima ya afya kwa wote hazijakamilika, Serikali ihakikishe fedha hizo zinalindwa ili zisitumike nje ya matumizi yaliyokusudiwa.

## SEHEMU YA TANO

### 5.0. MWELEKEO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI JUMLA NA BAJETI YA SERIKALI HADI JUNI, 2025

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia mwenendo wa kuridhisha wa viashiria jumla vya uchumi hususan Pato la Taifa pamoja na utekelezaji wa bajeti ambao hadi Desemba, 2024 ulikuwa umefikia **asilimia 51.9,** ni dhahiri kuwa Serikali itafanikiwa kufikia malengo na shabaha iliyojiwekea. Kwa kuzingatia mwenendo huo, Kamati inaushauri ufuatao:-

#### 5.1. Viashiria vya uchumi jumla

i. Katika mwaka 2024, uchumi unatarajia kukua kufikia **asilimia 5.4** ambapo katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2024

uchumi ulikuwa umefikia **asilimia 5.4.** Aidha, uchumi unatarajiwa kukua kwa **asilimia 6.0** mwaka 2025 na **asilimia 6.1** mwaka 2026.

Ili malengo haya yafikiwe ni vyema Serikali iendelee kutekeleza miradi ya maendeleo pamoja kuimarisha mahusiano yake na washirika wa maendeleo ili kuendelea kupata fedha za kutekeleza miradi nchini; na

ii. Ili mfumko wa bei uendelee kubaki katika wigo wa asilimia 3 hadi 8 Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuhakikisha kuna chakula cha kutosha nchini ili kuzuia mfumko wa bei unaoweza kusababishwa na ukosefu wa chakula.

### 5.2. Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali Januari – Juni, 2025

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia ufanisi kwenye ukusanyaji wa mapato katika kipindi cha nusu mwaka, utekelezaji wa bajeti ya Serikali unatarajiwa kufikia malengo yaliyokusudiwa. Aidha, katika kipindi cha Januari hadi Juni 2025, Serikali inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi trilioni 24.56** kutoka vyanzo vyote ikijumuisha mapendekezo ya nyongeza ya bajeti ya **Shilingi bilioni 845.7** na kutumia kiasi hicho katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kusimamia matumizi sahihi ya mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato, mifumo ya ununuzi pamoja na kuhimiza nidhamu ya matumizi sanjari na kupunguza matumizi yayasiyo ya lazima ya fedha za umma.

## SEHEMU YA SITA

### 6.0. UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE YALIYOTOKANA NA TAARIFA YA KAMATI YA MWAKA 2024

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitoa maoni na mapendekezo mahsusi 9 ambayo Bunge iliyapitisha na kuwa Maazimio ya Bunge kwa Serikali. Kamati imefanya ufatiliaji wa utekelezaji wa maazimio hayo na kubaini kwamba, Serikali imefanyia kazi kikamilifu mazimio 2, inaendelea kufanyia kazi maazimio 5 na maazimio 2 hayakufanyiwa kazi.

**6.1. Maazimio yaliyofanyiwa Kazi na Serikali**

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na**Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **kwa kutekeleza kikamilifu maazimio yafuatayo:-**

**6.1.1. Fedha za Mkopo wa ECF kujumuisha Sekta ya Utalii**

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ukuaji wa sekta ya utalii na changamoto zinazoikabili sekta hiyo kama uhaba wa miundombinu ya msingi kama vile barabara na viwanja vya ndege, Bunge liliazimia kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii iwasilishe mahitaji ya fedha za maendeleo Wizara ya Fedha ili wapate mgao wa fedha za ECF mwaka wa fedha 2024/25.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maliasili na Utalii iliwasilisha kwa Wizara ya Fedha maombi ya nyongeza ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo kutokana na hali ya kibajeti Wizara iliongezewa **Shilingi Bilioni 19**. Aidha, Wizara imepewa *retention* ya **asilimia 3** kwa ajili ya uhifadhi na **asilimia 6** kwa ajii ya kuendeleza utalii kupitia mapato ya baadhi ya Taasisi zilizo chini ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo na inaishauri Serikali kuongeza bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii katika mwaka wa fedha 2025/26 ili kutatua changamoto zinazoikabili sekta hiyo.

**6.1.2. Riba za Mikopo katika Sekta ya Benki**

**Mheshimiwa Spika,** Bunge liliazimia kwamba Benki Kuu ya Tanzania ifanye uchambuzi wa kina wa vigezo vinavyotumika na mabenki katika kupanga riba na kubainisha mikakati ya muda mfupi, wa kati na mrefu ya kupunguza gharama hizo ili mikopo ipatikane kwa riba nafuu kwa ajili ya uwekezaji na ufanyaji biashara.

**Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** alisikia kilio hicho na kuielekeza Wizara ya Fedha na Benki kuu ya Tanzania ambazo zimebainisha mikakati

ya kupunguza gharama za mikopo ili ipatikane kwa wananchi kwa riba nafuu kwa ajili ya uwekezaji na ufanyaji biashara.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya jitihada za Serikali za kuweka mikakati ya kupunguza gharama za mikopo, Kamati inaitaka Serikali kuwasilisha mbele ya Bunge lako vigezo vinavyotumiwa na mabenki katika kupanga gharama za kibenki na riba za mikopo.

Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuonyesha ni kwa namna gani mikakati iliyobainishwa imesaidia kupunguza viwango vya riba za mikopo nchini.

### 6.2. Maazimio ambayo yapo katika hatua za utekelezaji

**Mheshimiwa Spika,** maazimio ambayo yapo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji ni yafuatayo: -

#### 6.2.1. Kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti Fedha Haramu

**Mheshimiwa Spika,** Bunge liliazimia Serikali kubadilisha Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU) na kuwa Mamlaka ili ifanye kazi kwa kujitegemea kama ilivyo kwa nchi ya Zambia. Vilevile, Bunge liliazimia Serikali kufanya mabadiliko kwenye Kifungu cha 7(1) na (3) cha Sheria ya Utakatishaji wa Fedha Haramu Sura ya 423 ili kukiwezesha kitengo hiki kuwa na uwezo wa kuajiri na kuwajibisha watumishi kwa kuwa hivi sasa Kamishna wa Kitengo hiki hawezi kuwawajibisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliarifiwa kwamba Serikali ipo katika mchakato wa kutekeleza azimio hilo ambapo Serikali imeshakamilisha rasimu ya marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu kupitia utaratibu wa Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali pindi utakapokamilika na kuwasilishwa Bungeni. Aidha, Serikali inaendelea kufanyia kazi mapendekezo ya kuiongezea FIU watumishi ili kuziba nafasi zilizowazi ikiwa ni suluhisho la muda mfupi *(temporary measure)* wakati mchakato wa marekebisho ya sheria unaendelea.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyofikiwa katika kutekeleza azimio la Bunge. Hata hivyo, Kamati

inaitaka Serikali kuhakikisha inakamilisha mchakato huo mapema ili kuiwezesha FIU kuwa Mamlaka kamili inayojitegemea.

### 6.2.2. Utekelezaji wa miradi ya Barabara kwa Mfumo wa Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)

**Mheshimiwa Spika,** Serikali iliitaarifu Kamati kwamba miradi mbalimbali imeainishwa na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kwa njia ya ubia. Moja ya mradi hiyo ni Barabara ya Dar es Salaam – Dodoma iliyogawanyika katika vipande vitatu (3) kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho namba 1B.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na majibu ya Serikali, Kamati inaona kwamba bado kasi ya utekelezaji wa miradi hii ni mdogo kwa kuzingatiwa miradi 9 ambayo ilitakiwa kuanza kutekelezwa katika mwaka 2024/25 kama ilivyoelekezwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya kina kuhusu changamoto zinazosababisha mfumo wa utekelezaji wa miradi kwa njia ya PPP usifanikiwe nchini. Baada ya tathmini hiyo vikwazo viondolewe ili Taifa lianze kunufaika na uwekezaji kwa njia ya PPP.

### 6.2.3. Serikali Kuandaa Sera na mkakati wa Ununuzi, Ugavi na uondoshaji Mali za Umma

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipewa taarifa kwamba, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuandaa Sera na Mkakati wa Ununuzi wa Umma baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri tarehe 16 Januari, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hizo, hata hivyo Kamati inapendekeza mchakato huo kupewa kipaumbele na Serikali ili ukamilike kwa wakati. Itakumbukwa kwamba takribani **asilimia 70** ya bajeti ya Serikali hutumika katika masuala ya ugavi. Hivyo, kukamilika kwa mchakato huu kutaokoa fedha za Serikali.

### 6.2.4. Kutungwa kwa Sheria na Sera ya Usimamizi wa Mali za Serikali *(Government Assets Management Act)*

**Mheshimiwa Spika,** Bunge liliazimia kwamba Serikali iwasilishe Bungeni Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mali za Umma ili kuweka msingi wa kisheria utakaoongeza uwajibikaji, uwazi, udhibiti na ufanisi katika usimamizi wa mali za umma. Kamati ilijulishwa kwamba Sheria hiyo bado haijatungwa na itaandaliwa mara baada ya Serikali kuidhinisha rasimu ya Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi ambayo iko katika hatua za awali za maandalizi kwa kushirikiana na Wadau.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inajumla ya mali zenye thamani ya **Shilingi trilioni 77**. Mali hizi zinasimamiwa na Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali kutoka Wizara ya Fedha. Endapo Idara hii itaendelea kusimamia Mali hizi bila Sera wala Sheria ni wazi kwamba kutakuwa na upotevu na ubadhirifu wa mali za Serikali. Kamati inatambua kwamba Serikali imeshindwa kutekeleza azimio la Bunge kutokana na mchakato wa kutunga Sera ya usimamizi wa mali kutokukamilika kwa wakati. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kukamilisha mchakato huo mapema iwezekanavyo na kisha kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mali za Serikali Bungeni.

### 6.2.5. Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya Kutekeleza Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi kuhusu utekelezaji wa Azimio hili na kubaini kwamba vipengele viwili kati ya vinne vimetekelezwa. Vipengele hivyo ni kupanua wigo wa kodi pamoja na matumizi ya mifumo katika kukusanya kodi. Vilevile, kipengele cha kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kimefanyiwa kazi kwa kiasi. Vipengele ambavyo havikutekelezwa ni:-

i. Kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija ili kufikia **asilimia 1** ya Pato la Taifa ambapo hivi sasa misamaha ya kodi ni **asilimia 1.3** ya Pato la Taifa; na

ii. Kuangalia uwezekano wa kufuta madeni ambayo Taasisi za Umma zinadaiana kama hayasababishi hasara kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Serikali kutekeleza vipengele vilivyobaki katika azimio hili kikamilifu.

**6.3. Maazimio ambayo hayajafanyiwa kazi**

**Mheshimiwa Spika,** maazimio ambayo hayajafanyiwa kazi na Serikali ni yafuatayo: -

**6.3.1. Uwepo wa Sera na Sheria ya Ufuatiliaji na Tathmini**

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na changamoto ya miradi kutokukamilika kwa wakati, kutekelezwa kwa muda mrefu kuliko ulivyokusudiwa, kutokufikia malengo na kutekelezwa chini ya kiwango, Bunge liliazimia kwamba Serikali ikamilishe utungaji wa Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini na kisha kutunga Sheria ambayo itabainisha mgawanyo wa majukumu na adhabu katika kufanya Ufuatiliji na Tathmini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati bado inaitaka Serikali kutekeleza azimio hili kikamilifu hadi ifikapo mwezi Machi, 2025.

**6.3.2. Matumizi ya Seti ya Mitambo ya kuchimba visima na mabwawa**

**Mheshimiwa Spika,** Bunge liliazimia Serikali kuweka utaratibu wa kutoa ruzuku kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ili kuziwezesha Halmashauri zisizokuwa na mapato ya kutosha zinufaike na mitambo hiyo. Vilevile, kuhakikisha Halmashauri zenye mapato ya kutosha na zenye uhitaji wa mitambo hiyo zinatenga Bajeti katika mwaka wa fedha 2024/25. Kamati ilitaarifiwa kwamba Serikali kupitia Wizara ya Maji inaendelea na Programu ya Uchimbaji wa visima 900 ambapo kila Jimbo/Halmashauri itachimbiwa visima 5 kwenye Majimbo 184.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na jitihada za Serikali za kuchimba visima 900 nchini, Serikali haijaweka bayana utaratibu wa kutoa ruzuku kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini

(RUWASA) ili kuziwezesha Halmashauri zisizokuwa na mapato ya kutosha zinufaike na mitambo hiyo. Vilevile, Serikali haikueleza Halmashauri zenye mapato ya kutosha na zenye uhitaji wa mitambo hiyo zinatenga Bajeti kiasi gani katika mwaka wa fedha 2024/25. Ikumbukwe kwamba baada ya mitambo hiyo kumaliza kuchimba visima 900 mitambo hiyo haitaendelea kutumika kwa sababu ya ukosefu wa fedha.

## SEHEMU YA SABA

## 7.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA UJUMLA

### 7.1. Diplomasia ya Uchumi

**Mheshimiwa Spika,** Diplomasia ya uchumi ni mkakati unaolenga kukuza maslahi ya kiuchumi ya Taifa kupitia sera na mbinu za kidiplomasia. Serikali imekuwa ikitekeleza diplomasia ya uchumi kwa ajili ya kuvutia uwekezaji, kuimarisha biashara, na kupata teknolojia ya kisasa. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo: -

i. Kuhakikisha sera na sheria za kiuchumi ni thabiti, wazi, na zinazochochea uwekezaji. Aidha, kupunguza urasimu na kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji mpya;

ii. Kuunda na kuimarisha mikataba ya biashara na ushirikiano wa kiuchumi na nchi na Mashirika mbalimbali duniani; na

iii. Kuanzisha na balozi katika nchi ambazo ni washirika wakubwa wa kibiashara ili kukuza biashara na uwekezaji.

### 7.2. Mabadiliko ya Sera za Kodi

**Mheshimiwa Spika**, mabadiliko ya mara ya mara ya Sera za kodi yamekuwa na matokeo hasi katika kuchagiza ukusanyaji wa mapato. Mfano, kodi ya majengo haikusanywi kwa ufanisi kutokana na mabadiliko ya mara kwa mara ya usimamizi. Katika kipindi cha miaka 8 (2016-2024) yamefanyika mabadiliko

mbalimbali ya usimamizi wa chanzo hiki kati ya TRA na Serikali za Mitaa.

Aidha, mabadiliko mengine yaliyofanyika kwenye chanzo hiki ni kutoza kwa kutumia uthamini na baadae kwenda kwenye viwango mfuto ambapo hivi sasa Serikali inatarajia kurudi kwenye utaratibu wa kutoza kwa kutumia uthamini ifikapo mwaka 2026. Vilevile, kodi hii imekuwa ikikusanywa kwa mifumo tofauti kutoka Mfumo wa *Property Rate Management System* (PRMS), Lipa Umeme Kadiri Unavyotumia (LUKU) na Mfumo wa TAUSI.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuwa na Sera himilivu na zinazotabirika. Vilevile, Serikali ione umuhimu wa vyanzo vyake vya kodi kusimamiwa na Taasisi moja badala ya kusimamiwa na taasisi mbili tofauti kama ilivyo hivi sasa ambapo kodi hiyo inasimamiwa na Serikali za Mitaa lakini mfumo wa makusanyo upo chini ya TANESCO.

**7.3. Mifumo ya Serikali kutokusomana**

**Mheshimiwa Spika,** changamoto kubwa inayoikabili mifumo ya Serikali ni kutokusomana kwa mifumo hiyo na kuweza kubadilishana taarifa. Serikali imepiga hatua katika kujenga uwezo wa kuandaa mifumo yake yenyewe. Changamoto iliyopo ni mifumo kushindwa kusomana na kubadilishana
Taarifa.


**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kupitia Ega kwa ajili ya kuunganisha mifumo.

**7.4. Ukopaji kwa kutumia Sarafu zaidi ya Moja**

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia changamoto ya kushuka kwa thamani ya Shilingi na kusababisha kuongezeka kwa gharama ya malipo ya deni la Serikali, Serikali imepanga kuendelea kukopa kupitia sarafu nyingine zaidi ya dola ya Marekani *(Currency Diversification)* ili kupunguza utegemezi wa deni la Serikali kwa kiasin kikubwa kuwa kwenye dola ya Marekani. Pendekezo hili ni zuri hata hivyo, mara nyingi masharti yanayoambatana na mikopo kwa kutumia sarafu nyingine tofauti na dola hufanya

marejeo ya viwango vya kubadilisha kwa dola ya Marekani pindi malipo yanapofanyika. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza hatua hiyo kwa uangalifu mkubwa na kwa kuzingatia maslahi ya Taifa.

**Kielelezo Na. 3: Mwenendo wa Deni la Nje kwa Aina ya Sarafu**




### 7.5. Matumizi ya Sarafu Mtandao *(Cryptocurrency)*

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Sheria ya Fedha Na.6 ya Mwaka 2024, ilianza kutoza kodi ya zuio ya **asilimia 3** kwenye mapato yanayotokana na uhamishaji au ubadilishanaji wa mali za kidijitali *(digital assets)*. Lengo la mwaka lilikuwa ni kukusanya **Shilingi milioni 465** kutoka katika chanzo hiki. Hadi kufikia mwezi Desemba 2024 Serikali ilifanikiwa kukusanya **Shilingi milioni 988.60** sawa na ufanisi wa **asilimia 212.60**. kwa kuwa biashara hii ipo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Benki Kuu kuona namna bora ya kudhibiti Sarafu Mtandao kwa sababu hata kama Benki Kuu haiitambui, biashara hiyo ipo.

### 7.6. Mchango wa Sekta ya Fedha na Bima

**Mheshimiwa Spika,** mchango wa sekta ya Fedha na Bima katika ukuaji wa uchumi umezidi kuongezeka kutoka **asilimia 2.4** mwaka 2021 hadi **asilimia 13.7** mwaka 2024 ambapo bima ya vyombo vya moto iliongoza kwa kuchangia zaidi kwa **asilimia 26.6.** Hata hivyo, Takwimu za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) zinaonyesha kwamba, katika kipindi cha miaka 6 (2016 hadi 2021) zaidi ya

**asilimia 63** ya vyombo vya moto ukiondoa magari ya Serikali na mitambo nchini havikukatiwa bima. Hii ni kinyume na kifungu cha 4 (1) na (2) cha Sheria ya bima za Vyombo vya Moto Sura ya 169. Ili kuepusha wananchi wengi kutopoteza mali zao pindi wanapopata majanga, Kamati inaishauri Serikali kusimamia Sheria na kuhakikisha wananchi wote kukata bima.

## SEHEMU YA NANE

## 8.0. MAONI NA MAPENDEKEZO MAHSUSI

### 8.1. Ukusanyaji wa Kodi ya Majengo

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Serikali kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI inaendelea kusimamia utekelezaji wa jukumu la ukusanyaji wa Kodi ya Majengo kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 Kifungu cha 6(1) (t) na 7(1) (y).

**NA KWA KUWA,** moja ya mabadiliko yaliyofanywa na Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023 katika Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, SURA 289 ni kuondoa jukumu la ukusanyaji wa kodi hiyo kutoka TRA kwenda katika Serikali za Mitaa.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia yafuatayo:-

i. Kuhakikisha kiwango cha mapato cha asilimia 20 cha kodi ya majengo kinarejeshwa katika Halmashauri kwa wakati, pamoja na kuangalia uwezekano wa kuongeza kiwango hicho; na

ii. Katika mwaka wa fedha 2024/25 Serikali iongeze kiwango kinachorejeshwa kutokana na kodi ya majengo kutoka **asilimia 20** ya sasa hadi walau **asilimia 50** kwa kipindi cha zoezi la usajili wa majengo ili kuharakisha zoezi la utambuzi na uthamini wa majengo pamoja na kuandaa rejesta na kisha kurudisha **asilimia 20** ya awali;

iii. Kuboresho mfumo wa Tausi ili kuwezesha ukusanyaji wa Kodi ya Majengo ikiwa ni pamoja na usimikaji wa Moduli ya Kodi ya Majengo katika mfumo wa Tausi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 137; na

iv. Kuajiri wataalam wa kutosha katika Halmashauri kwa ajili ya kufanya zoezi la uthamini wa majengo

**8.2. Misamaha ya Kodi**

**Mheshimiwa Spika**, **KWA KUWA** Serikali imekuwa inatoa misamaha ya kodi mbalimbali kwa wawekezaji pamoja na wafanyabiashara kwa lengo la kuvutia uwekezaji nchini.

**NA KWA KUWA**, kiwango cha utoaji wa misamaha ya kodi kinatakiwa kutozidi **asilimia 1.3** ya Pato la Taifa kwa mwaka 2024. Tafiti zinaonyesha kwamba changamoto kubwa za uwekezaji nchini ni mazingira mabovu ya ufanyaji biashara na uwekezaji na sio viwango vya kodi.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali kufanya tathmini ya misamaha yote ya kodi ili kuhakikisha kwamba misamaha inayotolewa ina tija na inakuwa ndani ya kiwango kinachokubalika cha chini ya **asilimia 1.3** ya Pato la Taifa. Aidha, Serikali iendelee kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ilikuvutia wawekezaji nchini.

**8.3. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kupitia Kamishna Mkuu kupewa uwezo wa kufanya uchunguzi wa Kodi *(Tax Investigation)***

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** TRA imekuwa ikifanya uchunguzi wa masuala ya kodi, ili kubaini ubadhirifu unaofanywa na Kampuni au wafanyabiashara wasio waaminifu na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria za kodi pale inapobainika mfanyabiashara au Kampuni ina makosa.

**NA KWA KUWA,** katika kufanya chunguzi hizo huwa wanatumia askari Polisi ambao hawana utaaalamu kuhusu masuala ya kodi na wakati huo huo ndio wanatakiwa kuchukua maelezo ya mtuhumiwa. Hatua, hii imekuwa inafanya mamlaka ya Mapato kupoteza kodi ambayo inatakiwa kukusanywa pindi shitaka linapofika mahakamani.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani pamoja na Wizara ya Fedha kufanya kikao cha pamoja kabla ya Vikao vya Kamati vya mwezi Machi, 2025 ili kubainisha utaratibu utakaotumika kuondokana na changamoto hii. Endapo itaonekana kuna ulazima wa kufanya mabadiliko yafanyike kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2025. Aidha, Taarifa ya kikao hicho na maamuzi yake yawasilishwe kwenye Kamati.

### 8.4. Serikali kupunguza Matumizi yasiyo ya lazima

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Serikali katika kipindi cha miaka mitatu imekuwa ikibainisha mikakati mbalimbali ya kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ikiwemo kupunguza ununuzi wa magari ya Serikali na badala yake kuanzisha utaratibu wa kuwakopesha magari watumishi wenye stahili hiyo.

**NA KWA KUWA,** mikakati hiyo imekuwa haitekelezwi ipasavyo ambapo katika Mwaka wa Fedha 2022/23 kiasi cha **Shilingi bilioni 500** kilitengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba Serikali kufanya marejeo ya kina ya matumizi ya Serikali na kupunguza matumizi yasio ya lazima kabla ya kuanza utekelezaji wa mpango wa Taifa wa miaka mitano unaotarajiwa kuanza mwaka 2025/26 hadi 2030/31. Tathmini hiyo itasaidia kupata fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

### 8.5. Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** mifuko ya Hifadhi ya Jamii imekuwa inafanya uwekezaji usio na tija ambapo kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/22, 2022/23 Mfuko wa PSSSF umelipa mafao ya wastaafu yenye thamani ya **Shilingi trilioni 4.34** na kupata faida *(Return)* ya **Shilingi trilioni 1.8**. Takwimu hizi zinaonyesha kiasi kilicholipwa ni kikubwa ukilinganisha na faida inayotokana na uwekezaji wake. Vilevile, kiwango cha uhimilivu cha Mfuko ni **asilimia 36.4** ikilinganishwa na kiwango kinachokubalika cha **asilimia 60** na lengo la chini la uhimilivu la **asilimia 40**.

**NA KWA KUWA,** usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hufanywa na Benki Kuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu kwa mujibu wa Sheria ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba Serikali ihakikishe kuwa Mifuko hii inasimamiwa ipasavyo katika kuhakikisha kuwa uwekezaji unaofanywa ni wa tija na unaendana na michango. Hatua hii itasaidia kupunguza vihatarishi na kuwezesha Mifuko kulipa mafao ya wastaafu kwa wakati.

**8.6. Usimamizi wa Mashirika ya Umma**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Sheria ya Msajili wa Hazina Sura ya 370 inaipa mamlaka Ofisi ya Msajili wa Hazina kusimamia uwekezaji na mali nyingine za Serikali katika Taasisi, Mashirika ya Umma pamoja na Kampuni ambazo Serikali inamiliki hisa chache. Vilevile, Sheria hiyo inampa Msajili wa Hazina mamlaka ya kusimamia, kuweka malengo ya kifedha pamoja na kutathmini ufanisi wa utendaji kazi.

**NA KWA KUWA,** Mashirika mengi yamekuwa yakijiendesha chini ya ufanisi ambapo katika kipindi cha miaka mitatu (3) iliyopita kwa Mashirika ambayo Serikali inamiliki hisa chache, Serikali imekuwa ikipata gawio zaidi ikilinganishwa na Mashirika ambayo Serikali inayamiliki kwa **asilimia 100**. Vilevile, baadhi ya Mashirika Umma yanayojiendesha kibiashara na yalitakiwa kujitegemea bado yanapata ruzuku kutoka Serikali Kuu.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba Serikali kuondoa ruzuku kwa Mashirika yanayojiendesha kibiashara ili yaweze kujiendesha kibiashara, kukidhi bajeti zao na kutoa gawio kwa Serikali.

**8.7. Urejeshwaji wa ukusanyaji wa Mapato ya Taasisi na Mamlaka za Uhifadhi wa Wanyamapori**

**Mheshimiwa Spika**, **KWA KUWA** Sekta ya Utalii imeonekana kufanya vizuri kwa upande wa mapato yanayotokana na shughuli

za utalii ambayo yamepelekea kuimarika kwa urari wa biashara na huduma nje;

**NA KWA KUWA,** Taasisi za uhifadhi wa Wanyamapori zinajiendesha kwa misingi ya kibiashara, utaratibu wa utolewaji wa fedha kama ilivyo kwa Wizara au Idara za Serikali umekuwa unaathiri utendaji kazi wake;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba Serikali kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2025 kufanya mabadiliko ya kurejesha utaratibu wa Taasisi hizi kukusanya na kutumia mapato yake kulingana na bajeti zilizoidhinishwa. Vifungu vinavyotakiwa kufanyiwa mabadiliko ni Kifungu cha 9 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura ya 282, Kifungu cha 12(2) cha Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro Sura ya 284 pamoja na Jedwali la kwanza la Sheria ya Mamlaka ya Mapato Sura ya 399. Marekebisho haya yaende sambamba na kuondoa Sheria hizo kwenye jedwali la kwanza la Sheria ya Mamlaka ya Mapato Sura ya 399. Hatua hiyo itasaidia Taasisi na Mamlaka hizo kutumia mapato yake kuimarisha miundombinu ya msingi katika hifadhi ili kuvutia watalii wengi zaidi.

**8.8. Ulipaji wa madeni ya Wazabuni, Wakandarasi na Watoa huduma**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** changamoto ya ulipaji wa madeni ya wazabuni, wakandarasi na watoa huduma imekuwa ni jambo la muda mrefu na limekuwa likiathiri utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa miaka 5 mfululizo.

**NA KWAKUWA,** Tangu mwaka 2022 ilipofanyika tathmini ya kina na kubaini Serikali inadaidwa **Shilingi bilioni 3,200** na tangu kipindi hicho haijafanyika tathmini ya kina kama hiyo.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia masuala yafuatayo:-

i. Serikali kufanya tathmini ya kina ya madeni yote ya wazabuni, wakandarasi na watoa huduma kuanzia mwezi Februari hadi 30 Aprili, 2025 ili kubaini ni kiasi gani Serikali inadaiwa;

ii. Serikali kuweka ukomo wa siku 90 wa uhakiki wa madeni kwa kufanya mabadiliko kwenye Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Sura ya 348 ili kuondoa kisingizio cha kuchelewa kulipa kwa sababu ya kufanya uhakiki; na

iii. Serikali kuwasilisha Taarifa ya tathmini kwenye kamati ya Bajeti Sanjari na hatua za kulipa madeni hayo.

**Mheshimiwa Spika,** hatua hizi zikifanyika zitaondoa madhira ambayo sekta binafsi nchini inapitia ikiwa ni pamoja na baadhi ya watu kufilisika kutokana na Serikali kutolipa kwa wakati.

## SEHEMU YA TISA

## 9.0. MAFANIKIO NA CHANGAMOTO

### 9.1. Mafanikio

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika kutekeleza majukumu yake katika kipindi cha Februari, 2024 – Januari, 2025, ilipata mafanikio yafuatayo: -

a) Kupokea, kujadili na kutoa mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria mbalimbali za kodi kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2024 iliyokuwa na jumla ya Sheria 29;

b) Kuendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi ya REA, Kilimo na Uvuvi inayopokea fedha za mkopo kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF Extended Credit Facility* – ECF);

c) Kusimamia utolewaji wa fedha na utekelezaji wa miradi kupitia mifuko iliyozingirwa *(Ring Fenced Fund),* Mfuko wa Maendeleo ya Reli, Mfuko wa Maendeleo ya Barabara, Mfuko wa Dharula, Mfuko wa Maji na Mfuko wa Maendeleo ya Umeme Vijijini;

d) Kufanikisha utwaaji wa maeneo mapya ya Bunge na hivyo kuongeza eneo la Bunge kwa **mita za mraba 122,924** kutoka mita za **mraba 42, 312**;

e) Urejeshwaji wa ukusanyaji wa Mapato yanayotokana na wharfage kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA);

f) Kuwasilisha Bungeni jumla ya Taarifa nane. Taarifa hizo ni:-

i. Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka unaoishia 2023/24 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2024/25;

ii. Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Mfuko wa Bunge, Mahakama na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (NAOT) kwa mwaka 2023/24 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mifuko hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/25;

iii. Taarifa kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2022, Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/23, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2023/24 pamoja na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/25;

iv. Taarifa kuhusu Maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha kwa mwaka 2024 *(The Finance Bill, 2024)*; na

v. Taarifa kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2024/25 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2025/26.

g) Kamati ilifanikiwa kupokea na kuchambua jumla ya Taarifa 353 zilizowasilishwa kwenye Kamati na kuzitolea mapendekezo; na

h) Kamati ilifanikiwa kukutana na Wizara za Serikali zaidi ya 20, Taasisi za Serikali zaidi ya 34 pamoja na Taasisi za Sekta binafsi 38 ili kupitia, kujadili na kutoa mapendekezo na ushauri katika masuala mbalimbali.

## 9.2. Changamoto

### 9.2.1. Utofauti wa Takwimu

**Mheshimiwa Spika,** bado kumekuwa na changamoto ya utofauti wa takwimu ambazo zinakuwa zinatolewa na Wizara na Taasisi za Serikali zinazohusu suala moja. Mathalani, fedha za Mfuko wa Reli zilizotolewa katika kipindi cha nusu mwaka 2024/25 ambapo Taarifa ya Shirika la Reli ilionyesha imepokea **Shilingi bilioni 14.57** wakati Taarifa ya Wizara ya Fedha inaonyesha fedha zilizopelekwa kwenye kwenye Mfuko ni **Shilingi bilioni 145.05.** Vivyo hivyo taarifa za ukuaji wa uchumi ambapo sekta ya kilimo Desemba, 2023 ilikua kwa **asilimia 24.8** hata hivyo Taarifa ya Wizara ya Fedha kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha nusu mwaka 2024/25 inaonyesha sekta ya kilimo Desemba, 2023 ilikua kwa **asilimia 17.2**.

**Mheshimiwa Spika,** utofauti wa takwimu umekuwa ukisababishia Kamati kushindwa kufanya uchambuzi wa kina pamoja na kushindwa kutegemea taarifa za Serikali kufanyia maamuzi. Kamati inaishauri Serikali ihakikishe inaondoa utofauti wa takwimu zinazowasilishwa katika Kamati, ili kuondoa mkanganyiko katika uchambuzi wa taarifa.

## SEHEMU YA KUMI

## 10.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), pamoja na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mb Naibu Spika kwa miongozo yenu ambayo imeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na weledi. Aidha, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mb Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Mb Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mb Naibu Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mb Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji kwa kushirikiana na Kamati katika kipindi chote cha vikao vya Kamati. Nawashukuru pia

wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha wakiongozwa na Dkt. Natu Mwamba Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na mlipaji Mkuu wa Serikali pamoja na Wataalamu kutoka Wizara ya Mipango na Uwekezaji wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Tausi Kida, pamoja na Wataalamu kutoka Tume ya Mipango ambao walishirikiana na Kamati kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Mhe. Twaha Ally Mpembenwe, Mb na Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa utekelezaji wa shughuli za Kamati. Aidha, nawapongeza kwa michango, maoni na ushauri wao ambao umesaidia Kamati kuisimamia Serikali ipasavyo. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifauatavyo:-

| | |
|---|---|
| Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mwenyekiti |
| Mhe. Twaha Ally Mpembenwe, Mb | M/Mwenyekiti |
| Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb | Mjumbe |
| Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb | Mjumbe |
| Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb | Mjumbe |
| Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |
| Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| Mhe. Juma Hamad Omar, Mb | Mjumbe |
| Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb | Mjumbe |
| Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb | Mjumbe |
| Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb | Mjumbe |
| Mhe. Jonas William Mbunda, Mb | Mjumbe |
| Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb | Mjumbe |
| Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb | Mjumbe |
| Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo, Mb | Mjumbe |
| Mhe. Omar Ali Omar, Mb | Mjumbe |
| Mhe. Zaytun Seif Swai,Mb | Mjumbe |
| Mhe. Rashid Abdallah Rashid, Mb | Mjumbe |
| Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb | Mjumbe |
| Mhe. Bahati Keneth Ndingo, Mb | Mjumbe |
| Mhe. Yahya Mhatta, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** nimshukuru pia Ndg. Baraka Leonard Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake na kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha kazi za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya shukrani hizo, naliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili Taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**Oran Manase Njeza, Mb**
**MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**

**10 Februari, 2025**

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Oran Njenza, Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati kwa umakini mkubwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Wenyeviti wetu wote wawili wamekamilisha kufanya mawasilisho kwa ufanisi mkubwa, tunawashukuru sana. Naomba nitoe maelezo ya awali kabla sijawaalika Waheshimiwa Wabunge kuanza kuchangia.

Waheshimiwa Wabunge, tuna changamoto ya muda dhidi ya idadi ya wachangiaji. Wale ambao wataona siyo lazima wachangie leo au wachangie katika nafasi hii, wataleta taarifa Mezani wakati tunaendelea kuchangia, lakini wachangiaji wote leo pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wote tutatumia dakika tano, tano.

Waheshimiwa Wabunge, nawakaribisha na tunaanza na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, atafuatiwa na Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei ajiandae.

Waheshimiwa Wabunge, nawaomba tujielekeze moja kwa moja kwenye hoja.

Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, karibu.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia suala la ukusanyaji wa kodi, tunaliangalia kwa mitizamo miwili; wapo wanaosema kwamba hatukusanyi kiasi cha kutosha kukidhi mahitaji ya maendeleo ya Taifa letu kwa sababu wigo wa kodi ni finyu, lakini kuna mtazamo wa pili, wanasema hatukusanyi kiasi cha kutosha kinachokidhi matumizi ya Serikali kwa sababu mifumo ya ukusanyaji wa kodi siyo imara kiasi cha kutosha. Naunga mkono hoja ya pili ya mifumo na nitaeleza kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mapendekezo yangu kwenye maeneo manne. La kwanza, wataalamu wa uchumi wanasema kwamba nchi yetu ina uwezo wa kukidhi mahitaji yake iwapo sekta isiyo rasmi itaimarishwa, sekta hii isiyo rasmi ina uwezo wa kuchangia mapato ya Serikali kwa zaidi 40% iwapo itarasimishwa kiasi cha kutosha, kwanza, kwa kuwatambua wafanyabiashara, kwa kuwapa vitambulisho maalumu, lakini la pili, ni kuondoa utitiri wa kodi ili walipe kodi kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu la pili, naiomba Serikali itekeleze kwa vitendo ushauri wa Bunge wa kuiunganisha mifumo ya kisasa inayotumiwa na Mamlaka ya Mapato, halmashauri, Mamlaka ya Bandari na Mamlaka ya Manunuzi. Tumekuwa tukilisema jambo hili, kuna haja ya kuiunganisha mifumo hii ili isomane. Faida yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza itaongeza uwazi, itadhibiti ubadhirifu, na udanganyifu katika malipo ya kodi. Nimefanya

utafiti nikabaini kwamba kasoro kubwa ya mifumo hii, kwanza ni matumizi ya mawasiliano ya *internet,* yapo chini, na wakija wateja wanashindwa kuitumia kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, inatengenezwa na watu tofauti na baadhi yao wanatoka nchi za nje. Ushauri wangu kwa Serikali, imefika wakati tuimarishe vitivo vyetu vya sayansi ya kompyuta ili mifumo hii itengenezwe hapa hapa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa tatu, naiomba Serikali ianze kutekeleza ushauri wa Bunge wa kutumia malipo kwa kutumia mifumo ya kisasa. Wakati wa kutumia malipo kwa fedha taslimu, umeshapitwa na wakati, lakini ili mfumo huu uweze kutekelezwa kwa urahisi, nashauri Serikali iweke kiwango cha fedha kisichozidi shilingi 200,000/= ambazo zinaweza kutumika kama fedha taslimu na fedha zaidi zitumike katika mifumo ili matumizi na malipo ya Serikali yafanyike kwa uwazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu la nne na la mwisho, Serikali iweke mkazo katika kuhakikisha kwamba mazao tunayoyazalisha hapa nchini, yanaongezewa thamani pamoja na madini. Faida yake ni nini tukiongeza thamani ya madini na mazao yetu ya nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, thamani yake inaongezeka. Tunaongeza kiwango cha Dola za Kimarekani na fedha nyingine za kigeni ambazo zinaingia hapa nchini. Tukilifanya hili, bila shaka thamani ya shilingi ya Tanzania itaongezeka maradufu na uchumi wetu utaimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Naona ume-*set standards* ambazo tuliobaki tuna wajibu wa kuzifikia. Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, ajiandae.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi nami kuweza kuchangia Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, niseme kwamba naunga mkono hoja. Nataka nichangie katika kipengele kimoja tu cha kukua kwa Uchumi, na hapa nataka niweke rekodi vizuri sana kwamba uchumi huu tunaosema unakua, siyo tu unakua wenyewe wenyewe, kuna mtu yupo nyuma yake ambaye anafanya kazi nzuri na ana watendaji ambao wana uwezo wa kutafsiri maono yake. Mtu huyo sio mwingine, bali ni Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukua kwetu kwa uchumi kumechangiwa na mambo mengi sana, lakini nitataja machache tu. Moja, ni sekta nzima ya mambo ya kilimo. Katika sekta ya kilimo, uchumi wetu umechangiwa kwa 24.4%. Hii siyo miujiza, nataka Watanzania wajue kwamba bajeti ya kilimo imetoka shilingi bilioni 294, leo tunazungumzia shilingi trilioni 1.2. Nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nataka tuzungumzie vile vile suala zima la Bwawa la Mwalimu Nyerere kama tulivyokuwa tumelizungumza kwenye Taarifa ya Kamati. Watanzania walijue hili, Mheshimiwa Rais wakati anachukua nchi, hii Bwawa la Mwalimu Nyerere lilikuwa na 36% tu katika utekelezaji wake. Leo tunaongelea 99.9%, mitambo nane tayari inafanya kazi, mmoja upo njiani na kukatikakatika kwa umeme hakupo tena. Nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende mbele zaidi katika suala zima la kukua kwa uchumi. Tunazungumzia vilevile suala zima la bajeti ya maendeleo. Hii naomba ikae vizuri katika rekodi za Bunge. Hapa tulikuwa tumewaka fedha za bajeti ya maendeleo shilingi trilioni 14.08, lakini nataka nizungumze kwamba mpaka kufikia Desemba, 2024 fedha za bajeti ya maendeleo zilizokuwa zimepelekwa sawa sawa 104%, leo hii tunapozungumza, miradi inaendelea kutekelezwa katika majimbo yetu; miradi ya Kitaifa vilevile nayo inaendelea. Nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, vilevile, tunazungumzia suala zima la makusanyo. Katika eneo la makusanyo, hapa nataka niseme hivi, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba naomba nikupongeze sana ndugu yangu Waziri wa Fedha na taasisi yako ya *TRA*. Miujiza mikubwa sana imefanyika, fedha nyingi zinakusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukusanywa kwa fedha hizi, siyo hivi hivi tu, kuna mtu yupo nyuma hapa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameweza ku-*set standard* na kwa tafsiri hiyo watendaji wake wanatafsiri yale maoni yake. Leo ni kitu cha kushangaza sana walipakodi wanakaa, wanakula chakula na kunywa chai na anayekusanya kodi. Nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze yafuatayo katika kuweza kuishauri Serikali ili tuweze kwenda vizuri zaidi. Naomba niishauri Serikali, pamoja na kwamba tumeongeza makusanyo yetu, lakini ni vyema Serikali iweze kuweka mikakati ya ku-*extend* ile *taxbase,* kwani bado ipo *narrow*. Tunataka wengi waingie, waweze kuchangia katika suala zima la kukusanya mapato ili sasa bajeti yetu iwe *funded* na makusanyo yetu ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili vilevile ambalo nilikuwa naomba nilisisitize, Serikali iweze kuweka msisitizo katika suala zima la *cashless economy* ili sasa tuweze kuona maeneo yote ambayo yanakwenda kufanya malipo, yawe yanafanya malipo kwa kupitia mitandao na siyo fedha ziwe zinapita katika mkono mmoja na kwenda kwenye mkono mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine la msingi ambalo nilikuwa naomba niishauri Serikali, ni katika eneo zima la mambo ya *tourism*. Mheshimiwa Rais amefanya miujiza mikubwa sana na ninaomba niweke rekodi vizuri hapa. Katika eneo zima la mambo ya utalii, kazi kubwa sana imefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunavyozungumza, fedha zilizokuwa zimepatikana katika eneo la utalii ni takribani shilingi dola milioni 3.3. Hizi ni fedha nyingi sana. Hivyo basi, naomba

niishauri Serikali waweze kutatua changamoto zote zinazowakabili wale *tours operator* ili sasa tuweze kuona tunakusanya mapato ya kutosha na kuweza kuwavutia wale ambao wanakuja kuangalia vivutio vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, tulifanya maamuzi Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Maamuzi yale hayakuwa ya kubahatisha, na leo ndiyo maana tunasimama katika Bunge hili tunazungumza kifua mbele kwamba tunakwenda kumpa miaka mitano Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu ya kazi kubwa na nzuri ambayo alikuwa ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nawe pokea maua yako kwa kuzingatia muda. Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Kusema kweli ndani ya dakika tano hata muda wa kuweza kumshukuru Mheshimiwa Rais na kumhakikishia Wanavunjo wanasema mitano tena na kwamba wanaunga mkono maazimio ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya kumteua yeye kuwa mgombea pekee wa Chama pamoja na Dkt. Nchimbi kuwa mgombea mwenza; pamoja na Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Mwinyi kule Zanzibar, huo muda hatuna. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niende moja kwa moja kwenye masuala yanayohusiana na Kamati. Kusema kweli ujue kwamba Kamati yetu ya Bajeti ambayo mimi ni Mjumbe, tumetoa maagizo au tumetoa mapendekezo kwenye maeneo matatu makubwa au manne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ni kwenye upande wa kukuza mapato ya Serikali; pili, ni kwenye upande wa kuongeza ukuaji wa pato la Taifa kwa sababu ukiongeza pato la Taifa ina maana kwamba mapato ya Serikali yataongezeka; na eneo

lingine ni lile la kuona namna gani matumizi ya Serikali yaweze kuwa kwenye maeneo ambayo yanaleta tija zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa kuongeza mapato limerudiwa sana hili la kutumia mifumo, lakini pia hili la kutengeneza au kuhakikisha kwamba kasi ya kurasimisha shughuli zinazofanyika kwenye sekta isiyo rasmi inaendelea, na tunasema kwamba ili hiyo iendelee, au iweze kujionyesha ni vizuri kwamba sasa kila malipo ambayo yanafanyika au Serikali ichukue hatua ambazo itahakikisha kwamba malipo yanafanyika zaidi kutumia mifumo ya kidijiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na pendekezo moja hapo kwamba pengine tumwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha atangaze kiwango cha malipo ambacho hakistahili kifanyike kwa *cash*, (fedha taslimu) lazima kwa kutumia *digital* au kifanyike kwenye benki zenyewe. Ina maana kwamba tutaweza kufahamu watu wanalipwaje? Tunaweza tukaunda *data analytics* na kwenye *warehouse* hapo tukaweza kuchambua. Tutajua kwamba kuna watu ambao wanajificha kwenye sekta isiyo rasmi na ambao kusema kweli wanaweza wakawa ni walipakodi wazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa *issue* ya kuongeza ufanisi kwenye matumizi ya Serikali, Kamati imetoa mapendekezo hapa na pendekezo mojawapo ambalo mimi naliona ni hilo la kusema, kwa mfano *TAWA, Ngorongoro Conversation Unit* na *TANAPA* waweze kukusanya makusanyo yao na ku-*retain* 100%. Hiyo itasaidia sana upande ule kwa sababu na wenyewe wanachangia pia kwenye mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu matumizi yasiyo rasmi, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alikuwa mwepesi na mzuri sana alipokuwa anasoma bajeti yake na alituelekeza ni maeneo yapi na ndiyo tunahamasisha kwamba twende sasa kutekeleza zile hisia zake au ile *vision* yake kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *issue* ya ukuaji wa uchumi, kwanza kuna *good news* kwamba sasa hivi duniani, nchi zimeimarika sana kiutendaji na kiukuaji wa uchumi, na hivyo riba

zinashuka; *depletion* zinashuka na riba zinashuka licha ya kwamba kuna matatizo haya ya sera za Mheshimiwa Puttin na Trump zinaleta utata kidogo, lakini bado kila mtu anaamini kwamba hali hii ya uchumi wa dunia inaimarika, na kwa hiyo riba zitashuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, nafikiri kwamba tuna uwezekano sasa wa kupunguza gharama za kukopa za ile mikopo yetu ya nyuma kwa sababu *benchmark* inashuka. Kwa hiyo, hiyo itasaidia kuweza kukopa zaidi na kutekeleza miradi ambayo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hapa ndani kuna tatizo hilo la riba kupanda. Sasa hivi, riba za kuchukua amana inazidi 13.5%. Hata ile *Samia Suluhu Hassan Bond* ni 13.5% fedha wanayoichukua wakakopeshe. Kwa hiyo, ina maana kwamba riba za mikopo zitapanda na zikipanda, ina maana kwamba watu hawatakopa kupeleka kwenye shughuli za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tuombe Waziri wa Fedha na Benki Kuu wakae waone ni namna gani watafanya, kwa sababu hii Sera ya Fedha inaonekana imekaza sana. Licha ya kwamba tunasema iko *accommodative,* lakini siyo *accommodative*. Imekuwa *tight* na inasaidiwa na haya malimbikizo ya madeni ambayo *contractors* hawajalipwa. Pengine wakilipwa itafungua benki, ukwasi na mikopo pia itaongezeka na uchumi utakua kwa kasi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani wajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Nami naungana na Wabunge wenzangu, kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kuwa mimi ni Mbunge ninayetokana na wakulima, na sehemu

kubwa ya wananchi wa Ludewa ni wakulima. Nampongeza sana kwa kutoa ruzuku kwenye mbolea, kwenye mbegu na vilevile kwa kununua mahindi kwa wingi sana mwaka ulioisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wananchi wamepata fedha na mwaka huu wameweza kuanzisha mashamba zaidi, wameongeza maeneo ya kulima, ili wavune zaidi. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Bashe na wataalamu wake wajipange sana. Ingawa mvua ilisuasua, wananchi watakuwa na mahindi mengi sana. Kwa hiyo, ni lazima uwahakikishie soko la uhakika ili waweze kumudu majukumu yao mbalimbali kwenye familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama ambavyo nimesema, mimi ni Mbunge ambaye natokana zaidi na wakulima. Hoja zangu leo zitajikita zaidi kwenye eneo la kilimo. Kwa hiyo, tukiangalia Kamati zote; Kamati ya *PIC* na Kamati ya Bajeti, zimesisitiza kwamba, Serikali iendelee kufanya uwekezaji mkubwa kwenye eneo la kilimo. Sasa uwekezaji huu utafanyika namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tujitahidi sana kuhakikisha wakulima wetu wanapata mitaji kwa ajili ya kufanya kilimo kikubwa zaidi na fedha zile ziweze kuwasaidia kupata pembejeo za kilimo na kupata mitambo ya kufanya kilimo cha kisasa. Ukiangalia benki zetu sasa hivi, hakuna ambayo kwa kiasi kikubwa, na moja kwa moja inaweza kumtambua mkulima wa kijijini na kumpa mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuangalie eneo hili na Serikali iweke sera ambayo wale wananchi, yaani wakulima wa kule, nao wapate mikopo moja kwa moja, na ikiwezekana ule Mfuko wa Pembejeo uweze kufungua ofisi kwenye mikoa. Wakulima wanavyohangaikia mbolea, waweze kukopeshwa, kwani wanavyohangaikia dawa, waweze kupewa ili tuweze kuweka kilimo ambacho kina tija zaidi. Kwa sasa hivi ukiangalia, kwa kiasi kikubwa mikopo wanapewa wachuuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kuishauri Serikali izingatie, ni kutafuta masoko ya uhakika ya

mazao ya kilimo. Kukiwa na masoko ya uhakika, wananchi watapata kipato kikubwa zaidi na watavutiwa kuendelea kuwekeza zaidi katika kilimo. Kwa mtindo huo, tunaweza kupata mazao ya kuuza nje ya nchi na kuleta fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata zile *restrictions* za kufunga mipaka ili mazao kama mahindi ambayo yanalimwa sana mikoa ya kusini, ukiachia mipaka wazi, maana yake wakulima watapata mapato mengi zaidi, watazingatia mahitaji yao ya familia na mwaka ujao watajipanga wenyewe, watazingatia. Kwa hiyo, watalima kutokana na uwezo wa soko kuweza kumudu mahitaji ya wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni kwamba Serikali isaidie, aidha kwa mapato yake kupitia *NFRA* au kwa kushawishi wafanyabiashara mbalimbali waweze kujenga maghala au maeneo ya kuhifadhia mazao. Najikita hasa kwenye zao kama la mahindi mikoa ambayo wakulima wetu wanalima zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2024 *NFRA* walionekana wamepewa fedha nyingi sana na Serikali, na walikuwa na uwezo wa kununua mahindi zaidi, lakini maeneo ya kuhifadhi mazao haya yalikuwa na changamoto kidogo. Hata watu wa *TFRA,* nimeona ukurasa wa tisa, Kamati ya *PIC* wamezungumzia kwamba, Serikali inatumia zaidi ya shilingi trilioni moja kuagiza mbolea nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nao wanapendekeza kwamba, kwa nini mbolea isizalishwe hapa nchini? Kama itazalishwa hapa nchini, tutaokoa fedha za kigeni ambazo zinatumika kuagiza mbolea nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, malighafi nyingi ambayo inatumika kuzalisha mbolea inapatikana hapa nchini. Kwenye makaa ya mawe, imethibitika, hata yaliyopo Ludewa yana vitu vingi kama gesi, *oxygen, hydrogen*, *methanol,* ambazo ni *raw materials* muhimu sana kwenye viwanda vya mbolea, na pia, chokaa iko kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali iwekeze kuhakikisha kwamba, mbolea inazalishwa hapa nchini na haya ma-*godown* ninayoyaomba yanaweza kusaidia kuhifadhi mbolea na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo linaendana moja kwa moja na kuboresha sekta ya kilimo, ni miundombinu ya barabara, hasa vijijini. Kila jimbo linafahamu idadi ya barabara zake, kwa mfano Barabara ya Kigasi – Amani kupitia Ludende, Barabara ya Madilu mpaka Elininda mpaka Mdindi, na barabara nyinginezo. Tunavyoboresha hii miundombinu ya Barabara, mazao ya wakulima yanaweza kusafiri vizuri na wakulima watapata bei nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda umenikaba…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako umekwisha tafadhali.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani. Mheshimiwa John Danielson Pallangyo, ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nianze kabisa kwa kuwapongeza Wenyeviti wawili waliowasilisha Mezani taarifa zao. Kwanza ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na Mwenyekiti wa *PIC,* nawapongeza kwa jinsi walivyosoma vyema na tumewaelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natokea kwenye Kamati ya Bajeti. Kipekee nampongeza Waziri wetu wa Fedha kwa jinsi

ambavyo ameweza kusimamia utoaji wa fedha na utekelezaji wake akisaidiwa na Katibu Mkuu, Dkt. Natu Mwamba, na ambavyo tumeweza kuona mambo yameenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia kwenye sekta ya utalii. Sekta ya Utalii imetusaidia kupunguza nakisi ya urari wa malipo kutoka dola 810 mpaka dola 356. Hii isingewezekana kama siyo ubunifu wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuja na *Royal Tour.* Ametuletea watalii wengi, na jambo hili limefanikiwa sana. Pamoja na hayo yote kuwepo, nilitaka kusema haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya utalii ni maeneo nyeti ambayo mtalii akija, haji tu atembee kwenye gari akauone Mlima Kilimanjaro au aende tu Ngorongoro, inatakiwa sisi wenyewe wananchi tuweze pia kuwaandalia mambo mengine pembeni pamoja na *recreation,* maeneo ya kujifurahisha. Kama amekuja kupanda Mlima Kilimanjaro wawepo watu waliyojiandaa kuweza kuwa-*entertain,* wale machalari, wanywe mtori, wanywe mbege, ili wakienda kule waukumbuke mlima, lakini pia wakumbuke *culture* ya yale maeneo. Tunaomba Wizara ya Utalii isaidie jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni miundombinu kwenda kwenye maeneo ya utalii ukiwepo Mlima Kilimanjaro. Hakuna barabara nzuri ya kwenda kupanda mlima. Mnasema labda watu wa Kaskazini wanapenda lami, lami siyo ya kutembea wananchi wa hapa tu, hata hao wageni. Tunaomba sana sekta ya utalii isaidiwe ipate barabara nzuri kupandia mlima, kwenda Ngorongoro na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tunaomba wale wafanyabiashara ambao ni wa sekta binafsi wanao-*deal* na utalii, yale magari yao ya utalii yapunguziwe kodi. Yanakatwa kodi ya *cruiser*, kama *cruiser* la mtu mwingine. Watu hao hawawezi kutoboa. Tunaomba sana tuangalie jinsi gani sekta hii itaangaliwa na watu hao waweze kusaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nikitoka kwenye utalii, naomba nizungumzie eneo la *export credit guarantee.* Hii

imeonekana tu kwamba, ni jambo la wafanyabiashara wakubwa wanaofanya *export,* lakini nikirudi Kilimanjaro, kule Same, wana-*export* tangawizi kwenda Kenya. Wanalima vanila, inakuwa *exported,* lakini hawa wakulima wadogo wadogo hawafaidi kabisa hii *export guarantee scheme.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba wapatiwe elimu ni jinsi gani wata-*access BoT* wataweza kupata *export guarantee scheme* ili tangawizi hiyo badala ya kulimwa kiduchu, walime kwa wingi na waweze kunufaika kwa mfuko huo uliopo Benki Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu *ethane. Ethane* inakuwa *produced* kwenye viwanda vya sukari, na ikishatengenezwa huwa ikiuzwa tu, wale watu wenye viwanda wanaanza kudaiwa. Sasa wanadaiwaje wakati ambapo hawajalipwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo lilikuja hapa Bungeni na tukapitisha hiyo sheria. Ni wakati mwafaka sasa tuone kwamba, labda hatukwenda vizuri, labda ihesabiwe hata wiki moja au mbili, ndiyo waanze kurejeshewa. Wanapata shida kwa sababu, sasa wanatumia pesa ile ya kuendeshea kiwanda kulipa kodi Serikalini kabla hajaweza kupatiwa marejesho. Mambo haya ni magumu, lakini niseme tu Kamati hii imefanya kazi vizuri sana, na imesaidiwa sana elimu na *CAG* na *TRA,* ili kupata na uelewa mpana wa kuweza kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shally Raymond. Anafuata sasa Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo. Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Nami niunge mkono hoja ya Taarifa za Kamati zote mbili. Kwa kuwa mud ani mchache nitajikita kwenye mambo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam, *BRT*. Naipongeza Kamati yangu ya Uwekezaji, tumefanya kazi ya kutosha, pamoja na kwamba wakati mwingine muda ulikuwa siyo rafiki. Uwekezaji uliyofanyika na Serikali kwenye *BRT* ni mkubwa sana, lakini tija yake haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huu umefanyika katika awamu tatu; awamu ya kwanza na ya pili imetumia shilingi bilioni 847, awamu ya tatu imetumia dola za kimarekani 148.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza imekamilika, awamu ya pili iko 55%, lakini ni yapi yalikuwa malengo ya uwekezaji wa eneo hili? Ilikuwa ni kupunguza changamoto ambayo wanaipata wananchi wa Dar es Salaam, lakini pamoja na hiyo awamu ya kwanza kukamilika, tija yake ikoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto bado ni kubwa. Naomba nishauri mambo yafuatayo: Kwanza, ukiangalia kwenye mabasi yenyewe, yaliyopo ni 100 wakati yanayohitajika ni mabasi 305. Kwa hiyo, bado hatuwezi kufikia malengo ya kuondoa hiyo changamoto ambayo wanaipata Watanzania wanaoishi Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, fedha hizi ni za mkopo, yaani awamu ya pili wana mwaka mzima hawajapata mkandarasi wa kuendesha wakati tumechukua fedha za mkopo. Huu ni uwekezaji ambao hatuwezi kufurahishwa nao kama Kamati, na kama Bunge. Tunahitaji uwekezaji wenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, badala ya kulipa mkopo ambao utakuwa hauna faida kwa Watanzania, tuchukue hatua za haraka kutafuta mtu ambaye anaweza kuendeleza hili jambo kwenye hii awamu ya pili. Pia kuna eneo ambalo lilikuwa linajaa maji pale Jangwani, tunajua kwamba, kuna fedha zimepelekwa pale, wachukue hatua za haraka ili jambo hili tuweze kufikia malengo ambayo tulikusudia. Miundombinu yote iboreshwe, ili tuone malengo ya uwekezaji ambao Serikali imeuweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda haraka kwa sababu ya muda. Jambo lingine ni suala la *SGR*. Serikali imefanya jambo kubwa kwenye hili eneo. Siyo jambo baya kusema kwamba, Serikali imefanya vizuri kwenye hili eneo, lakini pamoja na kufanya vizuri na fedha ambazo tumewekeza hapa, zaidi ya shilingi trilioni 27, usimamizi ukoje kwenye eneo hili? Huwezi kuwekeza fedha zote hizi halafu stesheni za mizigo zikakosa barabara. Hili jambo kwani lilihitaji nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri, kulingana na uwekezaji uliyofanyika kwenye eneo hili, tulipe kipaumbele kuboresha miundombinu kwenye hizo stesheni za mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tunajua kuna hujuma zinazoendelea kwenye hiyo miundombinu. Kama tumewekeza zaidi ya shilingi trilioni 27, tunashindwa nini kufunga *camera* kwenye hayo maeneo ili kuonesha tija ya uwekezaji ambao tumeufanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, ni jambo muhimu, tukithubutu, na tukisimamia vizuri, yawezekana tukawa mfano wa kuigwa upande wa Afrika na Afrika Mashariki, lakini tusiposimamia vizuri itakuwa ngumu na wajibu wa kamati hii ni kuona tija ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tunaweza tukajikita kwenye kutengeneza miundombinu. Kama kwenye usimamizi, bado ni shida. Tuwatafute wawekezaji waje na treni zao kuendesha kwenye miundombinu ambayo Serikali tumewekeza, kwa sababu shida ni kubwa sana kwenye usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaweza ikaonekana ni jambo geni, lakini hata ndani ya treni huduma zake bado ni hafifu. Kama sisi tutajikita kwenye miundombinu peke yake, halafu tukafungua milango, wawekezaji wakaja wakawekeza, tunaweza tukaona tija ya uwekezaji kwenye hili eneo ambalo tumewekeza kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba tunaona hizo huduma za humo ndani, tunaona kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais alifanya kwa upande wa *Royal Tour,* lakini

haiwezekani kuanzia asubuhi mpaka jioni, Dar es Salaam mpaka Dodoma, ni hilo moja tu, *Royal Tour, Royal Tour!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanaokuja ni wengi. Nashauri, tunaweza tukatumia eneo hilo kwa ajili ya matangazo mbalimbali na watu wakalipa, Serikali ikapata fedha. Watu waliomo mle ndani wengine ni wageni, ni vizuri wakanufaika na treni badala ya kupanda tu, wakaangalia matangazo na wakawekeza kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aida. Karibu Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, atafuatia Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu ajiandae.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa hii nafasi. Moja kwa moja nitangulie kuungana na wenzangu kuwapongeza Wenyeviti kwa taarifa nzuri ambazo wameweka Mezani, lakini pia na Waziri kwenye sekta hizi, kwa maana ya Waziri wa Fedha, Mipango na Uwekezaji, kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipo Kamati ya *PIC,* kwa hiyo, nitachangia kwa kifupi sana kwa sababu, taarifa iliyowekwa Mezani nilishiriki kuitengeneza, nilishiriki katika kuita zile taasisi husika kwenye mahojiano na ziara tulizozifanya nilishiriki pia. Kwa hiyo, niseme tu moja kwa moja kwamba, naunga mkono hoja ambayo imewekwa Mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *BRT,* Mheshimiwa Aida amelisema vizuri sana. Sitakuwa na mengi ya kusema hapo, lakini tuliita watekelezaji wa huu mradi, kwa maana *ya UDART,* tukakagua miradi ile kutoka Kimara mpaka Kivukoni, miundombinu imekamilika. Tukaondoka, tukaanzia Uhuru kwenda mpaka Mbagala, miundombinu imekamilika. Sasa hivi kutoka Mwenge kwenda Tegeta mkandarasi yuko kazini anafanya kazi nzuri sana ya kutengeneza miundombinu, lakini mabasi yako wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, adha ambayo wananchi wa Dar es Salaam wanaipata, ambao wanategemea usafiri huu, ni kubwa sana na kwa kweli, ni fedheha. Nashauri kwamba, Serikali kidogo ipambane, ijiongeze kidogo hapa kuhakikisha kwamba hizo fedha ambazo zimepatikana kwa mkopo, tija yake ionekane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni *TFC*. *TFC* imebaki kama wakala wa kuagiza mbolea, lakini hii ni kampuni ambayo, mwanzo ilikuwa na kiwanda. Sasa tunaona tunakoelekea siyo sawa. *TFC* iache uwakala, sasa iji-*engage* kwenye kujenga kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ya kuagiza mbolea kutoka nje ya nchi ni kubwa sana, lakini kama tukiweza kujenga kiwanda chetu cha mbolea, ile gharama tutaifuta, na ndani ya miaka michache, tutakuwa na kiwanda chetu.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Elibariki Kingu, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeguswa sana na mchango wa baba yangu, Mheshimiwa Mzee Dkt. Pallangyo. Naomba nimpe taarifa kwamba, maneno mazuri anayoyasema, nami huwa najiuliza, tunaposema tunazi-*task government enterprises* kuwa za kibiashara, leo nimpe taarifa, hakuna taasisi hata moja ya Serikali inayoruhusiwa kutoa *payment guarantee* inayoruhusiwa kutoa *Master LC* na *LC*.

Mnawezaje mkasema taasisi za Serikali zifanye biashara zipate faida kama kazi zote mmemwachia kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu mpaka Wizara ya Fedha aruhusu. Hawa watawekezaje kwenye hivi viwanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *if we want to make* taasisi zetu ziwe za kibiashara ni lazima tuziruhusu zifanane na *private sector*. Waruhusuni watoe *LC, payment guarantee* kwa makampuni ili waweze kufanya *trade*. Huyu Mzee anasema ujenzi wa kiwanda;

kitawezekanaje kama mpaka Mheshimiwa Dkt. Mwigulu afanye maamuzi ya kuwapa hawa *guarantee* ya kwenda kujenga kiwanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mheshimiwa Dkt. Mwigulu anaupiga mwingi lakini kwenye hili tutahitaji sheria ije hapa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Elibariki Kingu, ametumia fursa hiyo kuchangia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, unapokea taarifa ya Mheshimiwa Elibariki Kingu?

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili na ni sehemu ya mchango wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli *bottom line*, *TFC* iwezeshwe kujenga kiwanda cha mbolea hapa nchini. Kama tumeweza kujenga Bwawa la Nyerere, kama tumeweza kujenga *SGR* Dar es Salaam na Dodoma, sasa hivi *chemistry* ya maisha ya Dodoma imebadilika, tutashindwaje kujenga kiwanda cha kuzalisha mbolea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema nitazungumza kwa kifupi sana, lakini nimalizie kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais ambaye anaupiga mwingi. Wajumbe wa Mkutano Mkuu waliliona hili na wakampitisha kama mgombea pekee wa Urais kwa Chama cha Mapinduzi. Pia, tunamuunga mkono na tunamhakikishia kwamba, mitano tena ni kama ahadi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais anahangaikia sana maisha ya Watanzania mpaka wenzetu wa nje wameyaona haya. Juzi tumeona amepewa *award* kwenye sekta ya afya, ni kwa sababu ya jinsi ambavyo amejitolea kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, nami nashukuru kwa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo. Sasa namwita Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo ajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa nami niwe miongoni mwa wachangiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba niunge mkono hoja ya Kamati yetu ya Bajeti, nami ni Mjumbe kwenye Kamati hii. Kwa hiyo, nimetoa mchango na ninaomba niishukuru Serikali kwa sababu wamekuwa wasikivu na hasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na watumishi wote wamekuwa wakipokea kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa siku ya leo, nami naomba nijikite katika eneo moja ambalo nitaelekeza mchango. Mchango wangu naomba nielekeze kwenye Sheria ya Fedha *(Finance Bill)*. Bunge lako limekuwa likitumia muda mwingi sana katika kujadili juu ya matumizi. Hata hivyo, ni ukweli usiopingika kwamba, tumekuwa tukitumia muda mchache sana kujadili kuhusiana na mapato ya Serikali kwa maana ya vyanzo, lakini pamoja na kodi zinazotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwananchi wa kawaida anaguswa pale ambapo kuna habari ya tozo na kodi. Hicho ndicho ambacho kinamhangaisha mwananchi katika maisha yake ya kawaida. Kwa bahati mbaya sana, ni utaratibu ambao sijajua tumeutoa wapi wa kuwa na muda mchache sana juu ya kujadili mambo ambayo yanahusu mwananchi wa kawaida? Inaanzia wakati ambao *Finance Bill* inaletwa na Serikali, muda ambao Kamati inapewa na muda ambao Bunge linapewa kujadili ni muda ambao hautoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ambayo tumeitoa kama Kamati, tumeomba Serikali pale ambapo wanasoma bajeti yake, waje na *Finance Bill* ili tupate muda wa kutosha, wadau wapate muda wa kutosha kwa sababu haya ndiyo maisha ya Watanzania wa kila leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana kama haitoshi, nasi Bunge ambao jukumu letu la kutunga sheria, hakuna chombo ambacho tunaweza tukakasimu, ni sisi wenyewe. Pale ambapo sheria juu ya kuhusiana na masuala ya kukusanya kodi ikienda mtaani na ikafanya vibaya, lawama zinarudi kwenye Bunge, kwamba, tazama ambavyo Bunge limekuja na Sheria ambazo zinakwenda kuwaumiza wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha *taskforce* ya kwenda kuhakikisha kuwa wanapitia Sheria za Kodi ili marekebisho yaweze kufanyika. Kimsingi, laiti ingekuwa kwamba Bunge tunafanya kazi yetu vizuri zaidi, hata hayo maoni ambayo yanatolewa, wadau wangekuwa wameyaleta kwenye Bunge tukaweza kuyapatia na marekebisho yakafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine tumekuwa tukiilaumu *TRA*, lakini *TRA* hawana sheria yoyote juu ya kukusanya kodi. Sheria zote zinatokana na Bunge. Kwa hiyo, kama kuna sheria inaonekana haitekelezeki, tafsiri yake ni kwamba, sisi Bunge hatukufanya wajibu wetu inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hatujachelewa, ni wakati muafaka tuhakikishe kama Bunge *tuna-take role* ili tuhakikishe kwamba sheria zinazohusiana na kodi tunazipitia kwa muda wa kutosha, tujue na tafsiri yake ni nini kabla sheria haijakwenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana kwa kanuni zetu, Bunge tunafunga mikono Wabunge pale ambapo Serikali ikishaleta Muswada (Bajeti yake), eti tunasema Mbunge ukisema fungu fulani likatolewe, ukatafute chanzo kingine cha kuja kuziba pengo hilo. Sasa kwa muda mchache kwa Bunge na Mbunge mmoja mmoja, huo utafiti atakuwa ameufanya saa ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali wao wanakuwa na mchakato wa muda mrefu, wamekwenda kwenye utafiti, wanasema hivi ndivyo vyanzo vyetu. Sasa Mbunge ukisema

chanzo hiki hakifai, unaambiwa eti ukatafute chanzo kingine kwa ajili ya kuhakikisha kwamba pengo hilo linazibwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni wakati muafaka wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na muda wa kutosha, tupitie sheria zote zinazokuwa zinapendekezwa na Serikali kuhusiana na suala la tozo na kodi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikilipendeza Bunge lako, kama ambavyo tuna Kamati ya Sheria Ndogo, ipo haja ya kuanzisha Kamati ambayo itakuwa mahsusi kuhakikisha namna ambavyo utekelezaji wa Sheria za Kibajeti zinakwenda kuathiri kule ili kabla wananchi hawajaanza kupiga kelele, Bunge liwe lime-*take charge* na marekebisho yafanyike, tusisubiri mpaka miezi sita ipite wananchi wetu wakiwa wanaumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazingatia muda. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuzingatia Kanuni zetu za Kudumu za Bunge, naongeza muda mpaka shughuli za Bunge zitakapokamilika. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, atafuatiwa na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya dakika tano ya kuchangia kwenye taarifa hizi ambazo zimewasilishwa leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kwa kuunga mkono taarifa zote na kuwapongeza Wenyeviti wote kwa kuwasilisha vizuri. Kwa kuwa mimi ni Mjumbe katika Kamati ya Bajeti, maoni yote ambayo yamewasilishwa na Kamati yetu nayaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa dakika tano, kwanza utajielekeza kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliewa tena kugombea nafasi ya Urais kupitia Chama cha Mapinduzi pamoja na Mgombea mwenza Dkt. Emmanuel Nchimbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua uamuzi ule wa Mkutano Mkuu Maalum wa CCM, Wajumbe tuliufanya kutokana na kazi nzuri ya utekelezaji wa Ilani ya 2020/2025. Kwa kuwa kazi ile nzuri ya utekelezaji wa Ilani, kama Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, tunaithibitisha kupitia kazi mbalimbali zilizofanywa na Kamati yetu ambazo zimekuwa zikiwasilishwa na Serikali kwenye Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa kipindi chote ambacho tumehudumu katika Kamati hii, najua kwa kuwa hii itakuwa ni taarifa yetu ya mwisho ya kazi za Kamati, naishukuru sana Serikali kwa kuwa Serikali sikivu kwa namna tulivyokwenda vizuri, changamoto mbalimbali tulizitatua kwa pamoja. Hongera sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, wataalam wako wote na wasaidizi wako wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, kwa kuwa taarifa ya utekelezaji wa kazi za Serikali, kazi nzuri iliyofanyika imetegemea mapato; kwa kuwa kipindi chote kwa kadri tulivyokuwa tunajadili tumeona kazi nzuri; kila mwaka wa fedha makusanyo yanaongezeka; fedha zinaenda kwenye miradi ya maendeleo, nitumie mwaka huu wa fedha 2024/2025 kuipongeza Serikali kwa kuweka rekodi mpya kupitia Mamlaka ya Mapato *(TRA)*, kwa kuvuka malengo ya ukusanyaji wa mapato miezi sita mfululizo. Haijapata kutokea tangu mamlaka hii ya mapato ianzishwe miaka 28 iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka Desemba, imekusanya shilingi trilioni 16.528 kutokana na lengo la shilingi trilioni 15.778 sawa na 104%. Kama haitoshi, imevunja rekodi pia ya kukusanya mwezi Desemba trilioni 3.5. Kwa hiyo, naipongeza sana *TRA* chini ya Kamishna mpya Yusufu Mwenda na wasaidizi wake wote. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwongezee kwamba, *DP World* nayo imechangia sana. Watu waliibeza, lakini kwenye ongezeko hili la mapato katika nusu ya mwaka huu *DP World* nayo ipongezwe.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kimei. Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nimeipokea hiyo taarifa na nilikuwa naelekea huko, kwamba namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uvumilivu na ubunifu, kwa sababu mchakato wa Mkataba wa Bandari ulileta maneno mengi. Nami nakumbuka nilipokuwa kwenye mkutano wa hadhara Mambali na Bukene nilisema, ipo siku Mheshimiwa Rais ataheshimiwa na ataweka rekodi katika masuala ya makusanyo ya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakushukuru, na kwa kweli ushauri wangu katika hili ni mmoja. Kwa kuwa tunatamani makusanyo ya mapato yaendelee kuongezeka zaidi, naiomba Serikali iendelee kuimarisha Mamlaka ya Mapato *(TRA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutoa kibali cha ajira za watumishi wapya 1,500. Hii ni mara ya pili kutoa kibali cha ajira kwa watumishi wengi. Naomba Serikali kupitia Wizara ya Fedha, pamoja na kwamba imetoa fedha nyingi zaidi ya shilingi bilioni 400 ya kuimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato, naiomba Serikali iangalie mipaka yetu yenye biashara nyingi, kwa mfano, Namanga na Tunduma inunue zile *scanner* kwa ajili ya kuongeza ukusanyaji wa mapato hususan ushuru wa forodha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala zima la bandari, naiomba Serikali pia ijielekeze kwenye bandari nyingine. Mfano, Bandari ya Bagamoyo tunao uwezo wa kuchangia makusanyo kwa kiwango kikubwa endapo Serikali itatuwezesha kuongeza

eneo la uwekezaji mizigo, kuwezesha wafanyabiashara wadogo wadogo wale wanaokopeshwa na Halmashauri ili waweze kupitisha mizigo na kukadiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kana kwamba haitoshi, naomba kwenye bandari ya Bagamoyo, licha ya kwamba inaingiza mafuta tu, lakini inao uwezo wa kuingiza bidhaa nyingine, kwa mfano bidhaa za vifaa vya umeme kutoka Zanzibar. Kwa hiyo, nina imani kwa kuwekeza zaidi kwenye uwezeshaji wa Mamlaka ya Mapato, na taasisi nyingine zinazokusanya mapato, nchi yetu inakwenda kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, pamoja na mambo mazuri waliyoyafanya kwenye ukusanyaji wa mapato na kupeleka haya mapato kwenye miradi ya maendeleo, nataka niseme, jamani mwenye macho haambiwi tazama. Kazi nzuri imefanyika *site*, miradi ya kimkakati, Bwawa la Mwalimu Nyerere, Ujenzi wa Reli ya Kisasa, na miradi mingine kama Daraja la Busisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, UWT Taifa lazima niitaje, chini ya Mama Mary Chatanda, tumeona miradi 1,265. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutupatia kazi ya kufanya kwa sababu kama isingekuwa kazi yake nzuri, tusingefanya ziara katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali na kuitakia kila la heri. Namshukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa namna alivyoiwezesha Kamati yetu, lakini na kwa namna alivyoiwezesha Serikali, mijadala mbalimbali Bungeni ambayo imewezesha kuja na Sheria za Fedha na hatimaye tumeona kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi, na kila la heri kwa Serikali yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu. Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, upande wa Serikali naomba mjiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ili nami niweze kuchangia kidogo kwenye hizi hoja zetu mbili zilizoko Mezani. Naomba nianze na hii ya uwekezaji wa mitaji ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba, katika kukuza uchumi ni lazima viwanda vyetu viendelee kufanya kazi na viwanda vyetu vikifanya kazi ndivyo vinavyoendelea kuongeza ajira kwa ajili ya watu wetu. Kwa masikitiko niliyonayo ni kwamba, wakati mwingine hata Serikali yenyewe inachangia katika kuua viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tu na nitoe mfano kwenye kiwanda kama kile chetu cha nguo cha *MUTEX* ni kiwanda ambacho kilikuwa kinafanya kazi, lakini kwa sababu yule mwekezaji alisuasua, nadhani Serikali ilikasirika ikamsimamisha. Baada ya kuwa imemsimamisha, kile kiwanda kimekufa, lakini hata wale waliokuwa watumishi wa kiwanda kile mpaka leo wanaendelea kudai mafao yao, lakini Serikali imeshindwa hata kuwapa gharama za kuwafanya warudi kwao. Kwa hiyo, hali hii ni kusema kweli inaendelea kudhoofisha uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tuko katika ushauri, basi ni vizuri Serikali iwe inaangalia na kuwasikiliza wale wawekezaji wote wenye viwanda kwa maana ya kwamba, hata pale wanapokuwa na changamoto zao, tuwe tayari kuwasaidia. Utakuta ziko changamoto mbalimbali zinazomsumbua mwekezaji, lakini hatuko tayari kusaidia mpaka kiwanda kinakufa. Kikishakufa hapo sasa ndipo tunapojitokeza tena kuanza kuhangaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano *MUTEX* na vile viwanda vya pamba ambavyo vimesimama, leo mwekezaji yeyote akija anataka kuwekeza. Kwa bahati mbaya sana unakuta Mkuu wa Mkoa ana mpango wake, *RAS* ana mpango tofauti, Mkurugenzi ana mpango tofauti, au hata Waziri bado utakuta kila mmoja bado ana mpango wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani kama tungekuwa na ule ushirikiano wa pamoja wa kuona kwamba sasa viwanda vilivyokufa, ni hivi, ule mpango mkakati wa namna ya kuwapata wawekezaji, wote tukiwa nao, inakuwa ni rahisi zaidi wote tukazungumza lugha moja na kuona namna ya kusaidia kuliko utaratibu uliopo ambao unaendelea, ambao hautusaidii sana na matokeo yake ni kwamba unasababisha watu wetu waendelee kukosa ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapokuja kwenye Kamati yetu ya Bajeti, tunaishukuru Serikali, lakini tunaishukuru kwa namna ambavyo imeendelea kufanya mambo makubwa (mambo ya uwekezaji), licha ya changamoto ndogo ndogo zilizopo ambazo na zenyewe Serikali inahitaji ijipange.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, tunaona ni ukweli usiopingika kwamba deni la Serikali limepanda, lakini pamoja na hiyo, matokeo tunayaona kwenye mambo makubwa ambayo yamefanyika, kwa maana ya uwekezaji, reli, viwanja vya ndege, umeme, na mambo makubwa sana yamefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wangu katika hiki kipindi kilichobaki sasa, ni vizuri sasa Serikali tukajielekeza katika zile fedha zote tunazozitafuta ambazo zinaongeza deni la Serikali, tuzielekeze katika maeneo sasa yanayoweza kukuza Uchumi, hasa tulenge kwenye namna ya kutatua ajira kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiangalia Serikali imeweka fedha nyingi za kutosha vyuo vikuu. Wanafunzi wengi wanamaliza vyuo, lakini wakishamaliza tunaangaliana mtaani, vijana hawana ajira. Leo, kati ya tatizo na changamoto kubwa ambayo inatumaliza ni suala la vijana kukosa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vizuri tuangalie kupeleka fedha kwenye yale maeneo ambayo yanaweza kuleta matokeo ya haraka na kuongeza ajira. Mfano, unapozungumza kwenye eneo kama la kilimo, ni eneo pekee linalochukua ajira kubwa, lakini kwa bahati mbaya sana ni vijana wachache sana wanaoweza kuchukuliwa. Kwa hiyo, nadhani ni vizuri katika kipindi hiki Serikali ingejielekeza huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo. Namwita sasa Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya atafuatia Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo na baadaye atafuata Mheshimiwa Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwenye hizi taarifa mbili. Kipekee namshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambazo anaendelea kuzifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maeneo mawili nitayachangia kwa kifupi sana, *TPA* na *SGR*. Nikianza na *SGR,* wote ni mashahidi, wakati Mheshimiwa Rais anachukua nchi, ile miradi ya *SGR* ilikuwa 34%, hasa *Lot I,* lakini sasa hivi tupo 99%. Kubwa zaidi ni kwamba ameshasaini *Lot III, to Lot VIII.* Kutoka *Lot* III mpaka *Lot* ya VIII, haya ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hilo, tulianza mwaka 2024 Juni mpaka Januari, wasafiri zaidi ya 1,500,000 walikuwa wametumia *SGR.* Ukiacha hilo tumekusanya shilingi bilioni 44 ndani ya miezi Sita. Haya ni mafanikio makubwa sana ambapo wastani kwa mwezi tunakusanya shilingi milioni 600, lakini wastani kwa mwezi takribani abiria 214 wanapanda *SGR.* Haya ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya kwa nini yametokea? Kuna mambo matatu; la kwanza, kumekuwa na uthubutu mkubwa sana. Hayati Dkt. Magufuli alithubutu kuanzisha, akaacha ipo 34%, lakini Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameitoa 34% ipo 99%, na bado amekwenda kusaini mikataba mingine; wa tatu hadi wa nane. Haya ni mafanikio makubwa sana kwa sababu kuna *commitment* ya viongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, huu ni mradi wa kipekee. Kwa nini mradi wa kipekee? Ukiangalia kwa Afrika hii ndiyo reli ambayo itakuwa ndefu kuliko reli nyingine za Afrika,

lakini pia kati ya reli za kidunia hii ni reli ya tano ndefu kidunia. Haya ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho la kipekee ni umuhimu wa *SGR*. Wote ni mashahidi kwamba *SGR* itafungua nchi za maziwa makuu pamoja na kufungua nchi za Kongo, Rwanda na kwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia hili, tunakwenda kukuza uchumi wetu. Mmeona ninyi wenyewe sasa hivi idadi ya abiria ambao wanasafiri kwa kupitia hii reli ya *SGR*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wangu ni nini? Sisi kama Kamati tumepitia, kuna mambo machache ambayo tungependa kuishauri Serikali. La kwanza, tunategemea kuanzisha *SGR* kwa ajili ya mizigo. Tunahitaji kuimarisha zile barabara ambazo zinakwenda kwenye zile *station* ili kuhakikisha kwamba kwenye yale maeneo tuwe na barabara ambazo zinafikika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna *overpass* ambazo zimejengwa, hususan kule kwangu Bahi na Manyoni kwa kipande kile cha *lot* ya kutoka Dodoma kwenda Makutopora zilikuwa hazijakamilika. Ningeshauri na Mheshimiwa Naibu Waziri yupo pale ananiangalia; hebu malizieni basi ili *SGR* ianze kufika na kule kwetu Manyoni. Watu wa Manyoni watashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni kuhusu *TPA*. Wote ni mashahidi kwamba *TPA* imefanya maboresho makubwa sana. Kuna maeneo mawili makubwa ambayo *TPA* imefanya. La kwanza, kuboresha miundombinu *(infrastructure development)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona Tanga wameboresha, Dar es Salaam wameboresha, Mtwara wameboresha, na Mbamba Bay wameboresha. Eneo la pili ni suala la ufanisi. Wote ni mashahidi, kulikuwa kuna *debate* kubwa kuhusu *DP world*. Kuna watu walibeza, lakini ujio wa *DP World* umeleta mafanikio makubwa sana kwenye Bandari yetu ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ukiangalia pale, sisi tulikwenda kama Kamati. Hata utendaji wa *TPA* umeongezeka

sana. Kumekuwa na *installation* ya mashine nyingi sana za kisasa, na vilevile kuna matumizi makubwa sana ya teknolojia. Hivi vyote vimekwenda kuboresha sana utendaji wa *TPA*. Sasa, ni vitu gani ambavyo vimeongezeka baada ya kuongezeka *DP World*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni kuhusu muda. Kabla ya kuja *DP World* muda wa kusubiri meli kupakua mizigo ulikuwa mrefu sana, lakini sasa hivi tumepunguza sana muda wa watu kusubiri meli pale. Lingine ni kuhusu mapato. Mapato yetu yameongezeka sana. Taarifa iliyotolewa na *TRA* kwa kipindi kilichopita, tumeona mapato yameongezeka sana kwa upande wa *TPA*. Vilevile wameleta mitambo ya kisasa ambayo imerahisisha sana usimamizi pamoja na utoaji wa mizigo bandarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa upande wa *TPA* ni mambo matatu. La kwanza, tunataka kujipima sasa hivi tukiji-*compare* na Mombasa, sisi tunasimamia wapi? Niishauri *TPA,* fanyeni *study*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, watuambie, nini mkakati wa *TPA* wa ku-*compete globally* kushindana na bandari nyingine kubwa ili nasi tuhakikishe kwamba tunaboresha *TPA,* Bandari yetu ya Tanzania, tunaboresha ukusanyaji wa mapato, na kubwa zaidi tuangalie sasa *impact* ya *DP World*, tuone ili tuwaambia wananchi vile vitu walivyokuwa wakibeza baada ya kuleta *DP World,* waone sasa kumbe ile ndoto ilikuwa ni halali na imeleta matunda makubwa ili hayo matokeo tuyatumie kwa kuboresha maeneo mengine….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya.

**10 FEBRUARI, 2025**

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake katika nyanja mbalimbali kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wenzangu wote kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali nzima ya Awamu ya Sita kwa jinsi wanavyoliongoza Taifa letu na kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 hadi 2025, Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli yapo mambo mengi sana yametekelezwa hususan miradi ya maendeleo iliyoshindikana katika sekta mbalimbali kwa muda mrefu katika jimbo langu la Mbulu Mjini na maeneo mengine mengi hapa nchini. Hivyo, naomba nitumie muda huu kuwaomba Watanzania kutambua jitihada hizi za Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia maoni na mapendekezo ya Kamati zetu zote mbili, kwanza, kwa kuwa lengo la kuanzishwa kwa mradi wa magari yaendayo mwendo kasi katika Jiji la Dar es Salaam ni kuondoa adha ya msongamano wa foleni ya magari na kuboresha huduma ya usafiri kwa wananchi.

Hivyo basi, Serikali ichukue hatua ya mradi ule kubinafsishwa kwa mwekezaji kwa utaratibu wa Serikali kupata gawio la fedha kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wastaafu wengi waliostaafu miaka ya zamani wanalipwa kiwango kidogo sana cha shilingi 100,000/= hadi shilingi 200,000/=, hivyo basi, naishauri Serikali iangalie upya utaratibu wa kuboresha kiwango cha malipo ya mwezi kwa wastaafu nchini, kwani kwa sasa kiwango kinacholipwa kwa wastaafu nchini ni kidogo sana kwa mwezi ukilinganisha na kupanda kwa gharama ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kumekuwa na ushindani mkubwa sana katika huduma za simu nchini, hivyo basi, kuna umuhimu wa Serikali kuangalia upya utaratibu wa kuboresha minara yetu, kwani kwa sasa huduma zetu za simu ya *TTCL* kwenye maeneo mengi nchini zinakosa wateja kwenye soko na kushindwa kukabiliana na ushindani mkubwa ulioko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa 100%, na ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Sasa tunahamia upande wa Serikali ambako pia tutatumia dakika tano tano kuchangia na watoa hoja wajiandae kwa dakika zisizozidi kumi kwa kila mmoja. Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwanza kwa kunipa nafasi. Pili, nataka niipongeze Kamati zetu zote mbili kwa taarifa zao za kina na uchambuzi makini sana na mapendekezo ambayo wameyatoa ambayo baadaye Bunge lako likiridhia yatakuwa ni Maazimio ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *PIC* wametoa mapendekeo 12 ambayo yanaihusu Ofisi yangu moja kwa moja, na niwaahidi kwamba sisi hatuna tatizo na mapendekezo hayo na tupo tayari kuyapokea na kuyatekeleza. Pia Kamati yetu ya Bajeti imezungumzia sana kuhusu suala la ruzuku kwa Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu mambo mawili. La kwanza ni kuhusu mashirika ya umma ambayo yanasuasua na yale ambayo yanapaswa kufanya biashara, lakini hayafanyi vizuri. Kama mnakumbuka, mwaka 2024 na mwaka 2023, Serikali iliamua kufanya uchambuzi na tathmini ya utendaji wa mashirika ya umma. Tulibaini mashirika ya umma ambayo baadhi yao majukumu yao yanaingiliana, na mengine majukumu yao yamepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya uamuzi wa kuanza ama kuyaunganisha mashirika ya namna hiyo na mengine

kufutwa. Tayari kufuatia uamuzi huo, Serikali ipo katika hatua mbalimbali za kuleta Miswada ya Sheria hapa Bungeni kwa lengo la kutekeleza uamuzi. Wakati wowote, kwa jinsi ambavyo Bunge litatupangia, tunaingiza Muswada hapa kusomwa kwa mara ya pili ambao utaunganisha kwa mfano, *TIC* na *EPZA* kama sehemu ya kutekeleza maamuzi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote hiyo ni katika kuboresha Mashirika ya Umma. Lengo la Serikali ni kuona kwamba kwanza mashirika ya umma yanafanya kazi kwa ufanisi. Yale ambayo yanaweza kutoa huduma, yafanye kazi kwa ufanisi. Pili, yale mashirika ya umma ambayo tumesema yafanye biashara, yafanye biashara kweli bila kuingiza Serikali gharama yoyote. Huo ndiyo mwelekeo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, tusingetaka kuona mashirika ya umma yashindane na sekta binafsi. Tumeshakubaliana kama nchi kwamba muhimili wa uchumi hii ni uimara wa sekta binafsi. Kwa hiyo, tusingetaka kuweka kikwazo chochote katika hilo. Kwa hiyo, mashirika ya umma yafanye kazi ya ku-*complement* pale ambapo sekta binafsi haiwezi kufanya lazima ifanywe na mashirika ya umma. Kwa hiyo, hayo ndiyo maelekezo ya Serikali na tutaendelea kuyasimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni suala la mbolea. Kamati yetu ya *PIC* imetoa mapendekezo kwamba *TFC* na Serikali kwa ujumla tujenge kiwanda cha mbolea ili kuondokana na changamoto ya mbolea, ambapo karibu kila mwaka tunatumia takribani zaidi ya trilioni moja kwa ajili ya kuagiza mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba Serikali imeshaweka mazingira mazuri sana ya kuvutia wawekezaji, na tayari mnafahamu kuna kiwanda kikubwa hapa Dodoma kimejengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nitoe taarifa kwamba Serikali ipo katika mazungumzo na wawekezaji kutoka Indonesia ambao wanakwenda kujenga kiwanda kikubwa sana cha kutumia gesi pale Mtwara kwa mara ya kwanza katika suala la

mbolea na kwa ukubwa wake, kiwanda hicho kikikamilika changamoto ya mbolea itaisha kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mwelekeo wetu sisi kama Serikali mwelekeo ni kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji, kuvutia makampuni makubwa kutoka duniani kuja kujenga viwanda vya mbolea. Hapa kulikoni Serikali kujenga viwanda yanyewe? Huo ndiyo mwelekeo, na ninaamini tunakwenda vizuri. *Otherwise* nirudie tena kusema kwamba sisi tunapokea mapendekezo haya na tupo tayari kuyatekeleza, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Prof. Kitila Mkumbo kwa mchango wako, Mheshimiwa Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye hoja zilizoko Mezani. Nianze kwa kuzipongeza Kamati zetu mbili kwa hoja nzuri walizoweka Mezani; na kwa sababu na sisi ni sehemu ya Kamati, mambo mengi ambayo wameongea, tumeweza kupata *engagement* na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo ilivyo utamaduni, Serikali pamoja na Kamati za Bunge zinazosimamia sekta tunafanya kazi kwa ukaribu. Kwa hiyo, tunakubaliana na mapendekezo ambayo Kamati zimekuja nayo, nasi kama Serikali, tumeyapokea masuala hayo ambayo wameyawasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umahususi tu, nisemee maeneo mawili. Moja, yale yote ambayo yanahusiana moja kwa moja na hatua za kikodi, ikiwemo jambo la *refunds* za masuala ya kodi, kwa kuwa tuko kwenye muda huu, mchakato wa mambo makubwa mawili; tuna jambo moja kubwa ambalo Serikali inafanya. Kwanza, kurekebisha mifumo yetu ya kikodi kutoka kwenye masuala ya kianalojia ambayo shughuli hizi za ukusanyaji wa mapato zinazofanyika kwa namna ya mikono kwa mikono ama kwa madirisha kwenda kwenye *automation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshafanya hatua kubwa upande wa *customs* na tumeshafanya hatua kubwa upande wa kodi za ndani. Kwa upande wa *customs,* nadhani tayari tumesha-*navigate,* ambapo tumekwenda kwenye mfumo mpya na sasa tunamalizia malizia upande wa kodi za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ndilo lililokuwa linasababisha utaratibu wa kutoa *refunds* uchukue muda mrefu utaratibu wa *assessment* uchukue muda mrefu na hata utaratibu wa makusanyo ya kodi za miaka ya nyuma. Sasa tutakapokuwa tumekamilisha haya masuala ya kimfumo, tutaweza kutaja rasmi ni lini tunaweza tukatekeleza yale ya kupunguza muda wa *refunds*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii tulisema wakati wa bajeti kuu na sasa tunasema kwamba tunaelekea hatua nzuri kwenye masuala ya mifumo, na tukishamaliza masuala ya mifumo tutapunguza kwa kiwango kikubwa matatizo yaliyokuwa yanajitokeza yaliyotokana na *backlogs* ambazo zilikuwa zinasababishwa na ufanyaji kazi *manually*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili kwa kuwa tunaelekea sasa kwenye maandalizi ya masuala ya kodi, nadhani tutalitolea tamko pamoja na hili, kwamba tuko kwenye hatua gani katika utekelezaji wake. Tunalifanya hili tukijua kwamba litaongeza ufanisi na likishaongeza ufanisi, litatutoa kwenye matatizo yaliyokuwa yanajitokeza. Tulifanya hivyo, na tulifika hata kuvumilia matatizo ya aina hii ili tusiathiri masuala ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelipa lingine linalohusiana na masuala ya *guarantee*; tumepokea kama Serikali kwa sababu tutakuwa na muda mrefu wa kufanya *engagement* na Kamati za Bunge. Haya nayo tutajadili kwenye Kamati na tutayatolea matamko tutakapokuja kwenye kipindi kirefu ambacho tutakuwa tunajadiliana masuala ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote kwa yote, tupongeze pia mjadala wa Bunge. Bunge limetoa hoja nzuri na Bunge lako hili limeendelea kuthibitisha kwamba ni Bunge lenye Wabunge makini na hata wapigakura wasisite kuwarejesha tena Wabunge

hawa ambao wanafanya kazi usiku na mchana kwa ajili ya kusimamia maslahi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha. Sasa nawaita watoa hoja. Kama ambavyo nimeelekeza kila mtoa hoja atatumia dakika zisizozidi kumi kukamilisha hoja yake. Naanza na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)*.

**MHE. VUMA A. HOLLE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nyingine ya kuja kuhitimisha hoja ya Kamati. Awali ya yote, nawapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hoja yetu ya *PIC* na wengi wamejikita kwenye maeneo kama matatu hivi, wamejikita kwenye mradi wa *BRT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama niliivyosema *BRT* ni mradi ambao kimsingi Serikali imeweka fedha nyingi sana. Awamu ya kwanza na ya pili Serikali imeweka zaidi ya shilingi bilioni 847, awamu ya tatu Serikali imeweka dola milioni 148.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni fedha nyingi sana za Watanzania, kwa sababu hata hii mikopo ambayo tumekopa inaenda kulipwa na kodi za Watanzania. Tija yake inakuwa ndogo kama alivyosema na tulivyosema kwenye Kamati. Ni kwa sababu, awamu ya kwanza yanatakiwa ya-*operate* mabasi 305, lakini yana-*operate* mabasi 100 peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya pili, mradi umekamilika lakini hakuna mwekezaji ambaye anaendesha mradi ule. Awamu ya tatu, tuko *almost 50%* ya utekelezaji, lakini mchakato wa kumtafuta mwendeshaji haujaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii haikubaliki hata kidogo. Lazima Serikali ichukue hatua kuhakikisha kwamba hizi fedha nyingi

ambazo ni za walipakodi wa Tanzania, usimamizi unakuwa ni mzuri, kuhakikisha kwamba mradi huu unakuja kuwa na tija ambayo ilikusudiwa wakati wa kubuniwa kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezunguzia kuhusu *TFC,* na nimpongeze hata Mheshimiwa Waziri amezungumzia jambo hili. Sisi hapa tunataka kiwanda cha kutengeneza mbolea, siyo cha ku-*blend* mbolea. Kuna kiwanda cha kuchanganya mbolea na cha kutengeneza mbolea. Hapa Tanzania hatuna viwanda vya kutengeneza mbolea, bali tuna viwanda vya kuchanganya mbolea. Kwa hiyo, tunataka kiwanda kikubwa cha kutengeneza mbolea ili tusiagize *UREA* kutoka nje. Tumekaa na *TFC,* tumezungumza nao, ina-*cost* kati ya dola bilioni moja mpaka dola bilioni 1.5. Wakati huo huo sisi kila mwaka tunatumia zaidi ya dola milioni 500 kwa ajili ya kuagiza *Urea* kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijenga kiwanda hapa, maana yake tunapunguza matumizi ya fedha za kigeni kwenda nje ya nchi, lakini pia ile tunayozalisha hapa hatutaimaliza, tutawauzia mpaka wa *East Africa* hapa. Kama tumeweza kujenga reli, tumeweza kujenga Bwawa la Mwalimu Nyerere, hili jambo haliwezi kuishinda Serikali. Tunataka Serikali itujengee kiwanda cha kuzalisha mbolea hapa, na siyo cha kuchanganya mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Waheshimiwa Wajumbe wengi wamezungumza kuhusu *ATCL.* Tunaipongeza sana Serikali, inafanya uwekezaji mzuri sana kwenye ndege. Imenunua *so far* ndege 15. Kwa hili, kweli tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifanya. Tulikuwa tumezoea ukienda huko nje ndiyo unakuta ndege za watu zimepangwa, sasa hivi ndege zetu nazo pia zinaonekana mpaka nje ya nchi huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya msingi ni kwamba hizi ndege hazimilikiwi na *ATCL. TGFA* ndiyo wanaomiliki. Hao wote ni Serikali. Sasa kwa sababu ziko chini ya *TGFA,* maana yake ni kwamba vitabu vya *ATCL* havisomi vizuri, mizania yake inakuwa haiko vizuri. Hakopesheki kwa sababu anaonekana ana madeni anadaiwa, hali ambayo inakuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yote ni Serikali tunataka tu ule umiliki na mchakato unaendelea, sema umechukua muda mrefu na ndiyo maana tumesema angalau mpaka Juni mwaka huu 2025 shughuli hii iwe imeshakamilika ili tuwe na vitabu safi vya *ATCL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuhitimisha hoja yangu na kwa namna ambavyo umetupa nafasi ya kutu-*guide* na kutuongoza katika kikao hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kuhusu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma na Maoni na Mapendekezo yake, wanaoafiki waseme ndiyo, na wasioafiki waseme siyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma yalipitishwa na Bunge kuwa Maazimio ya Bunge)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Bunge sasa limepitisha taarifa hii, maoni na mapendekezo yake kama yalivyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati kwa niaba ya Kamati nzima.

Namwita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuhitimisha hoja za Kamati yetu. Kwanza,

nianze kwa kuwashukuru sana, tena sana, Wabunge 13 ambao wamejadili hoja hizi wakiwemo Mawaziri makini wawili. Nawashukuru sana kwa sababu wote wameunga mkono hoja na kwa kweli inaonyesha kwa kiasi gani Bunge lako linatilia maanani ushirikiano kati ya Serikali na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ambayo yamezingatiwa ni yale ambayo yapo kwenye taarifa zetu. Kwa upande wa Wabunge wamesisitiza kuboresha mifumo ya *TRA* ili iweze kusomana, pia iweze kuongeza mapato. Hili nafikiri liwe la msisitizo kwa Bunge lako ya kwamba *TRA* inahitaji mifumo yake iweze kuboreshwa, iweze kusomana na iweze kufanya kazi zote zile zinazotakiwa. Kwa sasa hivi kwa sababu kuna *artificial intelligence,* iingize hata mifumo ya kisasa kama *artificial intelligence* ili kila anayepaswa kulipa kodi aweze kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limesisitizwa ni suala zima la ku-*promote cashless economy* (malipo yasiyo ya pesa taslimu). Ukiangalia kwenye Taarifa yetu ya Kamati ya Bajeti, tumekuwa tunalisisitiza hili mara nyingi na tunaendelea kusisitiza kuhakikisha kwa uharaka zaidi Serikali ilete tamko la kwamba malipo yote yasifanyike kwa pesa taslimu. Hili litalenga kuongeza hata wigo wa mapato na malipo ya pesa taslimu, iwe kwa kiasi kidogo kama alivyowasilisha au alivyopendekeza Mheshimiwa Nahodha, isizidi shilingi 200,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo tumeona hata majirani zetu wamekuwa wakifanya hivyo, kwamba ukipanda bajaji au daladala hulipi kwa *cash;* ukilipa kwa *cash* majirani zetu wanatushangaa, wanasema, "Tanzania mbona bado mko nyuma sana!" Kwa hiyo, tunakuomba hili liweze kusisitizwa na hili litasaidia sana kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limesisitizwa sana ni kuongeza mapato ya *forex*. Hili msisitizo wake utauona kwa namna wakulima kwanza wanavyompongeza Mheshimiwa Rais kwa kuongeza bajeti kwenye kilimo kwa sababu bajeti ya kilimo na kilimo ndiyo kinaibeba Tanzania, na kinaajiri zaidi ya 60% ya watu. Kwa hiyo, ukiongeza bajeti ya kilimo, ina maana itaongeza hata ukuaji wa uchumi kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuongeza bajeti ya kilimo, tuhimize Serikali iangalie ni jinsi gani tuweke viwanda kwa ajili ya kuchakata mazao yetu. Tusipeleke mazao yetu ambayo hayajachakatwa kuuzwa nje. Nchi yetu imebarikiwa na Mwenyezi Mungu, na hili linaweza kuwa kapu la chakula, siyo kwa Afrika tu bali kwa dunia nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tulione hilo la kwamba ukiangalia na nchi nyingine, kwa hili, sisi tuna-*competitive advantage*. Kwa hiyo, hata Waziri wa Mipango anapotayarisha mpango wake, mpaka mwaka 2030 azingatie hilo. Tanzania iwe na mikakati ya makusudi ya kuhakikisha kuwa sisi kilimo ndiyo kinatubeba na kilimo kitatubeba kuweka ufanisi na kitatubeba kuhakikisha kuwa tunaweka viwanda ili wakulima wetu waweze kupata bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limezungumzwa kwa kiasi kikubwa ni suala zima la maboresho ya bandari yetu. Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia zaidi kuhusu uwekezaji wa *DP World* kwenye Bandari yetu ya Dar es Salaam. Kwa kweli mwenye macho haambiwi tazama. Hili limeonesha dhahiri ya kwamba ni kiasi gani sekta binafsi inaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa kuweka msukumo kwenye uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato yanayopatikana sasa hivi kwa kiasi kikubwa yanatokana na uwekezaji wa *DP World.* Ni kweli hata Wabunge tulipigwa madongo na Serikali ilipigwa madongo kwa ajili ya *DP World.* Kuna msemo unasema, *the best revenge is success and good work.* Huna haja ya kujibishana na maadui zako. Wewe lenga kwenye kufanya kazi kwa bidii, matokeo ndiyo yatakubeba. Hicho ndicho ambacho amekifanya Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, kwamba hata walipopiga kelele wote, yeye alikaa kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kimya kimya, wao wenyewe wanasema, kwa kweli lile jambo ni zuri, na hilo litatuweka mahali pazuri sana, ukiangalia na ushindani wa bandari yetu kwamba inashindana na nchi mbalimbali. Sisi ili tushindane, reli zetu ziweze kufanya kazi vizuri, ni uboreshaji wa bandari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni mapato yatokanayo na mashirika yatu ya umma. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango, amelizungumza hilo kuwa azingatie kuhakikisha kuwa Serikali inatazama kutoa ruzuku kwenye mashirika yetu yanayofanya kazi kibiashara, lakini kalisema kuwa Serikali isishindane na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwenye taarifa yangu ya kwamba mashirika yetu ambayo Serikali ina asilimia kidogo, ndiyo yameleta mapato makubwa kwenye kapu la mapato ya Serikali. Kwa hiyo, tuangalie namna gani haya mashirika ambayo yanafanya kibiashara kuya-*prune* kuhakikisha kuwa tunabaki na mashirika ambayo yatafanya vizuri badala ya kuwa mzigo kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuhitimisha na ninawashukuru mno Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nawahoji kuhusu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti pamoja na maoni na mapendekezo yake. Wanaoafiki waseme ndiyo, wasioafiki waseme siyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti yalipitishwa na Bunge kuwa Maazimio ya Bunge kwa Serikali)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na Mawaziri

ambao mmepata nafasi ya kuchangia hoja ambazo zililetwa Mezani leo. Kipekee nawashukuru sana Serikali ambao walipata nafasi ya kupokea hoja hizo na kuahidi kwenda kuzifanyia kazi.

Kwa namna ya pekee sana, nazipongeza Kamati zetu mbili; kwanza, Kamati yetu yetu ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma chini ya uongozi wa Mheshimiwa Vuma Augustine Holle na Makamu Mwenyekiti wake kwa wasilisho zuri na kwa kuhitimisha hoja vizuri.

Aidha, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya uongozi wa Mheshimiwa Oran Manase Njeza, pamoja na Makamu Mwenyekiti wake na Wajumbe wote wa Kamati kwa kuwasilisha na kuhitimisha hoja ya Kamati yao vizuri na sasa zimegeuka kuwa hoja za Bunge.

Ni matumaini yetu kwamba Serikali baada ya kuzipokea hoja hizi, watakwenda kuzifanyia kazi na Bunge litapata mrejesho kwa utaratibu ambao Bunge limejiwekea.

Baada ya hayo nahitimisha kikao cha Bunge mpaka kesho siku ya Jumanne, tarehe 11 Februari, 2025, saa 3.00 Asubuhi.

*(Saa 7.48 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne Tarehe 11 Februari, 2025, Saa Tatu Asubuhi)*